

29 MEI, 2013

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 29 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Zungu Azzan) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA  
KIMATAIFA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

29 MEI, 2013

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA KAZI NA AJIRA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Kazi na Ajira Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 295

**Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino Kuhamia Chamwino**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE** aiuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imeendelea kufanya kazi zake Dodoma Mjini tokea kuundwa kwake karibu miaka kumi iliyopita.

(a) Je, Serikali itatoa maelekezo kwa watumishi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kuhamia Chamwino yaliyoko Makao Makuu ya Wilaya hiyo?

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu malipo ya uhamisho kwa watumishi wa Halmashauri hiyo watakaohamia Chamwino?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya ya Chamwino bado unaendelea. Hadi sasa Serikali imepeleka shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hizo na kwa mwaka 2013/2014 zimetengwa milioni 500. Sambamba na ujenzi wa ofisi, Serikali imeidhinisha shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba sita (6) za watumishi ambapo nyumba tatu ziko katika hatua ya umalizaji.

Aidha, Serikali imepima viwanja 3500 kule Chamwino ili pamoja na shughuli nyingine ziweze kutumika kujenga nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za ujenzi wa nyumba za watumishi ni kubwa, Serikali peke yake haiwezi kukidhi gharama za ujenzi kwa Halmashauri zote zinazoanzishwa. Tunatoa wito kwa taasisi mbalimbali za kifedha ikiwemo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mashirika binafsi kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba za watumishi.

Aidha, Serikali inaziagiza Halmashauri zote ambazo hawajahamia kwenye Makao Makuu yake wahamie mara moja.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhamisho wa watumishi, mwajiri anapaswa kuzingatia taratibu zote za uhamisho wa watumishi kwa mujibu wa Kanuni L8 na L33 za Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma toleo la mwaka 2009. Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino inashauriwa kutenga katika bajeti yake fedha za uhamisho kwa ajili ya watumishi wake.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili.

Kwanza, swali langu lipo *very specific*, ninataka maekelezo kutoka Serikalini kwa watumishi kuhamia Chamwino. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri juu ya hatua mbalimbali za ujenzi wa Makao Makuu yanaashiria kuwapa mwanja watumishi hao waendeleo kusubiri mpaka majengo yaishe. Sasa bado nashikilia kwamba Serikali itamke ni lini watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino watahamia kwenye Makao Makuu ya Wilaya ukiachilia mbali ujenzi huu unaoendelea kwa sababu pale zipo nyumba za kutosha na isitoshe DC yuko kule kutoka Wilaya hii ianzishwe?

Pili, kwa sababu azma ya kupata Wilaya mpya ni kuwasogezea wananchi huduma za utawala, sasa kwa kubakia muda mrefu baada ya kutangazwa Wilaya mpya watumishi hawajahamia bado, haioni kwamba inakinzana na azma rasmi ya kupata Makao Makuu ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Chamwino nimekwenda na Makao Makuu ya Wilaya anayoyoyazungumzia nimefika na Mheshimiwa Chibulunje anafahamu kwamba tumefika katika yale maeneo. Maelekezo ni kwamba Halmashauri zote mpya na Wilaya zote mpya ambazo zimeanzishwa watumishi wake wanatakiwa wawe katika Makao Makuu ya Wilaya yaani pale ambapo huduma zinatolewa.

Sasa lakini kitakuwa ni kichekesho kama unajua kabisa kwa mfano hapa tumeanzisha karibu 16 yaani Wilaya mpya nyingi tu, hivi tunavyozungumza ukienda katika Makao Makuu ni pori, tulichofanya pale ni kwamba tumekodisha tu maeneo

29 MEI, 2013

au tumetafuta maeneo ili watu wakae kwa muda. Naelewa anachozungumza Mheshimiwa Chibulunje, kwa maana ya maelekezo ya Serikali, maelekezo ni kwamba Halmashauri zote na Watumishi wake wote wakae kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Lakini katika uhalisia wake ukienda kule hakuna nyumba za watumishi, wako wengine ambao wamehamishiwa katika maeneo ya Vijijini kama tunavyozungumza hapa, ndiyo maana nimezionyesha jitihada za Serikali kwamba zipo nyumba za Serikali zinazojengwa kule.

Sasa najua kwamba anapozungumza pia habari ya posho, posho ya kuwahamisha hao watumishi kwenda kule ni shilingi milioni 750 ndiyo utakuwa umemaliza zoezi lote zima na ninajua watakwenda pale halafu kimyakimya watarudi tena utawakuta wamebana hapa Dodoma. Ni pamoja na Bahi ambao tumeshawelekeza kwamba waondoke waende Makao Makuu ya Bahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ili nisichukue muda wako nataka niseme kwamba sisi tunajitahidi pamoja nao, hizi fedha wala hazikutengwa kwa hiyo, kwamba mimi nitamwambia njoo uchukue shilingi milioni 750 kachukue, hazipo, lakini tutakaa na yeye Mheshimiwa Chibulunje na wenzake tukae wote kwa pamoja tulitafakari jambo hili tuone tunapata wapi fedha hizi ili tuweze kuwahamisha hawa watumishi ili ugomvi uishe. *(Makofi)*

Na. 296

### **Kujenga Mabweni kwa Ajili ya Wasichana**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. RIZIKI SAID LULIDA)**  
aliuliza:-

Mkoa wa Lindi ni wa mwisho kwa idadi ndogo ya mabweni ya wasichana hali inayopelekea kuongezeka kwa tatizo la mimba za utotoni.

Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kujenga mabweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kila mwaka hutenga fedha za ujenzi na ukamilishaji wa mabweni na hosteli. Aidha, Serikali inatoa fedha za ruzuku ya maendeleo (LGDCG) kwa kila Halmashauri kwa ajili ya utekelezaji miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu ya shule kulingana na vipaumbele vya Halmashauri.

Mwaka 2012/2013 Serikali kupitia Bajeti na mipango ya Halmashauri ilitenga zaidi ya shilingi bilioni 10.8 kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa hosteli mwaka 2013/2014 zimetengwa shilingi bilioni 5.

Serikali mwaka huu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inajenga hosteli katika shule mbalimbali nchini. Katika shule za sekondari Nkowe, Ng'apa na Nachingwe ujenzi wa hosteli zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 288 unaendelea kwa thamani ya zaidi ya shilingi milioni 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi unahitaji hosteli 280 ili kukidhi mahitaji kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Serikali. Kati ya mwaka 2005 hadi 2012 wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa kushirikiana na Serikali na wadau wengine wa maendeleo wamekamilisha ujenzi wa hosteli katika shule 20 zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,514, hivi sasa wanafunzi wa kike 1,435 wanatumia hosteli hizo ikiwemo katika shule za sekondari Mnala, Nongogo, Nakiu, Chingongwe, Nangamo na Matekwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa mandeleo itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia nchini kila mwaka. Aidha, hatua hali zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wanaobainika kusitisha masomo kwa watoto wa kike. Natoa wito kwa jamii na wadau mbalimbali kushirikiana kwa dhati katika jukumu la kumlea, kumlinda na kumsaidia mtoto wa kile popote alipo ili aweze kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni dhahiri kwamba kuna mahitaji makubwa ya mabweni nchini na kwamba kwenye miji miji mikubwa kama Dar es Salaam watoto wetu wanapata adha kubwa sana asubuhi na jioni wanapokwenda shuleni kwa sababu daladala huwa zinawasumbua sana na tena wamewabandika majina ya kusoma. Kwa nini sasa Serikali isiwe na mkakati maalum wa kutafuta fedha ili kuhakikisha tunamaliza tatizo hili la mabweni katika nchi yetu yote?

Pili, kumekuwa kunajitokeza tatizo la mimba hapa nchini linaloamuliwa rejareja kati ya wazazi na Walimu au waweka mimba na kadhalika, jambo ambalo linashusha sana idadi ya vijana wetu kuwa na elimu hapa nchini.

Je, ni hatua gani za dhati zinachukuliwa na Serikali kutoa adhabu kali kwa wale wanaowasababishia watoto wetu wa kike mimba?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwamba tunaweza tukapitisha bajeti hapa, fedha hizi zinazokwenda katika shule hizi tunazozitungumzia yaani kujenga shule na hata zahanati ni fedha zinazotoka katika *Local Government*

29 MEI, 2013

*Capital Development Grants* na hizi ni fedha ambazo zinaletwa na wahisani, ndizo tunazozitungumzia hapa na namna nyingine ya kuondoka ili kuweza kufikia lengo ambalo Mheshimiwa Njwayo analizungumzia hapa ni kwenda kwenye *own sources*. Tandahimba ya kwake pale, ukienda katika *products* yeye anapata *1.9 billion T.shillings* kutokana na Korosho, ukienda katika *products*.

Lakini ukichukua hiyo ukaiweka katika mpango au katika lengo na lengo linakupa mpango na mpango unakupa mkakati na mkakati unakupa mbinu na mbinu zinakupa ushindi, akajipanga hivyo, akajiweka pale, tutaondoka katika tatizo hilo.

Lakini kwamba tutalimaliza sisi wote hapa mpaka Urambo, Siha na kadhalika wote wana hosteli na kadhalika nitakuwa naahidi kitu ambacho hapa hakipo. Lakini naiona nia yake nzuri anayoizungumzia kwa hiyo sisi tutakuwa tunapanga na takwimu nimewapa, shule za kwake ninazo na orodha za hosteli zilizojenga tunazo hapa zimefanyika vizuri lakini tunaiona *point* yake na tutashirikiana naye katika kuondoa tatizo hili.

Hili la pili linalozungumzwa hapa la watoto wa kike kutiwa mimba na matatizo mengine. Sheria iko pale kulinda utamaduni na kuzuia utamaduni mbovu. Sheria kama ikikaa hivi haina msimamizi wa kuisimamia watoto wataendelea kupigwa mimba na sisi watu wazima tunakaa tunaangalia. Hili jambo haliwezi kuanza na Serikali tu ni lazima lianzie nyumbani, mtoto akiondoka nyumbani begi lake cheki, ukikuta ameweka pensi nyanya mwulize wewe unapeleka shuleni hii ya nini?

Ili ujue kwamba huyu akimaliza atakaa pale. Haiwezekani binti anaondoka nyumbani ni lazima kuwepo na *guidance* ya wazazi wafuatilie mwenendo wa mtoto, kama ndani amebeba simu ya mkononi ameweka kwenye begi, simu ile ndiyo itakayotumika kama kifaa cha kumfikisha huko anakotakiwa na matatizo haya kuendelea kutokea.



Lakini wakati huohuo kila mtu anatakiwa asimame katika nafasi yake, Mwenyekiti wa Kijiji asimame katika nafasi yake, Diwani asimame katika nafasi yake, Mkuu wa Wilaya asimame katika nafasi yake aseme hapigwi mtoto mimba hapa wakati mimi nikiwa kiongozi hapa. Tukishafanya hivyo tukasimamia sheria watoto wetu watakwenda watasoma barabara na watakwenda mpaka chuo kikuu hawatakuwa na matatizo na sisi tunaendelea kukuhakikishia tuta-*deal* na hawa watu *perpendicular* na tutatafuta kwamba ni nani ambao wanahusika na mpango na kuhakikisha kwamba tunawaweka katika sheria. (*Makofi*)

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Jana wakati Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi akijibu swali la Mheshimiwa Mpina kuhusu vigezo vya kuanzisha shule ya sekondari yaani *high school*, Naibu Waziri alijibu kwamba pamoja na vigezo vingine ni lazima kigezo kimojawapo iwe ni kuanzisha hosteli au kujenga mabweni. Je, hicho kigezo ni kwa *high school* tu au pamoja na shule za *O-level*? Kwa sababu si watoto wa kike tu wanaopata mimba kwa kutokukaa hosteli bali hata vijana au watoto wa kiume pia huwa wanaingia kwenye magendo ya kuvuta bangi na madawa ya kulevya na kuleta uharibifu. Hicho kigezo ni kwa *high school* tu?

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda kama ifuatavyo.

Kwanza alivyojibu Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa ni ni sahihi kabisa, huwezi kuanzisha *form Five* na *Six* halafu ukatuambia watalala nyumbani, hiyo hakuna kitu cha namna hiyo, ukianzisha *form Five* na *Six* wote watalala kwenye hosteli.

Lakini pia Mheshimiwa Christowaja anauliza kwamba je na *O-level* nayo ina masharti hayo? Sasa kuna watoto ambao wanatoka katika mazingira magumu ni pamoja na hao wa kiume ambao unazungumza, ni kweli nakubaliana na wewe ambao wanakwenda wanavuta bangi na kadhalika unakuta anatokwa na udende na kadhalika anabaki hapo barabarani. Katika *O-level* tumesema katika mazingira hayo mara nyingi inajitokeza katika maeneo ya wafugaji ambao wanatakiwa wafuatane na wazazi wao kwa ajili ya malisho na vitu vingine.

Wanapoanzisha kule Halmashauri inaweka utaratibu wake inasema sisi tunataka tuanzishe hosteli hapa lakini *O-level* hakuna sharti lolote unapoanzisha *O-level* lazima kuwepo na hostel pia, hakuna kitu cha namna hiyo, tunasema wale waliopo katika mazingira magumu na kipaumbele tumekitoa kwa watoto wa kike lakini tunazingatia pia na hili ambalo Mheshimiwa Christowaja amezungumza na watoto wa kiume ambao wapo pale.

Kwa hiyo, ukienda katika maeneo haya ambayo nimeyasema na maeneo mengine ya namna hiyo ambayo yako *highly vulnerable* kwa matatizo haya tunayoyasema hapa *O-level* tunasema kwamba tunawawekea na hostel pale ili waondokane na matatizo haya, linakuwa ni suala la mtoto anapoondoka anakwenda nyumbani sasa mzazi ndiyo anakuwa ana-*manage* hali ya maisha mpaka mtoto atakapokabidhiwa tena shule yaani atakaporudi baada ya likizo.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa, tatizo la idadi ndogo ya mabweni ambayo ipo katika Mkoa wa Lindi inafanana sanasana na idadi ndogo ya mabweni ya shule katika Wilaya ya Kondo. Lakini vilevile ukosefu huo wa mabweni huchangia sana ufaulu mdogo wa wanafunzi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia wasichana wa Wilaya ya Kondo nao waweze ku-*excel* katika maisha yao? Ahsante sana!

29 MEI, 2013

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi tu, maswali mawili tumechukua dakika 20, *only short and clear.*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *I'm going to be very clear, short and brief.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, issue hii ni ya kuiweka katika mipango ya halmashauri ya Wilaya ya Kondoaa. Kwa hiyo, wakiingiza katika mipango, ikiingia kule na sisi tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge, kuhakikisha kwamba, tunafanya hivyo. *(Makofi)*

Na. 297

### **Kuboresha Mazingira ya Walimu Wanaopangiwa Vijijini**

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA** aliuliza:-

Walimu wengi wanaopangiwa kufundisha maeneo ya vijijini (pembezeni) hukataa kwenda kutokana na ubovu wa miundombinu na ukosefu wa motisha ya mazingira magumu:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuboresha huduma na mazingira na kuweka nyongeza ya fedha za kujikimu kwa walimu wanaopangiwa vijijini?

(b) Je, Serikali ipo tayari kujenga nyumba bora za walimu kwenye maeneo hatarishi kama hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Mishahara na Maslahi kwa Watumishi, inaendelea kufanya uchambuzi kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kazi ya watumishi nchini katika maeneo ya mishahara, posho, mazingira ya kuishi na vitendea kazi.

Aidha, Serikali inazingatia Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma kulipa posho za kujikimu kwa watumishi wote. Katika kuondoa adha kwa watumishi wapya fedha za posho ya kujikimu hutumwa katika mamlaka za Serikali za Mitaa kabla walimu hawajaenda kuripoti. Mwezi Februari mwaka 2013 Serikali ilitoa shilingi bilioni 8.1 kwa ajili ya kulipa stahili za Walimu wapya na halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ilipata shilingi milioni 95.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo dhamira ya kukabiliana na changamoto zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu nchini. Katika kutekeleza azma hii mwaka 2013/2014 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika halmashauri 40 zilizobainishwa kuwa na mazingira magumu na halmashauri ya Wilaya ya Kasulu imetengewa shilingi milioni 500 katika Bajeti ya mwaka 2013/2014.

Aidha Serikali imekuwa ikitoa fedha za ujenzi wa nyumba za walimu kupitia *program* ya MEM na MMES ambapo katika kipindi cha mwaka 2009/2010 hadi 2012/2013 zimetolewa shilingi bilioni 13.9 na halmashauri ya wilaya ya Kasulu imepata shilingi milioni 150. (*Makofi*)

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake na hasa kwa kutoa shilingi milioni 500 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa Walimu katika mikoa ya pembezoni ni ukweli ambao haupingiki na kila mtu anaelewa. Ukiangalia kwa mfano kwa mwaka jana walimu ambao walipangwa katika halmashauri ya wilaya ya

29 MEI, 2013

Kasulu, ambao ni zaidi ya walimu 40 hawakuripoti katika Halmashauri ile, tatizo ni ukosefu wa miundombinu.

Hoja yangu ni kwamba, Serikali haioni sasa upo umuhimu wa kuweka posho maalum kwa ajili ya mikoa kama ya Rukwa, Katavi, Kigoma na mikoa mingine yenye matatizo makubwa kama hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kulingana na ukubwa wa tatizo hili jimbo la Kasulu Vijijini lina shule za Sekondari 15 na tunakamilisha shule ya 16 mwaka huu, lakini katika shule zote hizo tuna tatizo kubwa la ukosefu wa walimu wa masomo ya sayansi. Katika shule 15 hatuna hata mwalimu mmoja wa sayansi. Ninaomba tamko la Mheshimiwa Naibu Waziri, baada ya kikao hiki cha Bunge yuko tayari kuongozana na mimi kwenda kutembelea shule hizo nilizozitaja abaini upungufu huo wa walimu na matatizo mengine ili kuleta usawa wa haki ya kikatiba ya Mtanzania kupata elimu sawa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi, mkiongozana tu utamaliza mambo yote haya. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa hili swali la kwanza tunakubaliana na anachosema Mheshimiwa Mbunge. Wale tuliokuwa tunamsikiliza Mheshimiwa Celina Kombani, alipokuwa anatoa hotuba yake hapa alieleza pia na mkakati ambao umewekwa na Serikali wa kupita na kuangalia watu wote, kwa sababu hii kitu hatuangualii walimu tu, tunaangalia na madaktari na kada zile nyingine zote, makarani na wale wote ambao ni watumishi wa Serikali.

Mheshimiwa Waziri alieleza kwamba, upo mpango wa Serikali wa kupita na kuweza kuangalia na ku- *establish* hata na vigezo tuone ni nini kinachoweza kufanyika kwa watu walio katika mazingira haya tunayoyazungumza. Ndiyo

maana unapata hilo tatizo la kwamba, kuna walimu 40 ambao walikuwa wamepangwa kwenda Kasulu, hawakwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunataka tuseme jambo moja, hiyo isije ikatumika kama ndiyo excuse kwa hiyo, walimu, manesi na madaktari wakasema hatuendi. Walimu na madaktari wetu tunawaomba wawe na moyo wa kizalendo pia katika jambo hili. Tunajua mazingira ni magumu na nimeeleza hapa jitihada zinazofanyika. Katika hali hiyo tunazungumza hapa kwamba, tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge na tutakwenda kuangalia hali hiyo anayoizungumza kama kweli watoto wamekaa kule na hawana walimu kabisa ili tuweze kuona namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nithibitisha pia hapa na ninajibu pia swali la pili ambalo ameliuliza Mheshimiwa Mbunge hapa kuhusu Kasulu, hili tatizo la walimu wa sayansi wala Mheshimiwa Mbunge asije akafikiri liko Kasulu tu, liko Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwako utalikuta lipo pale, hili ni suala la *enrolment* kwa hiyo tutashirikiana kuona walimu hawa pia wanapatikana especially wa Hesabu, Fizikia, Kemia na Kiingereza. Haya ni maeneo ambayo yana matatizo, tunaliona hilo na tutashirikiana wote kwa pamoja. Kama ikibidi niye Kasulu mimi sina tatizo la kuja Kasulu, tufuatane twenda tukaangalie tatizo hilo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, matatizo pamoja na mazingira magumu katika nchi hii yameleta tabaka la taaluma katika shule zetu. Watoto wengi waliopo vijijini wanapata alama sifuri kwa wingi.

Je, Serikali haioni kwamba, hili tabaka la elimu limetokana na mazingira magumu na hivyo ifanye haraka sana kusahihisha tatizo hili?

29 MEI, 2013

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa na Kaka yangu Lekule Laizer, jirani yangu, najua nikijibu hili najibu pia kwa ajili ya jimbo langu na kwa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue ya division 0* na *IV ime-draw attention* ya taifa mpaka tumefika hapa tulipofika na ripoti imetoka na Serikali imechukua hatua ilizochukua. Nasema nina hakika tutaambiwa kwamba, kuna mambo mengi sana yanachangia ikiwa ni pamoja na mazingira magumu katika kupatikana kwa *divisioni 0*.

Ninachoweza kusema ni kwamba, najua Serikali sasa hivi ina mkakati wa kuhakikisha tuna- *address* matatizo hayo yote ili tuweze kuondokana na *division* sifuri kwani si jambo la kujivunia na si zuri, kila mtu hajisikii vizuri, wazazi hawajisikii vizuri, Wabunge na Madiwani hatujisikii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika baada ya taarifa ile kuwa imetoka mle ndani tutaona pia mkakati na mbinu ambazo tutatumia katika kuondokana na tatizo hili. Nina hakika Bajeti ya Wizara ya Elimu itakapojadiliwa hili jambo litakuwa limeondokana, na ni pamoja na jirani yangu Lekule Laizer. (*Makofi*)

Na. 298

**Halmashauri Kushindwa Kutoa Motisha kwa Watumishi Wake**

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Halmashauri nyingi (ikiwemo ya Rufiji) zinashindwa kutoa motisha kwa watumishi wao wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu kama vile Walimu na Wauguzi kwa madai kuwa mapato ya ndani hayakidhi:-

29 MEI, 2013

Je, Serikali haioni haja ya kutoa ruzuku hiyo ili wananchi wanaoishi maeneo hayo waweze kupata huduma bora?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba Halmashauri nyingi ikiwemo ya wilaya ya Rufiji zinashindwa kutoa motisha kwa watumishi wao wanaofanya kazi kwenye mazingira magumu kama vile walimu na wauguzi kutokana na ukweli kwamba mapato ya ndani hayakidhi. Kwa kuzingatia mazingira magumu ya wilaya ya Rufiji, Serikali katika Bajeti yake ya 2013/2014 imeidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 500 ambazo ni kwa ajili ya mazingira magumu.

Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Halmashauri hii ilipatiwa Boti nne ambazo zimesaidia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza tatizo la usafiri katika eneo la Delta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa sasa kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imekuwa katika zoezi la kubaini maeneo ya nchi ambayo kwa vigezo vya kitaaluma yatabainika kuwa ni mazingira magumu.

Kwa kuwa, zoezi hili linaendelea, naomba tuendelee kuwa na subira, nilieleza kule nyuma na imani ya wataalamu wetu mpaka hapo tutakapota ripoti kamili ya mapendekezo juu ya namna bora ya kuwapa motisha watumishi ambao wako katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaendelea kuzishauri mamlaka za Serikali za mitaa zipanue wigo wa mapato ya ndani na ziweze kutenga Bajeti na kuandaa mpango wa motisha kwa watumishi wake.



**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza jibu limenisikitisha sana, eti leo Serikali iko kwenye mchakato wa kutaka kubaini maeneo yenye mazingira magumu, wakati maeneo yanajulikana. Hivi Serikali haijui kwamba, maeneo ya Kigoma pembezoni ni magumu, *Delta Rufiji* ni mazingira magumu? Wakati wao wanasema wanaendelea kubaini maeneo ambayo yanajulikana, wananchi walioko *Delta Rufiji* wanakosa huduma, wanakufa kwa sababu hakuna wauguzi, watoto hawapati elimu kwa sababu hakuna walimu.

Je, hivi kweli Serikali haioni inawanyima haki Watanzania ambao walikuwa wanastahili kuipata kutokana na mapato ya nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mwaka 2009/2010 walipeleka Boti nne, nakubali, lakini Boti hizi hazina mafuta, ni changa la macho kwa watumishi wa wilaya ya Rufiji.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka fedha ili kuendesha zile Boti kwa uhakika ili watu waweze kupata huduma? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Utumishi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchuchuli, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya motisha pamoja na mishahara imeanza kutekeleza jukumu lake. Bodi ya mishahara imeundwa tarehe 1 Julai, 2012 na imeishabainisha wilaya 33 ambazo zina mazingira magumu. Ripoti hiyo tunayo mezani, tumeishaanza kuifanyia kazi na ndiyo maana unaona tumetenga shilingi milioni 500 kwa kila wilaya zile zenye mazingira magumu ili waweze kujengewa nyumba.

29 MEI, 2013

Kwa hiyo, hiyo ripoti tunayo tunaifanyia kazi na kila mwaka tutakuwa tunatenga fedha kwa ajili ya kukidhi maeneo hayo yenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenye mazingira magumu yanatofautiana kati ya sehemu moja na nyingine, sehemu nyingine ni matatizo ya nyumba, nyingine hawana umeme, nyingine hawana maji, nyingine hawana mawasiliano na kadhalika. Kwa hiyo matatizo yanatofautiana kati ya wilaya na wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mchuchuli hajaitendea haki kwa Serikali kwa kutoshukuru zile Boti nne. Kwa kweli naona hajatutendea Serikali vizuri kwa sababu *Delta* kulikuwa hakufikiki na sasa hivi kunafikika. Boti ni kama usafiri mwingine wa magari ya Serikali, inastahili kupewa mafuta kama ilivyo kwa magari ya Serikali na magari mengine.

Kwa hiyo, nawashauri wilaya ya Rufiji kuhakikisha wanatenga fedha kwa ajili ya mafuta ya Boti zile ambazo tumezinunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kazi inafanyika na Bajeti tumeishaiona kwa kila wilaya wametuletea ofisini na tutakuwa tunaifuata kwa kila mwaka fedha zitatolewa kwa ajili ya kutatua matatizo katika mazingira magumu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira, wilaya hizo zitafunguliwa hivi karibuni ikiwa ni pamoja na kutengenezewa miundombinu mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru kwa majibu ya jumla. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kibona kwa niaba ya Mheshimiwa Kilufi.

### **Ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira**

**MHE. ALIKO N. KIBONA (K.n.y. MHE. MODESTUS D. KILUFI)** aliuliza:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira yenye urefu wa kilomita 80 utaanza kujengwa kwa kutekeleza ahadi ya siku nyingi ya Mheshimiwa Rai?

(b) Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Igawa – Ubaruku yenye urefu wa kilomita 18 inayojengwa kwa kiwango cha lami nyepesi utakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Rujewa – Madibira – Kinanyambo (Km. 152.1) ni barabara ya mkoa ya kiwango cha changarawe na udongo. Usanifu wa barabara hii ulianza mwaka wa fedha 2007/2008 na kukamilika mwaka wa fedha 2010/2011. Usanifu uligawanywa katika sehemu mbili; Rujewa – Madibira (km. 81.0) na Madibira – Kinanyambo (km. 71.1). Kutokana na usanifu wa sehemu ya Rujewa – Madibira kupita ndani ya hifadhi ya taifa ya Ruaha, baada ya majadiliano na *NEMC*, *TANAPA*, na wadau mbalimbali ilikubalika kwamba sehemu ya barabara iliyo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ichepushwe.

Hivyo Wizara yangu kupitia wakala wa barabara kwa sasa inaendelea kufanya usanifu wa barabara ya mchepuo kati ya kijiji cha Iwalanje hadi Mapogoro (km. 25) ili kukwepa hifadhi ya taifa ya Ruaha. Aidha Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami na ujenzi utaanza pindi fedha zitakapopatikana.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Igawa – Baruku – Mbarali nayo ni ya mkoa yenye urefu wa km. 17.2 Kutokana na umuhimu wake Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 na hadi kufikia mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya kilomita 6.4 zimeishajengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi milioni 715.02. Ili kukamilisha barabara yote Serikali inaendelea na ujenzi kwa awamu kila mwaka kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa ajili ya majibu mazuri, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa vile Serikali imekuwa na utaratibu mzuri wa kujenga kwenye baadhi ya miji ya wilaya zetu barabara zenye lami nyepesi. Ipo barabara kutoka Itumba – Isongole ambayo pia inafanana na barabara inayojengwa kutoka Igawa – Madibira. Barabara hii inajengwa kwa kasi ndogo sana kati ya kilomita moja kila mwaka. Je, ni lini barabara hii inaweza ikakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema upembuzi unaendelea kwa ajili ya barabara ya kuchepusha kwenye hifadhi ya Ruaha. Nataka kujua ni lini sasa wananchi wa Mbarali watapata barabara kamili au upembuzi huu utakamilika lini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza Mheshimiwa Mbunge anauliza barabara inayoanzia Itumba – Isongole. Tuliishotoa majibu kwenye hili kwamba, barabara ile inafanyiwa usanifu wa kina. Kwanza ilifanyia upembuzi yakinifu, baada ya pale tukaingia kuanza kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, hatutaendelea kujenga kwa lami nyepesi barabara ambayo tayari tumeishaamua kujenga yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sehemu ya pili ya swali la Mheshimiwa Mbunge, kile kipande ambacho tumechepusha kwenye hifadhi kilomita 25, mwaka huu wa fedha tutakamilisha usanifu na kama nilivyosema kwenye jibu la msingi baada ya hapo tutatafuta fedha kwa ajili ya kujenga barabara yote kilomita 151 kutoka Rujewa – Kinanyambo kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, swali langu linafanana sana na swali lililoulizwa na Mheshimiwa Kibona.

Kwa kuwa, sasa hivi kutoka Ludewa kuja Madaba kuunganisha mkoa wa Ruvuma, Wilaya ya Songea Vijijini, jimbo la Peramiho na Ludewa kulikovumbuliwa makaa ya mawe, kuna barabara ambayo iliwekwa katika mpango wa kuwekwa lami kwa muda mrefu sana. Sasa hivi kwa kuwa makaa ya mawe yanaanza kuchimbwa kule uharibifu wa barabara hiyo utakuwa ni mkubwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, shemeji yangu anasema nini kuhusu kutengeneza barabara hiyo kutoka Ludewa – Madaba – Njombe, katika jimbo la Peramiho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa tutapitia kuangalia huo mpango ambao anausema ulikuwepo toka siku nyingi wa Ludewa/Madaba kwa kiwango cha lami.

Vinginevyo barabara hiyo tutaendelea kuitengeneza kiwango cha changarawe kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zinatengwa kila mwaka na mwaka huu tuna shilingi bilioni 353.

29 MEI, 2013

Kwa hiyo, tutaongeza uwezo wa kutengeneza barabara hii ili iweze kupitika kwenda kwenye hilo eneo. Lakini kama kuna mpango ambao upo wa kuweka lami basi tutaushughulikia.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, katika swali la msingi la Mheshimiwa Kilufi ilizungumziwa ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kama ilivyo kwa Mheshimiwa Kilufi na mimi katika jimbo langu la Muleba Kaskazini Mheshimiwa Rais wakati ananadi sera za chama chetu mwaka 2010 alizungumzia ujenzi wa barabara ya kutoka Muhutwe/Luhanga mpaka Kamachumu kwa kiwango cha lami, kazi imeanza. Nataka kujua Mheshimiwa Waziri mtamaliza lini hiyo ahadi ya Mheshimiwa Rais ambaye alijinasibu kwa kusema "Jungu Kuu halikosi ukoko, watu wa Wilaya ya Muleba Kaskazini hii barabara itatengenezwa?"

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyosema jungu kuu halikosi ukoko na kama Rais wa nchi hii Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ameahidi kwamba barabara itajengwa naomba niseme mbele ya Bunge hili kwamba barabara hiyo itajengwa kama alivyoahidi. *(Makofi)*

Na. 300

### **Uhamasishaji wa Soko la Mazao Nchini**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Uhamasishaji wa masoko nchini umekosa mwamko kwa sababu ya usimamizi mdogo:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani katika uhamasishaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi?

(b) Je, Serikali inatarajia kuuza wapi mazao yanayovunwa kwa wingi nchini mwetu?

(c) Serikali katika kusisitiza “Kilimo Kwanza”. Je, haioni kwamba iko haja ya kutafuta masoko ya ndani na nje ya nchi kwa ajili ya mazao yanayozalishwa katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ni kivutio kikubwa katika kuchochea uzalishaji. Aidha, Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali za kuhamasisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo kwa kuimarisha miundombinu ya masoko ili kurahisisha usafirishaji na uhifadhi wa mazao na hivyo kupunguza uharibifu wa mazao baada ya mavuno.

Aidha, hivi sasa Wizara kwenye utaratibu wa kuimarisha usimamizi wa Idara zake zote kupitia Kitengo cha Usimamizi na Ufuatiliaji (*Monitoring and Supervision*) inaboresha mfumo wa kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za masoko kwa wadau kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na mitandao ya kompyuta, ujumbe wa simu za mikononi, luninga (*TV*) na redio na kufanya majadiliano na nchi wanachama wa Jumuiya za kikanda yenye lengo la kuondoa vikwazo vya biashara ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa masoko ya mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao mengi yanayozalishwa nchini huuzwa katika soko la ndani na katika masoko ya nchi za nje kama nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*).

Aidha, fursa nyingine za masoko ya mazao ni pamoja na soko la AGOA, Masoko ya upendeleo (*Preferential Market*) ya India, China, Canada na Jumuiya ya Ulaya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Finland na Norway inaandaa utaratibu wa kutumia mfumo wa *mobile farming (m-farming)* utakaotumia simu za viganjani kwa ajili ya kuwezesha wakulima kupata na kuwasilisha taarifa za masoko, pembejeo za kilimo na huduma zingine za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kufanikisha kilimo Kwanza, Serikali pia inakamilisha maandalizi ya kuanzisha Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*) ili kuhakikisha kuwa ongezeko la mazao linalotarajiwa yatakayotokana na uwekezaji unaofanyika kupitia mipango mbalimbali ikiwemo mpango wa *SAGCOT* na Programu nyingine za uendelezaji mazao yanakuwa na soko la uhakika.

Serikali pia inafanya jitihada mbalimbali za kutangaza mazao ya kilimo kupitia kwenye mitandao mbalimbali ya kibiashara duniani pamoja na Balozi zetu nje ya nchi. Aidha, mkakati ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo nchini kabla ya kuuzwa nje ili kuongeza thamani na kumpatia mkulima mapato mazuri zaidi.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa jibu zuri alilolitoa ili kujenga amani kwa wana-Tanzania na masoko yaliyokuweco nchini. Lakini hata hivyo nina masuala mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali haitoi matumaini mazuri kwa masoko yake ya ndani kikamilifu. Je, haioni kwamba inawazidishia umaskini Watanzania ili kutokuwa na uhakika wa masoko yao ya ndani?

La pili, elimu ndio msingi wa maisha. Je, Mheshimiwa Waziri unaweza kuniambia taasisi ngapi hapa nchini zinatoa elimu ya masoko ili kumfanya Mtanzania kuwa na kipaji cha kujua nini anachokitekeleza? Ahsante sana. (*Makofi*)



**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la kuimarisha masoko ndani nimelisema katika majibu yangu ya msingi. Kimsingi masoko ya ndani yana *limit* katika matumizi ya chakula ambacho tunazalisha ndani. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba haya masoko ya ndani yanataka kukidhi kile chakula ambacho tutatumia ndani, ile ziada itakwenda nje kwenye masoko ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masoko yetu ya ndani moja ni sisi wenyewe kwanza kama Serikali tunanunua chakula, tumepanga kununua zaidi ya tani laki mbili za mahindi na mtama mwaka huu, tumeboresha Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili tuweze kununua mazao mengine yanayolimwa na wakulima kama vile mpunga, maharagwe na kadhalika. Hiyo ni mikakati ya ndani. Lakini mikakati mingine pia ni kuongeza uwezo wa kufikia masoko hayo kupitia uwekezaji kwenye barabara ya *rural roads* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la elimu ya masoko ndicho tulichosema hapa kwamba kwenye elimu ya masoko tatizo ni kwamba kitu kikubwa kinachomuathiri mkulima ni upatikanaji wa habari yale masoko. Kwa hiyo, kupitia huu mtandao wa *m-farming* ambao tunakadiria kuanzisha mwaka huu wakulima watakuwa na uwezo wa kuwasiliana na Idara *specific* ili kupata bei za masoko, bei za mazao na kadhalika. Kwa maana hiyo tutafikisha elimu hiyo kupitia redio, *TV* na kadhalika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba mahitaji katika masoko ya ndani yanawiana na uzalishaji. Lakini kumekuwepo na tatizo kubwa la kwamba wakati ambapo kuna mazao yanaoza baadhi ya maeneo nchini kwenye maeneo ya mijini ikiwemo Dar es Salaam ambapo kuna masoko makubwa ya bidhaa bei za bidhaa ziko juu sana kutokana na matatizo ya uhaba na hivyo kuwaongezea mzigo wa gharama za maisha wananchi maskini.

Je, ni hatua gani za haraka Serikali inachukua kuoanisha baina ya uzalishaji vijijini na mahitaji mijini ili kutoa faida kwa wananchi wanaolima vijijini, lakini vilevile kupunguza gharama za maisha kwa wananchi walio mijini ambao kuna soko kubwa la chakula?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya msingi nimesema wazi kwamba kuna tatizo ambalo linafanya palepale mashambani mazao yanaanza kupoteza *value* na hili moja ni tatizo la uhifadhi na tatizo la usafirishaji.

Kwa hiyo hata kama watu wanazalisha kiasi kikubwa cha mazao pale lakini wakati mwingine kuyatoa inakuwa ni tatizo gumu. Kwa hiyo Serikali kwa makusudi kupitia Wizara ya Ujenzi imeweka mikakati makusudi ya kupata miundombinu kwenye maeneo yenye uzalishaji mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo na hilo linaonekana sina haja ya kuliieza sana. Lakini hili la pili la uhifadhi ambalo ndio linatoa thamani zaidi kwenye mazao kwa sababu yanahifadhiwa na tunapunguza kupoteza upotevu wa mazao.

Hili tumelizungumza tumesema kwamba Serikali itaweka mkakati makusudi wa kuwekeza kwenye *silos* ili pawe na upungufu wa uharibifu katika mazao yanayolimwa na yanayovunwa pale katika maeneo ya palepale katika uzalishaji. Kwa hiyo, hili nadhani litapelekea sana kwa wakulima kupata faida zaidi kuliko wanavyopata sasa hivi kwenye uzalishaji wao. (*Makofi*)

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa soko na bei nzuri kwa wakulima ndio lililotupelekea Taifa hili kushindwa kufikia malengo ya *millennium* ya kupunguza umaskini.

Mfano mwaka jana bei ya pamba iliporomoka kutoka bei ya shilingi 1,100/= mpaka shilingi 660/= na kupelekea wakulima wa pamba kuingiwa na umaskini mkubwa sana kwa sababu hawakuweza hata kurudisha zile gharama zao za uzalishaji.

Je, sasa na kwa kuwa Serikali iliahidi ikasema kwamba katika miaka ijayo itarekebisha utaratibu huu. Leo Waziri atasemaje, atashirikiana vipi na sekta binafsi kuhakikisha kwamba bei nzuri ya pamba mwaka huu inapatikana angalau ya shilingi 1,500?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya pamba mwaka juzi ilipanda sana kwa sababu mzalishaji mkuu wa pamba ambaye ni Texas na maeneo ya Louisiana kule *New Orleans* Marekani walipata matatizo makubwa ikawa pamba yao imekosa uzalishaji mkubwa, sisi wengine wote wazalishaji wadogo pamba yetu ikapanda.

Kwa hiyo, pamba ni zao linalotegemea *movement* ya wazalishaji wakubwa China, India, Marekani na kadhalika. Tunachosema sisi kama Watanzania ni kwamba kile kiwango chetu cha uzalishaji kwanza kilipungua lakini na ubora wa pamba yetu ilishuka.

Serikali kupitia Bodi ya Pamba inachofanya sasa hivi ni kuongeza ubora wa pamba yetu ninawasihi wakulima kutumia mbegu bora na kanuni bora za kilimo ili tupate pamba yenye ubora zaidi na tukifikia hapo na bei ya pamba yetu itaweza kushindana na bei ya pamba zingine za duniani. *(Makofi)*

29 MEI, 2013

Na. 301

**Kufungua Kituo cha Polisi na  
Kupewa Gari la Patrol**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Jimbo la Manyovu lina maeneo mengi ambayo hayafikiki kiurahisi kwa masuala ya kiulini:-

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Kituo cha Polisi katika Kanda za Janda na Manzeze ili kukomesha matukio ya uhalifu?

(b) Je, Serikali itatoa lini gari la *patrol* kwa sababu kuna uhaba mkubwa wa magari?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo la Manyovu Mkoani Kigoma kuwa, lina maeneo mengi ambayo hayafikiki kwa urahisi kama yalivyo Majimbo mengi hapa nchini. Ni azma ya Serikali kufikisha huduma ya Polisi karibu na wananchi kwa kujenga vituo vya Polisi kila Tarafa na kila Kata/Shehia sambamba na kutoa vyombo vya usafiri, Kata ya Janda na Manzeze zitanufaika kwenye mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limeainishwa katika Mpango Kazi (*Workplan*) wa Mpango wa Maboresho ya Jeshi la Polisi ambao unatekelezwa kwa awamu ya miaka mitano mitano kuanzia mwaka 2010/2011. Hata hivyo, kasi ya mpango huu inakwamishwa na ufinyu wa Bajeti ya Maendeleo ambayo imekuwa na mwelekeo wa kupungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali haikutenga fedha za ujenzi wa Kituo cha Polisi Janda na Manzeze na kutoa gari la doria kwa maeneo hayo. Kwa sasa maeneo hayo yataendelea kupata huduma kutoka katika Kituo cha Manyovu.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge kuwahamasisha wananchi wa maeneo aliyoyataja kujenga Vituo vya Polisi na nyumba za kuishi askari sambamba na kuvipatia nyenzo za usafiri kupitia mpango wa Polisi Jamii. *(Makofi)*

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Majibu yenyewe hayajatulia sana kulingana na nilivyouliza. Lakini ninayo maswali mawili.

Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba kuna maeneo hayafikiki na haya maeneo tunayoombea vituo vya Polisi vya Munzeze na Janda ni takribani kilomita 42 kutoka hicho kituo cha Manyovu, lakini ieleweke kwamba tumejenga kituo kingine cha Muyama ambacho nacho hakina usafiri.

Ikumbukwe tena Jimbo la Manyovu tumepata Wilaya mpya ambayo tutahitaji kituo kipya cha Wilaya na uhalifu umeendelea kuwa mwingi sana. Upande wa Katundu watu wameuawa kwa ujambazi, upande wa Kilelema watu wameuawa kwa ajili ya ujambazi, upande wa Munzeze kule wafanyabiashara wanatekwa na mali zao na kazi ya Polisi ni kuhakikisha kwamba ustawi wa wananchi unakuwa mzuri.

Je, Waziri kwa majibu yako unataka kuliambia Bunge hili na Taifa kwamba sasa kujenga vituo vya Polisi, nyumba za Polisi, kutoa magari ya Polisi ni kazi ya wananchi? *(Makofi)*

Swali la pili, tumekupitishia fedha hujaonyesha nia kabisa kuonyesha kwamba utasaidia vipi vituo hivi, nini kauli ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimkubalie sana kwamba maeneo mengi kule hayafikiki na mimi nafahamu kwa sababu nimeshafika kwa taabu. Pia ni maeneo ambayo yana ujambazi mwingi na kwa vyovyote magari na vituo vinahitajika zaidi. Ninachomwambia Mheshimiwa Ntabaliba kwamba kwenye mpango vituo alivyovisema vipo, lakini uharaka alionao na shida ambayo ipo inaweza ikapungua kwa kutumia wananchi.

Kwa hiyo sisemi kwamba hata kwenye swali lake (b) sisemi kwamba wananchi ndio moja kwa moja wabebe huu mzigo, lakini wananchi wana wajibu wa kusaidiana na Serikali ili kazi hii itimie kwa haraka na iwe nyepesi zaidi.

**MWENYEKITI:**Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Said Haji. Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwisha umebakia dakika 4 tu kwa maswali.

Na. 302

**Wahamiaji Haramu**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la Wahamiaji haramu katika nchi yetu hasa kutoka Ethiopia, Eritrea na Somalia ambao wengi wao hupitia Tanzania na kufanya kituo, wengine wakiendelea na safari zao kuelekea Afrika Kusini na Msumbiji.

(a) Je, Serikali inakabiliana vipi na tatizo hili na ni mafanikio gani yameshapatikana?

(b) Je, ni wahamiaji haramu wangapi wamekamatwa na kati yao ni wangapi wamerudishwa makwao, wangapi wako Magerezani na ni wangapi wamelipishwa faini?

(c) Je, Serikali imewawezeshaje Askari wa Uhamiaji kwa kuwapatia zana, vifaa bora vya kukabilliana na kazi hiyo katika kuhakikisha usalama wa nchi yetu na watu wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kukabilliana na tatizo la Wahamiaji haramu, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji na kwa kushirikisha vyombo vyote vya ulinzi na Usalama, imekuwa ikifanya doria na misako ya mara kwa mara na operesheni ambazo zimefanikisha kukamatwa wageni wanaoishi kinyume na taratibu na kuchukuliwa hatua stahiki za kisheria. Pia Serikali inawapatia mafunzo watumishi wake ili waweze kukabilliana na mbinu mpya zinazotumiwa na wageni wasiofuata taratibu za kiuhamiaji. Aidha, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji inaelimisha umma kuhusu uhamiaji na Uraia kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na redio na programu televisheni. Elimu hii inasaidia upatikanaji wa taarifa kutoka kwa raia wema kwenda kwa wasimamizi wa sheria hizi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari, 2012 hadi Desemba, 2012 jumla ya Wahamiaji haramu 10,045 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria kama ifuatavyo:-

- Walioshtakiwa ni 3,115;
- Waliorudishwa makwao ni 4,698;
- Waliolipa faini ni 501;
- Waliopo Magerezani ni 398; na
- Wanaoendelea na kesi ni 183.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajitahidi kununua zana/vifaa bora vya kukabiliana na kazi ya kupambana na Wahamiaji haramu kama vile magari, pikipiki na Boti ili kuimarisha doria na misako. Pia Serikali inaendelea kuboresha taratibu makazi ya askari na majengo ya Ofisi.

**MHE. KHATIB SAIDI HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2007/2008 wakati Waziri aliyekuwa na dhamana hii Mheshimiwa Joseph Mungai akiwasilisha Bajeti ya Wizara yake hapa Bungeni aliliambia Bunge kwamba Serikali katika kukabiliana na janga hili la wahamiaji haramu limeitaka Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Mzumbe kufanya utafiti utakaobainisha ukubwa wa janga hili na chanzo chake ili Serikali kupitia utafiti huo ijue hatua za kuchukua.

Ningependa kujua je utafiti huo ulifanyika na kama ulifanyika ni yapi matokeo yake kwani tunaona ongezeko la wahamiaji haramu linazidi badala ya kupungua?

Suala la pili, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limekuwa likitumika katika operesheni maalum za kuwadhibiti wavuvi haramu ndani ya Tanzania, ukubwa wa janga hili la wahamiaji haramu ni kubwa zaidi kuliko wahamiaji haramu wa Kitzania. Je, Serikali haioni haja sasa ya kullitumia Jeshi kukabiliana na ongezeko hili kubwa ambalo ndani ya mwaka mmoja wahamiaji haramu 10,000 ndiyo waliokamatwa ukichanganya waliokuwa hawakukamatwa wanaweza kufika 50,000.

Je, Serikali haoni umuhimu sasa wa kutumia jeshi la wananchi wa Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri swali refu majibu yawe mafupi.



**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Khatib, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza ni kuhusu utafiti ni kweli kuwa kulikuwa na ahadi hiyo na utafiti huu ulifanyika na wataalamu waelekezi walikuwa ni Chuo cha Mzumbe, mambo ambayo yalibainika hasa ni changamoto ambazo Idara ya Uhamiaji inapambana nazo na kushauri kutoa mapendekezo ya namna ya kuyashughulikia moja katika matataizo ambayo yalielezwa kuwa yana kwaza kazi ni kukosekana kwa mawasiliano ya moja kwa moja ya kimtandao baina ya Makao Makuu na maeneo mbalimbali ya Mikoani.

Kupitia hilo utekelezaji ni kwamba sasa hivi tuna mpango wa (*E IMMAGRATION*) au *ELECTONIC MIGRATION* ambayo tunaunganisha Mikoa mbalimbali na Makao Makuu, lakini lingine lilikuwa walishauri kuwa kuna tatizo la vitendea kazi nalo ni kwamba ilishauri Serikali ipatie fedha zaidi Idara ya Uhamiaji ili iweze kuhimili matatizo ambayo yapo na hili pia kwa bahati mbaya badala Idara ya Uhamiaji kupata rasilimali zaidi kumekuwa na upungufu lakini ni moja katika mambo ambayo yalionekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mafunzo kwa ajili ya wafanyakazi na taratibu za kuwaelimisha na kuwapatia mafunzo ya mambo mbalimbali yanayo badilika inaendelea, swali la pili ni kutumia Jeshi la Wananchi.

Jeshi la Wananchi linatumika sana na watu wa Uhamiaji kwa sababu ndiyo wanapanga operesheni za pamoja au wanapanga hata misako ya pamoja lakini kabla ya Mhamiaji hajaja basi ni lazima apite kwenye *franterer* au mipaka ambalo Jeshi hilo pia ndiyo lenye dhamana. Labda kama kuna mbinu nyingine ya kuwashirikisha au tuwape moja kwa moja hili jukumu hilo wazo labda tulitizame lakini kushiriki kwa Jeshi la Wananchi ni jambo ambalo lipo na halina wasiwasi. (*Makofi*)

29 MEI, 2013

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Ntukamazina Waheshimiwa muda wetu umekwisha ninajua kila mtu ana makini lakini muda wetu umekwisha.

Na. 303

**Hatari ya kutoweka kwa Amani Wilayani Ngara  
Kutokana na Wakimbizi na Wahamiaji Haramu**

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Wilaya ya Ngara inayopakana na nchi ya Rwanda na Burundi imekumbwa na tatizo kubwa la kutoweka kwa amani kutokana na vitendo vya ujambazi na mauaji vinavyofanywa na Wakimbizi wa nchi hizo mbili pamoja na wahamiaji haramu kutoka Uganda.

Je, Serikali ina mpango gani kumaliza tatizo hilo ili wananchi wa Ngara waweze kuwa na amani na kuweza kuendelea na kazi za maendeleo bila wasiwasi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratius Aloys Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za Serikali katika kukabiliana na tatizo la Wahamiaji haramu katika Mkoa wa Kagera ikiwemo Wilaya ya Ngara ni pamoja na:-

- Kuimarisha Kamati za Ulinzi na Usalama za Vijiji na Kata ili zisaidie katika kukabiliana na tatizo hilo.
- Kuendelea kutoa elimu kuhusu Uraia ili viongozi na wananchi wawe sehemu ya utambuzi.
- Kufanya Vikao vya Ujirani mwema baina ya Vijiji ambavyo viko mpakani upande wetu na upande mwingine.

29 MEI, 2013

- Kuimarisha Vituo vya Jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ) na polisi vilivyoko mpakani na kuvipatia vitendea kazi vinavyohitaji kwa ajili hiyo.
- Kufanya operasheni za mara kwa mara katika mapori hasa katika Wilaya ya Ngara, pori la Burigi, Biharamulo na Kimisi na kuwachukulia hatua za Kisheria Wahamiaji haramu wanaokutwa huko ambao shughuli zao kubwa ni ufugaji na Ujangili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabaliana na tatizo hili, kwa sasa lipo zoezi linaloendelea la kukusanya upya takwimu za Wahamiaji haramu waliopo Mkoani Kagera ambapo kila Kata imekabidhiwa vitabu vya kuorodhesha Wahamiaji walipo katika Kata husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kulinda amani, kuwalinda wananchi na rasilimali zao dhidi ya uporaji unaofanywa na wageni. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa kufuatana na majibu mazuri ya mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja wakati wananchi wangu sita wameuawa na Wahamiaji haramu katika Kijiji cha Murubhanga Kata ya Murusagamba niliondoka na aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na alipokuwa kule akatoa ahadi kwa kungekuwa na operesheni ya Mkoa mzima kuwaondoa Wahamiaji Haramu, mpaka sasa operesheni hiyo haijafanyika ni lini operesheni hiyo itafanyika?

Swali la pili, wakati Waziri ameondoka Ngara Uongozi wa Wilaya ya Ngara ulimua kuwanyang'anya Wahamiaji halali siyo Wahamiaji Haramu, halali vibali vya kuishi nchini na vikapelekwa Wizarani, watu hawa wantaabika sana ni lini vibali hivyo vitarudishwa kwa wananchi hawa ahsante sana?

29 MEI, 2013

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi na ninaomba iwe kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kuhusu ahadi ya operesheni ambayo Mheshimiwa Nahodha aliitoa kwa niaba ya Serikali ni kwamba maandalizi ya operesheni hii yako katika hatua za juu na tunatafuta rasilimali ambayo *infact* ni shilingi 650 kwa ajili ya Ngara Mkoa wa Kagera. Lakini tulikusudia kufanya operesheni katika Mikoa yote ambayo iko pembezoni kwa sababu ukifanya mmoja wanaweza kuhamia Kigoma, wanahamia Mara. Kwa hiyo, tunatafuta rasilimali ambayo ni bilioni 1 na milioni 900 ikipatikana basi operesheni hii itafanyika mara moja.

Kuhusu vibali hili ndiyo kwanza nimepata habari yake na ninamwahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa ninalichukua na tutawasiliana nimwambie ni lini vitapatikana. (*Makofi*)

Na. 304

### **Mkataba wa Kulinda Wazee Wasiojiweza**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED** alijibu:-

Mwaka 1984 Tanzania iliridhia Mkataba wa Kimataifa wa Afrika (Banjul) Unaohusu Haki za Binadamu wenye kipengele kinachosema kuwa wazee wasiojiweza watakuwa na haki ya kuchukuliwa hatua maalum za kuwalinda kulingana na mahitaji yao ya kimwili na kimaadili.

(a) Je, ni kwa kiasi gani nchi yetu imeweza kutekeleza kipengele hicho?

(b) Je, ni wazee wangapi na maeneo gani Tanzania ambao wamenufaika na Mkataba huo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mkataba, Serikali iliweka mikakati ya kuwalinda wazee wasiojiweza kama kundi maalum kwa kufanya yafuatayo:-

- Kutunga Sera za Taifa ya Wazee (2003), ambayo inatoa Mwongozo katika kuwahudumia wazee katika maisha yao ya kila siku.

- Kuwezesha uanzishwaji mtandao wa wazee Tanzania (*Top Tanzania Older People Platform*) wenye vyama 18 ambavyo ni majukwaa ya kutetea na kudai haki za wazee. Mfano Chama cha Wazee – Morogoro (*MOROPEO*), Chama cha Wazee Mara (*CHAWAMA*), Chama Cha Wazee Wastaafu Mtwara (*CHAWAM*) na kadhalika.

- Kuendesha na kutoa huduma za matunzo kwa wazee wasiojiweza katika makazi 17 yanayomilikiwa na Serikali na kuratibu huduma hizo katika makazi 24 yanayoendeshwa na Mashirika ya dini, pamoja na kutoa mafunzo ya ujasiliamali katika jamii,

- Kutoa msamaha wa matibabu kwa wazee nchini na kuanzishwa kwa dirisha maalum la huduma ya matibabu kwa wazee katika hospitali zinazomilikiwa na Serikali.

- Kuhamasisha jamii ili kutambue haki na ustawi wa wazee kwa kutumia maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na Kimataifa, ikiwamo siku ya wazee duniani.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wamenufaika kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na na uwepo wa madirisha maalum, katika vituo vya Serikali vya kutolea huduma za afya nchini kote. Aidha, Halmashauri

zimehamasika na zimeanza kuingiza masula ya wazee katika mpango huo. Wazee wapatao 1500 wanatunzwa na Serikali katika makazi ya wazee wasiojiweza, yaliyopo katika Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Kigoma, Mara, Manyara na Kilimanjaro. (*Makofi*)

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Naibu Waziri ambayo hayana hata chembe ya utafiti, ninaomba niulize masuala mawili ya nyongeza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaomba *Order please.*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee katika nchi hii sasa hivi wako takribani 800,000 na ushee, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Bado wazee wanapata taabu katika kupata msamaha wa matibabu. Mheshimiwa Waziri ninaomba uniambie katika wazee hawa 800,000, ambao wako katika hesabu ya sensa ya mwaka huu ni wazee wangapi hadi sasa wanapata huduma hii?

La pili, ninaomba nifahamu vigezo ambavyo Waziri au Serikali inatumia kuweka nyumba hizi za wazee katika sensa ya mwaka 2002 Mkoa wa Pwani ndiyo ambao unaongoza kuwa na wazee wengi zaidi, wale kuanzia miaka 75 kuendelea mbele wako takribani 25,000 hadi sasa Mkoa huu haujapatiwa nyumba kwa ajili ya wazee hawa.

Je, ni vigezo gani Serikali inatumia ili kuweka nyumba za kuhudumia wazee wasiojiweza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza majibu haya tuliyoyatoa yamefanyiwa tafiti na yamepitiwa ili kuweza kutoa majibu sahihi. Lakini tunafahamu kwa wastani katika jamii tunayoishi 4% ndiyo kundi la wazee na wastani huu wa 4% uko katika matabaka mbalimbali kutegemea na eneo ambalo watu wapo. Lakini tunapoulizwa swali kwamba sasa wamepata watu wangapi msamaha kwenye matibabu, siyo wazee wote 4% wanaenda kutibiwa na wanapokuwa wanaenda wana tofautiana kutegemea na hali zao kutegemea na magonjwa ambayo wazee hao wanaugua na hivyohivyo inatofautiana na kituo ambacho huyo mzee ameenda kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo sitaweza kukuambia ni wazee 20 au wazee 100,000 walioenda kutibiwa kwenye hospitali hizo kutokana na hali zao za magonjwa hayo ya uzee au katika tafsiri za kuanza kupata msamaha. Nilikuwa ninapendekeza pia kwamba jukumu la kulinda wazee siyo jukumu la serikali peke yake ni jukumu letu sisi wenyewe kama watoto kutunza wazazi wetu.

Lakini pia ni jukumu la sisi wenyewe kujitayarisha kwa sababu sisi kesho ni wazee watarajiwa ni vyema ujitayarishe kwamba utafikia katika umri wa wewe kuwa mzee na ukaweza kutayarisha mazingira yako mazuri badala ya kusema kuwa sasa Serikali iandae nyumba, iandae kila kitu kwa ajili ya mzee sisi tunajua kuwa kesho kutwa tutakuwa wazee ni lazima tujitayarishe kufika kule ili angalau katika umri wetu wa uzee tuutumie vizuri na tuwe katika maisha mazuri.

Inapokuwa ni lazima ndiyo Serikali itaweza kuweza matunzo haya ya wazee, majengo maalum, vituo hivyo na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuhakikisha wazee wanapata huduma nzuri zinazostahili. Suala la Mkoa wa Pwani kuwa ni kwa nini hakuna makazi ya wazee.

Makazi haya ya wazee yalianzishwa katika kihistoria kutokana na sababu mbalimbali zilizokuwa zimetolewa huko nyuma na hatujasema kwamba kila Mkoa lazima uwe na

29 MEI, 2013

Makazi ya wazee lakini ni juhudi za Serikali kushirikiana na Halmashauri, kushirikiana na wanachi kuweza kuona kuwa katika maeneo yote ambayo kuna makambi hayo kuna nia ya kuanzisha makambi basi makambi haya yanaweza kuanzishwa katika fursa hiyo. Lakini kitu kikubwa niseme ni jukumu letu sisi kutunza wazazi wetu na ni jukumu letu sisi kujitayarisha kwa umri wa uzee. *(Makofi)*

Na. 305

### **Tiba ya Walioumwa na Mbwa**

**MHE. SAID A. ARFI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa bure tiba kwa watu wanaoumwa na Mbwa ambao wengi wao ni watoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imekuwa ikinunua na kusambaza chanjo kwa ajili ya watu walioumwa mbwa bila malipo kwa miaka mingi.

Kutokana na ufinyu wa Bajeti , kuanzia mwaka 2012/2013, Wizara ililazimika kusitisha ununuzi wa chanjo hiyo ili kuzijulisha Halmashauri zote nchini kujitegemea kwa kutenga bajeti ya kununua chanjo hiyo, kupitia ' *basket fund* ' au vyanzo vingine vya mapato vya Halmashauri.



Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa chanjo hii ni bure kwa Wilaya 24 za Mikoa ya Dar es salaam, Lindi, Pwani, Morogoro na Kisiwa cha Pemba. Wilaya hizi ziko kwenye mradi wa majaribio ya kutokomeza kichaa cha mbwa kwa kipindi cha miaka mitano 2009- 2014. (*Rabies Elimination Project*). Mradi unaosimamiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi nchini chini ya ufadhili wa Mfuko wa *Bill and Melinda Gates* kupitia Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*). Lengo la mradi ni kuibua mikakati itakayotumika kutengeneza mpango wa kitaifa wa kutokomeza kichaa cha mbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hupokea chanjo toka Shirika la Afya Ulimwenguni (*WHO*) na kuzigawa kwenye Wilaya husika kupitia Bohari Kuu ya Dawa.

Kuanzia mwaka 2009-2012, Serikali ilipokea chanjo ya *'rabies* vichupa (vials) 24,133 kwa ajili ya mradi, ambayo hutolewa bila malipo katika vituo vilivyopangwa kutoa huduma hiyo. Muda wa mradi utakapokwisha Wilaya zilizo kwenye mradi zitajitegemea kujinunulia chanjo kama ilivyo sasa kwa Wilaya ambazo haziko kwenye miradi.

Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza Sera ya Afya ya kutoa huduma za Tiba na Kinga kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano bila malipo. Chanjo zinazonunuliwa na Halmashauri hutolewa bila malipo kwa wanaoumwa na mbwa. (*Makofi*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nina maswali mawili ya nyongeza pamoja na kwamba swali langu lilikuwa ni mstari mmoja na Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo marefu, Mheshimiwa Waziri wewe ukiwa kama Daktari unajua kabisa kuwa mtu yoyote ambaye ameumwa na Mbwa mwenye kichaa kama hatapata tiba sahihi na katika wakati muafaka mwisho wake ni kifo.

Matukio haya ya kuumwa na mbwa siyo mengi sana kama jinsi yalivyo magonjwa mengine kama malaria na magonjwa mengine.

Ni kweli Serikali ya CCM inashindwa kutoa huduma hii bure kwa Watanzania na kukubali kufa kwa sababu gharama za chanjo hii au Tiba hii ni zaidi ya shilingi 60,000 kwa mtu wa kijijini hawezi kumudu mnakubali kufa Watanzania kwasababu ya kushindwa kutoa tiba hii bure suala langu lilikuwa ni tiba.

Suala la pili, kwa sababu kiini cha swali langu ni uhai na maisha ya watu niwapongeze sana Hospitali ya *CCBRT, VIDACOM FOUNDATION* kwa namna ya kipekee wanavyoshughulikia tatizo la Fistula,

Je, Serikali sasa ipo tayari kushirikiana na Hospitali ya *Ocean Road*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu la kwanz hilo la Fistula halifiki hapa.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninahajribu kutengeneza swali langu lakini umenikatisha na kusema kuwa Fistula haihusiki lakini ninataka.

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Arfi wewe endelea.

**MHE. SAID A. ARFI:** Nilichokuwa ninataka kumalizia ni kwamba. Je, sasa Serikali itakuwa tayari kushirikiana na Hospitali ya *Ocean Road* na Taasisi nyingine kama walivyofanya kuwasaidia wagonjwa hawa wa *Fistula* kuwasaidi Albino ambao wana matatizo ya Kansa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana hatun muda tena.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali haijashindwa kutoa dawa za chanjo pamoja na tiba ya watu wanaoumwa ugonjwa wa kichaa cha mbwa bila malipo. Maagizo ya Serikali ni kwamba chanjo hizi zinatakiwa zinunuliwe na Halmashauri na wenyewe wanazipata kutoka Bohari yetu ya Dawa, lakini zinatakiwa zitolewe bure. Tumeagiza kila Halmashauri kutenga fedha katika bajeti zao kwa kutumia *Basket Fund* pamoja na mapato yao mengine kununua hizo dawa moja kwa moja *MSD* na hizo dawa zipo na wanapozipata wazitoe bure. Kama ikiwa zinauzwa tunaomba na tutaandaa utaratibu ili angalau tuwe tuna taarifa na hao watu ambao wanauza hizo chanjo wachukuliwe hatua stahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la pili kusema kweli amezungumzia mambo mengi ambayo nashindwa kuyapata vizuri kwa sababu amezungumzia Fistula lakini ameunganisha *CCBRT* na baadaye kasema tushirikiane na taasisi ya *Ocean Road*. Taasisi ya *Ocean Road* ni sehemu ya Serikali, ni kituo cha Serikali kwa hiyo ni sehemu yetu, kinatekeleza kazi ambazo Serikali inafanya. Vilevile nimtoe wasiwasi, tunashirikiana kwa karibu sana na *CCBRT* ambayo alikuwa anasema kwamba inatoa matibabu haya na huduma za wagonjwa wenye matatizo ya Fistula, hata juzi nilikuwa kwenye hizo shughuli zao na kuwapongeza katika kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa huduma kwa akina mama wanaopata matatizo ya Fistula.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha, sasa natangaza wageni.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo jukwaa la Spika ni Katibu Mkuu Wizara ya Kazi na Ajira ambaye ameambatana na Wenyeviti wa Bodi na Watendaji 30 kutoka Wizara na Taasisi ambazo zipo chini yake. (*Makofi*)

Wapo Maafisa kutoka Ubalози wa Uholanzi, Norway na Sweden ambao ni *Diplomat* kutoka Ubalози wa Uholanzi Madam Agnes Hant, Ubalози wa Norway, Madam Elizabeth

29 MEI, 2013

Swate, Ubalozi wa Sweden Margareta Brisman. *Welcome to the Parliament and this Parliament cherishes your relation with our Government. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, wapo wanafunzi wa vyuo mbalimbali kutokana na muda sitoweza kuwataja, wageni wa Waheshimiwa Wabunge wote ambao mnajijua mmekuja na ninyi karibuni sana. *(Makofi/Kicheko)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia Mwongozo!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia Kanuni ya 68 (7) kuhusu Mwongozo wa Spika. Kanuni inasema hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambako hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo ninaoomba ni kwamba katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea wa bajeti, jana Waziri wa Ardhi alipokuwa anaulizwa swali kuhusu bajeti ya kuendeleza Mji wa Kigamboni wa shilingi bilioni 50, alisema fedha zile hazihusiki na kulipa fidia, wana *extra budgetry* au aliita *ex-budget* nyingine tofauti na inayopitishwa na Bunge hili. Hali kadhalika, Wizara ya Nishati na Madini wanatumia zaidi ya shilingi trilion 1.5, kila siku shilingi bilioni 5.45 kwa ajili ya *TANESCO* na haipo kwenye vitabu vya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kama bajeti zipo mbili, bajeti inayopitishwa na Bunge lako

29 MEI, 2013

Tukufu kwa ajili ya matumizi ya Serikali na Serikali wana bajeti yao nyingine tofauti na inayopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbatia, swali lako na hoja yako ni *very valid*, lakini suala hili halijatokea mapema leo. Kwa vile ni *valid* na halikutokea mapema leo, tutaipokea na tutakujibu baadaye, Katibu! (*Makofi/Kicheko*)

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 - Waziri wa Kazi na Ajira**

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15) kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*) kwa mwaka 2012/2013. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Tume kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Nane wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu na jamaa za Mbunge Mwenzetu aliyefariki katika kipindi hiki cha mwaka mmoja ambaye ni marehemu Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani aliyekuwa Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kutuongoza na kutoa maelekezo katika utekelezaji wa kazi katika sekta ya Kazi na Ajira hasa katika kusaidia hatua zitakazowezesha kutatua tatizo la ajira hususan kwa vijana. Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia na kuimarisha utawala bora, demokrasia na mapambano dhidi ya rushwa kwa mafanikio makubwa. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza nchini kwetu na hivyo wadau wa maendeleo kuona haja ya kuendelea kutuunga mkono. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalilia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru kwa namna ya pekee kabisa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kwangu na heshima kubwa aliyoionesha ya kuendelea kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu sana kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa William Lukuvi, Mbunge wa Isimani kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vema mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2013/2014. Malengo, maelezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Mchinga Lindi, iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya

Matumizi ya Wizara yangu tarehe 4 na 5 Aprili, 2013. Wizara yangu imezingatia ushauri walioutoa na ambao umesaidia sana kuiboresha bajeti hii ninayoiwasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya awali, naomba sasa kuelezea mapitio ya utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015, utekelezaji wa Mpango na Kazi kwa mwaka 2012/2013, Mpango wa Kazi wa mwaka 2013/2014 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kazi kwa mwaka 2012/2013. Wizara yangu ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo kuhusu viwango vya kazi, usawa na kazi za staha, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji sehemu za kazi, masuala ya tija na hifadhi ya jamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati tuliyojipangia ili kufikia malengo hayo kwa ufanisi ni pamoja na kuboresha na kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kukuza Ajira kwa kuimarisha taarifa za soko la ajira, kutoa elimu ya ujasiriamali na kuhamasisha watu kuweza kujiajiri ili kupunguza umaskini wa kipato na ukosefu wa ajira, kusimamia urekebeshaji na utekelezaji wa Sheria za Kazi ili kuleta amani na tija sehemu za kazi, kuwa karibu na wafanyakazi na kutatua matatizo yao kwa wakati, kusuluhisha na kuamua migogoro ya kikazi, kufanya kaguzi za kazi, ajira na usalama na afya mahali pa kazi na kusimamia masuala ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango kazi wa Wizara ya Kazi na Ajira na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka 2012/2013, umezingatia Sera, Mpango na Mikakati ya Kitaifa ikiwa ni pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II). Katika kipindi hiki tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi na ukaguzi wa viwango vya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sheria za Kazi, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu za kazi, kuboresha hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Wizara (Fungu 65) iliidhinishwa bajeti ya jumla ya shilingi 15,945,298,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 13,109,498,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,835,800,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2013, Wizara ilikuwa imetumia jumla ya shilingi 9,552,307,487.75 ambazo ni sawa na asilimia 72.87 ya shilingi 13,109,498,000 zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida. Aidha, Wizara katika kipindi hiki haikupokea fedha zozote kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi. Kufanya ukaguzi sehemu za kazi. Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Utekelezaji umefanyika kwa kukagua sehemu za kazi, kutoa elimu ya Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri na kuchukua hatua za kisheria kwa wasiozingatia Sheria za Kazi. Aidha, Wizara imeendelea kuwa karibu na Wafanyakazi na kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Wizara imeendelea kuhimiza mahusiano mema baina ya Waajiri na Wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Wizara imefanya jumla ya ukaguzi 3,094 katika sehemu mbalimbali



za kazi nchini kwa lengo la kuona namna Sheria za kazi zinavyozingatwa na kutekelezwa na waajiri na wafanyakazi, utekelezaji wa viwango vya kazi, haki za msingi za kazi pamoja na haki za kuanzisha na kujiunga na vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukaguzi uliofanyika waajiri kadhaa walibainika kukiuka sheria za kazi ikiwemo kutowapatia wafanyakazi wao mikataba ya ajira, kulipa mishahara chini ya kima kilichowekwa kisheria; wafanyakazi kufanya kazi kwa saa nyingi bila malipo ya ziada na kutowapa likizo ikiwemo likizo ya uzazi. Waajiri hawa walichukuliwa hatua za kisheria kwa Wizara kutoa Amri Tekelezi (*Compliance Order*) kwa waajiri 118, kuwafungulia mashtaka mahakamani waajiri 33. Aidha, Wizara pia imehakiki mikataba ya ajira ipatayo 56,000 kati ya hiyo mikataba 19,247 ni madereva wa malori yanayosafirisha bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mpango wa Utatu kwa ajili ya mchakato wa kuridhia Mkataba Na. 189 kuhusu Kazi za Staha kwa wafanyakazi wa Majumbani (*Tripartite Action Plan for Promotion of the Decent Work for Domestic Workers Convention No. 189*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutoa elimu ya Sheria za Kazi katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa wafanyakazi 3,474 na Waajiri 385 wa sekta za Viwanda, Kilimo, Usafirishaji, Madini, Ujenzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa vyombo vya ushirikishaji wafanyakazi na waajiri. Kwa kuzingatia dhana ya utatu, Wizara imeratibu na kusimamia vikao 2 vya Baraza la Ushauri wa masuala ya Kazi, Uchumi na Jamii (*LESCO*) ambavyo vilijadili na kushauri kuhusu marekebisho ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 na Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 za mwaka 2004 na rasimu ya marekebisho hayo itawasilishwa Bungeni mwaka ujao wa fedha. Aidha, Wizara

iliratibu vikao viwili vya majadiliano baina ya Serikali na viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi nchini. Vikao hivyo viliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi. Wizara imekamilisha utafiti na majadiliano ya kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi 12. Sekta hizo ni Ujenzi, Shule Binafsi, Nishati, Viwanda na Biashara, Hoteli na Huduma za Majumbani, Ulinzi Binafsi, Madini, Afya, Uvuvi na Huduma za Majini, Usafirishaji, Mawasiliano na Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu, wafanyakazi na waajiri wote nchini kuwa kima cha chini cha mshahara katika sekta zote 12 kimeongezwa kwa asilimia zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda na Biashara imeongezwa kwa asilimia 25, kitabu kinaonesha ni asilimia 43.8 lakini ni asilimia 25, Hoteli na Huduma za Majumbani 55.2%, Ulinzi Binafsi 46.4%, Madini 25.2%, Afya 65.0%, Uvuvi na Huduma za Majini 21.2%, Usafirishaji 49.0% na Kilimo 42.9%. Aidha, sekta nne mpya zilizoanzishwa ambazo ni Ujenzi, Shule Binafsi, Nishati na Mawasiliano nazo vima vyake vimeongezwa. Viwango hivyo vipya vya kima cha chini cha mshahara vitaanza kutumika mwezi Julai 2013 na viwango halisi kwa maana ya pesa ni kiasi gani, vitatangazwa rasmi katika gazeti la Serikali hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumerekebisha na kuboresha utaratibu wa viwango vya mishahara katika sekta ya hoteli, ujenzi, madini, ulinzi binafsi na usafirishaji ambapo kama ilivyokuwa mwanzoni, badala ya kuwa na kiwango kimoja cha mshahara katika sekta hizo, tumeweka kiwango kulingana na madaraja au makundi mbalimbali, ili wafanyakazi walipwe kulingana na uwezo uliopo. Kwa mfano, wafanyakazi katika hoteli za nyota nne na tano na hoteli za kitalii watalipwa kulingana na hadhi ya maeneo haya ikilinganishwa na wale waliopo katika migahawa, baa

na nyumba za kulala wageni. Aidha, katika sekta ya ujenzi, tumezingatia madaraja ya Wakandarasi. Mfano, daraja na sita na daraja la saba na wale waliopo katika madaraja 1 - 3 na daraja la 4 - 5. Vilevile katika ulinzi binafsi kwa makampuni makubwa na kwa makampuni madogo viwango hivi vinatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza hizo za mishahara zimezingatia tija na hali ya uzalishaji na utoaji wa huduma nchini; uwezo wa waajiri na wazalishaji katika kila sekta; mfumuko wa bei na kulinda ajira nchini ili wafanyakazi wasipunguzwe kazi au uwekezaji kuhamishiwa nchi nyingine zenye gharama nafuu ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa wafanyakazi. Wizara inaendelea na mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata maradhi wakiwa kazini. Hatua za kuwapata Watendaji Wakuu wa mfuko zinaendelea na mfuko huu unatarajiwa kuanza kazi katika mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Jamii. Katika kuhakikisha huduma za hifadhi ya jamii zinaendelea kuimarika, Wizara imeshirikiana na Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) katika kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo ya kuanzisha Mpango wa Pensheni kwa wazee nchini (*Universal Pension*). Mpango huo utanza kutekelezwa baada ya kukamilisha kwa taratibu na maandalizi ya utekelezaji wake kwa lengo la kuufanya kuwa bora na endelevu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Hifadhi ya Jamii nchini zimefanya utafiti na tathmini ya tatizo la malipo (FAO) ya kujitoa katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wafanyakazi wanaopoteza ajira kabla ya umri wa kustaafu. Mapendekezo ya namna ya kushughulikia suala hili yameandaliwa na yatajadiliwa na wadau kabla ya kuwasilisha Bungeni katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vita dhidi ya Ajira Mbaya kwa Mtoto. Wizara imeendelea kuratibu juhudi za kukomesha utumikishwaji na ajira mbaya ya mtoto kwa kutekeleza

Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Utumikishwaji wa Mtoto. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali pamoja na Serikali za Mitaa inatekeleza miradi mitatu (3) ya kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali linaloitwa *Winrock International* kwa kupitia mradi wa kuhamasisha juhudi endelevu za kukomesha utumikishwaji wa mtoto (*PROSPER*) unaotekelezwa katika Mkoa wa Tabora, Wilaya za Urambo na Sikonge, imeweza kuwaondoa katika utumikishwaji jumla ya watoto 1,594 kati yao wavulana 855 na wasichana 739. Aidha, watoto 2,194 walizuiwa kuingia kwenye utumikishwaji. Vilevile wazazi wapatao 12,000 wakiwemo wanaume 5,000 na wanawake 7,000 wanaoishi na watoto walio katika maeneo hatari ya kutumikishwa walipatiwa elimu kuhusu madhara ya kuwatumikisha watoto. Vijana 322 wakiwemo wavulana 147 na wasichana 175 walipatiwa elimu ya ufundi stadi. Halikadhalika, wanawake 510 walipatiwa elimu ya ujasiriamali na kupatiwa mikopo kati ya dola za kimarekani kati ya 50 hadi 100 kulingana na mahitaji ya kila mmoja. Mradi huu unafadhiliwa na nchi ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeshirikiana na *Plan International* kutekeleza mradi katika kata kumi za Wilaya ya Geita ambapo jumla ya watoto 4,000 wenye umri wa kati ya miaka 5-7 walizuiwa kuingia kwenye utumikishwaji, kati ya watoto hao, watoto 789 (wavulana 369 na wasichana 420) wamepatiwa vifaa vya shule na kuwezesha kujiunga na shule za msingi. Aidha, watoto 3,252 wenye umri wa chini ya miaka saba wamewezeshwa kujiunga na shule za awali. Pia Walimu 116 walipatiwa mafunzo ya namna ya kuwahudumia watoto wa shule za awali. Mradi huu unafadhiliwa na nchi za Jumuiya ya Ulaya (EU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, Wizara imeingia makubaliano na Shirika la "*International Rescue Committee (IRC)*" kutekeleza mradi wa kuzuia ajira mbaya kwa mtoto katika Wilaya za Korogwe, Tanga mjini na Muheza mkoani

Tanga pamoja na wilaya za Kasulu, Kigoma mjini na Uvinza mkoani Kigoma. Mradi huu unatarajia kuwaondoa watoto 8,000 wenye umri wa miaka 5-17 katika utumikishwaji wa mtoto. Aidha, mradi unakusudia kuwapatia elimu ya ufundi stadi vijana 4,200 wenye umri wa miaka 15-17 na kuwapatia vifaa mbalimbali ili kuwawezesha kujiajiri na kujitegemea na hivyo kujiepusha na janga la kutumikishwa katika kazi hatarishi. Halikadhalika mradi unatarajia kuziwezesha kaya 3,360 kwa kuzijengea uwezo wa kujiongezea kipato kwa kuwapatia elimu ya uzalishaji mali na ushirika kwa lengo la kupunguza umaskini katika ngazi ya kaya ambao unachochea kwa kiasi kikubwa watoto kujiingiza kwenye utumikishwaji. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi. Wizara imeendelea kusimamia na kufuatilia uzingatiaji wa usalama na afya mahali pa kazi, ambapo Rasimu ya Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi na Rasimu ya Sheria Mpya ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi zimeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa ajira nchini. Wizara imeratibu juhudi za kukuza ajira nchini na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 kwa kuhamasisha na kuwahusisha wadau mbalimbali katika utekelezaji wake. Katika kipindi hiki Wizara imetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa Programu ya Kitaifa ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) 2013/14 – 2015/2016. Utekelezaji wa programu hii unatarajia kutoa fursa za ajira zipatazo 600,000 kwa vijana. Mkakati wa utekelezaji wa program hii utahusisha kuwajengea uwezo na ujuzi katika stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali; kuwapatia mitaji, nyenzo na vifaa vya uzalishaji mali; kuhamasisha mazingira wezeshi kisera, kisheria na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara. Aidha, Wizara imeshirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine *SUA* na Benki ya *CRDB* kuandaa kuandaa program ya ajira kwa wahitimu wa elimu ya juu nchini

ambapo Serikali itathamini jumla ya miradi 200 ya kilimo na ufugaji katika mwaka wa fedha 2013/2014. Utekelezaji wa Programu hii utahusisha pia Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Taasisi za Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwezesha vijana kujijiri, Wizara imekwisha tambua vikundi vya vijana wajasiriamali 502 kutoka Mikoa 17 ya Tanzania Bara vinavyohitaji kuwezesha kwa kuwapatia mitaji na mafunzo ya ujasiriamali. Vikundi hivyo vina jumla ya wanachama 5,385 (wanawake 2,519 na wanaume 2,866). Kazi hii inaendelea katika mikoa mingine iliyosalia. Hatua itakayofuata itakuwa ni kuwawezesha kwa mitaji na mafunzo ili waweze kujijiri katika shughuli mbalimbali za biashara na uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeshirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika utekelezaji wa mradi wa "Kazi Nje Nje" unaotekelezwa na Shirika la Kazi Duniani; ambapo katika mwaka 2012/2013 jumla ya vijana 5,338 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali katika Mikoa 15. Mikoa hiyo ikiwa ni Mwanza, Singida, Pwani, Tanga, Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Tabora, Mara, Ruvuma, Mtwara, Iringa, Arusha, Mbeya na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ukusanyaji taarifa na takwimu za ajira. Wizara imeendelea kuimarisha utaratibu wa ukusanyaji wa taarifa za ajira nchini ambapo mwaka 2012/2013 jumla ya ajira 274,030 zimepatikana. Kati ya hizo, ajira 56,746 zilitolewa na Serikali, ajira 8,603 zimetangazwa na sekta binafsi kupitia vyombo mbalimbali vya habari na ajira 208,681 zimetokana na utekelezaji miradi ya maendeleo. Miradi hiyo ni: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) ajira 50,246, Shirika la kuhudumia viwanda vidogo vidogo (*SIDO*) ajira 2,436, miradi ya ujenzi wa barabara ajira 1,033, uwekezaji katika sekta za mawasiliano ajira 86,702, uwekezaji kupitia Kituo cha Taifa cha Uwekezaji (*TIC*) ajira 59,010, Uwekezaji kupitia *EPZA* 9,254. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha mfumo wa taarifa za soko la ajira kwa kushirikiana na wadau wengine kama vile *NBS*, *TAMISEMI* na *ILO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na takwimu sahihi kuhusu hali ya tatizo la ajira nchi, Wizara imefanya maandalizi ya Utafiti wa Hali ya Nguvu Kazi yaani *integrated labour force survey* nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Utafiti huu umepangwa kufanyika mwaka 2013/2014 iwapo pesa itapatikana. Zoezi hili ni muhimu sana katika kutoa picha ya hali halisi ya ajira na tatizo la ajira nchini. Matokeo ya zoezi hili yatawezesha kuwa na takwimu za karibuni zaidi kuhusu hali ya ajira nchini, badala ya takwimu za mwaka 2006 ambazo ndiyo zinatumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utambuzi wa fursa za ajira katika Mipango na Programu za Maendeleo Wizara imetoa miongozo kuhusu namna ya kuhuisha masuala ya ukuzaji ajira na kazi za staha katika sera, mipango na programu za maendeleo kwa Wizara 23, Sekretarieti za Mikoa 25 na Halmashauri za Wilaya zote katika Mikoa husika. Aidha, Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa mwongozo huo na kupata taarifa kama ilivyoelekezwa katika mwongozo wa bajeti ya Serikali ya 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa Wizara na Taasisi zote za umma kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kukusanya taarifa za ajira ili tuweze kutoa taarifa sahihi za ajira nchini kwani Serikali imetekeleza miradi mingi ya maendeleo ambayo inazalisha fursa nyingi za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeratibu na kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali wadogo 87 kati yao wanawake 66 na wanaume 21 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kwenye Maonesho ya 13 ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 2 hadi 9 mwezi Desemba, 2012 huko Bujumbura nchini Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa watu wenye ulemavu. Wizara imehamasisha wadau mbalimbali kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira inayosisitiza kukuza usawa wa fursa za ajira na kipato kwa makundi yote ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi wakiwemo watu wenye ulemavu. Elimu kuhusu utambuzi wa haki na fursa za ajira kwa

walemavu imetolewa kwa waajiri 252 na vyama vitano vya walemavu nchini na hivyo, lengo la fursa za ajira na haki sawa kwa wote litazingatiwa na wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya ajira za wageni. Katika kipindi hiki, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi 6,424 ya vibali vya ajira za wageni vya daraja B. Kati ya hayo, maombi 5,918 (asilimia 92.1) yalipendekezwa kupewa vibali na 506 (asilimia 7.9) yalikataliwa. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi katika kampuni 148 kwa lengo la kuhakiki vibali vya ajira. \_Kampuni zilizoonekana kukiuka taratibu zilichukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kusitishwa vibali vyao vya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha na kuongeza ufanisi katika kutoa vibali vya ajira, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Vibali vya Ajira kwa Wageni. Muswada huu utawasilishwa Bungeni mwaka ujao wa fedha 2013/2014. Lengo la Muswada huu ni kuwa na Sheria moja ya kusimamia masuala ya vibali vya ajira za wageni, na hivyo kuondoa ulopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti; usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri. Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka 2012/2013 kazi zifuatazo zimetokeleza:-

(i) Vyama vitano vya Wafanyakazi vimesajiliwa. Chama cha Wafanyakazi wa Usafirishaji kwa njia ya Barabara Tanzania (TARWOTU), Chama cha Wafanyakazi Madaktari na Wafamasia Tanzania (TMDPWU), Chama cha Wafanyakazi wa Nyumbani, Huduma za Jamii, Hoteli na Utalii Tanzania (DOSHIWU), Chama cha Wafanyakazi wa Uchapishaji, Uchapaji na Vifungishaji Tanzania (PRIPPAWUTA) na Chama cha Wafanyakazi wa Tasnia ya Migodi na Nishati Tanzania (NUMET).

(ii) Maombi mapya matatu kutoka Shirikisho la



Vyama vya Walimu linalojulikana kama *Federation of East African Teachers Union (FEATU)*, Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari Tanzania *Tanzania Media Workers Union (TAMU)* na *Tanzania Locomotive Drivers Union" (TALODU)* yalipokelewa na kushughulikiwa. Kati ya hayo maombi mawili yalikubaliwa na moja lilikataliwa.

(iii) Kufanya mkutano wa viongozi wa kitaifa wa vyama vilivyosajiliwa kujadili masuala mbalimbali ya kiutendaji na kuibua changamoto zinazowakabili ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa sheria za kazi na waajiri kutumia mbinu mbalimbali za kuwafanya wafanyakazi wasione haja ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi.

(iv) Kufanya ukaguzi wa kumbukumbu za vyama pamoja na kuhakiki matumizi ya fedha na hesabu za mwaka ambapo jumla ya ukaguzi 10 zilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga uwezo wa Wizara. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imechukua hatua mbalimbali za kujenga uwezo wake ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuwapatia watumishi 12 mafunzo ya muda na muda mrefu ndani na nchi. Kutoa mafunzo ya maadili kwa watumishi 41, mafunzo ya utunzaji siri za Serikali kwa watumishi 30, mafunzo kuhusu UKIMWI kwa watumishi 103 yalitolewa na watumishi 32 waliwezesha kufanya mtihani wa sheria za kazi.

(ii) Watumishi 40 walipandishwa vyeo, 22 waliajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni, watumishi wanne walithibitishwa kazini na watumishi wawili walibadilishwa vyeo.

(iii) Kuwahudumia watumishi wa Wizara wanaoishi na virusi ya UKIMWI.

(iv) Mazingira ya kazi yaliboreshwa kwa kununua

vifaa mbalimbali vya ofisi katika ofisi za makao makuu ya Wizara na Mikoani.

(v) Watumishi 303 waliopo Makao Makuu na Mikoani waliwezesha kujaza malengo ya kazi kwenye fomu za *OPRAS* kwa mwaka 2012/2013 na walifanyiwa tathmini ya utendaji kazi kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za umma chini ya Wizara. Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi sita za umma zilizochini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TAESA*), Shirika la Tija la Taifa (*N/P*), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*), Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*). Utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2012/2013 kupitia taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*). Wakala umefanya kaguzi 6,907 za kawaida na asilimia 58 na kaguzi maalum 5,940 sawa na asilimia 58 na kaguzi maalum 5,940 sawa na asilimia 59 ya kaguzi zilizopangwa. Kaguzi hizi zilihusu umeme, *boiler*, mitungi ya hewa, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira. Aidha, wafanyakazi 26,531 sawa na asilimia 133 walipimwa afya zao. Pia, mafunzo ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi yalitolewa kwa wafanyakazi 808 kutoka sehemu mbalimbali za kazi. Jumla ya sehemu za kazi 1,179 sawa 51 za makampuni 74 yalipewa vyeti vya kukidhi vigezo vya Sheria Na. 5 ya Usalama na Afya mahala pa kazi. Aidha taratibu zinakamilishwa za kuridhia mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani *ILO* kuhusu Usalama na Afya Mahala pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa kuridhia mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi umefanyika. Mikataba hiyo ni Mkatoba Na.155 *Occupational Safety and Health Convention, 1981*, Mkatoba Na.187 (*Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006*) Mkatoba Na.167 (*Occupational Safety in Construction Convention, 1988*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya sehemu za kazi 1,179 kati ya 2,300 zilizopangwa zilisajiliwa sawa na asilimia 51 na makampuni 74 yalipewa vyeti vya kukidhi vigezo ya sheria namba 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo na kozi mbalimbali kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi yamefanyika kwa maafisa 808 wa afya na usalama mahali pa kazi. Kozi hizi zinajumuisha kozi ya Taifa ya Usalama na Afya, kozi ya utoaji wa huduma ya kwanza makazini (*industrial first aid*), usalama katika kufanya kazi za juu (*safety in working at height*) na kozi ya namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala katika kuongeza uelewa wa masuala ya afya na usalama mahali pa kazi kwa jamii umeendelea kujitangaza kupitia tovuti yake ya [www.osha.go.tz](http://www.osha.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Ajira (*TaESA*). Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TaESA*) imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuhudumia jumla ya wateja 1431 kati ya hao, watafutakazi ni 1295 na waajiri ni 136 katika sekta za usafirishaji na majumbani. Aidha, watafutakazi 590 waliunganishwa na waajiri wenye fursa za ajira na vile vile kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania nje ya nchi ambapo watafuta kazi 345 walipata ajira katika nchi za Oman, UAE, Denmark na Saudi Arabia. Wakala uliendelea kushirikiana kwa karibu na Ofisi zetu za Ubaloji wa Tanzania zilizopo nje ya nchi ili kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata kazi za staha na maslahi yao yanalindwa.

(ii) Maombi 26 ya wakala binafsi wa kutoa huduma za ajira hapa nchini yalipokelewa na kupata usajili wa kuwa wakala binafsi wa kutoa huduma za ajira hapa nchini. Maombi yote 26 yalifanikiwa kupata usajili wa kutoa huduma hiyo mara baada ya kukidhi vigezo vilivyopo.

(iii) Kutoa mafunzo elekezi kwa watafuta kazi 880 kuhusu namna ya kubaini vyanzo vya ajira na fursa zilizopo katika soko la ajira, jinsi ya kuandika wasifu binafsi, kuandika barua za maombi ya kazi na kuziainisha dondoo muhimu za usaili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) limetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Mapato ya kiasi cha shilingi milioni 678,708.5 sawa na asilimia 88.7 ya lengo yamekusanywa na kutumika katika kulipa mafao ya wanachama, kuwekeza katika vitega uchumi, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo.

(ii) Semina 542 zimeendeshwa kwa Waajiri na Wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii.

(iii) Mkutano Mkuu wa Tatu wa wadau umefanyika mwezi Februari 2013 ambao ulihudhuriwa na wadau wapato 745. Vilevile Shirika limeweza kupima afya (*preventive Health checks*) za wanachama wake wapatao 6,283.

(iv) Wanachama 78,670 ambao ni sawa na asilimia 68.11 ya lengo la wanachama 115,500 wameandikishwa. Aidha, Shirika limelipa mafao mbalimbali ya jumla ya shilingi bilioni 185.32 ambazo ni asilimia 183.03 ya lengo la shilingi bilioni 101.24 kwa wanachama 54,840.

(v) Mchakato wa utekelezaji wa mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 150 katika eneo la Mkuranga. Hivi sasa mradi upo katika hatua ya kupata Washauri Elekezi (*Consultant*) kwa ajili ya usanifu wa njia ya kusafirishia umeme (*transmission line*) kutoka Mkuranga hadi kwenye Gridi ya Taifa Kinyerezi- Dar es Salaam. Mradi huu, utatekelezwa kwa ushirikiano na *TANESCO*. Vilevile taratibu za kupata Mshauri Elekezi kwa ajili ya Kituo cha kufua umeme wa megawati 300 zitaanza mwaka wa fedha 2013/2014, baada ya

kufahamu mazingira ya mradi na njia ya usafirishaji umeme. Lengo ni kufanya miradi hii itekelezwe na kumalizika kwa wakati mmoja.

(vi) Ujenzi wa daraja la Kigamboni unaendelea vizuri. Aidha, daraja la muda la kusaidia ujenzi wa daraja la kudumu limekamilika na kazi ya ujenzi wa daraja la kudumu imeanza. Mbali na mafanikio hayo, kuna changamoto ya kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo ya upande wa Kurasini na Kigamboni ambayo yamo ndani ya eneo la barabara unganishi ambapo tathmini imefanyika. Mradi wa ujenzi wa daraja unategemewa kukamilika Januari, 2015.

(vii) Ujenzi wa ofisi na vitega uchumi umekamilika katika Mikoa ya Arusha, Kigoma pamoja na Wilaya ya Kahama. Aidha, ujenzi unaendelea katika Mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Kilimanjaro na Mwanza, Wilaya za Ilala na Temeke pamoja na ujenzi wa Kambi ya Jeshi eneo la Kihangaiko, Wami za Jeshi la Wananchi (*TPDF*) kwa kutumia mitambo ya *UBM*. Ujenzi wa ofisi za kumbukumbu za wanachama katika Mikoa ya Kilimanjaro na Mara umekamilika. Mradi wa ujenzi katika Mkoa wa Mbeya unasubiri Mshauri Elekezi kupatikana mwezi Juni, 2013.

(viii) Limekamilisha utayarishaji wa eneo la zahanati ya Apollo kwenye jingo la Mwalimu Julius Nyerere lililopo barabara ya Bibi Titi/Morogoro, Dar es Salaam. Ujenzi wa wa ofisi za Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*) unaendelea na ujenzi wa jengo la Mzizima jijini Dar es Salaam umeanza. Aidha, ujenzi wa hoteli ya kisasa Mwanza, ujenzi wa kijiji cha kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu "*Farm*" upo katika hatua za kupata makampuni ya ujenzi (*prequalification*))

(ix) Katika kutekeleza mpango wa kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam mpaka Chalinze, *NSSF* imeingia makubaliano na kampuni ya Malaysia kwa kuwasilisha maombi ya kazi (*Expressions of Interest*) ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*).

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2012/2013, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) liliendelea kutoa mafunzo mbalimbali, tafiti pamoja na ushauri ili kuinua tija sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Shirika liliendesha mafunzo 79 ya tija na kujenga uwezo sawa na asilimia 99 ya lengo lililopangwa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa washiriki 974 sawa na asilimia 81 ya lengo. Aidha, tafiti mbili zilifanyika sawa na asilimia 67 ya lengo na kutoa huduma za uelekezi katika kukuza tija kwa wateja 10 kutoka Taasisi za umma na binafsi sawa na asilimia 33 ya lengo. Vilevile Shirika limejitangaza kupita tovuti yake ya [www.niptz.org](http://www.niptz.org) na vyombo vingine vya habari na magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*). Katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukamillisha tathmini ya uwezo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*). Matokeo ya tathmini hii yamesaidia kuandaa na kuboresha mfumo na mafao wa taarifa za wanachama na hivyo kupunguza usumbufu na malalamiko ya wanachama.

(ii) Kufanya ukaguzi katika Mifuko sita ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa Mifuko hiyo inatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyopo.

(iii) Kutoa miongozo mitano ya uendeshaji katika sekta ya hifadhi ya jamii ambayo ni Mwongozo wa Taarifa (*Data Management Guidelines*), Mwongozo wa Kufanya Tathmini (*Actuarial Guidelines*), Mwongozo wa Uendeshaji wa Bodi za Wadhamini za Mifuko (*Conduct of Affairs of Board of Trustees Guidelines*), Mwongozo kuhusu ujumulishaji wa vipindi vya michango ya kwenye mifuko Hifadhi ya Jamii (*Totalization of Contribution Period Guidelines*), na Mwongozo wa Uanachama wa Mifuko (*Schemes Membership Guidelines*).

(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama magazeti, redio, televisheni, makongamano na semina. Aidha, Mamlaka imeandaa na kushiriki katika jumla ya semina 15 za kuelimisha makundi maalumu ya wadau kama vile Waheshimiwa Wabunge, Wahariri wa Vyombo vya habari, Wafanyakazi wa Migodini, Vyama vya Wafanyakazi na Vyama vya Waajiri na baadhi ya Mabaraza ya wafanyakazi wa Taasisi na Idara za serikali.

(v) Kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo ya kuanzisha Mfumo bora na endelevu wa Pensheni kwa wazee nchini (*Universal Pension*).

(vi) Kuandaa mapendekezo ya Mpango wa Marekebisho ya Sekta ya Hifadhi ya Jamii. Lengo la Mpango huu ni kutoa dira ya marekebisho ya sekta ya Hifadhi ya Jamii.

(vii) Kukamilisha taarifa ya tathmini ya hali ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini na kuandaa mapendekezo ya maboresho ya mafao yanayotolewa na mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hii ni pamoja na mapendekezo ya kushughulikia suala la nakisi ya Mfuko wa *PSPF*. Lengo ni kuwainisha mafao ya wanachama katika mifuko yote ya hifadhi ya jamii.

(viii) Kuandaa na kusaini Hati ya Maelewano (*Memorandum of Understanding*) baina *SSRA* na Mamlaka zingine za usimamizi katika sekta ya fedha yaani, Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*), Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*), Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Shughuli za Bima (*TIRA*), na Taasisi ya Fidha ya Wateja wa Benki (*DIB*). Lengo kuu likiwa ni ushirikiano katika kudhibiti na kuifanya sekta ya fedha kuwa imara na endelevu (*financial Stability*).

(ix) Kupokea na kutolea ufafanuzi hoja 87 kutoka kwa wadau mbalimbali (wafanyakazi, waajiri na mifuko ya pensheni) kuhusu tafsiri ya sheria na kanuni za Hifadhi ya Jamii, uhamaji wa wanachama baina ya mifuko, mafao na usajili wa wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*). Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*Commission for Mediation and Arbitration*), ni chombo chenye jukumu la kusuluhisha na kuamua migogoro ya kikazi. Upande ambao hautaridhika na maamuzi ya Tume unaweza kupeleka shauri hilo Mahakama ya Kazi. Vilevile Tume ina jukumu la kutoa elimu ya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2012/2013, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15), iliidhinishwa jumla ya shilingi 2,131,329,000/-. Kati ya fedha hizo Shilingi 1,131,329,000/- ni kwa ajili ya mishahara (*PE*) na Shilingi 1,000,000,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (*Other Charges*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2013, Tume imetumia jumla ya Shilingi 1,527,201,850/- sawa na asilimia 71.65 ya Shilingi 2,131,329,000/- zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu na kazi kwa mwaka 2012/2013. Katika mwaka 2012/2013, Tume iliendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Tume ilishughulikia jumla ya migogoro 5,722, migogoro mipya ni 3,354 na migogoro ya zamani 2,368 ambayo haikuisha katika mwaka 2011/2012. Jumla ya migogoro 3,727 sawa na asilimia 65.1 ilishughulikiwa na kuisha. Kati ya migogoro iliyoisha, migogoro 2,214 ambayo ni sawa na asilimia 59.4 iliisha kwa njia ya usuluhishi na migogoro 1,513 sawa na asilimia 40.6 iliisha kwa kutokukubaliana na hivyo kupelekwa katika hatua ya uamuzi. Migogoro 1,995 inaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali.

(ii) Tume imewezesha uundwaji wa mabaraza ya wafanyakazi 72 katika Halmashauri 20 za Wilaya, Miji na Majiji na Taasisi 52 za Serikali.



(iii) Taasisi 62 zilipewa mafunzo ya namna ya kuzuia na kutatua migogoro sehemu za kazi ambazo ni; Halmashauri tisa za Wilaya, Miji na Ofisi za Makatibu Tawala za Mikoa (RAS) , Taasisi 47 za Serikali na Sekta binafsi sita.

(iv) Tume imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Huduma Muhimu (*Essential Services Regulations, GN.323 of 2012*).

(v) Tume imeratibu uapishwaji wa wajumbe wa Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee*) ambayo kwa sasa imeanza kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

(vi) Tume kupitia vikao vya ushauri vya mikoa (*Regional Consultative Committee - RCC*) imetoa elimu ya uelewa kuhusu kazi za Tume na utatuzi wa migogoro katika Mikoa saba Tanzania Bara ambayo ni Mwanza, Dar es Salaam, Morogoro, Kigoma, Tanga, Rukwa na Njombe.

(vii) Imeandaa na kuchapa toleo la pili la Kitabu cha Rejea cha Maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Vol.2.*) yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi.

(viii) Imeandaa na kuchapa kitabu cha mwongozo wa namna ya kuzuia na kutatua migogoro ya kikazi (*Labour Dispute Prevention and Resolution Training Guide*).

(ix) Tume imewaendeleza watumishi 10 katika fani za sheria, uhasibu, ukatibu muhtasi na utunzaji wa kumbukumbu ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kazi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia sheria na viwango vya kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa

huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa kazi na huduma za ukaguzi:-

(i) Kufanya kaguzi za kazi 4,800 katika maeneo mbalimbali ya kazi nchi nzima hasa katika sekta ambazo zinaongoza kwa kuwa na migogoro mingi ya kikazi kama vile sekta ya viwanda na biashara, ulinzi binafsi, Hoteli na majumbani pamoja na sekta ya usafirishaji.

(ii) Kutoa elimu kuhusu sheria za kazi kwa waajiri wapatao 1,000 na wafanyakazi 5,000 katika sekta mbalimbali zikiwemo zinazoongoza kwa kuwa na migogoro mingi ya kikazi.

(iii) Kuratibu na kukuza majadiliano ya utatu kupitia Baraza la Ushauri katika Masuala ya Uchumi, Kazi na Jamii (*LESCO*) na vyombo vingine kama Bodi za Mishahara za Kisekta. Katika kipindi hiki tunatarajia kuweka jitihada zaidi katika kuhamasisha na kukuza majadiliano ya pamoja (*collective bargaining*) baina ya wafanyakazi na waajiri kama njia bora zaidi ya kutatua migogoro ya kikazi na kukuza tija mahali pa kazi.

(iv) Kuendeleza jitihada za kutokomeza utumikishwaji wa watoto kwa kushirikiana na Halmashauri na Serikali za Mitaa, mashirika yasiyo ya kiserikali na wabia wa maendeleo. Katika kipindi hiki tunakadiria kuwaondoa kwenye utumikishwaji watoto 11,000 na pia kuwazuia kuingia kwenye utumikishwaji watoto 3,500. Halikadhalika jumla ya kaya 3,360 zitajengewa uwezo wa kujiongezea kipato kwa kuwapatia elimu ya uzalishaji mali na ushirika kwa lengo la kupunguza umaskini katika ngazi ya kaya ambao unachochea kwa kiasi kikubwa watoto kujiingiza kwenye utumikishwaji.

(v) Kuratibu vikao viwili vya Kamati ya Kitaifa ya

kuratibu masuala ya kukomesha utumikishwaji wa watoto (*National Intersectoral Child Labour Committee*). Vikao hivi vinapangwa kujadili na kushauri kuhusu utekelezaji wa miradi na mikakati mbalimbali ya kutokomeza utumikishwaji wa watoto nchini, ikiwemo Mradi wa kuhamasisha juhudi endelevu za kutokomeza utumikishwaji wa watoto (*Promoting Sustainable Practices to Eradicate Child Labour in Tobacco*) utaotekelezwa katika mashamba ya tumbaku wilayani Urambo na Sikonge mkoani Tabora, Mradi wa *Plan International* unaotekelezwa katika kata kumi za wilaya ya Geita pamoja na Shirika la *International Rescue Committee (IRC)* linalotekeleza shughuli zake katika wilaya za Korogwe, Tanga mjini na Muheza mkoani Tanga pamoja na wilaya za Kasulu, Kigoma mjini na Uvinza mkoani Kigoma.

(vi) Kukamilisha na kutekeleza Mkakati wa maboresho katika sekta ya hifadhi ya jamii ikiwa ni pamoja na Mpango wa Pensheni kwa wazee.

(vii) Kukamilisha na kuwasilisha Bungeni mpango wa kushughulikia malipo (fao) ya kujitoa kwa wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi ya jamii kabla ya muda wa kustaafu.

(viii) Kuratibu uanzishwaji wa mfuko wa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata maradhi wakiwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji wa ajira nchini. Ili kukuza ajira na kazi za staha nchini, katika mwaka 2013/2014 Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Ajira kwa vijana nchini itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3) 2013/14 – 2015/16. Utekelezaji wa programu hii unatarajia kutoa fursa za ajira zaidi ya 600,000 kwa vijana na imelenga Kujenga Uwezo wa Vijana wa Ujuzi na Stadi Mbalimbali za kazi; Kuwapatia vijana Mitaji na Mikopo nafuu; Kuwapatia Vijana Maeneo ya Uzalishaji na Biashara; Kuhamasisha Mazingira wezeshi Kisera na Sheria. Utekelezaji wake utahusisha Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Taasisi za Elimu na Taasisi za fedha nchini.

Kama sehemu ya utekelezaji wa programu hiyo, Wizara itashirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Benki ya *CRDB* kuwawezesha vijana walio hitimu elimu ya juu kuwapatia elimu ya ujasiriamali na mikopo yenye masharti nafuu kwa udhamini wa Serikali. Jumla ya miradi 200 itanayotarajiwa kubuniwa na vijana wahitimu wa elimu ya juu itawezeshwa na kutoa zaidi ya ajira 6,000 za moja kwa moja kwa vijana wahitimu.

(ii) Kuratibu uhuishaji wa masuala ya ukuzaji ajira katika mipango na programu za maendeleo za kisekta kwa kutoa mafunzo kwa mikoa 4, na kufuatilia utekelezaji wa mwongozo wa namna ya kuhuisha ukuzaji ajira katika sera, mipango na programu za maendeleo katika Wizara 23, Sekretarieti za Mikoa 25 na Halmashauri za Wilaya zote katika Mikoa husika. Aidha, kupitia miradi ya maendeleo chini ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano, Serikali katika mwaka wa fedha 2013/14 inategemea kuwawezesha upatikanaji wa fursa za ajira zaidi ya 300,000. Ajira hizi ni mbali na ajira 61,915 za watumishi watakao ajiriwa Serikalini.

(iii) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa za soko la Ajira nchini kwa kukamilisha mfumo wa kielekroniki ambao utatumika kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri. Mfumo huu utasaidia vijana kupata taarifa zitakazowawezesha kufahamu vema fursa za ajira zilizopo nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira kutoka Idara za Serikali, Mamlaka za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa mwongozo wa bajeti wa 2013/2014. Pia Wizara itaendelea kuratibu upatikanaji wa takwimu za ajira zinazotokana na uwekezaji wa Serikali kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile kilimo, madini, uchukuzi, maji, ardhi, elimu, afya na utalii.

(iv) Kufanya Utafiti wa Hali ya Nguvukazi nchini ambao utatoa picha ya hali ya ajira nchini. Utafiti huu utatoa taarifa kuhusu ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi, utumikishwaji wa watoto, ongezeko la ajira kwa kipindi cha mwaka 2006 hadi 2013 na matumizi ya muda. Kupatikana

kwa taarifa hizo kutawezesha nchi kutathmini mafanikio ya malengo ya Milenia, MKUKUTA II na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Aidha, matokeo haya yatatumika kuboresha sera, kupanga na kufuatilia mipango ya kimaendeleo.

(v) Kuandaa Sera ya Taifa ya Uhamaji wa Nguvukazi nchini ili kuwezesha watazania kutumia fursa za ajira zilizopo nje ya nchi pamoja na kuvutia wataalamu wetu kurudi kuwekeza utaalam wao hapa nchini. Aidha, sera itaweka mazingira mazuri ya watu wetu walioko nje ya nchi kutuma fedha (*Remittances*) kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

(vi) Kukamilisha muswada wa sheria ya utoaji vibali vya ajira kwa wageni ili kuimarisha na kuongeza ufanisi katika kutoa vibali vya ajira. Muswada huu utawasilishwa Bungeni mwaka ujao wa fedha 2013/2014.

(vii) Kuratibu na kufuatilia ubora wa utoaji wa huduma za ajira zinazotolewa na wakala binafsi 60 ndani na nje ya nchi kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo.

(viii) Kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali 250 wa Tanzania katika Maonesho ya kumi na nne ya Nguvukazi/Juakali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(ix) Kushughulikia maombi ya vibali vya ajira za wageni na kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola, kuhakiki uhalali wa vibali vya ajira za wageni katika kampuni zilizoajiri wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri. Kuhusu usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri katika mwaka 2013/2014, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kushughulikia maombi ya usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri na Mashirikisho kadiri yatakavyowasilishwa kwa ajili ya kuimarisha ushirikishwaji sehemu za kazi.

(ii) Kufanya kaguzi za kumbukumbu za Wanachama, kuhakiki na kukagua matumizi ya fedha na hesabu za mwaka za vyama katika Mikoa 15.

(iii) Kushughulikia migogoro ya vyama inayojitokeza pamoja na kuwaelimisha Viongozi wa vyama juu ya Sheria za kazi na kanuni zake.

(iv) Kushughulikia kesi za Mahakamani zinazotokana na maamuzi ya Msajili na masuala yanayohusu katiba za vyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga uwezo wa Wizara katika mwaka 2013/2014, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuwajengea uwezo watumishi 65 kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na watumishi 5 kupatiwa mafunzo ya muda mrefu ili waweze kutoa huduma bora.

(ii) Kutoa mafunzo ya maadili, vita dhidi ya Rushwa na Utawala Bora sehemu ya kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI kwa watumishi 100.

(iii) Kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ofisi kama vile ulinzi, usafi na matengenezo ya vifaa vya ofisi katika kuboresha utendaji kazi.

(iv) Kuratibu ushirikishwaji wa kuimarisha mahusiano bora kwa watumishi wa wizara kwa kufanya mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi.

(v) Kufanya vikao vinne vya kamati ya ajira kwa ajili ya kuajiri, kupandisha vyeo na kuthibitisha watumishi kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za umma chini ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA):-

(i) Kufanya ukaguzi 20,000 za kawaida na kaguzi 25,000 maalum za usalama na afya mahali pa kazi na kupima afya za wafanyakazi 50,000 katika sehemu mbalimbali za kazi na vilevile kuendelea kuwachukulia hatua stahiki waajiri sugu watakaoshindwa kutekeleza sheria ya usalama na afya mahali pa kazi.

(ii) Kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya usalama na afya mahali pa kazi kwa wafanyakazi 1,500.

(iii) Kuanzisha mifumo mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi wa Wakala; mifumo hiyo ni mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi, mfumo wa kutunza kumbukumbu, mfumo wa usimamizi wa fedha na mfumo wa usimamizi wa vifaa.

(iv) Kuendelea kuelimisha wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati ili waweze kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendesha warsha, semina na makongamano mbalimbali katika mikoa ya Tanzania Bara.

(v) Kuwasilisha Bungeni mapendekezo ya kuridhia mikataba mitatu (3) ya kimataifa (*ILO Conventions*) inayohusiana na Usalama na afya mahali pa kazi. Mikataba hiyo ni; Mkataba Na.155 *Occupational Safety and Health Convention, 1981*, Mkataba Na.187, (*Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006*) na Mkataba Na.167 (*Occupational Safety in Construction Convention, 1988*).

(vi) Kukamilisha Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi kama zifuatazo: Kanuni ya kuhusu kemikali "*OSH (hazardous chemical substances) rules*", Kanuni ya kuhusu umeme *OSH (electric machinery safety) rules* na Kanuni ya ujenzi na majengo, "*OSH (building and construction)*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (*TaESA*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wakala wa Huduma za Ajira (*TaESA*) umepanga kufanya yafuatayo:-

(i) Kuwaunganisha watafuta kazi 1,500 na waajiri ndani na nje ya nchi na kufanya utafiti katika nyanja za upatikanaji wa fursa za ajira.

(ii) Kukusanya, kuchambua na kusambaza Taarifa za Soko la Ajira.

(iii) Kutoa mafunzo kwa watumishi 10 ili kuongeza tija na ufanisi.

(iv) Kusimamia na kuratibu shughuli za Wakala binafsi 60 zinazotoa huduma za ajira hapa nchini na kupokea na kushughulikia maombi mapya kadiri yatakavyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) katika mwaka 2013/2014 Shirika la Taifa la Hifadhi ya jamii litatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 1.2 na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, gharama za uendeshaji na miradi ya maendeleo.

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo wa hifadhi ya jamii.

(iii) Shirika litaendelea na mpango wa kupima Afya za wanachama wake (*Preventive Health Checks*).

(iv) Kufanya Mkutano Mkuu wa Nne wa wadau wa *NSSF*.

(v) Kufanya tathimini ya uwezo wa mfuko kifedha ili kulipa mafao kwa wanachama wake kwa muda mrefu ujao.



(vi) Kuanza utekelezaji wa mradi wa uzalishaji umeme wa megawati 300 katika eneo la Mkuranga na mradi wa uzalishaji umeme megawati 49 katika eneo la Malagarasi mkoa wa Kigoma.

(vii) Kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigamboni.

(viii) Kuendelea na ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mikoa ya Morogoro, Shinyanga, Mbeya, Kilimanjaro, Mara, Mwanza, Wilaya za Ilala, Temeke na Kinondoni.

(ix) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Apollo jijini Dar es Salaam, na kuendelea na ujenzi wa ofisi za RITA na ujenzi wa jengo la Mzizima jijini Dar es Salaam, hoteli ya kisasa Mwanza, ujenzi wa kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu "*Farm*"), ujenzi wa kijiji cha kisasa Kigamboni (Azimio) na Ujenzi wa Jengo la Maadili Dar es Salaam.

(x) Kuanza ujenzi wa kituo cha mabasi Mwandiga Kigoma, Kijiji cha Bunge Dodoma (*MP's Village*); ofisi za Bunge Dar-es-Salaam na nyumba za watumishi wa Serikali nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika la Tija la Taifa limepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuendesha mafunzo 80 ya uongozi kwa watumishi 1,200 kutoka taasisi za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali (*NGO's*).

(ii) Kutoa huduma za ushauri kwa wateja 30 katika sekta za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali (*NGO's*).

(iii) Kufanya tafiti nne katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi na

Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*). Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) itaendelea na hatua za kuboresha sekta ya Hifadhi ya jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali ambayo itajikita katika kuboresha sekta ya Hifadhi ya Jamii na kuifanya kuwa endelevu na yenye mchango katika maendeleo ya wanachama wa Mifuko na nchi kwa ujumla.

(ii) Kusajili Mifuko, Mameneja Uwekezaji (*Fund Managers*) na Watunza Mali (*Custodians*) kwa ajili ya kutenganisha majukumu kwenye uendeshaji wa Mifuko ili kuleta ufanisi zaidi.

(iii) Kuratibu mikakati ya kupanua wigo wa hifadhi ya jamii nchini ili makundi mbalimbali hasa ambayo yako kwenye sekta isiyo rasmi yaweze kufaidika na huduma zitolewazo na taasisi za hifadhi ya jamii.

(iv) Kutoa elimu kwa umma kuhusu sekta ya hifadhi ya jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile magazeti, redio, televisheni, makongamano, Wiki ya Hifadhi ya jamii na mtandao.

(v) Kufanya ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha kuwa Mifuko hiyo inatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria zilizopo.

(vi) Kukamilisha maandalizi ya utekelezaji wa mfumo bora na endelevu kwa ajili ya kutoa Pensheni kwa Wazee (*Universal Pension*) nchini.

(vii) Kutoa Mafunzo kwa bodi za wadhamini na watendaji wa mifuko ya Hifadhi ya Jamii juu ya kanuni na miongozo inayotolewa na Mamlaka ili kurahisisha utekelezaji wake.

(viii) Kuendelea kujenga uwezo wa Mamlaka ili kudhibiti na kusimamia kwa ufanisi sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2013/2014, Wizara ya Kazi na Ajira (Fungu 65) inatarajia kutumia kiasi cha Shilingi 13,034,148,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wake wa mwaka. Fedha hizi ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA). Naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014. Tume imeweka kipaumbele katika kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusuluhisha na kuamua migogoro 3,500 ya kikazi na kuandaa taarifa.

(ii) Kutafiti vyanzo vya migogoro na migomo ya wafanyakazi mahala pa kazi kwa nia ya kuitatua.

(iii) Kufanya tathmini ya hali ya ushirikishwaji wa wafanyakazi katika sehemu za kazi Tanzania Bara.

(iv) Kuendesha mafunzo 150 ya uelewa na ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya namna ya uandaaji wa mikataba ya kuunda mabaraza ya wafanyakazi na kuunda mabaraza 100 ya wafanyakazi sehemu za kazi.

(v) Kujenga uwezo wa Tume ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwaendeleza watumishi kitaaluma na kuboresha mazingira ya kazi na vilevile kujengea uwezo Kamati ya Kuduma Muhimu (*Essential Services Committee*).

(vi) Kuanzisha mfumo wa Electroniki kwa ajili ya uandaaji na utunzaji wa taarifa za Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa mwaka 2013/2014, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi inaomba jumla ya Shilingi 1,924,748,000/- kwa ajili ya matumizi ya kawaida (*OC na PE*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yote niliyoyaeleza yametokelezwa kwa ushirikiano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Viongozi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa. Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa Mheshimiwa Dokta Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Mbunge wa Segerea kwa ushirikiano na ushauri wake wa karibu. *(Makofi)*

Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu Bwana Eric F. Shitindi pia ninawashukuru sana Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Bodi zao kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia ya pekee, naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii – *(LESCO)*, Chama cha Waajiri Tanzania *(ATE)* na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)*, kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya Washirika wa Maendeleo ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na Washirika wa maendeleo mbalimbali ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yetu. Hivyo, napenda shukrani za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani *(ILO)*, *UNDP*, *UNICEF*, *UNFPA*, Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark *(DANIDA)*, *Plan International*, Serikali ya Marekani, Serikali ya Brazil, Umoja wa Ulaya *(EU)* na Benki ya Dunia *(WB)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru wewe binafsi, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. Natoa pia shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao ya mara kwa mara kuhusu Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kwa kuijadili bajeti hii tarehe 4 na 5 na mapendekezo yao ambayo yamesaidia sana kuweka hotuba hii na pia kwa ushirikiano wao wa karibu katika kufanya kazi ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa Mkoa wangu wa Mara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Aidha, kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa mchango mkubwa ninaoupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu na kazi kwa mwaka 2012/2013 na Mpango wa Kazi kwa mwaka 2013/2014, Wizara inawasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2013/2014 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 na Fungu 15 kama ifuatavyo:-

**(a) Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira**

Matumizi ya Kawaida Shilingi 13,034,148,000.00

**(b) Fungu 15: Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Matumizi ya Kawaida Shilingi 1,924,748,000.00

**Jumla Kuu 14,958,896,000.00**

29 MEI, 2013

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru tena wewe, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya [www.kazi.go.tz](http://www.kazi.go.tz). (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja iliitolewa iamuliwe)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, anaomba kuwatangazia wajumbe wa kamati hiyo kwamba leo saa nane mchana hadi saa kumi alasiri, Kamati hiyo itakutana na wawakilishi wa asasi za kiraia na kufanya mjadala juu ya fursa na changamoto za kuongeza mapato ya Serikali. Mjadala huo umeandaliwa na Asasi ya *Civil and Political Right Watch* kwa niaba ya AZAKI zinazoshiriki katika maonyesho yanayoendelea katika viwanja vya Bunge kuhusiana na shughuli za Asasi hizo.

Waheshimiwa Wabunge, mbali na wajumbe wa PAC pia Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati zote za Bunge wanaalikwa kuhudhuria na kushiriki katika mjadala huo. Ili kuokoa muda kutakuwa na huduma ya chakula kuanzia saa saba na nusu mchana katika *Canteen* ya Bunge. Tafadhalini mnaombwa kuzingatia muda.

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati.

**MWENYEKITI KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9), Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya

Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014; na kuliomba bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira Jijini Dar es Salaam tarehe 3 Machi, 2013. Katika vikao hivyo, Kamati ilipokea na kujadili kwa kina Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Kazi na Ajira. Napenda kulialifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2012/2013. Katika mwaka wa Fedha 2012/2013, Wizara ilipangiwa bajeti ya shilingi bilioni 18.8 kati fedha hizo shilingi bilioni 15.94 ni kwa ajili ya matumizi ya Fungu 65 ya Wizara na shilingi bilioni 2.13 ni kwa ajili ya Fungu 15 Tume ya Usuluhishi na Maamuzi. Hadi Kamati ilipokutana na Wizara mwezi Machi, fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 6,329,572,613/= ambazo ni sawa na asilimia 48.28. Aidha, Wizara katika kipindi hicho haikupokea fedha kwa matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali ikamilishe utoaji wa fedha hizi kwa kipindi kilichosalia ili Wizara iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa Mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa Bajeti na Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2013/2014. Makadirio ya Matumizi ya Kawaida. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara imetengewa jumla ya shilingi bilioni 17.79 kati ya feadha hizo shilingi bilioni 15.86 ni kwa ajili ya matumizi ya

Fungu 65 ya Wizara na shilingi bilioni 1.92 ni kwa ajili ya ya matumizi ya Fungu 15, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 2,835,800,000/= zote zikiwa ni fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013, pamoja na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadilio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2013/2014, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ndogo inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Kazi na Ajira. Ukichukua taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii utaona kwamba kwa zaidi ya miaka mitatu mfululizo Kamati imekuwa ikitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Kiasi kilichotengwa kwa mwaka 2013/2014 kimepungua kutoka shilingi bilioni 18.8 hadi shilingi bilioni 17.79, bado kiasi hiki hakitoshi kutekeleza majukumu ya Wizara katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria za Ajira zenye kuweka mazingira ya kuwawezesha Watanzania wanakuwa na viwango bora vya kazi, usawa na staha katika kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti hii ya Wizara inahusisha pia bajeti ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ni wazi kuwa kupungua kwa bajeti hii kutaathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo ambayo miongoni mwake ni kupokea na kusajili migogoro ya kikazi, kuisuluhisha na kuitolea uamuzi. Kwa mwaka huu wa fedha (CMA) imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.92 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na majukumu ya Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa nchi nchi



nyingi duniani, nchi yetu inaendelea kukabiliwa na tatizo la ukosefu wa ajira ambapo waathirika wakubwa ni vijana na wanawake, ukosefu wa ajira hapa nchini umefikia asilimia 12. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza fursa za ajira nchini ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta mbalimbali ili kuongeza ajira. Pia Kamati inasisitiza Serikali kupanua fulsa za Elimu katika ngazi zote na kuhimiza mafunzo ya ujasiriamali na ufundi. Aidha, Serikali iendeele kukuza na kuimarisha program za kuwawezesha vijana kujijiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Jamii nchini. Hifadhi ya jamii ni haki ya kila Mtanzania. Haki hii imeainishwa katiaka Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ibara 11 (1) na Sera ya Taifa ya Jamii ya mwaka 2003. Haki hii pia imeainishwa kwenye Mkataba wa kimataifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 1948 pamoja na Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Jamii ni utaratibu ambao jamii husika imejiwekea wa kuweka akiba kwa lengo la kuwakinga watumishi wa umma, au sekta binafsi walioajiriwa au kujijiri dhidi ya matukio yasiyotarajiwa. Matukio hayo ni kama maradhi, ulemavu, kupoteza kazi, kuacha kazi kwa sababu ya uzee kustaafu aidha kwa hiyari au kwa lazima na mengineyo ikiwemo huduma za matibabu na gharama za msiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mataifa yaliyoendelea Hifadhi ya Jamii imekuwa msaada mkubwa katika kuwalinda wananchi dhidi ya majanga kama vile ugonjwa, ulemavu na kukosa ajira na hivyo kujenga hali ya usawa wa kipato jambo linalopunguza kiwango cha umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali pia kuiga utaratibu huo wa mataifa yaliyoendelea wa kutumia hifadhi ya jamii katika kupambana na umasikini na kuwaondolea wananchi kero zinasababisha na ukosefu wa

kipato. Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa viwango vya pensheni vinavyolipwa vinawawezesha watu wa rika zote na Watanzania wote kuishi maisha yenye staha kwa kuwawezesha kupata mahitaji na huduma muhimu kama vile afya. Hata hivyo, kabla ya kuanza kutekeleza utaratibu huo, elimu ya kutosha inapaswa kutolewa kwa wananchi kwani ni kitu kigeni kwao ili waweze kujua wanapaswa kufanya nini ili kunufaika na mifuko hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuandaa Muswada ulioliwezesha Bunge kutunga Sheria Na. 8 ya mwaka 2008 ambayo inaanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii yaani *SSRA*. Sheria hiyo pamoja na Sheria zote za Hifadhi ya Jamii zilifanyiwa marekebisho katika mwaka wa fedha unaoishia sasa kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Sheria Na. 5 ya mwaka 2012 yaani *The Social Security Laws (Amendments) Act, No.5 Of 2012* ili kuondoa kukinzana na Sheria za Mifuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tangu kufanyika kwa marekebisho hayo ya sheria kumekuwa na migogoro baina ya Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii na baadhi ya Wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii hapa nchini ambao wanadai marekebisho hayo ya sheria yatawaumiza kutokana na kuondoa fao la kujitoka (*withdraw benefit*). Kutokana na hali hiyo Kamati ilibaini mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

(i) Baadhi ya sekta kama vile madini ambayo inahusisha matumizi ya dawa na mionzi watumishi wake hawana uhakika wa kufanya kazi mpaka miaka 55 au 60, hivyo kuondoa fao la kujitoka ni kuwanyima wafanyakazi haki zao. (*Makofi*)

(ii) Watumishi wa sekta binafsi hawana uhakika na ajira zao na Tanzania haina utaratibu wa kisheria wa malipo ya watu wasio na kazi (*unemployment benefit*). (*Makofi*)

(iii) Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa umri wa kuishi wa Mtanzania (*demographic health survey, 2002*) ni kati ya miaka 47 hadi 53 hivyo kutokuwepo kwa fao la kujitoa ni kuwanyima wafanyakazi haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya *SSRA*, eneo hili liliibua mjadala mkali kwa wadau pamoja na Kamati walihofia kwamba kuondolewa kwa fao la kujitoa *withdraw benefit* kunaweza kuleta tatizo. Ili kuepusha hali ambayo ingeweza kutokea, Kamati ilitoa ushauri kwa mujibu wa taratibu zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, baada ya kutokea kukinzana kwa matumizi ya Sheria hiyo na hali halisi ya mahitaji ya wafanyakazi, Kamati inaona upo umuhimu wa kupitiwa haraka na kufanyiwa marekebisho kwa Sheria hiyo kwa kuzingatia masuala yafuatayo:-

(i) Sheria itengeneze mfumo mzuri utakaowezesha kuwepo kwa fao hili, lakini bila kuathiri anguko la mifuko ili kukidhi hifadhi ya uzeeni.

(ii) Mwanachama aruhusiwe kutumia sehemu ya mafao yake ya uzeeni kulipia mkopo wa nyumba yaani *home mortgage*. (*Makofi*)

(iii) Mwanachama aruhusiwe kutumia sehemu ya mafao yake ya uzeeni kwa ajili ya kugharamia shughuli yoyote nyingine kwa lengo la kuandaa mazingira mazuri ya maisha baada ya kustaafu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuzingatia masuala hayo, Kamati inaiagiza Serikali kuhakikisha kuwa mara baada ya kupitiwa upya kwa sheria hiyo, kanuni na miongozo iandaliwe itakayosaidia kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii kwa kuifanya iwe endelevu huku ikichangia na kujali maendeleo ya wanachama na taifa kwa ujumla. Vilevile Serikali kupitia *SSRA* iandae mikakati ya kupanua wigo wa

hifadhi ya jamii nchini ili makundi mbalimbali hasa ambayo yako kwenye sekta isiyo rasmi yaweze kufaidika na huduma zinazotolewa na taasisi za hifadhi ya jamii na inatokana na ukweli kuwa mpaka sasa wigo wa hifadhi ya jamii ni asilimia 6.5 tu ya Watanzania ndiyo wanafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inakubaliana na hatua ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2008 kuruhusu waajiriwa wapya kuchagua Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao watapenda kujiunga nao tofauti na awali ambapo walilazimika kujiunga na mfuko ulio kwenye sekta wanayoifanyia kazi tu. Hatua hii itaondoa ukiritimba katika utendaji wa mifuko na hivyo kuifanya itekeleze majukumu yake kwa ushindani ili kuvutia wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaiagiza Serikali juu ya umuhimu wa kuandaa mazingira ya kuiweka mifuko yote chini ya Wizara moja ili iwe rahisi kuisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuandaa miongozo ya uwekezaji yenye lengo la kiwezesha mifuko ya hifadhi ya jamii kufanya uwekezaji ulio salama na wenye tija unaomnufaisha mwanachama na taifa kwa ujumla na vilevile Kamati inaitaka Serikali ione uwezekano wa kuhakikisha kuwa mafao ya wanachama wa mifuko yanabadilika kulingana na hali halisi ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni kwa wazee. Wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote ile duniani na kwa Tanzania wazee wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Takwimu zinaonesha kuwa wazee hapa nchini ambao wanakadiriwa kufikia milioni 2.1 idadi hii ni sawa na asilimia 4.5 ya Watanzania wote (*Population Projection 2010*). Asilimia 83 ya Wazee wote wanaoishi vijijini (*Demographic Health Survey 2010*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila kaya inakadiriwa kuwa na mzee mmoja ambae anahitaji msaada kutoka kwa wategemazi. Kiwango cha umaskini katika kila kaya zenye wazee na watoto ni kikubwa na kinakadiriwa kuwa ni asilimia 22.4 ukilinganisha na kiwango cha umasikini kitaifa ambacho ni asilimia 33.4 (*NHBS*). Hali hii pamoja na mambo mengine inasababisha wazee na familia zao kukabiliwa na changamoto ya gharama kubwa za kuwawezesha kupata huduma muhimu za maisha kama vile matibabu ya magonjwa mbalimbali yanayowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa kundi kubwa la wazee lipo katika hatari kubwa zaidi ya kukabiliwa na matatizo ya kiafya na ulemavu kuliko kundi jingine lolote. Mpaka sasa asilimia 33 ya wazee wote nchini ni walemavu (*NHBS 2002*). Pamoja na kukabiliwa na hali hii, inakadiliwa watoto yatima ni milioni moja wanaoshi katika mazingira magumu sana na wanatunzwa na wazee maskini ambao hawajiwezi na ni walemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa pensheni tulionao sasa hauhusishi wazee wote. Huduma zinazotolewa kwa kundi dogo la wazee chini ya asilimia tatu, waliokuwa katika sekta rasmi za ajira kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii. Kundi kubwa la wazee wameachwa bila huduma za hifadhi ya jamii. Aidha, pamoja na Serikali kuendesha program mbalimbali za wazee kwa kushirikiana na wadau mbalimbali mfano; Mpango wa Afya kwa wazee, Mpango wa makazi/ Nyumba za wazee pamoja na Mradi wa *TASAF* ambao unatoa pensheni kwa wazee umri wa miaka 65+ wanaoishi katika mazingira magumu katika maeneo machache sana. Mipango hii ni mizuri lakini bado ina upungufu katika wigo na kukidhi mahitaji ya wazee wengi. Hata hivyo, kuna mitazamo mingi tofauti ikiwapo mtazamo kuona wazee ambao hawakuchangia kuweka akiba katika mfumo rasmi hawawezi kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtazamo huu siyo sahihi

sana kwa kuwa pato la Taifa kwa muda mrefu limetegemea kilimo. Wazee hawa ndiyo waliokuwa wanashiriki katika kilimo kwa muda mrefu na wakichangia pato la Taifa. Kamati inaiomba Serikali ikamilishe mchakato wa maandalizi ili fao hili pamoja na kuwa la kudumu wazee walipate kwa haraka na mapema iwezekanavyo. Sera na sheria ya kusimamia haki hii ya msingi iletwe haraka Bungeni na Wizara ili Wabunge waipitishie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sera na sheria zilizopo kuhusu huduma ya kwa wazee, utekelezaji wake bado haujaweza kuondoa changamoto zinazowakabili wazee. Sera hizo hazina nguvu kusababisha matamko yaliyopo kwenye sera mara nyingi yanabakia kuwa ya kinadharia. Aidha, Kamati inazidi kusisitiza ni muhimu sasa kuwapa wazee fao hilo la pensheni na Kamati inaamini fao hili sasa linaweza kusaidia kuondoa changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) ndiyo chombo cha hifadhi ya jamii kikongwe nchini. Mfuko huu ulianza kama Idara ya Serikali mwaka 1964 kabla ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Akiba ya Wafanyakazi NPF kwa sheria Na. 36 ya mwaka 1975. NPF iliendelea hadi mwaka 1997 Serikali ilipopitisha Sheria Na. 28 iliyoanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *NSSF* ili kuwa na mfumo wa hifadhi ya jamii unaozingatia kanuni na viwango vya kimataifa vya hifadhi ya Jamii. Mfumo huo ndiyo umeiwezesha *NSSF* kutoa mafao mengi na bora zaidi yakiwemo mafao ya pensheni kwani kabla ya hapo yalikuwa yakitolewa mafao ya uzeeni ambayo yalikuwa hafifu na yalitolewa kwa mkupuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mfumo wa hifadhi ya jamii kuwepo miongo kadhaa, bado ni sehemu ndogo sana ya nguvu kazi katika Taifa letu ndiyo inanufaika na huduma ya hifadhi ya jamii. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo ni asilimia 6.2 tu ya nguvu kazi ya Watanzania wanaokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 21 ndiyo inapata huduma ya hifadhi ya jamii. Hii ni ishara kuwa bado ipo safari ndefu ya kuwaelimisha

wale wote ambao wanapaswa kuwa wadau wa hifadhi ya jamii ambao ni watunga sera na sheria, waajiri, waajiriwa, wanachama na wananchi kwa ujumla. Kamati inaishauri Serikali kuangalia utaratibu ambao utafikisha elimu zaidi kuhusiana na mfumo wa hifadhi ya jamii nchini. Aidha, mfuko husika (*NSSF*) uendelee kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na wanachi wengi walio katika sekta binafsi ili waweze kuelewa vizuri mfumo wa hifadhi ya jamii kwamba unawagusa na waweze kujiunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* inaigusa jamii moja kwa moja kutokana na uwekezaji wake kwenye sekta za elimu (Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa hosteli za Mabibo kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya makazi (Kigamboni na maeneo mengine), afya (kushiriki ujenzi wa hospitali ya Apolo), nishati na daraja la Kigamboni. Hizi zote ni huduma muhimu zinazotolewa na *NSSF* kwa ajili ya kuisaidia jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza *NSSF* kwa kuendeleza uwekezaji katika vitega uchumi ambavyo mbali na kulenga kuongeza kipato cha mfuko, pia vinatoa huduma za kimsingi kwa jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mfuko uliweza kukamilisha ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika Mkoa wa Njombe. Mfuko pia ulifanikiwa kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa miwili ambayo ni mradi wa kuzalisha umeme wa Megawati 300 katika eneo la Mkuranga na ujenzi wa daraja la Kigamboni ambao umekuwa ukisubiriwa kwa hamu kubwa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha mfuko unatarajia kukamilisha miradi ambayo haijakamilika, kuendelea na miradi iliyoanza ambayo itachukua muda mrefu kukamilika na kuanza utekelezaji wa miradi mingine ambayo ni pamoja na:-

- (i) Kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigamboni.
- (ii) Kushiriki katika ujenzi wa Hospitali ya Apolo jijini Dar es Salaam.
- (iii) Kuendelea na ujenzi wa ofisi za *RITA Registration, Insolvency and Trusteeship Agency*.
- (iv) Ujenzi wa jengo la Mzizima, jijini Dar es Salaam.
- (v) Ujenzi wa hoteli ya kisasa jijini Mwanza.
- (vi) Ujenzi wa kijiji cha Kisasa Kigamboni-Tuangoma na Dungu "*Farm*".
- (vii) Kuanza ujenzi wa jengo la Maadili Dar es Salaam endapo taratibu za mazungumzo zitakamilika.
- (viii) Kuanza ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Hisabati (*College of Earth and Mathematics*) katika Chuo Kikuu cha Dodoma na nyumba za Polisi awamu ya tatu iwapo majadiliano na Serikali yatakamilika.
- (ix) Kuendelea na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Bugarika Mwanza.
- (x) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi na vitega uchumi katika Mikoa ya Kigoma na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Mfuko huu kutimiza wajibu wake kikamilifu, Serikali ambayo imekuwa ikitoa dhamana ya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo imekuwa ikichelewa kuanza kulipa gharama za miradi mara inapokamilika na kukabidhiwa. Kamati inaishauri Serikali kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati mwafaka ili kuuwezesha Mfuko uendelee na shughuli za kiutendaji na pia kuwekeza katika vitega uchumi vingine ikiwemo miradi ya kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mafanikio



makubwa, Mfuko huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto kadhaa na kubwa miongoni mwa hizo ni baadhi ya waajiri kutowasilisha au kuchelewa kuwasilisha michango ya wafanyakazi na pia kutozingatia viwango vya uchangiaji vinavyotakiwa. Hali hii inasababishwa na baadhi ya waajiri ama kutoelewa vyema umuhimu wa mfumo wa hifadhi ya jamii au kufanya kwa makusudi. Kamati inashauri Wizara kupitia *NSSF* isichoke kutoa elimu kwa waajiri, wanachama na umma kwa ujumla kuhusiana na hifadhi ya jamii pamoja na sheria na kanuni zinazosimamia uchangiaji katika uhifadhi wa jamii. Aidha, Mfuko uwe na ukomo wa uvumilivu kwa waajiri ambao wamekuwa hawachangii wafanyakazi wao kwa kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria ili kukomesha tabia hiyo ambayo si kwamba inaathiri uendeshaji wa mfuko bali pia inawanyima wafanyakazi haki ya kujiwekea akiba kwa ajili ya pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Mfuko kuangalia namna ya kuwekeza vitega uchumi katika maeneo ya nchi yetu ambayo yako nyuma kimaendeleo ili kupeleka chachu ya maendeleo. Aidha, Mfuko uangalie namna ya boresha zaidi mafao ya wanachama wake kwa kutumia faida ambayo inatokana na vitega uchumi vinavyowekezwa na Mfuko huo kwani fedha zinazotumika kama mitaji zinatokana na michango ya wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafanyakazi. Licha ya kuwepo sheria kadhaa zinazosimamia masuala ya kazi na ajira nchini kama vile Sheria Namba 6 na 7 zote za mwaka 2004 bado kumekuwepo na migogoro mingi ambayo imekuwa ikijitokeza katika maeneo ya kazi kama vile viwandani, katika makapuni na mashirika na kadhalika. Kwa sehemu kubwa migogoro hiyo imekuwa ikitokana na wafanyakazi kudai maslahi, mishahara na stahili nyingine na mazingira bora ya kazi. Zipo pia sababu nyingine za migogoro ambazo ni kukiukwa kwa mikataba, ubaguzi katika sehemu za kazi, kunyimwa haki ya kuwa na vyama vya wafanyakazi na uelewa mdogo wa sheria za kazi miongoni mwa waajiri na waajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupitia takwimu kuhusiana na migogoro inayopokelewa na kusajiliwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*), Kamati imebaini kuwa sekta inayochipukia ya usalama/ulinzi binafsi inaongoza kwa kuwa na migogoro mingi sana. Mfano Tume ilipokea na kusajili migogoro 2,368. Migogoro amabayo haikumalizika mwaka 2011/2012 jumla ni 2,368. Hivyo jumla ya migogoro iliyoshughulikiwa katika kipindi cha Julai 2012 hadi Desemba, 2012 ni migogoro 4,689. Kati ya migogoro iliyosikilizwa na kumalizika jumla ni 2,357 sawa na asilimia 50.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango hiki cha migogoro kinatisha hasa kwa kuzingatia kwamba, sekta hii ni ndogo ikilinganishwa na zile za viwanda, migodi, makampuni na nyingine ambazo zinaajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi katika nchi yetu. Kwa hiyo, iko kazi ya kufanya kwa kiasi cha kutosha ili kuinusuru sekta hii na wafanyakazi ambao wanahusika katika sekta hii. Ingawa kwa maelezo ya *CMA* hali hii ya migogoro katika sekta hii ya ulinzi inatokana na wamiliki wengi wa makampuni ya ulinzi kuwa wastaafu wa majeshi ya polisi na ulinzi, ambao wamekuwa wakitumia amri zaidi kuliko kufuata sheria na kanuni za kazi, bado Kamati inasisitiza kuwa linapokuja suala la sheria ni wajibu wa kila mmoja kuziheshimu kwani hakuna aliye juu ya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kupitia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*) kwa kutambua kuwa njia kubwa ya kupunguza migogoro maeneo ya kazi ni pamoja na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusiana na namna ya kutatua migogoro ya kikazi na pia sheria za kazi. Tume hiyo imeandaa na kuchapa kitabu cha Mwongozo wa Kuzuia na Kutatua Migogoro ya Kazi (*Labour Dispute Prevention and Resolution Training Guide*). Kamati inatarajia kwamba, iwapo mwongozo huo utatumiwa vyema utakuwa nyenzo muhimu itakayosaidia kupunguza tatizo la uelewa mdogo kuhusu taratibu za kutatua migogoro katika maeneo ya kazi. Aidha, Tume inapongezwa kwa kukamilisha Kanuni za Huduma Muhimu (*Essential Services Regulations, GN. 323 of 2012*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na pongezi hizo, Kamati inaishauri Wizara kupitia CMA iendelee kusajili migogoro yote ya ajira iliyopo nchini ya muda mrefu na muda mfupi na kuishughulikia kikamilifu.

Pia elimu iendelee kutolewa kwa waajiri kuhusu Sheria na Kanuni za Ajira na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake. Hatua hii italeti hali ya utulivu na amani sehemu za kazi kwani wafanyakazi na waajiri watatambua haki na wajibu wao na hivyo uzalishaji utaongezeka, utoaji wa huduma utaboreshwa na kwa ujumla uchumi wa nchi yetu utakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Wafanyakazi vipo kwa mujibu wa Sheria za nchi na lengo kubwa ni kusaidia kuleta tija katika kazi. Historia inaonesha kuwa chimbuko la Vyama hivi ni hatua ya wafanyakazi kuunganisha nguvu zao kwa lengo la kudai haki zao (malipo bora, mazingira mazuri ya kazi na kadhalika) wakati wa mapinduzi ya Viwanda kwenye karne ya 18 hasa katika nchi za Ulaya Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa tangu wakati huo kumekuwa na mabadiliko yanayochagizwa na maendeleo ya teknolojia na demokrasia bado malengo ya vyama hivyo yamejikita katika kupinga vitendo vinavyomkandamiza mfanyakazi, kudai maslahi bora zaidi na mazingira mazuri ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro katika Vyama vya Wafanyakazi ambayo imetokana na hali ya kutoelewana ama baina ya chama na chama au vyama, chama na wanachama wake, chama na waajiri au viongozi ndani ya chama. Hata hivyo, licha ya makundi hayo ya migogoro kwa hali ilivyo sasa migogoro ambayo inaonekana kushamiri ni baina ya vyama na waajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na tabia ya baadhi ya waajiri ambao hawataki kutimiza wajibu wao kwa wafanyakazi na hivyo kuona njia pekee ya kukwepa usumbufu ni kupinga Vyama vya Wafanyakazi. Waajiri hao ama wamekuwa hawataki kuruhusu Vyama vya Wafanyakazi

kuwepo maeneo ya kazi au wamekuwa wakiviruhusu lakini kwa shingo upande, jambo ambalo linaondoa ushirikiano na umoja baina ya wafanyakazi na waajiri na hivyo kuibua mivutano isiyo na msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kukemea tabia hiyo ya baadhi ya waajiri na wale ambao watabainika kufanya hivyo wachukuliwe hatua za kisheria kwani wakati mwingine wamekuwa wakisababisha migogoro ya kikazi isiyo ya lazima na wafanyakazi wao na hivyo kuathiri uzalishaji na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri vyama vya wafanyakazi kuwa imara katika kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa kuwaelimisha kutambua wajibu wao kwa mwajiri na haki za msingi ambazo wanastahili kuzipata kutoka kwa mwajiri kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa iwapo wafanyakazi watatambua wajibu na haki zao na wakazidai kwa mujibu wa sheria na Waajiri wakatimiza wajibu wao, kiwango cha migogoro katika maeneo ya kazi kitapungua na hivyo uzalishaji utakuwa wenye tija na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inaomba na kuiagiza Serikali kuwa, kwa kuwa yapo madai mengi sana kutoka wafanyakazi na hasa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Ongezeko la mishahara na hali maisha ya sasa imebadilika.

(b) Kuondolewa au kupunguzwa kwa kodi katika mishahara ya wafanyakazi.

(c) Kuboreshwa kwa mazingira na vitendea kazi kwa wafanyakazi, mfano, nyumba za Walimu, Madaktari, Wauguzi na Polisi, hasa maeneo ya vijijini bado ni duni kwenye vifaa vya tiba katika zahanati, zana za kufundishia na uzalishaji katika viwanda bado ni duni, hali hii inahatarisha sana kudumu kwa ajira kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama na afya mahali pa kazi vinapaswa kuzingatiwa kwa kiwango cha juu sana kwani si kwamba, vipikuuzwa vyaweza kuwa na madhara kwa mwajiri au mwajiriwa pekee, bali hata kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ni jukumu la wadau wa ajira yaani waajiri na wafanyakazi, kuhakikisha afya na usalama mahali pa kazi, bado Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inaweka viwango vya usalama na afya mahali pa kazi na kusimamia kikamilifu utekelezwaji wake ili kunusuru afya za wananchi wake na hivyo kulinda ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha wajibu huu muhimu unatekelezwa ndiyo maana Serikali kupitia Wizara ikaunda Wakala wa Serikali wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi (*OSHA*) ambao ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Utendaji Na. 30 ya mwaka 1997 ikiwa na jukumu la kuboresha usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa ingawa *OSHA* imepewa majukumu makubwa ya kuhakikisha kuwa afya na usalama vinazingatiwa mahali pa kazi, bado Serikali kupitia Wizara haijaiwezesha kikamilifu kutekeleza majukumu hayo. Wakala hii inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhaba wa rasilimali watu, rasilimali fedha pamoja vitendea kazi na vifaa vya ofisini. Kwa mfano, katika upande wa vifaa vya Ukaguzi (vikagua umeme na vifaa vya elektroniki) *OSHA* ina upungufu wa wastani wa asilimia 80. Hali hii inaashiria kwamba, *OSHA* haiwezi kutimiza majukumu yake kikamilifu na athari zake ni kwamba usalama na afya ya wafanyakazi vinawekwa rehani.

Aidha, ofisi za *OSHA* haziko katika hali nzuri kwani majengo ya ofisi zake ni ya kizamani na hayakidhi mahitaji ya nafasi na ubora unaotakiwa. Ni ukweli usiopingika kwamba, hali kama hii inawapa *OSHA* kigugumizi katika utendaji wao kwani hawawezi kuwa na ujasiri wa kuwataka wadau wa ajira kuhakikisha afya na usalama katika maeneo ya kazi wakati wao hawatimizi jukumu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Wizara kuongeza bajeti ya matumizi ya kawaida kwa *OSHA* katika mwaka huu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kujengea *OSHA* mazingira mazuri ya kiutendaji ili iweze kuonesha mfano kwanza kabla ya kuwaendea wadau wengine kwa lengo la kuwakagua na kuwataka wazingatie viwango vya usalama na usafi katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *OSHA* kujengewa uwezo wa kiutendaji ni la muhimu sana hasa kwa kuzingatia kwamba, kadri dunia inavyokumbwa na mabadiliko ya kiuchumi, sayansi na kiteknolojia ndivyo ambavyo wafanyakazi wanakuwa katika vihatarishi na hatari za mahali pa kazi kama vile kemikali, mnunurisho hatari, viumbe hatari/viumbe maradhi, hatari za mitambo, hatari za mazingira ambazo zinaweza kuharibu mwili na mifupa na hivyo kuathiri uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za shirika la Kazi Duniani (ILO) Mwaka 2008. Wafanyakazi wapatao milioni 2.3 wanapata ajali au magonjwa ya kazi duniani na kwamba wafanyakazi wapatao milioni mbili wanafariki na magonjwa yatokanayo na kazi. Takwimu zinaonesha kwa asilimia 3.9 ya vifo vinavyotokea duniani vinasababishwa na ajali au magonjwa yatokanayo na kazi

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za hapa nchini zinaonesha kuwa jumla ya ajali 74 zilitokea ambazo zilisababishwa na mazingira hatarishi mahali pa kazi, ambapo ajali 14 kati ya hizo zilisababisha vifo. Aidha, asilimia 45 ya ajali hizo zimeripotiwa ni Sekta ya Madini, asilimia 18 ni Sekta ya Ujenzi, asilimia saba ni Sekta ya Usafirishaji na asilimia tano kutoka sekta ya kilimo, Misitu na Uvuvi. Kamati inawasisitiza waajiri wote nchini kujisajili na Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi (*OSHA*) ili kuuwezesha Wakala huo kutimiza wajibu wake wa kuhakikisha usalama kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miongoni mwa changamoto ambazo *OSHA* inakutana nazo wakati wa ukaguzi ni pamoja na baadhi ya waajiri kutosajili sehemu zao

za kazi, kutotoa taarifa za ajali zinazotokea maeneo ya kazi pamoja, uelewa mdogo wa masuala ya afya na usalama na kutopima afya za wafanyakazi wao, Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za afya na usalama mahali pa kazi na kusimamia utekelezaji wake kikamilifu. Hii ni pamoja na kuhakikisha wafanyakazi wa mazingira hatarishi wanapewa vifaa maalum vya kujikinga (*Personal Protection Equipments*) ambavyo ni *masks, gloves, safety boots na overalls*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa kuwa tarehe 28 Aprili ya kila mwaka ni siku ya usalama na afya ya wafanyakazi mahali pa kazi, Kamati inashauri siku hiyo itumike hapa nchini kuwazawadia waajiri ambao walifanya vizuri katika kujali na kuzingatia afya na usalama wa maeneo yao ya kazi na hivyo kuwaweka salama wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia siku hiyo itumike kuwahimiza waajiri juu ya umuhimu wa kupima afya za wafanyakazi wao mara kwa mara ili kujua wako katika hali gani ya afya. Hata hivyo, Kamati inasisitiza waajiri kuweka mazingira ya kazi salama na hiyo kuongeza nguvu kazi ya Taifa kwa kuwa na watumishi wenye afya bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la ajira; tatizo la ukosefu wa ajira linazidi kuwa kubwa duniani ambapo Ripoti ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) ya mwaka 2011 inaonesha kuwa nguvu kazi inayofikia watu milioni 205 hawakuwa na kazi. Idadi hii ni sawa na ongezeko la watu milioni 27.6 katika kipindi cha miaka minne ikilinganishwa na nguvu kazi ya watu milioni 177.4 ambao hawakuwa na ajira mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii inaeleza kuwa vijana wasio na kazi duniani ni (miaka 15-25) walifikia milioni 77.7 mwaka 2010 ikilinganishwa na milioni 73.5 mwaka 2007. Ukilinganisha taarifa hiyo ya *ILO* na hali halisi ya hapa nchini utagundua kuwa, vijana wasio na ajira ni mbaya kwani wastani wa kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana ni kati ya miaka 15-24 ambao ni asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichambua takwimu hizi zinaonesha kuwa sehemu kubwa ya vijana wanaohitimu shule na vyuo wapo katika kipindi cha mpito na utagundua kuwa kuna kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kwa vijana. Aidha, tatizo hilo la ajira linatokana na Serikali kushindwa kuzalisha wahitimu walio na ujuzi na taaluma na ari ya kujijiri, vijana wengi walio katika shule na vyuo wanasomeshwa kwa kutumia rejea ya vitabu vya maprofesa wa Ulaya ambavyo hata huko Ulaya hakuna anayevisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii inadhihirisha kuwa itakuwa ni vigumu kufikia malengo malengo ya milenia ya kupunguza umaskini kwa nusu ifikiapo 2015, kwani ongezeko la ukosefu wa ajira linaendela kuwa kubwa na hivyo kulifanya Taifa kuwa na sehemu kubwa ya nguvu kazi isiyo na ajira au iliyo katika ajira zisizo kidhi viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwapatia vijana elimu itakayowawezesha kupata ujuzi na taaluma mbalimbali zitakazowasaidia kuwa wabunifu katika ulimwengu wa sasa ambao unahitaji watu wenye ujuzi na utayari wa kujijiri au kuajiriwa. Serikali itambue kwamba, elimu isiyofuata misingi ya maadili na mahitaji ya soko la ajira kwa vijana haifai kabisa. Ni lazima Serikali kuangalia mfumo mzima wa elimu katika kufanya utafiti juu ya mitaala itakayowawezesha vijana kijijiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba sekta ya kilimo ndiyo inaajiri sehemu kubwa ya nguvu kazi (74.6%) ya nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuboresha sekta hii na kuifanya ichangie katika kukuza uchumi na kuendelea kutoa ajira kwa nguvu kazi iliyopo kwani hata nchi zilizoendelea kiviwanda zilianza na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kikiimarika kitazalisha ziada, kitatoa msukumo wa kuanzishwa viwanda vya kusindika na kuyaongezea thamani mazao ambavyo si kwamba vitaongeze kipato kitakachotokana na mauzo ya mazao hayo bali pia vitatoa nafasi za ajira.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa ni vigumu kufikiri kwamba, kama Taifa tutaweza kupiga hatua katika kukuza uchumi na kuondoa tatizo la ajira kwa kutegemea sekta nyingine pasipo kujipanga kikamilifu katika kilimo, kwani ni wastani wa asilimia 15 tu ya Watanzania ndiyo wako katika ajira rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa ajira nchini. Ni vyema tatizo la ajira kwa vijana likapewa kipaumbele katika kulishughulikia kwa kutumia kila mwanya unaoonesha dalili ya kutengeneza nafasi za kazi kuanzia katika ngazi za kijiji, Halmashauri hadi Taifa. Kamati inaamini kuwepo kwa mpango wa makusudi wa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana kutachochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za wageni. Nchi zote duniani zilizoendela na zinazoendela zilizo na mtizamo wa kuongeza ajira kwa watu wake na kuimarisha uchumi ni lazima iwe na sekta ya uwekezaji. Utaratibu wa utoaji vibali vya ajira kwa wageni vimekuwa vikitolewa holela na kupelekea kuwa na wageni wengi ambao wanafanya kazi ambazo Watanzania wanao uwezo wa kuzifanya. Kwa mfano, ni jambo la kawaida kukuta nafasi za juu na hata zile za kawaida katika sekta za viwanda, hoteli, ujenzi na maeneo mengine zikiwa zimeshikwa na wageni, wakati wapo Watanzania wengi waliosoma na wenye ujuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba, Serikali ikiwa na sheria nzuri ya uwekezaji katika sekta mbalimbali, sheria hizo zitapunguza kwa kiasi kikubwa malalamiko na chuki miongoni mwa wazawa na wageni, hivyo zitasimamia ajira za wageni wanaokuja kufanya kufanya kazi nchini badala ya utaratibu wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inasisitiza kwamba ni vema tuwe na uwekezaji katika sekta zinazohitaji mitaji mikubwa na teknolojia, na si kuwa na uwekezaji hata biashara ndogo ndogo. Kwa kuzingatia kuwa nchi ina rasilimali nyingi na kutokana na ukweli tumejikuta tukitazamwa na Mataifa

mengi duniani ambayo yanaona mianya mingi ya kuweza kuitumia kupata rasilimali zetu kwa kigezo cha uwekezaji. Kamati haipingi uwekezaji kwa kuwa inatambua kuwa nchi haiwezi kupata maendelao bila ya kuwa na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza Serikali kuharakisha Sheria ya Kusimamia Ajira za Wageni wanaokuja kufanya kazi nchini. Sheria hii itasaidia kupunga malalamiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha, Kamati inaomba kuiagiza Wizara mambo muhimu na ushauri ifuatavyo:-

Moja, Wizara ione umuhimu wa kuhitimisha uanzishwaji wa Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii Wizarani, kwa kuwa mpaka sasa hakuna Kurugenzi inayosimamia hifadhi ya jamii Wizarani.

Mbili, Wizara inapokuwa inapokea ushauri na maagizo ya Kamati ijitahidi kuyafanyia kazi, mfano ,mchakato wa pensheni kwa wazee kwa kuwa ni nia na dhamira ya Serikali iliyojionesha wazi toka mwaka 2010, kwa tamko la Waziri Mkuu kuharakisha mchakato huu wa pensheni kwa wazee. Pia kamati inamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuonyesha dhamira na nia hiyo wakati akihutubia siku ya wiki ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Wizara kuyachukulia maagizo haya ya Viongozi Wakuu kama eneo la kipaumbele katika shughuli za Wizara, hivyo kuharakisha mchakato huo na kufanikisha zoezi la kuwapatia pensheni wazee na kulifanya liwe la kudumu.

Tatu, Wizara imepewa dhamana ya kukuza na kusimamia ajira nchini, hivyo Kamati inaigiza Wizara kufanya haraka kuwasilisha mpango wa kushughulika ukuzaji wa ajira nchini ili kusaidia kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira. Aidha, kwa kuzingatia dhana ya kusimamia ajira, Kamati inaishauri Wizara kujitikita zaidi katika sekta ya ajira rasmi na sekta zisizokuwa rasmi ziendeleo kufanyiwa na Wizara nyingine kwa

usimamizi wa Wizara hii, kwa kuzingatia kwamba migogoro mingi katika sehemu za kazi bado inahitaji kufanyiwa kazi hususani masuala yote yanayohusu sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na kwamba, zipo Wizara nyingine mtambuka kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii tayari ina Mfuko wa Maendeleo ya ajira isiyo rasmi, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pia ina Mfuko wa Maendeleo ya vijana wa kukuza ajira isiyo rasmi. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kusimamia na kutoa maelekezo ya kisera na kukusanya taarifa zinazohusiana na masuala ya ajira kutoka katika Wizara hizo.

Nne, Haki za wafanyakazi wengi katika sekta binafsi zimekuwa zikipotea, pamoja na jukumu hili kusimamiwa na Vyama vya Wafanyakazi, bado upo umuhimu wa Wizara kupitia Kurugenzi husika kusimamia ipasavyo mfumo wa ajira na mafao ya Watanzania katika sekta binafsi, mfano, wapo waajiriwa wengi wanaajiriwa katika sekta binafsi bila mikataba na wanafanyishwa kazi kwa masaa mengi bila malipo pia kukosa haki na stahili zao nyingi zikiwemo za kitaaluma. Kamati inaiagiza Wizara kuwa sasa ni wakati wa kusimamia sekta hiyo ili kupunguza migogoro katika eneo hili lenye Watanzania wengi wa hali ya chini.

Tano, tangu Sheria ya Malipo ya Kuumia Kazini (*Workers Compensation Act*) ilipotungwa na Bunge Mwaka 2008, mpaka sasa Sheria haijaanza kutumika. Kamati inaiomba Wizara kuharakisha sheria hii ili ianze kutumika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeza masuala ya kiutendaji yenye kipaumbele, Kamati inaliomba Bunge kufanya mabadiliko madogo katika kifungu 2002, kitabu cha matumizi ya kawaida kama ifuatavyo:-

Moja, Kifungu kidogo 221000 (*Travel in country*) kina jumla ya sh. 160,330,000/=, wakati Kamati ikipitia randama ya Wizara, Kamati iliamua kupunguza jumla ya shilingi milioni kumi (10,000,000/=) zilizopangwa kwa ajili ya kuhusisha ajira

katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili fedha hizo sasa zitumike katika kufuatilia huduma za ajira Serikalini na katika sekta binafsi. Mabadiliko haya hayabadilishi jumla ya kifungu hicho cha 221000 bali kinabadilisha matumizi katika randama ya Wizara.

Mbili, Kamati pia inaomba kuondoa shilingi milioni kumi (10,000,000/=) zilizopangwa kutumika kwa shughuli za maonyesho katika kifungu kidogo cha 221100 (*Travel out of Country*) na kuzipeleka katika kifungu kidogo cha 22100 (*Travel in country*) fedha hizi zitawezesha kukamilisha uhakiki na ukaguzi wa vibali vya ajira kwa wageni katika Mikoa yote Tanzania Bara. Pia kuiwezesha Serikali kupata taarifa ya maeneo yenye uhitaji wa ajira rasmi na kuwasaidia vijana wa Tanzania kupata taarifa za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaiomba, Kamati ya Bajeti iridhie kuwapatia Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ili Kamati ya Huduma Muhimu yaani *Essential Services Committee*, ipate kiasi cha shilingi milioni 350, ili Kamati ya Huduma Muhimu iweze kushughulikia migogoro ya kikazi katika sekta za huduma muhimu nchini kama Sekta ya Afya, Maji, Umeme, Zimamoto, Viwanja vya Ndege na Usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaiomba Kamati ya Bajeti kupitia Serikali kuiongezea Wizara kiasi cha shilingi milioni 400 katika Idara ya Ajira, kifungu 2002, kiasi hicho cha fedha kitasaidia kufanya utafiti wa Kitaifa na kuratibu mwenendo wa soko la ajira nchini na kuimarisha upatikanaji wa taarifa za soko la ajira yaani, *Labour Market Information System-LMIS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Niwapongeze pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo wanakusaidia kutekeleza majukumu yako. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu wa Wizara; Ndugu Erick Francis Shitindi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati wakati ikitekeleza majukumu yake. Nawatakia mafanikio zaidi katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati, pia kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mwenyekiti; Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa *Capt.* John Damian Komba, Mheshimiwa Mohamed Said Mohamed, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Dkt. Maua Abeid Daftari, Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany na Mheshimiwa Nassib Suleiman Omary.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Salvatory Naluyanga Macheleli, Mheshimiwa Jaddy Simai Daddy, Mheshimiwa Rose Kamili Sukumu, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Rosemary Kisimbi Kirigini, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo na Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillillah akisaidiwa na Katibu wa Kamati, Ndugu Happiness Ndaluhwa kwa ushauri wa kitaalam kwa Kamati na pia kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba yale yote yaliyoandikwa kwenye taarifa yangu yaingizwe kwenye *Hansard* kwa sababu taarifa ni kubwa na inazungumzia masuala mengi na Waheshimiwa Wabunge watayasoma kwenye kitabu chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista nakushukuru sana kwa kuwasilisha vizuri sana. Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mbilinyi, Mheshimiwa Paresso kwa niaba.

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. JOSEPH O. MBILINYI - MSEMAJI MKUU KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa yangu ni ndefu. naomba iingie yote kwenye *Hansard*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2013/2014. Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilianza hotuba yangu kwa kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wa wale wote waliofariki dunia kwa ajali ya *MV. Skagit*, mwaka huu naomba nianze hotuba yangu kwa kutoa pole kwa ndugu jamaa na marafiki wa wale waliofariki kwa ajali nyingine ya kizembe ya kuanguka kwa ghorofa la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwaka jana nilianza kwa kutoa pole kwa Mheshimiwa Joseph Selasini kwa kufiwa na baba yake na mwaka huu nianze pia kwa kutoa pole kwa Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse kwa kufiwa na baba yake mzee Yohana Natse. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake, mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ubishi wala ushindani kuwa Serikali yoyote makini duniani huweka sera na mifumo thabiti ya kuhakikisha kuwa ajira za kutosha zinatengenezwa, mazingira ya kazi yanaboreshwa na wafanyakazi wanalipwa ujira na mishahara yenye staha, si tu kwa ajili ya kuwawezesha kumudu gharama za maisha, bali pia kuwapa morali wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza kuwa Taifa lolote duniani ambalo haliwezi kutengeneza ajira na hivyo kuwafanya vijana wake wengi wenye uwezo wa kuajiriwa kuzurura mitaani na wale walio vyuoni wanashindwa kusoma kwa sababu ya Serikali kushindwa au kupuza kugharamia masomo yao; sote tunatambua kuwa Taifa hili limejaliwa rasilimali nyingi za utalii na madini ya thamani, lenye vyanzo vingi vya kodi na mapato, lakini limegubikwa na migogoro mingi ya mara kwa mara na isiyokwisha, ya wafanyakazi wanaodai haki na mafao yao halali, huku wakiishia kunyamazishwa kwa kauli laini zenye matumaini hewa; Kwa namna yoyote ile Taifa hilo, ni kielelezo cha nchi inayoongozwa na Serikali isiyo na vipaumbele, yenye viongozi wasiojali na wanaotekeleza sera wasizozijua au zilizoshindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Katika maoni yetu ya mwaka jana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilituhumu kwamba, Serikali hii ya CCM haijatekeleza ahadi zake kwa Watanzania kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama zilivyotajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 – 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni hayo tulidai kwamba, ahadi ya "...kurekebisha viwango vya mafao ili visipishane mno haijatekelezwa hadi sasa kwani viwango vya mafao vinavyotolewa na Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii ni vile vile vya kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2010."

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tulifafanua jinsi ambavyo ahadi ya "...ya kupanua wigo wa kinga ya hifadhi ya jamii ili Watanzania wengi zaidi wafaidike na huduma hiyo

nayo haijatekelezwa." Vile vile, tulionesha jinsi ambavyo ahadi ya "kuelimisha jamii ... juu ya umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa maendeleo ya wafanyakazi na ya nchi kwa ujumla", nayo haikutetelezwa kwa sababu Serikali yenyewe imekiri kwamba: "... bado kuna uelewa mdogo wa masuala ya hifadhi ya jamii kwa watunga sera, waajiri, waajiriwa, wanachama na wananchi kwa ujumla."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maoni yetu hayo tulionyesha kwamba ahadi pekee ambayo Serikali hii ya CCM imeitekeleza ni "... kuendelea kutumia fedha za wafanyakazi zilizomo katika Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika miradi ambayo haina manufaa yoyote kwa wafanyakazi wenyewe."

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya rejea pana ya Taarifa Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi Zingine kwa mwaka 2010/2011, iliyoonesha kwamba "... kuna udhaifu mkubwa katika vitega uchumi vinavyosimamiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa mfano, ukaguzi wa vitega uchumi vya *NSSF* ulionesha kwamba licha ya Mfuko huo kuwekeza zaidi shilingi bilioni 269.272 za wafanyakazi katika ujenzi wa Awamu ya Kwanza na ya Pili ya Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), sio tu Mfuko huo "... ulikuwa haujasaini mkataba na Serikali juu ya fedha za mradi huo", bali pia ulikuwa "... haujapokea fedha ya pango au malipo ya mkopo kutoka Serikalini ambao tayari umelimbikiza riba ya shilingi bilioni 14.157."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu tulionesha kwamba, sio fedha za *NSSF* tu ambazo zimetumiwa na Serikali hii ya CCM kwenye *UDOM*. Kama tulivyosema, "... *PPF* imekwishazamisha jumla ya shilingi bilioni 39.987; *PSPF* imechakachuliwa shilingi bilioni 105.921; *LAPF* imepoteza shilingi bilioni 22.030; wakati ambapo *NHIF* imekwishaunguza shilingi bilioni 13.403 za wanachama wake. Jumla ya fedha za wafanyakazi wanachama wa



Mifuko hii mitano ambazo zimeunguzwa katika ujenzi wa *UDOM* ni shilingi bilioni 450.615.... Vitega uchumi vyote hivi katika *UDOM* ... havirudishi fedha za mikopo ya Mifuko husika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, tulionesha jinsi ambavyo ujenzi wa Jengo la Idara ya Usalama wa Taifa ulivyotafuna shilingi bilioni 11.83 za *NSSF* na *PSPF* ambazo hadi tunaandika maoni yetu ya mwaka jana zilikuwa hazijaanza kulipwa pamoja na riba yake! Vile vile, tulionesha kwamba, jumla ya shilingi bilioni 19.77 zilitolewa kama mikopo na *NSSF*, *PPF* na *LAPF* kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi huu wa Bunge lako Tukufu "... hazijalipwa hadi sasa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, zaidi ya shilingi bilioni 152.6 zilizotolewa kama mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Jeshi la Polisi, *Machinga Complex*, *Continental Venture Tanzania Limited*, *Meditech Industrial Company Limited*, *General Tyre*, *Dar es Salaam Cement Company Limited*, *Kagera Sugar*, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (*HESLB*) na *Kiwira Power Limited* haikuwa imelipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizo, tulimnukuu Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akisema "... ukubwa wa biashara inayofanywa baina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na taasisi za Serikali na malipo yasiyokuwa na uhakika ya mikopo hiyo yanatia shaka juu ya uendelevu wa Mifuko husika katika siku chache zijazo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa yalitokana na Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye ni mteuliwa wa Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yalishambuliwa sana na Wabunge wa CCM na wawakilishi wa Serikali yake humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, *facts are very stubborn things*, kama mwanamapinduzi mmoja wa karne iliyopita alivyokuwa anapenda kusema: 'Ukweli ni vitu vikorofi sana'! Na ukweli juu ya afya ya Mifuko yetu ya Hifadhi ya

Jamii ni vitu vikorofi kweli kweli, ambavyo haviwezi kuzimwa na propaganda nyepesi nyepesi za watawala na wawezeshaji wao ndani na nje ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake wakati wa Sherehe za Mei Mosi mwaka huu kule Mbeya, Rais Kikwete alielezea tathmini ya afya ya kifedha ya Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini kama sehemu ya maboresho ya sekta hiyo. Tunaomba kumnukuu Rais *in extenso*:

“Tathmini hiyo imeonesha kuwa Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii ipo kwenye hali nzuri kifedha na ni endelevu. Kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*), Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya malipo ya michango ya watumishi waliokuwepo kabla ya mwezi Julai, 1999 Mfuko ulipoanzishwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali italipa shilingi bilioni 50 ikiwa ni sehemu ya malipo hayo. Napenda kuwatoa hofu wanachama wa Mfuko huo kuwa mafao yao yako salama. Hakuna atakayestaafu akakosa kulipwa mafao yake.

“Vile vile Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (*SSRA*) kwa kushirikiana na Benki Kuu wameandaa na kutoa miongozo ... yenye lengo la kuiwezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kufanya uwekezaji ulio bora na wenye tija unaomnufaisha mwanachama na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanza kutumika kwa miongozo hiyo Mei, 2012, uwekezaji wa mifuko hiyo umeongezeka kutoka shilingi trilioni 3.38 mpaka shilingi trilioni 4.24. Pia mali za Mifuko hiyo zimeongezeka kutoka shilingi trilioni 3.74 hadi kufikia shilingi trilioni 4.73.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, matrilioni haya ya Rais Kikwete yanahitaji kuchukuliwa kwa tahadhari kubwa na Bunge lako Tukufu. Hii ni kwa sababu takwimu hizi zimetiliwa shaka na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 iliyowasilishwa kwa Rais tarehe 28 Machi, 2013. Tunaomba kuiacha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ijisemee yenyewe:

“Ukaguzi wa Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali Kuu (*PSPF*) ulibaini kwamba, *actuarial valuation* iliyofanyika tarehe 30 Juni, 2010, ilionesha kuwa hali ya kifedha ya Mfuko iliendelea kuwa mbaya. Ukadiriaji thamani ulibaini hasara halisi ya shilingi trilioni 6.487 kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010. “Pia nilibaini kwamba katika mwaka wa fedha 2011, Serikali ilikubali kuanza kurejesha mafao yaliyolipwa na Mfuko kuanzia mwaka 2004 hadi 2010 kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 716. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki kilipaswa kurejeshwa kidogo kidogo na Serikali kila mwaka katika mgawanyo wa shilingi bilioni 71.6 kwa muda wa miaka kumi kuanzia mwaka 2010. Kufikia mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 kulikuwa na malimbikizo ya marejesho katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2012 na kufikia kiasi cha shilingi bilioni 133. Vile vile, ilibainika kwamba, Serikali ya Tanzania haikuweza kutoa fedha za kuziba pengo la upungufu uliojitokeza ... ikiashiria kuwepo kwa shaka kuhusiana na uwezo wa Mfuko kuendelea kulipa madeni yake yanapokuwa tayari kwa kulipwa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mwaka wa fedha uliopita inafichua ukweli korofi zaidi kuhusu afya ya kifedha ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini.

Hivyo basi, Ripoti hiyo inaonesha kwamba *PSPF* imetoa mikopo isiyolipika ya jumla ya shilingi bilioni 67.179 kwa Serikali na Taasisi Zisizo za Kiserikali “... na hakuna malipo yoyote yalifanywa kwa Mfuko katika kipindi chote cha mwaka. Hii inaweza kuharibu mtiririko wa fedha za Mfuko na matokeo yake kushindwa kulipa mafao yanapofika wakati wa kulipwa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi Zisizokuwa za Kiserikali zilizofaidika na mikopo isiyolipika ya fedha za watumishi wa Serikali hii ya CCM ni pamoja na *Tan Power Resources*, kampuni iliyokuwa inamilikiwa na familia ya Rais Mstaafu Benjamin Mkapa na ya swahiba wake Daniel Yona ambayo iliwahi kumilikishwa Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira kwa njia za kifisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, *Tan Power Resources* ina madeni yasiyolipika kwa *PSPF* ya jumla ya shilingi bilioni 5.421! Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inaeleza kwamba *PSPF* imeingia mkataba na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoa fedha za kujenga Chuo Kikuu cha Elimu, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, "mapitio ya mkataba yalibaini mkanganyiko wa tafsiri ambao unahitaji kutatuliwa mapema. Kutokuwa na mkataba sahihi kunafanya kuwa na tafsiri mbalimbali ambazo matokeo yake ni hasara kwa Mfuko iwapo mgogoro utajitokeza."

Mheshimiwa Mwenyekiti, *PSPF* sio Mfuko wa Hifadhi ya Jamii pekee ambao afya yake ya kifedha ni ya mashaka. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, *PPF* imetoa shilingi bilioni 71 katika ujenzi wa *UDOM* "... ingawa mkataba wa kutoa fedha kwa ajili ya mradi huu kati ya Mfuko na Serikali ... bado haujakamilika hadi ripoti hii inaandaliwa." Kwingineko katika Ripoti hiyo, inasemekana kwamba majengo ya *UDOM* yenye thamani shilingi bilioni 452 zilizofadhiliwa na Mifuko ya Jamii chini ya maelekezo ya Serikali "... hayajakabidhiwa rasmi kwa Chuo Kikuu Dodoma na Serikali ambayo ilisaini mkataba na Mifuko ya Jamii ya *NSSF*, *PSPF*, *LAPF* na *PPF*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhofia kwenda kinyume na matakwa ya kanuni ya 64(1)(d) na (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachelea kumwita Rais Kikwete mwongo kutokana na kauli yake juu ya afya ya kifedha ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua na Watanzania wanataka kujua, kati ya Rais na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni yupi anayesema ukweli kuhusu hali ya kifedha ya Mifuko ya Hifadhi ya Afya ya Jamii katika nchi yetu? Ni nani aaminiwe na Watanzania kati ya Rais Kikwete anayesema kwamba: "... Mifuko yetu ya hifadhi ya jamii ipo kwenye hali nzuri kifedha na ni endelevu"; na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anayesema kwamba "... hali ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uko katika hatari ya kutoendelea kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na pande zinazohusika"? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wafanyakazi wa Serikali ya Tanzania wampuuze yupi kati ya Rais anayewatoa hofu kwamba, "hakuna atakayestaafu akakosa kulipwa mafao yake" na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anayedai kuwa kuna "... shaka kuhusiana na uwezo wa Mfuko kuendelea kulipa madeni yake yanapokuwa tayari kulipwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM iwaambie Watanzania nani ni mkweli kati ya Rais Kikwete anayedai kuwa mali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imefikia shilingi trilioni 4.73; na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anayetuambia kwamba ukaguzi wake wa *PSPF* pekee unaonesha hasara halisi ya shilingi trilioni 6.487!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya kiza na utatanishi kama haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia wito wake wa mwaka jana kwa Serikali "... kusitisha mara moja matumizi haya makubwa ya fedha za wafanyakazi katika miradi ambayo inaelekea kuifilisi Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hivyo kuhatarisha maslahi ya moja kwa moja ya wafanyakazi wa Tanzania."

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarudia kauli yake ya mwaka jana: "... Ni wazi kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Tanzania inaongozwa, kuendeshwa na kusimamiwa na watu ambao

hawana uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ujuzi na uadilifu unaohitajika kwa maslahi ya wafanyakazi wanachama wa Mifuko hiyo. Ni wazi, kwa ushahidi huu, kwamba mabadiliko makubwa ya kimfumo na kiutendaji katika Mifuko hii yanahitajika na kwa haraka kabla mifuko hii haijafilisika kabisa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, Kambi Rasmi ya Upinzani, Bungeni inawataka wastaafu na wafanyakazi wa Tanzania sasa waelewe chanzo halisi cha mafao yao ya uzeeni kucheleweshwa ama kutokuongezeka ama kutokulipwa kabisa na Serikali hii ya CCM! Wakishafahamu sababu halisi za mateso yao, wastaafu na wafanyakazi wa Tanzania wachukue hatua stahiki dhidi ya wale wote ambao kwa sera zao na utekelezaji wao wa sera hizo, wamesababisha mateso hayo kwa wastaafu na wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, bila wafanyakazi kuchukua hatua hizo, maneno ya ibara ya 11(1) ya Katiba yetu kwamba “mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu ... kupata msaada kutoka kwa jamii wakati wa uzee, maradhi au hali ya ulemavu na katika hali nyinginezo za mtu kuwa hajiwezi ...” yatabaki dhihaka ya kikatili kwa wastaafu na wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kurejea pendekezo letu tuliloishauri katika bajeti ya Wizara hii ya mwaka 2011/2012, katika kuona umuhimu wa kuiunganisha mifuko yote ya hifadhi za jamii na kubaki katika Wizara moja ambayo ni ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi rasmi ya Upinzani inasisitiza kuwa lengo kuu la kuunganisha Mifuko hii ya Hifadhi za Jamii ni katika kuirahisishia Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi za Jamii (*SSRA*) katika kutekeleza Sheria moja na kuunda vifungu sawa vya kisheria vitakavyosimamia utekelezaji na uendeshaji wa Mifuko hii ambapo kwa sasa

Mifuko hii imekuwa chini ya Wizara tofauti na hivyo hata utekelezaji wake unakuwa mgumu na kuleta ukinzani kwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasisitiza kuwa pendekezo letu ni kuifanya *PPF* na *NSSF* iunganishwe na kuwa Mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta Binafsi vilevile *LAPF*, *PSPF* na *GEPF* iunganishwe na kuwa mfuko mmoja kwa ajili ya Sekta ya Umma. Pia, Kambi ya Upinzani inapendekeza mifuko yote isimamiwe chini ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi nchini: Katika hotuba yake ya Mei Mosi mwaka huu, Rais Kikwete alisema kuwa, naomba kunukuu:

“Kwa upande wa makusanyo ya kodi kwa mfano, mapato yameongezeka kutoka wastani wa shilingi bilioni 541 kwa mwezi mwaka 2011/2012 hadi kufikia shilingi bilioni 637 kwa mwezi mwaka 2012/2013, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18. Mapato yanapoimarika kama hivi, Serikali inakuwa na uwezo mkubwa wa kuwahudumia wananchi wake, kutekeleza miradi ya maendeleo na wakati huo huo kuboresha zaidi maslahi ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, lakini bado hatujafikia mahali ambapo tunaweza kuongeza mishahara kama vile ambavyo tungependa sote tupate. Hata kwa kiwango cha sasa ambacho sote tunakubaliana hakitoshi, bado mishahara inachukua sehemu kubwa ya mapato ya Serikali.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Rais kusema kuwa mishahara itaongezwa bila ya kutaja kiwango kama ilivyo desturi ya Mei Mosi haitoshi. Ni lazima Serikali iseme kiwango cha nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi nchini kwa mwaka ujao wa fedha wa 2013/2014 ni kiasi gani na je nyongeza hiyo itatatua matatizo ya wafanyakazi kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaiona kauli ya Mheshimiwa Rais kuwa, Serikali imedhibiti ubadhirifu wa umma, ni lazima ionekane katika mishahara ya wafanyakazi wa sekta zote za umma na za binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo la Kodi ya Mapato kwa Wafanyakazi (*PAYE*); pamoja na ugumu wa mazingira ya kazi, mishahara duni na hali ngumu ya maisha nchini, bado mfanyakazi anaendelea kunyonywa kwa kiwango kikubwa cha *PAYE*, ambacho ni moja ya vyanzo vya Serikali katika mapato, huku Serikali ikishindwa kutafuta njia nyingine mbadala za kukusanya kodi ikiwemo kufuta misamaha ya kodi isiyo na tija kwenye uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika maoni yetu ya mwaka jana, tulipendekeza kwamba kiwango cha *PAYE* ishuke kutoka asilimia 14 za sasa hadi asilimia tisa kwa kiwango cha chini kinachotozwa na asilimia 27 kwa kiwango cha juu kinachotozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika hotuba yake ya Mei Mosi, zaidi ya kusema kwamba Serikali imekamilisha uchambuzi wa maombi ya wafanyakazi na kwamba Waziri wa Fedha atayafafanua zaidi katika hotuba yake ya bajeti, Rais Kikwete hakusema kodi ya pato la mfanyakazi itapungua kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mapendekezo ya *TUCTA* kwamba kima cha chini cha mfanyakazi wa Tanzania kiwe 350,000, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba kiwango cha chini cha mishahara kitakachotozwa *PAYE* kiwe shilingi 350,000. Hii itawezesha wafanyakazi wote wanaopata kiwango hicho cha mishahara au pungufu yake kuwa na mapato zaidi na kukabili na mfumuko wa bei wa mara kwa mara na kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali hii ya CCM ikisita kupunguza mzigo wa maisha magumu unaowakabili



wafanyakazi, kwa kuwaongezea mshahara au kuwapunguzia *PAYE*, Serikali hiyo hiyo haijawahi kusita kutoa misamaha ya kodi kwa waajiri matajiri wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba, katika baadhi ya sekta zinazoongoza kwa mauzo ya fedha za nje, waajiri wamellipa kodi ya mapato ya chini kuliko kodi ya *PAYE* wanayolipa wafanyakazi wao licha ya waajiri hao kuwa na vipato vikubwa kutokana na mauzo ya bidhaa zao nje ya nchi. Kwa mfano, kwa mujibu wa hotuba ya bajeti Waziri wa Nishati na Madini iliyowasilishwa na Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Profesa Muhongo, katika kipindi cha miaka 14 (1992-2012), Makampuni ya Madini yalilipa jumla ya shilingi bilioni 468 kama kodi ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho hicho, wafanyakazi hao walilipa jumla ya shilingi bilioni 506 kama *PAYE* na tozo ya kuendeleza ujuzi (*Skills Development Levy*) inayolipwa *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizo zinaonesha kwamba, katika miaka sita ya kwanza (1999-2004) Makampuni ya Madini yalilipa shilingi sifuri kama kodi ya mapato, wakati waajiriwa wao wa Kitanzania walilipa shilingi bilioni 52 kama *PAYE* na *SDL* (*Skills Development Levy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika miaka nane iliyofuata, Makampuni ya Madini yalilipa kodi ya mapato ya shilingi bilioni 468 wakati waajiriwa wao walilipa shilingi bilioni 454. Kwa kipindi chote hicho kwa mujibu wa takwimu hizo za Mheshimiwa Profesa Muhongo, thamani ya madini yaliyouzwa nje ya Tanzania na makampuni hayo ilikuwa ni shilingi Trilioni 19.278.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi, sio tu kwamba Serikali hii ya CCM imeruhusu utajiri wa nchi hii kutajirisha makampuni ya kigeni bali pia imewanyonya waajiriwa wa Kitanzania wa Makampuni hayo kwa kuwatoza kodi kubwa ya mapato kuliko inayolipwa na waajiri wao wa kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali na kima cha chini cha mishahara sekta binafsi; katika mwaka wa fedha 2012/2013, katika Kifungu 2001, Wizara ilitenga jumla ya sh. 60,000,000/= kwa ajili ya kuratibu na kuwezesha utafiti wa kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi na pia zilitengwa sh. 55,000,000/= kwa ajili ya vikao vya Bodi 12 za kissekta za kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi na mwaka huu wa fedha 2013/2014, katika fungu hilo hilo zimetengwa kiasi cha sh. 60,600,000/= kwa ajili ya kuratibu na kuwezesha utafiti wa kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile zimetengwa tena sh. 22,325,000/= kwa ajili ya kuwezesha vikao vya Bodi 12 za kissekta za kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi'. Yaani kwa miaka miwili tumetumia jumla ya shilingi 197,925,000/= kwa ajili ya kufanya kinachoitwa utafiti na vikao kwa ajili ya kujua kama sekta binafsi inahitaji kuongezewa mishahara ama laa na kama ipo haja iwe ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, inasikitishwa sana na mtindo wa Serikali hii sikivu ya CCM ambayo inasema kuwa inasikia, lakini inaendelea kutenga fedha za kufanya utafiti kuhusiana na kima cha chini cha mishahara ya wafanyakazi, hivi ni kweli kuwa Serikali hii haijui wafanyakazi wanastahili kulipwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli kuwa hamkuwasikia *TUCTA* tangu mwaka 2010 walipopendekeza kuwa kima cha chini cha mishahara kiwe kiasi gani? Hivi hamjui kuwa gharama za maisha zimepanda sana na hivyo huhitaji kufanya utafiti kujua kama wafanyakazi wa sekta binafsi wanahitaji kuongezewa mishahara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa maombi mapya ya kutengwa kwa kiasi hiki cha fedha kinatoa taswira kuwa, hata kauli aliyoitoa Mheshimiwa Rais kwenye maadhimisho ya Mei Mosi mwaka huu kwa kusema nanukuu: "Katika kikao chetu tulichokutana na viongozi wa *TUCTA*, tarehe 27

Februari, 2013 tulijadili suala hili na kukubaliana kwamba Serikali iendelee kulichambua zaidi ili kutoa unafuu zaidi kwa wafanyakazi kila mwanya unapokatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuwaarifu kuwa kazi ya uchambuzi imekamilika na maombi yenu yamesikilizwa. Hii ni fedheha kwa Serikali makini na sikivu ya CCM, ambayo utendaji wake na kauli za viongozi wake wakuu ni wazi zinalenga kuwalaghai wafanyakazi na kuwanyonya kupitia matumizi mabaya ya kodi zao!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukosefu wa ajira nchini; tatizo hili limeendelea kukua kila kukicha huku likiambatana na ugumu wa maisha. Upatikanaji wa ajira katika soko la ajira nchini ni wa kusikitisha na jambo la kushangaza ni kuwa Serikali haitaki kukubali kuwa tatizo hili ni kubwa sana na lina athari kubwa si kwenye jamii ya Kitanzania bali hata kwenye uchumi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tukiwa tumefungua milango ya ushirikiano baina ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama Taifa hatujaweka mikakati ya jumla ya kukabiliana na changamoto za soko la ajira katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inajuliza kuwa wakati leo mfumo wa elimu wa Tanzania ukiwa katika hali tete yenye kuzalisha kizazi kisichoweza kushindana na nchi za Kenya, Rwanda, Uganda ambapo wazazi wengi wenye uwezo wanapeleka watoto wao huko, je, nchi ipo tayari kukabiliana na vigezo takwa vya soko la ajira la ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana leo hii si ajabu kukuta katika soko la ajira, hasa katika utalii kwenye Mikoa ya Kaskazini kama Kilimanjaro na Arusha, Wakenya wameweza kuliteka soko la ajira ya utalii kama waongoza watalii, wafanyakazi wa mahoteli makubwa ya kitalii huku

Watanzania wakishindwa kutumia fursa hizo kutokana na changamoto za kitaaluma ambazo zimesababishwa na mfumo duni wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iweze kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya ajira, lazima Serikali ikubali kuwa mfumo wa elimu uliopo sasa haukidhi matakwa ya soko la ajira duniani. Mfumo wa elimu uliopo hauzalishi wataalam wa kutosha wa fani mbalimbali wanaoweza kufanya kazi kwa weledi katika sekta mbalimbali ndio maana hata kwenye sekta ya madini nchini, leo hii asilimia kubwa ya kazi zenye kuhitaji ujuzi na sifa za juu, zimeendelea kufanywa na wageni na bila kufuata sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tufanikiwe katika soko la ajira hatuna budi kufumua mfumo mzima wa elimu yetu. Hakuna mabadiliko magumu duniani, kama mabadiliko ya mfumo wa elimu kwa kuwa unahusisha gharama kubwa, wakati na hata kuleta mtikisiko kwa kuwa utaathiri hata ajira za wale waliopo; lakini pia wataalam wanakiri kuwa mabadiliko ya mfumo wa elimu ndio njia pekee ya kuweza kukabiliana na changamoto kubwa za kiuchumi, kijamii, kisiasa na hata kiutamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa tukubali kufanya maamuzi magumu ili kuokoa nchi yetu ambayo sasa imekosa mikakati endelevu ya kukabiliana na tatizo la ajira. Kambi Rasmi ya Upinzani inajua kuwa jibu la Serikali katika kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira litakua, "mtikisiko wa uchumi duniani umeathiri nchi nyingi hata zilizoendelea nazo zina tatizo la ukosefu wa ajira".

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia Serikali ikiwatimua wafanyabiashara wadogo walioamua kujiajiri wenyewe na hivyo kuwakosesha amani na kuwakatisha tamaa. Cha kusikitisha zaidi ni kwamba; Serikali imekuwa ya kwanza kuzikimbia bidhaa zinazozalishwa na Watanzania hawa wanaojitahidi kutatua tatizo (la ukosefu wa ajira kwa kujiajiri wenyewe) na kukimbilia bidhaa za nje licha ya kuwa bidhaa zinazozalishwa na Watanzania zipo za

kutosha na zenye hadhi na ubora wa kutosha. Hivi Serikali haioni kuwa tunawakatisha tamaa hawa Watanzania ambao wameamua kujajiri?

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa ajira kwa vijana nchini; Tanzania, tumebarikiwa kwa kuwa na rasilimali nyingi, lakini asilimia kubwa ya Watanzania imeendelea kuishi katika umaskini mkubwa, huku soko la ajira kila mwaka likikua upande wa sekta ya kilimo na sekta isiyo rasmi ambapo kuna kiwango kidogo cha ujira na uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira nchini limeendelea kukua, huku viongozi wa Serikali wakiendelea kupoza wananchi kuwa tatizo la ajira si kubwa na kuwa Serikali imefanya jitihada katika kuongeza ajira nchini. Leo hii, tunashuhudia ongezeko la ajira, lakini ajira zisizo na tija kwa Taifa, ajira zisizo za staha kwa Watanzania na ajira zisizo na ujira wa kuridhisha kwa Watanzania. Je, tuendelee kujisifia kuwa tunajenga jamii yenye usawa na kuheshimu utu na thamani ya Mtanzania?

Mheshimiwa Spika, Serikali ya CCM iliahidi mambo mengi kwa mbwembwe ili kupata kura mwaka 2010, wakati ahadi zake kwa wananchi walizotoa kwa mwaka 2005 zikiwa zimetokelezwa kwa kiwango kidogo. Mojawapo ya ahadi hizo ni pamoja na ajira milioni moja za Rais Kikwete alizowaahidi wapiga kura. Serikali inayoongozwa na CCM haina budi kutambua kuwa ari na mwamko wa Watanzania leo hii si kama wa wakati ule wa "Ndiyo mzee", kwa kuwa Watanzania sasa wamegeuka na wanaelewa wajibu wao katika kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira nchini ni kubwa sana na Serikali isipokubali wazi kuwa hali ni mbaya na kuamua kuweka mkakati wa Kitaifa wa kukabiliana na tatizo hili, ni wazi kuwa, tunajichimbia kaburi, kwa kuwa uchumi wetu utaendelea kuporomoka huku asilimia kubwa ya Watanzania wakiishi katika maisha magumu yanayoambatana na maumivu ya kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani mtu akiokota chupa na makopo ya plastiki barabarani ama kwenye majalala, ni mwendawazimu, ila tulipofikia hata wazazi wetu, wazee ambao hawana pensheni na wanaishi katika mazingira magumu, wameingia mitaani na kuanza kuokota makopo kama sehemu ya ajira kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wetu wanaokota makopo, vijana wanaokota makopo, watoto wanaokota makopo, kwa kuwa Taifa sasa limekosa mwelekeo wa kuweza kuandaa mazingira kwa wazee, vijana na watoto katika kujikwamua kimaisha kwa mipango endelevu ya kazi na ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo ambayo yamesababisha ukosefu wa ajira nchini ni pamoja na kutolingana kwa uhitaji na upatikanaji wa ajira katika soko la ajira, uanzishwaji wa ajira katika shughuli za uchumi unaotokana na sera zisizotekelezeka za uwekezaji, kutokuwepo kwa programu mbalimbali za ajira zinazoweza kuchangia upatikanaji wa ajira katika sekta mbalimbali kuanzia ngazi ya Taifa mpaka Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa ambayo vijana wengi wa Kitanzania tunakutana nazo ni pamoja na kukosa elimu, maarifa, mafunzo na ujuzi unaotakikana katika soko la ajira hapa nchini na katika jumuiya ya Afrika mashariki. Wakati huo huo, kazi nyingi zinatoa ajira zisizoleta tija zenye masharti magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhasilia, kuna matatizo mengi ya kimuundo na vikwazo vinavyofanya ajira kwa vijana na uwezekano wa vijana kuajiriwa kuwa mgumu. Waajiri wengi, kwa mfano, wanatoa matangazo ya nafasi za kazi na ajira kwa kuweka vigezo kama ujuzi wa kazi wa kuanzia miaka mitano na kuendelea, wakati vijana wengi, kama inavyojulikana, hawana uzoefu wala ujuzi katika ajira hizo zinazotangazwa ingawa wana uwezo wa kuzifanya na kuzitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa waajiri wote katika sekta binafsi na umma, wanaweka masharti au vigezo vya ujuzi na uzoefu kuwa moja ya masharti magumu ya ajira kwa vijana, wanasahau kuwa Tanzania tumekosa mpango maalum wa mafunzo yanayoendana sambamba na elimu ya kijana, ili kumfanya kijana apate ujuzi katika taaluma yake na katika sekta inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasababisha ugumu kwa waajiri, katika kutoa nafasi za kazi kwa vijana, kwa kuwa kuajiri mtu asiye na ujuzi au uzoefu inachukuliwa kama ni gharama, kwa kuwa mwajiri lazima aingie gharama za kutoa mafunzo ya awali tena kwa vijana atakaoajiri. Hii inasababisha waajiri wengi kukwepa kuwaajiri vijana kwa kigezo cha kupunguza gharama za mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira kwa vijana pia linachangiwa zaidi kwa kutokuwa na uoanishaji mzuri na ushirikiano kati ya taasisi za elimu na mafunzo kwa upande mmoja na viwanda au soko la ajira kwa upande mwingine. Hii ni kwa kuwa, mitaala ya sasa ya elimu na mafunzo haindeshwi kwa kushirikisha wadau wengine, hasa katika masuala ya kazi na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko makubwa ya kisera yanatakiwa kufanyika katika sekta mbalimbali ambazo zina msukumo katika kuongeza thamani ya mtafuta kazi kwenye soko la ajira. Kati ya maeneo muhimu ambayo yanatakiwa kufanyiwa mabadiliko ni pamoja na kuazimia kufanya mabadiliko katika mfumo wa elimu uliopo sasa kwa kufanya maboresho kwanza; kwa kuhakikisha kuwa elimu ya msingi na sekondari inatolewa bure kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mfumo na mtaala wa elimu uliopo sasa urekebishwe ili uweze kukidhi mahitaji ya soko la ajira ambalo huwa linabadilika. Lazima Serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikubali kufanya mapinduzi ya sera ya elimu itakayomfanya kijana wa Kitanzania aweze kuajiriwa popote pale hasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ni kwa Serikali kuhakikisha mipango na mikakati ya ukuzaji wa sekta mbalimbali inaambatana na uanzishwaji wa kazi na ajira kwa vijana wa Kitanzania. Kila sekta iendane na mipango endelevu ya kukuza ajira kwa vijana. Kwa mfano, ukuzaji wa sekta ya miundombinu, uendane na kutoa nafasi za ajira kwa vijana wa Kitanzania pamoja na kuwalipa mishahara na posho zenye staha, zitakazoweza vijana kujikwamua na hali ngumu ya kiuchumi na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindani wa kidunia unafanya uchumi wa nchi mbalimbali kuendana na mabadiliko mbalimbali, hasa mabadiliko ya teknolojia. Hapa nchini, tumeshuhudia mabadiliko makubwa na mapinduzi ya teknolojia kuanzia kwenye uzalishaji, kilimo, habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko makubwa yanayoendelea katika vigezo na masharti ya kazi, ni kiashiria kikubwa kuwa vijana lazima wasaidiwe katika kukabiliana na changamoto za ukuaji wa kazi wa teknolojia. Hata vijana ambao wanapata fursa ya ujasiriamali lazima wapate mafunzo ya kukabiliana na ukuaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ahadi mbalimbali ambazo zilitolewa kipindi cha uchaguzi wa mwaka 2010 za kuongeza ajira kwa vijana na kukabiliana na tatizo la ukosefu kwa ajira za vijana, ikiwemo kutatua changamoto za vijana waliopo katika sekta isiyo rasmi ; Wamachinga, wachuuzi wa bidhaa ndogo ndogo, wakulima wadogo wadogo, wasanii, wavuvi, wajasiriamali, mamalishe, wafanyabiashara ndogo ndogo, wachimba madini, waliopo kwenye sekta ya utalii; matumaini ya vijana wengi yalikuwa ni utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa wakati. Pamoja na Taifa kuwa na takribani ya vijana milioni 16, ambapo katika kupitisha bajeti ya vijana, fedha zilizotengwa kwa ajili ya vijana zilikuwa ni kiasi kidogo cha bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuweka fursa sawa kwa wote na kuleta usawa katika mgawanyo wa rasilimali



za nchi hii, kwa tengo hilo la fedha za kiasi cha bilioni tatu kwa vijana milioni 16 wa Kitanzania, basi kila kijana ana uwezekano wa kupata kiasi cha shilingi za Kitanzania 187.5 kama mtaji.

Mheshimiwa Spika, huu si upotoshaji kama mnavyouta bali ni ukweli halisi ambao Watanzania leo wanakumbana nao kwa kuwa na Serikali ambayo haina vipaumbele katika kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana. Kumekuwa na ongezeko la vijana wanaojihusisha na biashara za madawa ya kulevya, ujambazi, ukahaba, hali inayochangiwa na fursa chache za kufikiwa kwa malengo na miradi mbalimbali ya programu za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada za kutengeneza mazingira kwa vijana na Watanzania kwa ujumla hasa wanaofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi maarufu kama Wamachinga, unaleta changamoto katika uchumi wa Taifa letu na katika utatuzi wa migogoro inayotokana na ukosefu wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa kuweka mpango mkakati wa kuoanisha idadi ya vijana ambao wamekuwa wakifanya biashara zao katika maeneo yasiyokubalika na kuwatengea maeneo ambayo yatawakutanisha na wateja wao ili waendeshe biashara zao bila bughudha kwa wengine. Hii iambatane na mifumo thabiti ya kuhakikisha kuwa vijana wanapata fursa ya mikopo katika taasisi za fedha nchini yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya Serikali kuanzisha mpango wa kuwadhamini vijana waliotimiza masharti ya kibiashara inayoambatana na michanganuo kwa kushirikiana na Benki ambazo zina matawi mpaka sehemu za vijijini, ili mipango ya kifedha ya kuwanufaisha vijana iwafikie kwa ukaribu na kwa wakati ili kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira nchini bado ni kubwa sana na linazidi kuwa siku hadi siku huku kukiwa

hakuna ufumbuzi wa kuaminika unaotolewa na viongozi wa nchi. Vijana wamekuwa wakiendelea kuhitimu katika vyuo mbalimbali nchini huku wakiwa wanakosa kazi maalum za kufanya na hivyo kujikuta wakiishi maisha ya dhiki na yasiyotamanika huku wakiwa wamekata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kutatua tatizo la ukosefu wa ajira nchini, wataalam mbalimbali wamekuwa wakishauri kwamba, suluhisho la kuwanusuru vijana ni kuwahamasisha na kuwajengea mazingira ya kujijiri wenyewe kwenye sekta binafsi kama ufundi, kilimo, ujasiriamali na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni dhahiri kuwa vijana wengi wameendelea kuhitimu elimu ya juu nchini kila mwaka katika fani mbalimbali. Pamoja na ugumu wa soko la ajira nchini, lazima Serikali iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa kundi hili linapewa elimu na mafunzo ya kuwawezesha kutumia taaluma zao ili waweze kusaidia kada mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati ambayo Serikali inaweza kuitumia ni pamoja na kuingia ubia na makampuni yaliyo katika sekta mbalimbali nchini ambayo yatakuwa yanatoa nafasi za mafunzo ya kazi *internship* kwa muda utakaopangwa kama moja ya wajibu wa mashirika kwa umma *Corporate Social Responsibility*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si tu itawajengea vijana uwezo wa kujifunza bali pia italisaidia Taifa kutunza thamani ya mtaji rasilimali watu (*Human Capital Value*) na kuwa Taifa lenye ujuzi na maendeleo ya nguvu kazi (*human resoures development*). Lazima Serikali sasa itambue kuwa kundi la vijana ndilo chachu ya mabadiliko ya kila kitu hivyo wakishirikishwa ipasavyo katika sekta mbalimbali wanao uwezo wa kuliletea maendeleo ya kweli Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haitakuwa makini katika kuutafutia ufumbuzi mgogoro huu wa ajira, ni

wazi kuwa vijana wataendelea kudai mabadiliko hata kwa kutumia nguvu pale inapobidi kutokana na ugumu wa maisha na ufuya wa fursa za kuwakwamua kimaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa ajira kwa Makundi Maalum na changamoto zake za Kiseru; Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuitaka Serikali kuboresha sera za kazi na ajira, sera za usalama wa mahali pa kazi pamoja na sheria mbalimbali ambazo zitatoa nafasi na fursa kwa makundi maalum yalipo katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mifumo mbalimbali ambayo ipo nchini, kuanzia mifumo ya elimu, mifumo ya kifedha na mifumo ya uendelezaji wa mtaji watu, makundi maalum hasa walemavu wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi ambazo zimewakatisha tamaa. Soko la ajira na kazi leo, halijawekea mfumo utakaohakikisha kuwa unatoa fursa kwa walemavu ili nao wapate nafasi za ajira na majukumu ya kazi yatakayoweza kuwaendeleza na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mawasilisho ya bajeti kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Waziri alieleza kuwa kuna jumla ya watu wenye ulemavu 308 (kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Kazi na Ajira Mheshimiwa Gaudencia M. Kabata, Agosti, 2012 - Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013, Ukurasa wa 19) walipatiwa mafunzo ya ujuzi wa fani mbalimbali kwa kupitia mafunzo ya ujuzi kwa kushirikiana na wadau kama *CCBRT* (*Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania*), *CEFA* na *Radar Development* ambapo kati ya wahitimu hao 145 wameajiriwa na 163 wamejajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi hii haiteti taswira halisi ya makundi maalum katika jamii ambayo yana Watanzania wenye elimu, ujuzi na utaalum katika fani mbalimbali lakini wamekosa fursa za ajira kutokana na hali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Wizara kutoa takwimu za jumla ya

Watanzania walio kwenye makundi maalum walioajiriwa katika sekta mbalimbali na waliojijiri pamoja na kutoa tathmini ya ufuatiliaji wa utekelezwaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 katika kuhakikisha kuna usawa wa fursa za ajira na kipato kwa makundi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kiasi gani cha fedha za maendeleo ambacho Wizara imetenga kwa mwaka huu katika kuwawezesha walemavu nchini katika kukabiliana na changamoto za maisha, aidha, kwa kuwaandaa kujijiri ama kwa kuwaongezea ujuzi na maarifa ili waweze kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira mbaya kwa watoto na athari zake; kwa miaka mingi haki za watoto zinakiukwa hasa katika suala la kuwaajiri kinyume cha umri wao, ambapo kimsingi ni kosa na ni kinyume na sheria na taratibu za nchi. Hali hii inachangiwa na ugumu wa maisha hasa kwa watoto wanaoishi vijijini na wale ambao wamekumbana na athari mbalimbali ikiwemo wale ambao wazazi wao wamefariki kutokana na ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi pia inatokana na hali mbaya ya umaskini uliokithiri katika familia nyingi za Kitanzania, hali inayomnyima mtoto kufanya maamuzi sahihi kutokana na umri wake na hivyo kukimbilia kwenye ajira hatarishi kwa misingi ya kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni wazi kuwa watoto walio katika ajira mbaya wananyimwa elimu na fursa ya kukua na kujenga vipaji na uwezo utakaoweza kuwakwamua wao, familia na jamii zao kutoka kwenye mzunguko wa umaskini. Tumeshuhudia ajira mbaya za watoto ambao wengi wanafanya ajira hatarishi na zenye kuleta madhara si tu ya kiafya bali kisaikolojia ikiwemo ajira za kwenye mashamba makubwa ya kahawa, chai, tumbaku; ajira za viwandani; ajira za kazi za nyumbani; ajira hatarishi kwenye migodi ya madini na machimbo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii si tu ni hatari kwa Taifa ambalo tunasema watoto ni Taifa la kesho, bali kwa mustakabali wa Taifa ambalo linaamini katika misingi ya haki na usawa pamoja na kuwalinda watoto dhidi ya mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo la ajira mbaya kwa watoto, mwezi Machi mwaka huu, Marekani ilitoa ruzuku ya shilingi bilioni 16 kwa Kamati ya Uokoaji wa Kimataifa Nchini (*IRC*) kwa ajili ya kukabiliana na ajira mbaya kwa watoto katika Mikoa ya Kigoma na Tanga ambapo fedha hizo zitatumika kupitia kwenye mradi mpya ujulikanao kama "Wekeza" na kuwa *IRC* itashirikiana na wabia wake kukabiliana na ajira kandamizi na za kinyonyaji dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti Spi, Balozi Lenhardt alikaririwa akisema kuwa: "Mradi utalenga Wilaya sita katika Mikoa ya Kigoma na Tanga ambako kuna tatizo kubwa la utumikishwaji wa watoto katika ajira mbaya kwenye shughuli za kilimo na kazi za majumbani na utawahudumia waathirika pamoja na kujenga uwezo wa Serikali kulishughulikia tatizo hilo,"

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na msaada wa Marekani katika kukabiliana na ajira mbaya kwa watoto, Serikali kwa kupitia Wizara itupatie majibu ni mkakati gani uliowekwa katika kukabiliana na ajira mbaya kwa watoto katika sehemu mbalimbali za Taifa hili tofauti na Wilaya hizo sita zilizofadhiliwa na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni kwa Wazee wote nchini; katika maoni yake kuhusu Bajeti ya Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kazi na Ajira ya mwaka 2011 na 2012 kwa nyakati mbalimbali, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA imeitaka Serikali kuharakisha kuanza kutoa pensheni kwa wazee wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali hii inayoongozwa na CCM yamekuwa ni ahadi kwa wazee

kwamba, pensheni hiyo itaanza kulipwa kwa kuwa Serikali iko katika hatua ya mwisho ya kufanya utafiti na kuandaa mfumo wa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 6 Agosti, 2012 wakati akijibu maswali Bungeni hatimaye Waziri wa Kazi na Ajira Gaudencia Kabaka akatoa ahadi mahususi kwamba mwanzoni mwa mwaka 2013 ingetungwa Sheria ya Wazee ambayo pamoja na mambo mengine ingeweka mfumo madhubuti wa wazee wote kuanza kulipwa pensheni kuanzia mwaka huu wa 2013. Waziri aliihakikishia Bunge kwamba Serikali iko katika hatua za mwisho za kuandaa mpango madhubuti wa ulipaji wa pensheni kwa wazee nchini kuanzia mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kutimiza ahadi hiyo huku mwanzoni mwa mwaka 2013 ukiwa umepita bila sheria husika kutungwa wala pensheni kuanza kulipwa, Rais Jakaya Kikwete akihutubia kilele cha wiki ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mkoani Dodoma tarehe 17 Mei, 2013 aliagiza Wizara ya Kazi na Ajira kuanza kufikiria kuwalipa pensheni wazee wote na kujiridhisha kabla ya kuanza kutoa mafao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo hilo la Rais, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Wizara ya Kazi na Ajira itoe taarifa ya kina kwa Bunge kueleza Mpango Madhubuti ambao ilijibu Bungeni kwamba uko katika hatua za mwisho umeishia wapi na kuwasilisha Bungeni rasimu ya mpango huo iliyokuwa tayari mpaka wakati Waziri alipojibu Bungeni mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ya Kazi na Ajira ieleze juu ya matumizi ya fedha za umma zilizotumika kufanya tathmini na utafiti ambao Wizara ilieleza katika majibu yake ya wakati uliopita iwapo ni sasa ndipo Wizara hiyo imeagizwa ianze kufikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaona kauli hizo za Serikali inayoongozwa na CCM ni za kutowajali wazee na za

kukwepwa kuwajibika kutimiza ahadi kuwa, tathmini na tafiti zimefanywa mpaka na asasi za kiraia na Serikali kupewa nakala. Aidha, kufuatia tafiti hizo Wizara iliahidi Bungeni kwamba, wameanza kuandaa mfumo wa kuorodhesha wazee ikiwa ni sehemu ya kuanza kuandaa mchakato wa malipo ya pensheni hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali inayoongozwa na CCM kuanza kutoa kauli ya kuanza kulipa pensheni hiyo kwa Wazee mwaka huu 2013 na kuingiza katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014, kwa kuzingatia maoni na mapendekezo tuliyotatoa mwaka 2011 na 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inaitahadharisha Serikali inayoongozwa na CCM kwamba, ahadi hii isipotekelezwa, tutawakumbusha wazee wote juu ya ahadi alizotoa Waziri Mkuu Mizengo Pinda katika kilele cha Siku ya Wazee Duniani tarehe 1 Oktoba, 2010 alipotumia vibaya nafasi ya Kiserikali kutafuta kura za wazee kwa niaba ya CCM ili wazee wafanye maamuzi sahihi ya kukikataa chama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inayoongozwa na CHADEMA inawakumbusha wazee wote nchini kwamba miaka takribani kumi imepita toka Sera ya Wazee itungwe mwaka 2003. Hata hivyo, utekelezaji wake chini ya Serikali inayoongozwa na CCM umekuwa ni wa kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za Kazi na haki za wafanyakazi; tumeendelea kushuhudia kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika maeneo mengi ya kazi. Tatizo hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na wafanyakazi kutosimamia au kutojua haki zao za msingi kama wafanyakazi na hivyo kusababisha waajiri kutumia fursa hiyo ya wafanyakazi kutozijua sheria, kuvunja sheria na haki nyinginezo za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kwa mfanyakazi wa sekta yoyote ile kujua haki zake za msingi kama mfanyakazi na mwajiri kuziheshimu haki za kila mfanyakazi kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Kazi, Na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria za Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004. Sote tunatambua kuwa mfanyakazi ni mtu ambaye ameingia mkataba na mtu, taasisi au Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimantiki, mkataba, kulingana na Sheria ya Ajira Na. 6 ya mwaka 2004, kifungu cha 14, kimetoa aina tatu za mikataba ambayo ni mkataba usio na muda maalum kwa ajili ya watalaam, Mkataba wenye muda maalum kwa ajili ya wafanyakazi wasio kwenye taaluma ya utawala na mikataba kwa ajili ya shughuli maalum kwa muda muafaka na kifungu cha 15 cha Sheria ya Ajira kimefafanua kwamba, mikataba yote lazima iwekwe katika maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna pengo kubwa la sheria katika kulinda haki za wafanyakazi pindi kunapotokea uhamisho wa shughuli yaani (*Transfer of Undertakings*) kwa upande wa mwajiri hususani kwenye sekta binafsi ambapo kumekuwa na migogoro mingi baina ya pande mbili hizi inayotokana na upungufu wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wakati nikiwasilisha hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii kwa Mwaka 2012/2013, Kambi Rasmi ya Upinzani iliishauri Serikali kuleta Muswada wa Sheria Bungeni utakaosimamia maslahi ya wafanyakazi katika suala hili, jambo ambalo linaonekana ni kitendawili mpaka sasa kwa Serikali inayojiita sikivu masikioni pa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki na wajibu wa mfanyakazi; mwajiriwa ana haki ya kupata likizo ya siku 28 ambapo kifungu cha 31 kinamtaka mwajiri kutoa likizo ya siku 28 mfululizo kwa kila mwaka wa ajira. Siku 28 hizo zinajumuisha sikukuu iwapo zitaangukia ndani ya siku hizo na



siku za mwisho wa juma. Mwajiri anaweza kupunguza siku za likizo iwapo mwajiriwa aliomba mwenyewe likizo fupi za muda na ambazo alipokea malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa katika Sheria ya Ajira, likizo ni suala la lazima kwa kila mfanyakazi na tabia ya kuzuia likizo kati ya mwajiri na mwajiriwa hairuhusiwi kwani sheria inamlazimisha mwajiri kumlipa mwajiriwa au mfanyakazi fedha ya likizo, ambayo ni nauli ya mfanyakazi, mke wake na watoto wasiozidi wanne na wategemezi wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hiyo ya kazi kuna likizo ya uzazi, kifungu 33, ambapo mfanyakazi atakayekuwa mjamzito anapaswa kutoa taarifa ya maandishi ya miezi mitatu kabla ya kuanza likizo yake ya uzazi na taarifa hiyo ni lazima iambatanishwe na cheti cha daktari. Mjamzito anaweza kuanza likizo yake wakati wowote, ilimradi tu yawe yamebaki majuma manne kabla ya kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malipo baada ya kuachishwa kazi; mara baada ya kuachishwa kazi, mfanyakazi anatakiwa kulipwa mafao yake yote yanayotokana na ajira yake kwa kipindi chote cha ajira. Malipo hayo ni pamoja na mapunjo ya mshahara, kiinua mgongo na nauli ya kumsafirisha hadi kituo cha karibu na nyumbani kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kumekuwepo na usumbufu mkubwa kwa wafanyakazi wa sekta binafsi na Serikali mara baada ya kustaafu katika kufuatilia na hata kulipwa stahili hizo jambo ambalo ni ukiukwaji wa sheria ambazo zipo kwa ajili ya kulinda na kuhifadhi haki za wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama vya Wafanyakazi nchini; uhuru wa Vyama vya Wafanyakazi nchini unatambuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uangalizi wa Sheria za Kazi na Mahusiano ya Kazi ya mwaka 2004. Uhuru huu una umuhimu sana katika

maeneo ya kazi na historia yake ipo tangu mapinduzi ya viwanda nchini Uingereza karne ya 19, katika Bara la Ulaya na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa Vyama vya Wafanyakazi ni msingi muhimu wa haki za binadamu kwa kutoa haki za kila mmoja, kuunda na kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi katika eneo lake la kazi, haki ya kugoma na kuandamana na maridhiano /matakwa ya Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hali hii ni tofauti kwani vyama hivi vimeendelea kupigia kelele madai na maslahi mbalimbali kupitia vyama vyao, lakini Serikali imeendelea kuwa kimya na kukimbilia Mahakamani kunyamazisha madai/malalamiko yao, jambo ambalo si suluhisho la masuala hayo bali ni sawa na kujifunika shuka katikati ya mvua kubwa ya mawe huku ukidhani utaikwepa mvua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka na kuishauri Serikali kushughulikia kwa dhati masuala yote ya wafanyakazi ikiwa ni malimbikizo ya mishahara, kuboresha mazingira mahali pa kazi na bima za afya kwa wafanyakazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za rasilimali watu nchini; katika mkutano wa mwaka wa 47 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), uliofanyika Juni, 2012, Jijini Arusha (kwa mujibu wa Mwananchi ya tarehe 2 Juni, 2012; <http://174.132.155.185/>, *magazines/31-uchumi/24697-jk-tatizo-la-ajira-kwa-vijana-litavuruga-uchumi-wa-afrika.html*), Waziri wa Kazi na Ajira alisema tatizo la ajira kwa vijana limepungua kutoka asilimia 12.9 mwaka 2000/2001 hadi asilimia 11.7 mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Kabaka alisema, kitendo cha wanasiasa kuendelea kusema tatizo la ajira kwa vijana ni bomu linalosubiri kulipuka, siyo kweli kwani utafiti uliofanywa na Wizara yake kwa kushirikiana na Taasisi

ya Takwimu ya Taifa (*NBS*), unaonesha kuwa tatizo hilo limepungua kwa asilimia 1.2. Waziri aliendelea kueleza kuwa, utafiti uliofanywa na *NBS* mwaka 2006, kwa kushirikiana na Wizara hiyo umebainisha kuwa, nguvu kazi ya Tanzania ni milioni 20.6 kati ya watu milioni 37.5, kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, ni wazi hali ya uchumi duniani kwa sasa si nzuri hasa kwa nchi zinazoendelea na changamoto kubwa ni hali ya uchumi pamoja na kubadilika kwa vigezo na masharti katika soko la ajira. Majibu ya Serikali kuwa tatizo la ajira kwa vijana limepungua, kwa kuangalia takwimu za mwaka 2006 halitoi taswira halisi ya tatizo hili, hivyo kutoa majibu kwa makadirio ya takwimu kuwa tatizo la ajira limepungua si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Waziri wa Kazi na Ajira alikiri kuwa, tatizo la takwimu za ajira ni changamoto kwa kuwa linaleta picha hasi na aliahidi kuwa Wizara yake kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) imempata Mshauri Mwelekezi anayeandaa mfumo wa taarifa za soko la ajira utakaokamilika katika mwaka 2012/2013 (kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudencia M. Kabaka kwa makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013) na kwa kuwa wakati akijibu swali la Mheshimiwa Naomi Kaihula, tarehe 13 aprili 2011, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi na Ajira alikiri kuwa ni vigumu kupata taarifa za uwiano wa vijana wanaomaliza shule na vyuo na wanaopata ajira kutokana na kukosekana mfumo wa ufuatiliaji (*Trace Study*) kamilifu, ambao ungetuwezeshwa kufahamu ni vijana wangapi kati ya waliomaliza shule au vyuo wameweza kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo, Naibu Waziri aliahidi kuwa Wizara inaandaa mfumo wa upatikanaji wa taarifa za soko la ajira ambao ungeanza kufanya kazi mwishoni mwa mwaka 2011 na kusaidia kupatikana kwa taarifa hizo (kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 13 Aprili, 2011).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*) ilianzishwa kwa kutumia Sheria ya *Executive Agencies Act, No. 30* ya mwaka 1997 na wajibu wa *OSHA* ni kufanya kaguzi na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na afya na kuhakikisha kuwa waajiri wanazingatia sheria na kanuni za usalama mahali pa kazi hasa Sheria ya Afya na Usalama katika Maeneo ya Kazi (*OSHA*) Na. 5 ya mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia Mei 2012, jumla ya kesi 16 (kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Kazi na Ajira Mheshimiwa Gaudencia M. Kabaka, Agosti, 2012; Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2012/2013, Ukurasa wa 25) zilikuwa Mahakamani. Tunaitaka Wizara itupe mrejesho wa kesi hizo dhidi ya waajiri waliokiuka sheria na kanuni za usalama mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Wizara kuiwezesha *OSHA* kwa kuipatia rasilimali za kutosha ili iweze kufanya kaguzi zake ikiwemo kutekeleza wajibu wake wa uainishaji na usajili, ukaguzi wa usalama na afya, tathmini za maafa yawezayo kutokea mahali pa kazi na athari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matukio mbalimbali ambayo yanatokea nchini ambayo yanasababisha athari si tu kwa raia wengine bali kwa wafanyakazi ambao wanakuwa ni wahanga wa matukio hayo. Katika kuporomoka kwa jengo la ghorofa 16, Jijini Dar es Salaam ni kielelezo cha kutofanyika pia kaguzi za usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali ya CCM ikiri kuwa imeshindwa kuhakikisha kuwa mahali pa kazi ni salama kwa kila Mtanzania. Ni fedheha kuwa na wakala wa Serikali mwenye dhamana ya kuhakikisha usalama na afya mahali pa kazi unazingatiwa, lakini inashindwa kuwa na vitendea kazi pamoja na rasilimali za kutosha kwa ajili ya kulinda usalama na afya mahali pa kazi kutokana na ufinyu wa bajeti na rasilimali kazi.

**Idadi ya Mahali pa kazi zilizosajiliwa kulinganisha na zizosajiliwa nchini (kwa mujibu wa takwimu za *OSHA* Januari, 2009 – Desemba, 2012)**

<b>Mwaka</b>	<b>Makadirio ya Mahali pa Kazi Nchini</b>	<b>Sehemu za Kazi Zilizosajiliwa</b>	<b>Asilimia ya Sehemu za Kazi Zilizosajiliwa</b>
2009	6,825	1,747	25
2010	11,691	2,069	22
2011	21,068	5,045	24
2012	27,500	6,599	24

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara, kulipatia Bunge majibu ya maswali yafuatayo kutokana na takwimu zilizopo hapo juu. Je, ni sababu zipi ambazo zimeifanya *OSHA* ifanye kaguzi za usalama wa afya na mahali pa kazi bila ya kufikia nusu ya sehemu hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia takwimu ambazo Waziri alizitoa katika Bunge hili wakati wa mawasilisho ya bajeti kwa mwaka wa 2012/2013, kwa kutoa taswira kuwa *OSHA* imefanya asilimia 85.6% ya kazi zilizopangwa kufanyika mahala pa kazi, ni wazi kuwa Waziri alikuwa anaupotosha umma kuwa *OSHA* imefanikiwa kwenye kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, huku ukweli ukiwa kuwa Wizara imeshindwa kwa asilimia 76% kusajili mahali pa kazi nchini, hali ambayo inaonesha kuwa si kipaumbele cha Serikali hii ya CCM katika kujali usalama wa watu wake sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi inataka kujua ni hatua gani za kisheria ambazo asilimia 75 ya mahali pa kazi ambazo hazijasajiliwa zitachukuliwa kama ambavyo sheria inaelekeza kutoa adhabu? Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha kuwa kila mahali pa kazi nchini panasajiliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa inakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi milioni 600 zinahitajika kwa *OSHA* ili

kuweza kusajili sehemu zote za kazi nchini, je, Wizara imetenga kiasi gani kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua pia kama Wizara imefanya usimamizi na tathmini ya kaguzi zinazofanywa na *OSHA* na kama wamefanya tathmini ya shughuli za *OSHA*, ni vigezo vipi ambavyo vimetumika katika kupima na kusimamia utendaji wa *OSHA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji Bajeti 2012/2013 na Makadirio ya Mwaka 2013/2014; katika fungu 1001, utawala na rasilimali watu katika mwaka wa fedha 2012/2013 zilitengwa jumla ya sh. 2,780,306,000/=, aidha kwa mujibu wa randama ya Wizara ni kuwa jumla ya sh. 705,400,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya kulipia pango la ofisi ya Wizara, maji, umeme na simu na hii ni kwa mujibu wa randama ya Wizara, shughuli Namba *D-03-S07*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaona kuwa fedha hizi ni nyingi sana kutengwa kila mwaka kwa ajili ya kulipia pango la ofisi ya Wizara na ikizingatiwa kuwa ni Wizara ambayo inasimamia haki za wafanyakazi ambao kila leo wanalia kutokana na kiwango kidogo cha mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujua Wizara ina mpango gani wa kujenga ofisi zake ili iachane na mpango wa kulipia mamilioni ya walipa kodi kila mwaka kama pango na ofisi hizo zijengwe Dodoma kama ambavyo Serikali mara zote imekuwa ikisisitiza kuwa ofisi zake zitajengwa Dodoma kama sehemu ya maandalizi ya kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika fungu hilo hilo la 1001, Namba ya mradi *D-03-S08*, randama ya Wizara inaonesha kuwa jumla ya sh. 8,000,000/= zilitengwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa ajili ya gharama za safari za Waziri na Naibu Waziri kwenda Majimboni na hadi mwezi Mei, 2013,

jumla ya sh. 5,600,000/= zilikuwa zimetumika kwa ajili ya safari tatu za Majimboni kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka huu wa fedha Wizara imeomba kutengewa kiasi cha sh. 16,710,000 (randama ukurasa wa 21) kwa ajili ya kuwezesha safari nne za Majimboni kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, maana yake ni kuwa kila safari moja inatumia wastani wa shilingi milioni nne (4,000,000) hata kwa Naibu Waziri ambaye Jimbo lake lipo Ukonga, Dar es Salaam .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua kuhusiana na safari ya Waziri Jimboni kwani tunajua kuwa huyu ni Mbunge wa Viti Maalum na hana Jimbo, hiyo ziara alifanya kwenye Jimbo gani na fedha za mwaka huu anategemea kwenda kufanya ziara Jimbo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tunataka kujua fedha wanazolipwa kama posho ya mafuta na Bunge kwa ajili ya kufanya ziara Majimboni huwa wanazitumia kufanya nini wakati Wizarani nako wanajitengea fedha kwa ajili ya kwenda Majimboni? Ni kwa nini wao Mawaziri na Manaibu wawe wanalipwa mara mbilimbili fedha kwa ajili ya kazi moja? Pia ni mamlaka gani huwa inapanga na kuidhinisha viwango hivyo, au kila wizara inajipangia kutokana na wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Paresso.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji sita (6) kwenye Wizara hii. Sasa namwita Mheshimiwa Jenista J. Muhagama, ajiandae Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na ajiandae Mheshimiwa Felister A. Bura.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ambayo iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kumpongeza sana Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi nzuri ya kusimamia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno ya kutaka kumpakazia uongo na ukweli Rais, siyo maneno yenye tija kwa Taifa hili. Nasema siyo maneno yenye tija kwa sababu gani? Hamna baba yeyote wa familia anayeweza kutoka hadharani na kuzungumzia masuala ya familia yake kama hana uhakika na kile anachokisema. Kwa hiyo, leo tunapotaka Bunge eti limtathmini Rais kama amesema kweli ama amesema uongo, huu kwa kweli ni utovu pia wa nidhamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tumwache Mheshimiwa Rais aendelee kutenda kazi kwa kuzingatia *instruments* alizonazo na kwa ukweli ambao anaupata kwa kuzingatia kazi anazozifanya na usimamiaji wake wa Serikali yake anaoufanya. Ni nani leo hii anayekataa kazi nzuri iliyofanywa na Mifuko ya Hifadhi za Jamii katika nchi yetu? Watoto wa Tanzania hii leo wanafaidika sana kwa sababu ya uwezo wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda Malaysia, nchi ya Malaysia imepiga hatua kubwa sana kwenye maendeleo, lakini kilichowawezesha Malaysia kupiga hatua kubwa ni Mifuko ya Hifadhi za Jamii kuwekeza kwenye miradi mikubwa ya maendeleo katika nchi ile. Sasa leo sisi Mifuko hii tunaona akina Halima wanakaa kwenye Bunge hili limejengwa na Mifuko ya Hifadhi za Jamii, wadogo zake Halima wanasoma *UDOM*, Chuo Kikuu kilicho jengwa na Mifuko hii, halafu mtu hapa ndani anasimama na kusema kwamba hiyo ni kazi isiyokuwa na tija kwa Taifa letu, hapana!



Mheshimiwa Mwenyekiti, nakataa na naipongeza Mifuko pia naiomba isonge mbele ili iwakomboe Watanzania katika miradi hiyo yenye tija ambayo itaboresha huduma na hali ya Watanzania. Dkt. Dau pamba moto, simamia *NSSF*, songa mbele; Erio, songa mbele; Maingu, songa mbele; Sanga, songa mbele; Irene simama imara, simamia Mifuko hii isife kwani ndiyo kazi tuliyokupa kupitia Bunge hili. Msibabaike wala msitikisike, tupo imara tunawaunga mkono na tunaiona kazi mnayoifanya ya kukomboa Taifa la Tanzania, kazi kwenda mbele hakuna kulala kwani tunataka maendeleo kwenye nchi hii ambayo imekuwa nyuma kimaendeleo kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sioni kama lipo tatizo hapa, yote tunayashuhudia kwa macho yetu, hayo mengine kama yapo mambo ya ubadhirifu, kama yapo mambo ya kuchelewesha mafao, kama yapo mambo mengine yanayohusiana na Mifuko hii tutaendelea kuyafuatilia kuzingatia uadilifu na utaratibu wa usimamiaji wa Mifuko hii na Mdhimiti upo na ananisikia na atafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa Watanzania. Leo naomba niseme neno moja, naipongeza Wizara kwani inafanya kazi vizuri, lakini nadhani lipo tatizo mahali, ni lazima tutafute suluhu ya tatizo la ajira. Tunamshukuru Mungu nchi hii ameipa rasilimali nyingi na rasilimali zenye manufaa makubwa, leo kuna gesi, kesho tutapata mafuta na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema leo ni kwamba, Mheshimiwa Waziri na Serikali yetu tusibaki kufurahia uwekezaji mkubwa unaoingia katika nchi yetu bila kujipanga sawasawa. Uwekezaji katika nchi hii haukuanza jana wala juzi, lakini tatizo la ajira katika nchi hii limeendelea kuwepo kwa nini? Hapa ndipo pana tatizo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tukijiuliza hapa tunakwenda kuwekeza miradi 50 Mtwara tunajua miradi ile 50 inahitaji mafundi wa namna gani, inahitaji wataalam wa namna gani, mikataba tukayokwenda kusaini kwenye ile

miradi ya uwekezaji kabla hatujakubaliana uwekezaji huo tumeshajua Watanzania wetu au watoto wa Kitanzania 1200 ambao ni *graduates* wetu wamesoma nini na wanahitaji nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa ndiyo kuna shida na suala hili nimekuwa nikiliongea kila siku na hata Bwana Mipango nimekuwa nikimweleza na Mheshimiwa Wassira naomba anisikilize sana. Kabla mtu hajawekeza kwenye nchi hii atuambie atachukua Watanzania wangapi waliosoma, atachukua Watanzania wangapi wenye elimu ya kati, atachukua Watanzania wangapi ambao watakuwa ni vibarua katika uwekezaji wake na Wizara iendelee kutayarisha *database* iwajue watoto wetu wa Kitanzania walipo na wanahitaji nini ili waandae kwa kuwawezesha kupata hizo ajira, hapa ndipo tunapotakiwa kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifurahie uwekezaji bila kuandaa mazingira ya watoto wa Kitanzania na Watanzania kufaidika na uwekezaji huo kama hatutawatengenezea mazingira bora ya kujiajiri. Narudia kusema kwamba, uwekezaji umekuwepo na tatizo la ajira limekuwepo, ni lazima tutafakari tatizo ni nini? Tukilijua hilo tatizo, naomba Serikali kupitia Wizara zote zishirikiane, wapate majibu na uwekezaji huu uwe na manufaa kwa Watanzania kwa hali zote. Nashauri sana hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba ukitazama kwenye mfumo mzima wa ajira hapa nchini bado hatuwezi kukwepa jinsi hali ilivyo ngumu kwenye suala zima la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye pensheni kwa wazee. Hatuwezi kukimbia kuacha 33% ya wazee vilema au wenye ulemavu, 83% ya wazee wanaoishi vijijini na watoto milioni moja wanaendelea kulelewa na wazee wasiojiweza, halafu bado tunaendelea kusuasua kuanzisha pensheni kwa wazee, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu niombe Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi kama matamko haya

yalianza toka mwaka 2010, kikwazo ni nini? Hao wazee hawakuchangia kwenye mfumo rasmi, lakini hawa walichangia kwenye kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo wa nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunawataka wachangie kwenye urasmi gani zaidi ya kuchangia asilimia kubwa ya uchumi wa nchi hii ya Tanzania? Jamani tufanye maamuzi, tunalalamika watoto wa mitaani wanalelewa na hawa wazee ambao ni maskini waende wapi? Tunalalamika hali duni za maisha vijijini, ni kwa sababu wazee hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu hali za wafanyakazi; ni lazima tutazame hali za wafanyakazi wetu katika nchi yetu ya Tanzania. Wafanyakazi kwenye sekta binafsi wanapata shida sana, viwanda vinaajiri watu bila kufuata mikataba na bila kufuata Sheria za Ajira mpaka lini? Tuwasikilize hawa Watanzania wanalalamika kila siku, hebu mifumo yetu ya ajira iwasikilize hawa Watanzania na iwakoe, wanakuwa kama hawana mwenyewe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaangalia kwenye vyombo vya habari maeneo mengi, halafu tutazame suala la kuwaongezea posho wafanyakazi wa nchi hii kwa mfano, Walimu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, Manesi wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, Polisi hawana nyumba zinazoweza kustahili na wafanyakazi wengine wengi kwenye sekta mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ni sikivu na nakushukuru Mheshimiwa Waziri amesema ametoa tamko la kuongeza mishahara, hebu tuwasaidie wafanyakazi tusimtazame mfanyakazi kama yeye bali tutazame mchango wake na tija kwenye uchumi wa nchi ya Tanzania. Hayo ndiyo maeneo ambayo yatatuwezesha nchi yetu kupiga hatua za kimaendeleo kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana na namwomba Waziri kupitia kiti chako aendelee kukaza buti kuhakikisha migogoro ya wafanyakazi na yenyewe inazidi

kupungua. Hakuna haja katika Taifa la amani kama hili wafanyakazi kuendelea kuwa na migogoro ambayo inaweza kutatulika kwa wakati na ikawasaidia wafanyakazi na wananchi wa Tanzania kuendelea kuishi na kuchangia michango yao katika kuendeleza maisha na uchumi wa nchi yetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie suala la mwisho kwamba, kumekuwa na mgogoro mkubwa wa fao la kujitoa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri fanyeni haraka, tuleteeni sheria ambayo itakidhi matakwa ya Watanzania katika mfumo wa ajira uliopo sasa, sheria hiyo ikajibu kero na matatizo ya wafanyakazi wengi katika nchi hii ya Tanzania. Hatuna sisi mafao haya yanayomwezesha mfanyakazi ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nafikiri ujumbe umefika. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana na sasa namwita Mheshimiwa Mwaiposa na ajiandae Mheshimiwa Bura.

**MHE. EUGINE E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishukuru kupata nafasi kwa ajili ya kuchangia hoja hii, lakini niendeleo pia kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na changamoto kubwa ya ajira walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwenye kundi la wazee. Wazee ni hazina kubwa ya Taifa hili la Watanzania, ni wazee hawa ambao walipigania mpaka tukapata uhuru wa nchi hii kutoka kwa Wakoloni. Lakini ni wazee hawa hawa ambao walituzaa na wametutunza na wengine wamekuwa vijana na wengine watu wa makamo kama nilivyo mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni wazee hawa hawa ambao wameifikisha nchi hii ya Tanzania kiuchumi hapa ilipo. Kwa maana hiyo basi na maana nyingine nyingi ambazo sikuweza kuzitaja hapa, wazee ni watu wa kuenziwa, wazee ni watu wa kutunzwa na Serikali hii na wana haki ya kufanyiwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wazee ni kama milioni 2.1 katika nchi hii, lakini tumesikia kabisa kwamba 33% ya wazee katika kaya ni maskini, lakini ni wazee hawa ambao wameachiwa watoto yatima baada ya wazazi wao kufariki na wanawatunza. Lakini kwa kushindwa wazee wengine kuwatunza watoto hawa, basi watoto wengi wamekimbililia mijini kwa ajili ya kuombaomba fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee hawa wengi wao hawalipwi pensheni, wanaolipwa pensheni kwa utaratibu wa kawaida uliozoeleka hapa nchini ni wale waliokuwa wanafanya kazi katika sekta rasmi. Naishukuru sana Serikali kwamba ilikwisha kukubaliana na wazo la kuwapa pensheni wazee wote wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni wazo zuri na nawashukuru sana watendaji pamoja na Mheshimiwa Waziri, nimwombe sasa kwamba hilo sasa lianze kufanya kazi ili wazee hawa waweze kupata hizo fedha. Kama tunataka kupunguza asilimia kubwa ya umaskini katika nchi ya Tanzania kwanza tutoe kipaumbele kuwalipa wazee hawa pensheni kwa sababu kwa kufanya hivyo watawasaidia sana wale watoto ambao wanawatunza katika familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee walio wengi tumesikia kwamba, ni wagonjwa, 32% ya wazee ni walemavu. Ulemavu huu ni dhahiri kabisa kwamba umetokana na lishe duni na uwezo mdogo wa kiuchumi walionao. Naomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu, hebu kasaneni basi mwaka huu angalau wazee hawa waweze kujulikana wapo wapi, lakini kwa kipindi hiki kifupi kinachokuja miaka miwili hii basi waweze kupewa pensheni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *culture* ya Watanzania ni vibaya sana mzazi kuendelea kulalamika kwa sababu ya uwezo wa kiuchumi, hii inawezekana ikawa hata laana kwa nchi yetu, tuwaache wazee hawa wamalize umri wao au muda wao wa kuishi hapa duniani salama bila kuendelea kutulalamikia. Naomba sana na najua kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha nadhani suala hili atalitolea ufafanuzi kwamba Serikali imefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nije kwenye tatizo la ajira kwa ujumla. Sina kipingamizi cha kusema kwamba, ajira ni tatizo Tanzania lakini siyo Tanzania tu, dunia nzima kila mahali wanalalamika hakuna ajira, hata kwenye nchi zilizoendelea ndiyo sababu wanakimbilia huku kwa ajili ya kuja kutafuta ajira, lakini kwa Tanzania sasa tuna fursa nyingi ambazo zinaweza kutufanya tukaondokana na tatizo hili la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishauri Serikali kwamba, mambo haya ya ukosefu wa ajira yanachangiwa na mambo mawili makubwa. Upande mmoja ni upande wa Serikali, lakini upande mwingine ni upande wa wahusika hawa wanaotafuta ajira wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Serikali unahitajika uanze sasa kuendelea kuandaa mazingira mazuri yatakayowawezesha wahitimu mbalimbali kuweza kujijiri katika sekta binafsi. Ni vema tukaanza kutoa elimu sasa kwa wahitimu hawa kwamba, muda wa kupoteza kutembea na vyeti maofisini kutafuta kazi umepitwa na wakati, waanze kuandaa kutoka kwenye shule za msingi na kwenye vyuo vyote ili wahitimu wajue kabisa kwamba, wanapomaliza shule wanakwenda kujijiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ianze kufundisha sasa elimu ya ujasiriamali, ubunifu na mambo mengine kama jinsi ya kupata soko na mitaji, waanze kufundisha watoto kutoka darasa la saba na kwenye vyuo

vyote. Hii itawasaidia sana vijana wetu kwenye vyuo vyote na itawasaidia vijana wetu kutoku-*panic* na kutokuona kwamba hawana kazi ya kufanya watakapomaliza vyuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanaomaliza wanapoteza muda kwa kutaka kuajiriwa na sekta rasmi, sehemu ambayo sasa hakuna mlango mkubwa wa ajira na tatizo hili limechangiwa sana na jinsi ambavyo Watanzania tunakuwa kwa wingi, watu wanazaliwa kwa wingi lakini ajira zinabakia zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Serikali katika kusaidia upande huu wahakikishe kwamba, wanaandaa sasa mfumo mzuri katika mabengi yetu ili mabengi haya yaweze kuwa na utaratibu wa kuwakopesha kama ambavyo wameanza na *CRDB* pamoja na *SUA* kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye hotuba yake. Lakini iende zaidi ya hapo sasa kwa sababu huu ni mpango maalum, lakini wale ambao wapo wapo tu waweze kupata fursa ya kuingia benki na kukopa bila masharti magumu. Tukifanya hivyo, vijana wetu wengi watapata ajira na tutaondokana na tatizo hili la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie upande wa pili nikitoka kwenye Serikali, lipo tatizo la vijana wenyewe, vijana wetu wengi wa Tanzania hawataki kujijajiri lakini pia hawana sifa za kuajiriwa, wanaweza wakawa na sifa moja tu kwamba amesoma ana cheti lakini kuna sifa nyingine zaidi ya hapo kama kuwa mwaminifu katika kazi, kuwa *committed* katika kazi, kuwa *hardworking* katika kazi na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu jamani wakiajiriwa leo kwenye sekta binafsi hata kama ni huko kwenye Serikali, kesho anataka awe na nyumba nzuri na gari zuri na avae vizuri, hataki kusubiri. Kwa hiyo, wanakuwa siyo waaminifu na ndiyo sababu unakuta kwenye mashirika mengi na benki nyingi na taasisi za watu binafsi hata kwenye kazi za nyumbani wameshaanza kuajiri watu kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu watu hawa wanaonekana wako *committed* zaidi, lakini sisi Watanzania tuna *excuses* nyingi, leo mke wa mjomba kafiwa sijui wapi huko, anaomba *excuse* anataka kwenda kuzika, leo sijui anaumwa kidogo, hataki kuja kazini. Hapa sisi hatutafika, lazima wafanyakazi wa Tanzania wawe *committed*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waajiri wengine na hata hapa kuna Waheshimiwa wana mashirika yao binafsi au wana *NGOs* zao watakubaliana na mimi kuwa, unapomwajiri mtu unapoteza muda mrefu sana kufanya *follow up* badala ya kuendelea kufanya mambo mengine, wewe unamfuatilia nyuma tu karipoti saa ngapi, katoka saa ngapi, simu anaongea nayo masaa mengi. Hatuwezi kwenda hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anatumia masaa mengi kunywa chai, masaa mengi ni simu. Katika nchi nyingine hakuna kuongea na simu ofisini, simu hizi zinachukua muda mrefu sana, zinawaibia sana waajiri. Kwa hiyo, pamoja na malalamiko ya Serikali, lakini nitoe wito kwa vijana kwamba, wabadilike na wawe na zile sifa za ziada, yaani siyo cheti tu bali sifa nyingine za ziada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba niunge mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwaiposa. Sasa namwita Mheshimiwa Bura, ajiandae pia Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa moyo wangu wa dhati kwa kunipa nafasi ya kuchangia na nimshukuru Mungu wangu kwa kunipa nafasi na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe semina kwa Wabunge ambao hawajui namna Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanavyopata fedha kwa ajili ya kuwalipa wanachama wao.



Mwanachama anapoandikishwa uanachama, siyo kwamba zile fedha zake anazochangia ndizo atakazolipwa pale atakapoacha kazi au atakapostaafu. Mwanachama analipwa na riba ambayo inatokana na uwekezaji ambao Mifuko hii inaufanya kila mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko hii imefanya mambo makubwa sana na mwenye macho haambiwi tazama. Wanaobisha utaratibu huu waende Mwanza waone Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilivyobadilisha Mji wa Mwanza. Waje Dodoma waone Mifuko ya Hifadhi ya Jamii walivyobadilisha Mji wa Dodoma kwa kujenga Chuo Kikuu. Huu Ukumbi ambao baadhi ya Waheshimiwa Wabunge tunapinga uwekezaji katika Mifuko hii, ni Mifuko hiyo ndiyo imeujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kutafuna maneno naomba kabla wengine hawajazungumza wakafanye utafiti na kuuliza. Serikali iliishaingia mikataba na Mifuko hii, *UDOM* imeshanunuliwa na Serikali na iko mikononi mwake, siyo kwamba fedha za *UDOM* hazijarudishwa, fedha zimesharudishwa na *UDOM* iko mikononi mwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wakurugenzi na Bodi zao za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi nzuri wanazozifanya. Sasa hivi wanataka kujenga daraja la Kigamboni na wamefanya mambo mengi. Kama hawana fedha wasingaji-*commit* kujenga daraja la Kigamboni, Hospitali ya Apolo, barabara ya Chalinze – Dar es Salaam na kwa mambo mengi ambayo yametajwa na Waziri katika hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe ndugu zangu Dkt. Dau na wenzake hatuna wasiwasi na waendeleo kuchapa kazi. Pia wafanyakazi walioko katika Mifuko hii nawapongeza, maana wanafanya kazi nzuri ndiyo maana hakuna hata siku moja mfanyakazi amelalamika kwamba, hakulipwa mafao yake. Wafanyakazi wanalipwa mafao yao tena kwa riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawalipwi mafao bila riba na riba hiyo inatokana na uwekezaji ambao unafanywa na mifuko hii. Nawapongeza sana Wafanyakazi, Wakurugenzi na Bodi kwa kazi nzuri ambayo imeonekana. Hata mtu akibisha, mwenye macho haambiwi tazama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ningependa kusema ni kwamba, Watanzania asilimia 6.2 ndiyo ambao wako kwenye mpango wa hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, kitu ambacho tungeangalia ni kuona Watanzania wanaingiaje kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili waweze kulipwa pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ndilo jambo muhimu. Wazee wamelitumikia Taifa hili, lakini wapo ambao wamelitumikia Taifa hili kwa njia nyingine, hawana pensheni, wanahangaika katika vijiji vyao, mijini, hawana pensheni. Kati ya Watanzania milioni 44 ni asilimia 6.2 tu ndiyo wako kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali iangalie mpango mahususi wa kuhakikisha Watanzania na hasa wazee wanalipwa pensheni. Hata hivyo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inafanya kazi nzuri sana, Mtanzania unapofikia hatua sasa hujiwezi, mfanyakazi akifa, familia yake inalipwa pensheni na yeye mwenyewe analipwa pensheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la *General Tyre*, ambalo limezungumzwa katika hotuba mojawapo. Niiombe *NSSF* na Serikali waone namna ya kuwakabidhi *NSSF General Tyre* ili wafanye uwekezaji pale. Tuache mambo ya kutafuta nani afanye uwekezaji pale, *NSSF* waliotoa fedha wana uwezo, siyo kwamba hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walioko pale Arusha, vijana walioko kule kwa Mheshimiwa Lema watapata kazi. Tuiache *NSSF* iingie mkataba na Serikali ijenge na iendeleze Kiwanda cha *General Tyre*. Hakuna ubabaishaji pale, najua wanaweza, Dkt. Dau anaweza kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizingumzie tatizo la ajira. Kila Mtanzania anatakiwa kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi hii. Kila Mtanzania, aliyesoma na asiyesoma. Tunafanyaje ili kila Mtanzania ashiriki katika kujenga uchumi? Vijana waliosoma wanasubiri ajira, Serikali haina nafasi za kuajiri vijana wote waliotoka vyuo vikuu, waliomaliza kidato cha sita, kidato cha nne, darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina uwezo, lakini hata tukisema sekta binafsi iwachukue wote haiwezi kwa sababu wengi wako majumbani wanatembea na vyeti mikononi na hawana namna ya kupata ajira. Je, tumewaandaaje hawa wasomi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaandaaje kujitegemea hawa wanaomaliza kidato cha nne na cha sita, kwa sababu kila anayetembea na cheti chake mkononi, anasubiri ajira kutoka Serikalini? Wanasubiri kufanya kazi maofisini na Bodi ya Mikopo inawasubiri kurejesha mikopo na kila siku tunasema fedha haitoshi kuwapa vijana wote mikopo kwa ajili ya masomo ya elimu ya juu, lakini tufanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiwaandae hawa vijana tangu shule ya msingi au hata wanapofika sekondari? Wenzetu wa China mbona wamefika mbali, kila mtaa kuna viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya vijana? Hivi Serikali yetu haiwezi? *VETA* ipo inafanya kazi gani? *SIDO* ipo inafanya kazi gani? Kwa nini isitusaidie kuandaa elimu ya ujasiriamali kwa vijana wetu tangu wakiwa *primary school*, *secondary* na vyuo vikuu ili kijana anapomaliza elimu aone namna ya kuweza kujisaidia katika ujasiriamali au kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa, lakini tumewaandaaje hawa vijana katika kuanzisha vikundi? Ni lazima tuwaandae vijana. Kuna wengi wanaotafuta *consultation*, namna ya kushauriwa, lakini tunao vijana waliotoka vyuo vikuu hawana hata ofisi ya kuweza kukaa na kufanya ushauri kwa watu wanaotafuta ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaandae vijana waweze kuanzisha vikundi vidogo vidogo vya ujasiriamali na hata ofisi za ushauri wanaweza wakafanya vizuri, kwani Wachina wamewezaje kufika huko? Matokeo yake vijana wanaomaliza darasa la saba wamekuwa wavuta bangi mitaani. Ni lazima tuliangalie hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kuhusu wafanyakazi. Serikali imeamua kuwakopesha wafanyakazi fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na zingine zinajengwa na Serikali na wafanyakazi wanakopesha. Je, ni wafanyakazi wa ngazi zipi? Je, mfanyakazi anaweza kupata nyumba iliyojengwa na Serikali na akaweza kurudisha ule mkopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wanatozwa kodi mara mbili, anakatwa kodi kwenye mshahara wake, lakini pia anapojengewa nyumba na Serikali analipishwa VAT. Ie VAT ni kama kodi mara mbili kwa mfanyakazi. Serikali iangalie namna ya kuwasaidia wafanyakazi kujenga nyumba ambazo ni *affordable* kwao hasa wale wa ngazi za chini kwa sababu hawana namna. Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii inajenga nyumba kwa ajili ya kuwakopesha wanachama wao, lakini nyumba ya shilingi milioni 80 ni mfanyakazi gani wa ngazi ya chini anayeweza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la ajira kwa wageni. Ni aibu kukuta kwenye hoteli zetu za kitalii Dar es Salaam na Arusha, wapo wafanyakazi kutoka Kenya na maeneo mbalimbali wakati tuna Watanzania ambao wanaweza wakafanya kazi vizuri katika maeneo hayo. Hili suala litazamwe upya na Wizara na kuona namna ya kuwasaidia Watanzania ambao wanaweza kufanya kazi hizo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Bura kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Christowaja Mtinda, ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu wa leo.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia machache kwenye bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba, CHADEMA hapa tulipokaa hatupingi kabisa miradi inayoendelezwa na *NSSF*. Tuko pamoja na Mfuko wa Hifadhi wa *NSSF* kuendeleza miradi mikubwa katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Tunachopinga sisi ni ile tabia ya Serikali kuigeuza Mifuko ya Hifadhi kuwa *ATM* yao na hailipi madeni kwa wakati. Hilo ndiyo ambalo tunapinga kwa sababu hizo ni fedha za wanachama na miongoni mwao nikiwepo mimi na wanachama wengine hapa Wabunge wa CHADEMA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *UDOM* wanasoma wanafunzi wa kada zote, wanafunzi wa wazazi wa CHADEMA wako wengi pale *UDOM*. Kwa hiyo, hatupingi miradi hiyo, tunaiunga mkono kwa asilimia mia moja, lakini Serikali itimize wajibu wa kulipa fedha ambazo inakopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu hata ripoti ya Kamati imesisitiza. Katika ukurasa wa 11, Kamati inasema kwamba, licha ya Mfuko huu kutimiza wajibu wake kikamilifu, Serikali ambayo imekuwa ikitoa dhamana ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo imekuwa ikichelewa kuanza kulipa gharama za miradi mara inapokamilika na kukabidhiwa. Kamati inaishauri Serikali kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati muafaka. Hilo ndiyo tatizo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa mchango wangu hapo hapo kwenye *NSSF*. Pamoja na pongezi nyingi sana kwa *NSSF* kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini pia bado

kuna upungufu mkubwa. *NSSF* inatoa fao la matibabu, nilizungumza wakati wa semina iliyokuwa inaendeshwa na *SSRA*, narudia tena kusema kwamba, hili fao haliwafaidishi wanachama wake sawasawa. Ukikagua hesabu za *NSSF* utakuta kwamba, fedha nyingi za matibabu zinabaki kwenye Mifuko yao kwa sababu hazifanyi kazi sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano mdogo, mimi ni mwanachama tangu mwaka 1994 ilipokuwa *NPF* na nilihama na Mfuko mpaka ilipoanzishwa *NSSF*. Mimi ni mwanachama hai na mpaka sasa hivi ni mwanachama tena wa lazima, lakini fao hili la matibabu lina masharti magumu. Hatukatai hayo masharti, unachaguliwa hospitali ya kutibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba, niliugua nikiwa hapa Bungeni, nikatibiwa, lakini nikalipa fedha zangu. Bahati nzuri sana mwaka jana Kamati ya wakati huo *POAC* wakati inazungumza na *NSSF*, nikiwa Mjumbe, nilieleza hili suala na kwa nia njema uongozi wa *NSSF* walichukua risiti na mpaka leo sija rudishiwa hiyo fedha, iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mimi Mbunge ambaye nawakilisha wananchi na ambaye naweza kuzungumza hapa, hizo fedha sija rudishiwa mpaka leo, je, mwananchi wa kawaida ambaye ni mwanachama anafanywaje huko? Kwa kweli, hilo *NSSF* wajitahidi kujirekebisha katika utendaji wao. Katika fao la matibabu kuna urasimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii iko hata kwa wategemezi na watoto wetu. Watoto wetu hawakai mahali pamoja, ni wanafunzi wanasoma, leo wako Dar es Salaam, kesho Arusha na kesho kutwa wako Mwanza. Hawa watoto wakati wanasajiliwa kutibiwa pengine walikuwa Dar es Salaam, wakati wanaendelea na shule sasa wanahama kwenda labda Mwanza, watoto hawa bila kuwa na kadi wanapata usumbufu mkubwa sana. Mpaka faili lihame lifike Mwanza mtoto ameshapita umri wa kutibiwa. Hilo nalo *NSSF* ili angalie.

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. SLYVESTER MASELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anaongea sasa hivi anakuja kudai fedha kwenye Bunge, nadhani niombe kujua kama inaruhusiwa kweli, kuja kudai malipo yake Bungeni huku. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, bado niko hapo hapo *NSSF* kwa sababu tunaisifia sana. Ni lazima tuisifie, lakini *at the same time* tuipe *challenge* ili iweze kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* imeanzisha mradi wa kujenga nyumba kwa wanachama wake, hili nalirudia tena, imeanzisha mradi mkubwa sana na imekamilisha nyumba zake Mtoni Kijichi. Jana na juzi Wabunge walipigia kelele sana *National Housing* kwa shilingi milioni 60. Hicho ni cha mtoto, funga kazi ipo *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa mwanachama nimesema nilipata pia ofa ya kununua nyumba kwa mkopo. Nyumba ambayo nilichagua ilikuwa ni ya gharama ya shilingi milioni 103. Nilipokwenda kufanyiwa ukokotozi wa kwamba, nitalipa shilingi ngapi kwa huu mkopo ambao ni wa miaka 20, niliambiwa kwa mwezi utakatwa shilingi 1,600,000/= na kama una-*qualify* umri wako kwa mfano, utakatwa kwa miaka 20 na mpaka uinunue hiyo nyumba utakuwa umelipa shilingi milioni 384 kwa miaka 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mtumishi wa aina gani na Tanzania ipi ambaye anaweza kukatwa shilingi 1,600,000/= kwenye mshahara na akabakiza za kula na familia yake? *NSSF* haijatendea haki wanachama. Hizi fedha ni zetu sisi

tunaochangia pamoja na uwekezaji wao waliangalie hilo suala. Kwa kweli wamepitiliza na siyo sawa sawa kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nyumba ili uweze kulipa kwa miaka 20 ni mpaka uwe na miaka 35. Ni kijana gani wa Kitanzania huyo wa miaka 35 ambaye ana mshahara mkubwa akatwe hii shilingi 1,600,00/= na abakiziwe nyingine? Anafanya kazi wapi na *scale* gani ya mshahara? Hilo NSSF waliangalie kwani kwa kweli linawatia aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi, imezungumzwa hapa *OSHA*. Tunajua *OSHA* inakagua usalama mahali pa kazi kwa waajiri wanaolipa fedha. Pia katika nchi yetu tunatambua kuna watumishi wengine ambao wanajiajiri wenyewe kwenye sehemu zao, kwa mfano, mashambani, migodini na kadhalika. Hawa watu wako katika hatari kubwa ya kuumia mashambani na kwenye migodi. Je, *OSHA* inakagua mazingira hayo? Kama haikagui hawa wafanyakazi wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumzia pia kuhusu Mfuko wa Fidia wa Wafanyakazi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha atusaidie huu Mfuko ni lini utaanza? Huu Mfuko ni wa muhimu sana kwa ajili ya fidia za wafanyakazi. Wengi hawajui waende wapi, wanafidiwa kiasi gani na wengi wanaumia kila siku. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijahitimisha, tumeambiwa pia miradi ambayo imeanza kujengwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Naipongeza Serikali kwa kutumia *NSSF* kujenga miradi hiyo. Hata hivyo, kuna mradi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ambao ulikuwa uanze mwaka jana, fedha zilishatengwa shilingi bilioni 4.2 na zilishatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi ninavyozungumza huu mradi haujaanza na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajausema, sijui umerukwa au ni vipi.



Nafikiri Mbunge wa Jimbo atataka kujua huo mradi umefikia wapi. Tusije tukaleta hisia zingine kwamba, kwa sababu Jimbo lile ni la Mpinzani, hatutaki kufika huko, ila tunaomba tuelezwe mradi huo umeishia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hii barabara ya Dar es Salaam - Chalinze bado haijaanza kujengwa. Pamoja na kwamba, tumesikia imeanza kujengwa, bado haijaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie hapa ili na wengine waendeleo. Naomba Waziri atakapokuwa anahitimisha atusaidie kwa sababu Mfuko huu uko chini yake na hii miradi tunajua anajua, atusaidie ni jinsi gani wananchi wa kawaida hasa wanachama watafaidika na hii Mifuko? Tusiendeleo kuona majengo makubwa wakati sisi wanachama tunaochangia tunaishia kwenye nyumba za nyasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo sawasawa na tunaomba Serikali itoe tamko zuri ili wanachama tusiendeleo kujitoa. Mimi natoa rai kwa wanachama wote wa *NSSF*, wasijitoe kwa sababu wakijitoe imekula kwetu. *NSSF* haiumii, itakuwa imekula kwetu kwa sababu mafao ya uzeeni utakuwa hauna wa kukusaidia, ila tu marekebicho kama hayo yaendeleo kufanyika na wananchi waendeleo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge wachangiaji wetu wa mchana wamekwisha. Tumbakiwa na wachangiaji wawili ambao tukifika Saa 11 panapo uhai tutaanza na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli na tutamalizia na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, baada ya hapo mtoa hoja na Naibu wake watahitimisha hoja yao.

Mheshimiwa Iddi Azzan, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge

kwamba, leo asubuhi timu ya Bunge *Sports Club* ilicheza mechi ya kirafiki kwa mpira wa miguu na pete na timu ya *combine* ya shule za Serikali za Wilaya ya Kongwa na Chamwino. Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo:-

Mpira wa miguu Bunge *Sports Club*, goli moja na *combine* ya UMISETA goli moja. Nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Joshua Nassari ambaye kwa kweli alifunga penati kwa kichwa. Nampongeza sana.

Kwenye mpira wa pete Bunge *Sports Club* magoli 21 na *combine* ya UMISETA ya Chamwino magoli matano. Mchezaji bora wa mchezo huu alikuwa ni Rachel Mashishanga. Michezo hii ni kwa ajili ya maandalizi ya mechi ya Wabunge na *combine* ya Waandishi wa Habari na *NSSF*, ambayo itafanyika siku ya Jumamosi tarehe 1 Juni, 2013 katika uwanja wa Jamhuri Dodoma. Naomba kuwasilisha.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilibungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tuna wachangiaji wetu wawili waliobakia, tunaanza na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli ajiandae Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie machache katika Wizara hii. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya thabiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kuchangia hotuba hii katika kipengele cha tatizo la ajira nchini kwetu. Sio siri na kila mtu anafahamu kwamba ukosefu wa ajira limekuwa tatizo kubwa sana katika nchi yetu. Takwimu zinaonesha

kwamba mpaka kufikia mwaka 2011 Tanzania ilikuwa na nguvukazi watu takriban 22,152,320, lakini katika nguvu kazi hii watu wanaofanya kazi kwenye sekta rasmi walikuwa ni kama idadi ya watu 1,300,000 na kidogo, lakini watu ambao walikuwa wanafanya kazi kwenye sekta isiyokuwa rasmi ilifikia 2,500, 327. Lakini wakulima, wafugaji na wavuvi walikuwa wanafikia takribani 15,918,762.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hapa kama kweli Serikali ya CCM ingekuwa haina dhamira ya dhati ya kutoa tatizo la ajira katika nchi ilikuwa imeshapata mwanga, kwamba sasa kumbe sehemu pekee ambayo ni kimbilio ambapo Watanzania wengi wangeweza kupata ajira ni sehemu katika sekta ya kilimo. Kama kweli ingewekeza vizuri katika kilimo kwa sababu tunajua kwamba zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanaishi vijijini, tungeweza kuondokana na tatizo hili la ajira na vijana wetu wasingeweza kukimbilia mijini na kutangatanga kama tunavyoona hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 13 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameelezea hapa habari ya ukuzaji wa ajira nchini. Katika ukurasa wa 14 Mheshimiwa Waziri anasema kwamba naomba ninukuu: "Kwamba Wizara imeandaa programu ya Kitaifa ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu mwaka 2013/2014 mpaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri amekwenda mbali zaidi akasema kwamba Wizara itashirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Benki ya CRDB kuandaa programu ya ajira kwa wahitimu wa elimu ya juu ambapo Serikali itawadhamini miradi ya kilimo takribani 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na maneno mazuri yaliyokuwa kwenye makaratasi kwenda kwenye hotuba zetu, tukumbuke kwamba tulianzisha Mifuko ya Vijana (YDF) kwenye Halmashauri zetu za Wilaya. Tukasema Mifuko ile itaweza kutoa mitaji kwa vijana wetu ambao wanakaa

vijijini, vijana wetu ambao wapo kwenye miji yetu ili sasa waweze kujajiri kwa kuwa ajira katika Serikali, ajira rasmi sio rahisi kupatikana isipokuwa ajira ipo kwenye sekta isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpaka sasa hivi Mheshimiwa Waziri atuambie hivi ule Mfuko wa Kukuza Ajira kwa Vijana ambao ulikuwa kwenye Halmashauri zetu mpaka sasa umefanikiwa kwa kiwango gani kwa sababu bado tatizo lipo palepale na bado tunaletewa maneno mazuri ya kupendezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakumbuka tuliletewa MKURABITA tukasema ni Mkakati wa Kurasimisha Rasimali na Biashara za Watanzania wanyonge kwamba, sasa kumbe basi wafanyabiashara watapata fursa ya kurasimishiwa ili wapate mikopo waweze kufanya biashara, wapate kukopesheka waendeleo kujajiri. Mpaka leo tujiulize je, mpaka sasa hivi MKURABITA umerasimisha hizo biashara za hao wanyonge wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana napata hofu sasa itakuwa kila siku tunakuja na mipango mizuri ya kwenye kitabu tunaambiwa, leo tuna programu ya kilimo ekari 200. Nataka Mheshimiwa Waziri aniambie amejipanga vipi kuhakikisha kwamba, hiki ambacho amekiandika kwenye kitabu chake kinafanya kazi, kwa sababu tumeona hapa tumeshapitisha Azimio la Vijana mwaka jana kutokana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tuna mkakati hapa tunasema kuna ekari 200, Mheshimiwa Waziri amekuja nayo, atuambie amejipanga vipi, ni kweli hii programu itafanikiwa ili hawa vijana wapate ajira au ndiyo hizo kila siku hadithi za mama kuku, kwamba watoto wake watanyonya, lakini hawanyonyi mpaka wanazeeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanafahamu na wameshachoka sasa kila siku kusikia mipango mizuri

ambayo haitekelezeki. Namwomba Mheshimiwa Waziri aje kutueleza hapa, ili haya maneno ambayo ameyaweka hapa, hiyo miradi 200 ya kilimo ambayo itatekelezwa ndani ya mwaka 2013/2014, amejipanga vipi na kwa kiasi gani na kama kweli atafanikiwa itakuwa imetatua tatizo la ajira kwa vijana wetu hasa ambao ni wahitimu kutoka elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nielezee kidogo mambo ya Mifuko ya Hifadhi (*NSSF*), kuna Makampuni ya kizalendo yanaajiri vijana wetu, Watanzania wenzetu. Imekuwa ni kawaida wanaingizwa kwenye Mifuko ya Hifadhi, wanachangia fedha, lakini sasa ikitokea mtumishi wakati mwingine ametolewa kazini, inakuwa balaa kwa yeye kupata ile barua kutoka kwa mwajiri wake ili sasa aende akapate ile haki yake kule *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana na nina mifano hai ya watumishi ambao waliokuwa wanafanya kazi kwenye Kampuni ya *Mohammed Enterprise*. Watu wamefanya kazi kwa muda mrefu, lakini wamekuja kutolewa kazini, kupata ile barua ili waende kupata mafao yao imekuwa ni danadana, wakienda kwenye Idara ya kusimamia watumishi katika Wizara ya Kazi ni danadana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu wanakata tamaa, wananyanyasika katika nchi yao, wanakata tamaa kwa sababu Serikali ambayo ingekuwa iwasimamie haiwasimamii, hawapati yale mafao yao na lengo la mafao yawasaidie baada ya kazi, lakini sasa inaonekana mtu ameweka chake, ametumia nguvu yake, lakini hapati chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili la watu wanaofanya kazi katika Makampuni binafsi, wananyanyasika sana. Tunaona kwenye vyombo vya habari, watu wanafanya kazi katika Viwanda vya Korosho na kadhalika, wananyanyasika mazingira ya kazi magumu, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kama kweli Serikali inataka ipunguze tatizo la ajira, lazima ikubali kuangalia kwenye sekta ambazo nazitaja tena; kilimo, usafiri na utalii; hizi sekta zingeajiri vijana wetu wengi sana. Nataka nitoe mfano mchache tu, sasa hivi naona kuna balaa pale ukiangalia stendi ya Ubungo, vijana na *DABOA* na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wale wengine wamefanya zaidi ya miaka 14 kwenye Kampuni zile za mabasi na sehemu nyingine, lakini hawakuweka hata hifadhi yoyote na hawakuajiriwa takribani miaka 14. Lakini sasa hivi wale vijana pale *DABOA* wamekuja na kitu kipya vijana wanatolewa. Sisi hatukatai utaratibu mzuri kazini, lakini kuna baadhi ya Makampuni kama wale akina *New Force* na wengine wamesema wao hawawezi kufanya kazi na watu wawili tu.

Mheshimiwa Waziri vijana wanaotolewa pale Ubungo waende wapi? Tunakubali kutoa matatizo ya usumbufu lakini utaratibu ufanyike vizuri, naona Serikali hii ina lengo la kuturudisha kule kwenye vibaka. Vijana ambao wanafanya kazi pale Ubungo wale ambao wametoka pale ambao wameshafanya kazi kwa muda mrefu wanakwenda kuwa vibaka, hakuna kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie Makampuni ambayo yapo tayari, watu wanasema watachukua wafanyakazi zaidi ya wawili, lakini kuna watu ambao wamekuwa ni warasimu, wanasema wachukue wafanyakazi wawili tu ili kuwabana vijana wa Kitanzania. Naomba tuangalie maslahi ya vijana wetu ili wasiende kurudi tena kwenye wizi, wasiende kurudi tena kwenye vitendo vya hovy huko mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kidogo vijana, tumeona kwenye hotuba wamesifia kuna vijana ambao walikuwa kwenye Kambi kwa mfano, kama Pwani. Nakubali vijana walipelekwa kwenye Kambi wakafundishwa kupata ufundi stadi wa matofali ya kisasa. Lakini baada ya pale vijana wamekwenda wapi, wamepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusiwe mabingwa sana wa ku-*initiate* mipango ambayo tunaijadili kwamba ina mafanikio, lakini Mheshimiwa Waziri afuatilie vijana wale ambao walikwenda kwenye vikundi wakapewa ujuzi wameishia wapi. Ahadi waliahidiwa nyingi, waliahidiwa watapata mitaji, wengine mpaka leo hiyo mitaji hawajaipata. Vijana wamekwenda kuwa *scattered*. Kwangu Rufiji kule ninao, vijana wametoka kwenye Kambi Kibaha kwenye kufyatua matofali, waliahidiwa kwamba watapata mitaji na kadhalika, wamerudi wapo vijjini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pale pale nasisitiza tena, tuwe tunapanga mipango mizuri ambayo mnaileta, lakini sasa iwe mipango ambayo ina tija. Sasa wale vijana wamekaa takribani miezi mitatu, wametoka wamekwenda mtaani hawana kazi yoyote. Hivi kweli Serikali ina dhamira ya kuwakomboa vijana? Kwa hiyo, kama kweli mnajipanga kufanya hiyo mipango yenu ambayo mmeileta ambayo sisi tunaikubali, basi muwe mna ufuatiliaji kuona je, baada ya kufanya kitu hiki mmeipata mafanikio ya kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Kuruthum. Sasa basi nitamwita Mheshimiwa Rweikiza ndio mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naipongeza Serikali na nampongeza Mheshimiwa Waziri Gaudentia Kabaka na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla ya kuchangia hoja yangu niseme kwamba pale asubuhi au pale mchana saa saba kasoro niliwasikiliza wachangiaji waliomalizia malizia pale wa CHADEMA, nikafurahia sana niliposikia anasema kwamba hawapingi kazi inayofanywa na Mifuko ya Jamii *NSSF, PPF, LAPF* na mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikashangaa kusikia Mbunge anasema Serikali inafanya Mifuko hii *ATM*. Sasa nikasema huyu hapingi au anapinga maana yake kuifanya *ATM* maana yake nini, haina haja kuwa na akili nyingi kuona kwamba huyu ni Mpinzani, anapinga kazi za Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Mifuko inafanya kazi nzuri sana inapojenga vyo kama vya Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*), Hospitali ya Apollo ambaye inatakiwa kujengwa, daraja la Kigamboni, Ukumbi kama huu ni maendeleo ya Taifa hili, ni maendeleo ya wananchi wote na CHADEMA wakiwemo. Ukienda pale *UDOM* wamejaa wanafunzi wa vyama vyote na CHADEMA wakiwemo, sasa wanaifanya *ATM* namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maneno ya mitaani tu, ya vichochoroni kwamba wanaifanya *ATM*, ni ya Upinzani ambao hauna maana. Hii mifuko Serikali haichukui fedha pale kuja kujenga ukumbi kama huu au *UDOM* bila ya kurudisha, inakopa. Inakopa na inarudisha tena kwa faida, kuna na riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifuko ina wataalam waliobobea kwa mambo ya fedha na utawala, wanakopa wanalipa asilimia 17, ni kwa faida ya wale wanachama wao na Serikali inakopa. Hata wewe ukiwa na fedha yako unakwenda unanunua *Treasury Bonds* ile inaitwa Hati Fungani, unapata faida na ndivyo inavyofanywa kwenye Mifuko hii. Kwa hiyo, Mifuko inakwenda vizuri na Serikali inafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye mchango wangu niliokusudia na nianze na suala la ajira. Tuna tatizo la ajira, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine. Nasema hivi, tatizo hili tuna ufumbuzi wa aina mbili ninavyoona wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuliwahi kusema au niliwahi kusema kwamba, hawa vijana ambao hawana ajira, kwa kweli hata kama pangukuwa na ajira, ni vigumu



kuwaajiri, hawaajiriki, hawana ujuzi, hawana stadi zinazotakiwa, kuwe na vyo vya ufundi vya kutosha. Vijana kutoka kidato cha nne au cha sita haitoshi peke yake kuajirika, hawawezi kuajiriwa, hawawezi kujiajiri tujenge vyo vingi vya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mpango wa kujenga kila Wilaya Chuo cha Ufundi, sijui umeishia wapi? Mpango huo ukifanikiwa vijana wengi watapata ajira, wataajiriwa na sehemu mbalimbali, viwanda, Makampuni na kadhalika. Lakini pia watajiajiri, watafungua karakana zao, viwanda vya kujenga, kuchomea vyuma, magari na ufundi mbalimbali, tutapata ajira nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu la pili naliona kwenye kilimo. Mwaka jana nilichangia nikasema kwamba, tuwekeze kwenye kilimo kwa njia tofauti za sasa hivi. Tuna mipango mizuri kwenye kilimo, lakini tuingeze jitihada. Nikasema tuna maeneo mengi sana katika nchi hii ambayo ni mazuri sana, lakini hayalimwi, maeneo yenye rutuba, kuna mito, kuna maji, tuna mabonde, maziwa, lakini hayalimwi na hakuna wa kulima pale. Sasa Serikali ifanye mkakati maalum, ipeleke makundi ya vijana kwenye Kambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakisema vijana mia moja, mia moja, waende kwenye Kambi kama elfu moja katika sehemu mbalimbali kwa mfano, Kilosa kule kuna ardhi nzuri sana. Wakienda Mvomero, Tunduru, Sumbawanga, Kigoma na kila mahali, kuna ardhi nzuri na ina maji ya kutosha, waende vijana kwenye Makambi wawekewe Makambi kule. Serikali iwawezeshe kwa mkopo, iwawekee nyumba za haraka haraka kama ni *full suit* za mabati au maturubai kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapewe trekta kwa mkopo, wapewe *power tiller* zile, wapewe mbegu, pembejeo na madawa mbalimbali ili walime kisasa. Vijana mia moja wakipata trekta moja watalipa hata eka 3,000 kwa msimu na baada ya miezi mitatu tu, watavuna kama ni mahindi au

maharage mengi sana. Baada ya mwaka mmoja au miwili watalipa lile deni na tutakuwa na mazao mengi sana, tutakuwa na ajira za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wote wataajiriwa na hawatarudi mjini maana yake kule kutakuwa na maisha mazuri. Watajenga nyumba nzuri na hawalimi kwa jembe la mkono ambalo ni mateso, watalima kwa trekta na *power tiller*, wataweka mbolea, wataweka madawa, watapata mavuno mengi sana na tutauza mpaka nje. Kwa hiyo, kwa kutafuta ajira kwa vijana tutapata neema nyingi sana. Tutauza mazao nje, tutakuwa na chakula kingi, tutajikomboa katika shida mbalimbali na itakuwa ni ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama nilivyosema, hii itakuwa ni ufumbuzi mkubwa sana wa moja kwa moja. Hii mipango mingine inakuwa *indirect*, sio ya moja kwa moja, haitoi matunda ya moja kwa moja, lakini huu ni wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana mia moja wakienda kule kwenye Kambi na wakalima, ni ajira ya moja kwa moja, watakaa kule, baada ya muda utakuwa mji mdogo au makazi mazuri watakuwa na umeme hata wa majenereta, wataweka huduma za maji, kutakuwa na shule na zahanati na itakuwa ni maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa njia hiyo tutapata ajira nyingi sana. Kwa hiyo, nasema huu ndio ufumbuzi kujenga Vyuo vya Ufundi na kuwekeza kwenye kilimo kwa njia hii ambayo nimeipendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia ajira hii ina pande mbili, leo tunasema kwamba kuna vijana wengi au watu wengi ambao hawana ajira. Lakini kuna maeneo ambayo hayana wafanyakazi wa kuajiriwa, kwa mfano, Walimu, shule zetu hazina Walimu. Ukienda Uganda na Kenya kuna Walimu wengi hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fungueni milango waje wafundishe hapa watusaidie vijana wetu wasome, ndio

upande wa pili wa ajira ninaousema huo. Waje wafundishe vijana, nina shule kule Bukoba, zina Walimu wawili, sekondari za wanafunzi 400 au 500, lakini kuna Walimu watatu. Ukivuka mpaka pale Uganda Walimu wengi sana, hawana ajira kule, waje watusaidie kufundisha vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuhusu pensheni ya wazee wastaafu. Kila nikienda Jimboni wazee waliostaafu walikuwa watumishi wa Serikali, walikuwa Wanajeshi katika sehemu mbalimbali, walikuwa wanapata pensheni kidogo sana na wanachelewa. Niombe hii iangaliwe sana, pensheni zao ziwahi na ziongezwe. Mtu anapata sh. 40,000/= kwa mwezi, haiwezi kukidhi mahitaji ya maisha ya sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima kwa kweli hili jambo lifanywe haraka iwezekanavyo ili wazee hawa wapate maisha yanayostahili. Lakini vile vile na wengine ambao hawakuajiriwa walikuwa kwenye sekta za kilimo wamejajiri wenyewe, wamekuwa wazee, sasa mchango wao sio kama ilivyokuwa zamani walivyokuwa vijana, wapate na wenyewe wapate pensheni ya Serikali. Mpango uandaliwe kusudi na hao wazee wapate kipato cha kuaminika kwenye maisha yao yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie hapo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge orodha ya wachangiaji imekwisha, isipokuwa leo asubuhi wakati tunatambulisha wageni wa Mheshimiwa Waziri, tuliwatambulisha wageni wa Wizara yake na Watendaji Wakuu wa Mifuko, lakini Waziri vile vile ameambatana na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi.

Kwa heshima yote napenda kuwatambua ndani ya Bunge hili Viongozi wa Chama cha Waajiri (*ATE*), Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi *TUCTA, CWT, TUICO, TEWUTA, THTU, FIBUCA, TPAWU, TUGHE, TUPSE* na *TAFIMU*. Karibuni sana Bungeni na naomba mtoe ushirikiano mzuri kwa Mheshimiwa Waziri.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi ya awali kabisa, kuwapongeza Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Gaudentia M. Kabaka (Mb), Naibu Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Dkt. Makongoro Milton Mhanga (Mb), Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF* - Alhaji Ramadhani Dau pamoja na wote Watendaji walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri, yenye lengo la kuwaendeleza Watanzania husasan vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatia moyo kuona Serikali inajua ahadi yake ya kujenga Vyuo vya *VETA* kila Wilaya ili vijana wengi waweze kujiunga kupata ufundi wa aina mbalimbali kwa lengo la kujiajiri. Napenda kuishauri Serikali ni vyema itoe *tender* hii kwa Shirika la *NSSF* ambalo lina fedha na Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF* na Mtendaji mwenye moyo wa kuisaidia Serikali, kutekeleza ahadi zake kwa lengo kuwapatia maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujivunie kazi nzuri iliyofanywa na *NSSF* kusaidia Serikali kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*). Nina uhakika Mkurugenzi wa *NSSF* akipewa kazi ya kujenga *VETA*, muda mfupi tu Wilaya ambazo hazina Vyuo vya *VETA* vitapatikana. Naomba majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuliomba Shirika la *NSSF* kujenga jengo la ghorofa Singida ili kusaidia Taasisi mbalimbali za Serikali na ambazo siyo za Serikali kupata ofisi za kufanyia kazi, kwani Singida tuna shida ya majengo ya ofisi. Kwa kuwa Mkurugenzi wa *NSSF*, Alhaji Ramadhani Dau yupo, ningefurahi kupata majibu endapo upo uwezekano wa kujenga jengo Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiomba Serikali kuliomba Shirika la *NSSF* kuwapa wafanyakazi mikopo ya kujenga nyumba ili wanapofikia kustaafu, wasikose mahali pa kuishi na fedha hizo wawe wanakatwa kwenye mishahara yao. Nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ombi kuwa, Ofisi ya Singida ambayo inatumika kwa Idara mbili tofauti, ipanuliwe ili watendaji wapate nafasi ya kutosha kufanya kazi zao vizuri hata wasuluhisha migogoro wanapata shida, vilevile wanao upungufu wa watumishi. Nasubiri majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli usiopingika kuwa, uchochezi kwa wafanyakazi upo tena ni wa kisiasa. Vilevile ukweli wa madai ya fedha mbalimbali ya wafanyakazi yapo. Hivyo, naishauri Serikali isipuuze madai hayo, mara zote yachunguzwe inapobainika ni halali walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naishauri Serikali isipuuze madai hayo, mara zote yachunguzwe, inapobainika ni halali walipwe. Mfano halisi ni madai ya walimu. Vilevile Serikali iache tabia ya kulimbikiza madai, wafanyakazi wawe wanalipwa kwa wakati. Ninaomba maelezo walimu wasikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la vijana kuzurura mitaani, pamoja na juhudi ya Serikali kutoa ajira bado vijana wengi wanapomaliza mafunzo kwenye Vyuho wanabaki bila kazi. Hivyo, ninaomba kuwe na utaratibu wa kutoa ajira mara wamalizapo mafunzo ya Vyuho. Vijana kukaa mitaani tunatengeneza kundi la wazururaji, walevi na wezi, hatimaye majambazi. Ninaomba maelezo ya Serikali tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni ukweli usiopingika kuwa, Shirika la *NSSF* chini ya Uongozi wa Alhaji Ramadhan Dau, linafanya kazi nzuri. Ninaomba pongezi zitolewe mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwatia moyo na wengine waige tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mungu na moja kwa moja nichangie kwa kuanza na swala la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunajua kuwa, Taifa letu linakabiliwa na changamoto kubwa ya ajira hasa kwa vijana na tunatambua wazi kuwa ajira zinapopatikana, vijana hujikwamua katika dimbwi la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke pia ajira zisizo na faida ni sumu ya kuua nguvu kazi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewatelekeza Wananchi wanaoajiriwa kama vibarua kwenye kazi za msimu kama kazi za barabara, migodini na vibarua wa mashambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibarua huwa wananyanyasika sana, kuna wakati wanaumia, wanapigwa, wanadhulumiwa na mwisho wanapewa ujira mdogo. Hii yote ni kwa kuwa wamekosa mtetezi na Serikali yao imewatelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri mwenye dhamana atueleze ni lini Wananchi wa Tanzania wanaoajiriwa kama vibarua wataacha kunyanyaswa na wageni wanaowaajiri; na ni lini Serikali itatoa rasmi kiwango halisi ambacho kibarua anatakiwa kulipwa kwa siku? Na je, ni muda wa saa ngapi ambao kibarua huyo anatakiwa kufanya kazi kwa siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi iko hivi; vibarua wengi hufanya kazi kwa saa 12 na zaidi na hulipwa Sh. 2500, 3000 au 3500 kwa siku. Huu ni unyanyasaji na uonevu mkubwa. Naiomba Serikali iliangalie upya na kulitolea tamko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira zisizo rasmi kama za wafanyakazi wa nyumbani, maarufu kama *house boy or house girls*; watu hawa wamekuwa wakinyanyasika na kukosa msaada. Naiomba Serikali iitambue ajira hii kuwa kama ajira nyingine na Serikali iandae utaratibu wa mwajiri na mwajiriwa kupewa kibali na mkataba kwa Afisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imeepusha manyanyaso na dhuluma wanazopata waajiriwa wa ndani. Pia wakati umefika sasa wa Serikali kutangaza mshahara halisi unaotakiwa kulipwa mfanyakazi wa nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa watoto wadogo chini ya umri wa miaka 18. Suala hili linaharibu kabisa Taifa la kesho, kwani mpaka sasa haitoleweki ni kwa nini Serikali inashindwa kupiga marufuku ajira za watoto wadogo na kuwachukulia hatua wale wote wanaowatumikisha watoto hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira hizo hazina faida kwa watoto hao na zinawaharibia maisha. Namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapofanya majumuisho, alieleze Bunge lako Tukufu ni hatua gani Serikali itachukua kwa watoto wadogo wanaoonekana barabarani wakifanya biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea ajira na mkakati wa kukuza ajira, tunazigusa imani na matazamio ya vijana wasio na ajira. Lakini itakuwa ni ndoto kama Serikali inawapa moyo Wananchi hasa vijana kuwa wanatengenezewa ajira wakati hakuna mikakati inayoenda kuzaa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira inapaswa kukaa na Wizara ya Elimu ili kuweka mikakati ya Elimu Maalum ya Ajira, kwani kama mitaala ya ufundi, ujasiriamali na sanaa vitafundishwa mashuleni, wanafunzi watamaliza wakiwa na Elimu Maalum ya Ufundi ya kuwawezesha kujajiri na kukabiliana na soko la ajira. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imetatua tatizo la vijana kuwa tegemezi kwa ajira za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Kazi wa Mwaka 2012/2013, yanaonesha kwamba, Wizara ya Kazi na Ajira

haikuzingatia kikamilifu mchango wangu wa maandishi, niliutoa tarehe 7 Agosti, 2012 na haikutoa majibu aumrejesho wa utekelezaji kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ikiendelea, itapoteza umaana wa michango tunayotoa; hivyo, Wizara izingatie michango hii, ikiwa ni sehemu ya matatizo ya Katiba ya Nchi, Ibara ya 63(2) na 63(3). Hivyo, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2013/2014, Wizara ya Kazi na Ajira inipatie majibu juu ya hatua zilizochukuliwa kwa kurejea mchango wangu wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo itachangia utekelezaji mzima wa viwango vya kazi, usawa na kazi staha na nafasi za ajira za kutosheleza kwa kutoa na kusimamia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo tajwa. Mchango huo unapatikana katika Taarifa Rasmi (*Hansard*) ya Mkutano wa Nane, Kikao cha Arobaini na Mbili, tarehe 7 Agosti, 2012, ukurasa wa 160 mpaka 163.

Mosi, Wakala Usalama wa Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), kufanya ukaguzi katika viwanda ndani ya Jimbo la Ubungo hususan vya kufua chuma (*Steel Mill*) eneo la Mabibo.

Pili, Wakala wa Huduma za Ajira (*TaESA*), kuweka mfumo wa kuwaunganisha watafuta kazi katika Jiji la Dar es Salaam na fursa za ajira katika zabuni na kandarasi za mikataba mikubwa, ujenzi na huduma.

Tatu, Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kuhusiha Mbunge wa eneo husika na wadau wengine, juu ya ubia wa ujenzi wa Hospitali ya Apollo kuwa na uelewa na ushirikiano kuanzia hatua za awali za mradi. Pia, mrejesho kuhusu ufumbuzi wa mgogoro eneo la ujenzi wa Jengo la Maadili Dar es Salaam.

Nne, Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) kuingiza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na vitega uchumi vilivyo chini ya Halmashauri tajwa vya Shirika la Maendeleo Dar es Salaam



(DDC), Shirika la Usafiri Dar es Salam (UDA), Machinga Complex na Shirika la kupatiwa huduma ya ushauri wa mafunzo kutoka taasisi hiyo.

Tano, pamoja na kukamilisha kwa utafiti juu ya vima vipya vya mishahara katika Sekta 12, Serikali itoe maelezo ya kutozingatiwa kwa vima vilivyotangazwa katika miaka iliyopita. Mathalani, katika Kiwanda cha Nguo cha Urafiki na Hoteli ya Blue Pearl.

Sita, kutekelza ahadi ya Serikali ya toka mwaka 2011 ya kukamilisha mfumo wa utoaji wa pensheni kwa Wazee wote.

Saba, Wizara kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni na Wizara ya Viwanda na Biashara, kutekeleza ahadi ya kutengwa kwa eneo la wazalishaji wa viwanda vidogo vidogo ili kuchangia katika kuongeza ajira katika eneo la sasa la viwanda vilivyobinafsishwa na kudidimia. Serikali iliahidi Bungeni kuwa, Waraka ungepelekwa kwa Baraza la Mawaziri mwaka 2012. Hata hivyo, mpaka sasa hakuna majibu wala utekelezaji.

Nane, kupata ufumbuzi wa kudumu na endelevu juu ya mgogoro kuhusu gao la kujitoa (*Withdrawal Benefit*) kwa maslahi ya pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira katika utekelezaji wa bajeti na majumuisho ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2013/2014, izingatie Taarifa iliyowasilishwa na Kamati husika ya Bunge na Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ambayo nayaunga mkono. Wizara ikizingatia Taarifa hiyo na Maoni hayo, aya kwa aya, itachangia katika uhakika wa kuwepo kwa mahusiano mazuri, yenye kuleta tija, ufanisi na ya usawa mahali pa kazi na upatikanaji wa nafasi za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Kazi na Ajira ndiyo yenye dhamana juu ya uhibitaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ni muhimu ikatoa majibu kuhusu uendelevu

wa Mifuko yote na madai ya matumizi mabaya ya fedha za wafanyakazi katika Miradi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Wizara na Mamlaka ya Udhhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), itoe majibu kwa kulinganisha baina ya ukaguzi uliofanywa na Mkaguzi wa Serikali (CAG), kwa kurejea Ripoti ya tarehe 30 Juni, 2010 na ya ukaguzi wa mwaka 2011/2012, iliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais tarehe 28 Machi, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara na Mamlaka kwa pamoja, watoe majibu juu ya mkakati wa kutekeleza matakwa ya Katiba ya Nchi, Mikataba ya Kimataifa na Sera ya Taifa ya Jamii ya kuweka Mfumo wa Hifadhi ya Jamii na Pensheni kwa wote. Serikali itumie sehemu ya mapato toka rasilimali na maliasili, ikiwemo madini na gesi asilia kwenye Mifuko ya Hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira iwasilishe Bungeni, Programu ya Ajira kwa Vijana Nchini 2013/2014 - 2015/2016 ili iwekewe mfumo wa usimamizi wa Kibunge kwa kuzingatia Katiba ya Nchi, Ibara ya 63(2) na 63(3) na kutengewa rasilimali za kutosha kufanikisha utekelezaji wake. Aidha, wakati wa kuwasilisha Programu hiyo, Wizara ya Kazi na Ajira, iwasilishe pia taarifa ya utekelezaji wa sheria zenye kuchangia kuongezeka kwa ajira na mapendekezo yanayohitajika kuboresha mfumo mzima, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira, ihamasishe benki zingine ziige mfano wa *CRDB*, zishirikiane na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (*UDSM*), kwa wahitimu wa fani zenye kuchangia uzalishaji na ajira. Aidha, uratibu wa Wizara wa uhuishaji wa masuala ya ukuzaji ajira katika mipango ya maendeleo inayotekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam uhusishe Wabunge wa maeneo husika. Uratibu wa uhuishaji wa masuala ya ajira usiwe katika mipango ya Serikali pekee, bali ufanyike pia katika majadiliano ya mikataba mikubwa ya uvunaji na uendelezaji wa rasilimali pamoja na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa kazi, huduma za ukaguzi, migogoro ya wafanyakazi na masilahi ya wafanyakazi ni maeneo ambayo yanapaswa kushughulikiwa kwa karibu zaidi na Wizara ya Kazi na Ajira. Wizara ya Fedha inapaswa kuongeza fedha katika Wizara hii katika Idara na Taasisi zinazoshughulikia masuala hayo. Hii iende sambamba na kutenga fedha kwa ajili ya tathmini ya nguvukazi (*Labour Force Survey*), kufanyika katika mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Wizara ikishirikiana na Ofisi ya Taifa na Takwimu (*NBS*), ikiendelea na tathmini, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*), iandae na kuwasilisha taarifa Bungeni juu ya hali ya migogoro; Wizara ishirikiane na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), ifanye hivyo kuhusu mazingira ya kazi ili Bunge liishauri na kuisimamia Serikali vizuri zaidi.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pangezi kwa wote walio katika Wizara, kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuondokane na tatizo la ajira ni kutoa elimu ya kuwawezesha wahitimu wote kuwa tayari kujitegemea au kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwalipa pensheni watu ambao hawakuchangia fedha katika Mfuko wowote ni mzigo kwa Serikali. Jambo hili litazamwe kwa umakini sana, siyo kusukumwa na hisia za watu wasiofanya utafiti na kulazimisha mambo yaweze kufanyika ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa ambalo lengo la muda mrefu ni kufika kuwalipa pensheni watu wote, siyo busara wala hekima kuja na wazo la kuwaruhusu watu kuondoa fedha zao katika Mifuko kabla hawajafikia umri wa kustaafu. Je, iwapo hawatakufa kabla ya miaka yao kufikia 60 wataishi vipi; watatibiwa vipi?

Je, iwapo watafariki mapema huku wakiwa wamechukua fedha zao, familia zao zitaishi vipi? Watoto watasoma vipi?

Ushauri wangu, Kamati iliandika na kuja na majibu ya kuruhusu fao la kujitoa bila kujua athari zake au bila utafiti. Badala yake, itafutwe njia nyingine ya kuwaangalia watu waliodaiwa kufanya kazi katika mazingira hatarishi bila kuathiri mafao au pension ya watumishi hao siku za uzee wao. Siyo kweli kuwa kila aliye mtumishi katika migodi atakufa au ataumwa mapema kuliko watumishi wengine, vinginevyo walipaswa kuja na *data* (takwimu) katika hotuba siyo porojo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufikirie vizuri na kwa muda mrefu bila papara, tunaweza kuja na njia mbadala na kamwe siyo kuruhusu watu kujitoa.

**MHE. UMMY ALLY MWALIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri Gaudentia Kabaka na Naibu Waziri Dkt. Makongoro Mahanga, kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango ya Nchi kuhusu viwango vya kazi, usawa na kazi za staha na ukuzaji wa ajira nchini. Hata hivyo, ningependa kupata ufafanuzi au maelezo ya Waziri juu ya hoja ifuatayo:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya vitendo vya baadhi ya waajiri kufukuza kazi wanawake wajawazito? Ni mikakati gani ipo ya kulinda haki za wanawake wajawazito?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004, kifungu cha 7(4)(j); kinakataza ubaguzi sehemu za kazi na katika ajira kwa misingi ya ujauzito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwepo kwa Sheria hii, bado wanawake wengi hasa wasichana wanaoingia katika ajira, wamekuwa wakinyimwa kazi au kufukuzwa kazi kutokana na kuwa wajawazito. Hali hii licha ya kuwanyima wanawake haki ya kufanya kazi, kwa kiasi kikubwa, inarudisha nyuma jitihada za wanawake kupambana na umaskini.

Hivyo, ningependa kujua je, Wizara ina mikakati gani mahususi ya kuhakikisha Sheria inayolinda wanawake wajawazito inatekelezwa?

Je, Wizara inatoa kauli gani juu ya baadhi ya waajiri hasa katika sekta binafsi wanaowafukuza kazi wanawake kutokana na ujauzito?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipatiwe majibu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira hapa nchini ni changamoto kubwa kwa vijana wetu kadiri miaka inavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa ajira Serikalini ni finyu mno na tegemeo kubwa la ajira ni kutokana na sekta binafsi. Ili sekta hii ya watu binafsi iweze kuajiri Watanzania wengi, inabidi ziwepo Sheria na Kanuni za Kulinda Ajira za Vijana hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoonekana hapa nchini hivi sasa, kazi ambazo zingalipaswa kufanywa na wazawa, hivi sasa zinafanywa na wageni, kiasi ambacho kinasababisha Wananchi kuendelea kukosa ajira ambazo walipaswa wazipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini vipo viwanda vya aina mbalimbali ambavyo hutoa ajira kwa Wananchi mbalimbali. Katika viwanda hivyo zimo nafasi za kitaalam ambazo zingalipaswa zifanywe na Watanzania, lakini baadhi yake zinafanywa na wageni kutoka nje ya nchi. Hili siyo zuri, ipo haja ya Serikali kuwalinda wataalamu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kubwa hapa nchini ni dhahiri itatokana na kilimo kwa wakati huu. Bado vijana hawajaandaliwa kufanya kilimo, badala yake inavyoonekana vijana wengi wako katika biashara ya uchuuzi (Machinga). Kutokana na hali hiyo, ipo haja ya Serikali kuwa na mikakati maalum ili kuwawezesha vijana ambao watapendelea waingie kwenye kilimo, basi wafanye hivyo.

Ninashauri kuanzishwe makundi (*brigade*) ya vijana, wapewe ardhi na wawezeshwe kufanya kilimo katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira nyingine inapatikana kwenye uchimbaji wa madini. Nchi yetu katika sehemu mbalimbali kumegundulika uwepo wa dhahabu. Serikali kwa makusudi, ipange utaratibu utakaowawezesha wachimbaji wadogo wadogo kupata maeneo na vifaa, japo kwa njia ya mkopo ili waweze kuchimba hiyo dhahabu. Kama tutakuwa na utaratibu makini, basi vijana wengi wanaweza wakapata ajira kutokana na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa kuna mkanganyiko wa mshahara wa kima cha chini katika sekta binafsi. Je, ni lini kima cha chini katika sekta binafsi kitapangwa na kueleweka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa Hotuba nzuri, inayoeleweka, ila la msingi yapaswa kutekelezwa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kusoma kwenye Hotuba suala la ajira kwa watu wenye ulemavu, ikiwa ni jitihada ya Serikali kutoa haki sawa kwa wote katika suala la ajira. Hata hivyo, nataka ufafanuzi wa waajiri hao ni nani ili wenye ulemavu waweze kuomba kazi kwao kwa vile wamepata elimu hiyo ya utambuzi wa haki na fursa za ajira kwa walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa imekuwa vigumu kwa wenye ulemavu hata waliosoma vizuri kupata ajira rasmi Serikalini, ni vyema Serikali ikaweka mfumo maalum kwa wenye ulemavu wanaokidhi vigezo vya ajira husika. Kwa upande wa waajiri binafsi, yafaa wapewe motisha ili kuwavutia kuajiri watu wenye ulemavu wanaodhaniwa kuwa hawatoi tija iwapo wanaajiri. Dhana hii siyo kweli kwa vile

kuna mfano wa kampuni ya kutengeneza vifaa vya ngozi Arusha, ambayo imeajiri wenye ulemavu wengi na kampuni inatoa faida kubwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kima cha chini cha mshahara; sawa Serikali inatoa maelekezo mazuri tu kwa waajiri husika, lakini waajiri walio wengi hasa viwandani, wanaendelea kutolipa mishahara halali kwa wafanyakazi kwa kisingizio kuwa wamepata hasara. Je, Serikali inahakiki vipi kuhusu waajiri kama hao wanaowadhulumu wafanyakazi wao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama kazini linapaswa kuzingatwa kwa vile bado waajiri walio wengi hawajali kuhakikisha kuwa wafanyakazi wao wana mazingira salama ya kufanyia kazi. Kwa msingi huo, *OSHA* inapaswa kuongeza kasi ya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya kazi hasa viwandani kwani huko ndiko Wananchi wetu wanakoteswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa kuratibu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini na hata kuelimisha Umma, lakini nashauri *formula* ya kukokotoa mafao, ioanishwe kwenye Mifuko yote tofauti na ilivyo sasa. Yaelekea tofauti hizo husababisha tofauti za malipo ya mafao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi, nakubaliana na hoja za Kamati ya Kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchangia katika hoja hii, ambayo ni muhimu sana katika Taifa letu. Tuna nguvu kazi ya kutosha katika nchi yetu, takribani watu 22,152,320, hizi zote ni nguvukazi, lakini hazitumiki ipasavyo, kwani nguvukazi kubwa ipo katika kilimo na ufugaji, takribani nguvukazi 15,919,000. Hii ni nguvukazi ya

kutosha, lakini kwa kuwa haina mitaji ya kutosha, imekuwa ikifanya kazi kwa ugumu mkubwa, kilimo cha kizamani na mifugo kuwa ya kuchunga na kufuga kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sasa nguvukazi hii ikaangaliwa kwa ukaribu kwa upande wa mitaji ya pembejeo, masoko na utaalumu wa kilimo kwa wakulima, jinsi gani ya kufuga kwa kunenepesha mifugo, kutoa pembejeo ya dawa pia majosho. Kwa wafugaji kama tutafanya haya tutaokoa nguvukazi hiyo ya (15,919), milioni 15,919 kujikwamua na maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvukazi inayofuatia ni ajira isiyo rasmi, Machinga, wauza mboga na kadhalika. Nguvukazi hii ni muhimu lakini Serikali haiwatengei maeneo rafiki ambayo yanafikika kwa urahisi waweze kujipatia riziki waweze kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Matokeo yake, katika miji mikubwa na majiji, Mgambo wamekuwa tatizo kubwa, kuwanyang'anya bidhaa zao na kuzipeleka kusikojulikana. Huu ni uonezi na ni unyang'anyi wa kimachomacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea MKURABITA. Kama Mpango huu ungetekelezeka ni wazi watu wangepesheka na kuweza kufanya ujasiriamali wao, kukabiliana na ajira binafsi na hata kuweza kuajiri wenzao. Naiomba Serikali sasa iangalie eneo hili na kulitilia nguvu ili kupata ajira za uhakika na kupunguza wazururaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na vijana wengi ambao ni wavivu wa kutosha au niseme uvivu uliokithiri. Hivi kweli kijana mwenye nguvu asubuhi anaamka na kwenda kucheza *pool*/halafu kijana huyo anasema maisha magumu, huu ni ujinga na upumbavu wa kutosha. Ni wajibu wa Serikali sasa kuwachukulia hatua watu wanaofungua baa asubuhi na kuruhusu vijana kucheza *pool*. Pia vijana hawa ni vyema wakikutwa wanacheza ikawa bakora tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgambo ambao wanawasumbua akina mama wanaouza biashara ndogo



ndogo, wakawatandike vijana wanaocheza *pool*/asubuhi au askari polisi au hata Jeshi la wananchi ili kukomesha tabia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa tunaowaita makampuni binafsi ambayo yanawaajiri watu kufanya kazi katika makampuni yao, huwakata wafanyakazi katika mishahara yao fedha ya hifadhi ya jamii, lakini mfanyakazi anapoachishwa kazi, hapewi barua ya kulipwa mafao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi usio na haya, mtu anakatwa na kupelekwa kwenye mfuko lakini akifukuzwa hapewi barua ya kuchukua mafao yake; mfano, Kampuni ya *Mohamed Enterprises* huo ndiyo mtindo wao. Ukienda ofisi za kazi, dawati lake linakuwa ni danadana, kama si kupokea rushwa wafanyakazi wa dawati hili basi wanaogopa majina makubwa ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mchukue hatua kwa makampuni haya. Ahsante.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W.*), kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ina jukumu kubwa na muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu, kwani kazi ni kipimo cha utu na maendeleo ya nchi yoyote hayapatikani bila ya watu wake kufanya kazi. Na si kufanya kazi tu, lakini ziwe kazi zenye staha na mafao mazuri ili kujenga ustawi bora wa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana ni tatizo linaloendelea kukua kwa kasi kubwa. Serikali kwa ujumla wake na kwa kupitia Wizara hii, zinapaswa kulisimamia vizuri, usawa na haki. Bila ya kuwa na mkakati endelevu wa Serikali kutoa dira ya ajira kwa vijana, Taifa litakuwa butu kwani litakosa uzalishaji unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapaswa kuweka mkakati wa kuwawezesha vijana kujajiri katika sekta za uzalishaji mali, kilimo, uvuvi, ufugaji na ujasiriamali katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali iboreshe mishahara na mafao ya wafanyakazi wa sekta zote. Hii itaongeza ufanisi na kuongeza tija kwa sekta nyingine pia kama kilimo, kwani soko la mazao litaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi Serikali ina upofu wa kiasi gani hata ikawa haioni na hata pale inapooni, hushindwa kuchukua hatua kwa wageni wasiokuwa na sifa za kuajiriwa nchini kwa mujibu wa Sheria za Kazi wanamiminika nchini na kuajiriwa kila siku?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ugoigoi huu wa Watendaji wa Serikali kwa wageni hawa umepelekea Wananchi wetu wengi, hasa vijana, kukosa ajira hali ya kuwa wana sifa na uwezo wa kufanya kazi hizo! Je, Serikali ina kauli gani ya kukomesha ajira za wageni zisizoruhusiwa na sheria? Tusipoziba ufa leo, tutajenga ukuta na kuna hatari ya kushindwa kuajenga!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kuwa bado inajitahidi kufanya vizuri mpaka sasa, lakini napata wasiwasi na wingi wake! Kwa nini Mifuko hii inaongezeka siku hadi siku? Wengi wa Mifuko hii nini manufaa yake? Nionavyo mimi ni kugombania wafanyakazi wachache waliopo na kusababisha mgongano wa kimasilahi kwa Mifuko yenyewe (*conflict of interest*).

Kwa nini Mifuko hii isiunganishwe ikawa miwili tu au mitatu ili kupata Mifuko yenye nguvu na uelewano na itakayoleta tija bora zaidi kwa Taifa letu? Inawezekana, timiza wajibu wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania, Tanzania na watu wake!

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, pamoja na Wataalam, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ziandae mpango (*Polytechnics*), zitakazofundisha vijana wote baada ya "O Level/kama elimu ya ufundi lazima kwa kuwapa vijana stadi za kuwasaidia kujajiri katika sekta rasmi na isiyu rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya wafanyakazi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii igeuzwe kuwa hisa (*Shares*) na washirikishwe katika usimamizi na uendeshaji wa Mifuko hii. Kwa njia hii, *purchasing power* ya wafanyakazi itaendelea kukua na kustahimili *inflation*.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri yeye na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ni lini mradi wa Mchikichini utanza kujengwa chini ya usimamizi wa *NSSF*? Mradi huu umechukua muda mrefu sana, wananchi wataka kujua kinachoendelea. Naomba majibu wakati wa majumuisho.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, ili *TAESA* wafanye kazi nzuri wanahitaji pesa za kutosha. Je, kwa mwaka 2013 Wizara imetenga shilingi ngapi kwa ajili ya *TAESA*?

Mheshimiwa Spika, je ni lini ujenzi wa mradi wa Mchikichini chini ya usimamizi wa *NSSF* utanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii *NSSF*, *PPF* na *LAPF*, *PSPF* na msimamizi wa Mifuko hiyo *SSRA*.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ajira mbaya kwa watoto ni changamoto kubwa inayoendelea hapa nchini kwa muda mrefu. Watoto wanaojiriwa katika mashamba ya maua Wilayani Meru – Arusha wanapata athari mbaya ambazo hata wao wenyewe hawana habari. Inaaminika kwamba madawa yanayotumika *ku-preserve/* kuhifadhi maua yasiharibike huleta madhara katika uzazi, kuna uwezekano wa kutoweza kuzaa pindi watakapokuwa watu wazima.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mashamba hayo ya maua hayatoi vitendea kazi vya kujikinga na athari itokanayo na dawa ya kuhifadhi maua. Mamlaka husika isikae kimya, wenye mashamba wakaguliwe na udhibiti ufanyike ili kukomesha ajira kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, watoto wa kike wanafanya kazi katika mashamba ya maua Wilayani Arumeru, wametoa ushuhuda wa athari mbaya inayowapata katika afya zao. Baadhi yao wamesema kwamba, dawa zinazotumika kuhifadhi maua yasiharibike, husababisha mzunguko wao wa kila mwezi wa wanawake usikome na hivyo kuendelea bila kukoma kwa miezi mingi.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo mengi yanayotokea katika kuwaajiri watoto walio chini ya umri wa kuajiriwa, wengi hushindwa wamwelezee nani na wengine huogopa kusema kwa kudhaniwa watapoteza ajira. Hata hivyo, Mamlaka husika inatakiwa kufuatilia suala hilo ili kupata ufumbuzi na kuwaokoa watoto wetu na ajira mbaya kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 15 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, inaelezea kwamba kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, mradi wa “Kazi nje nje” unaotekelezwa na Shirika la kazi Duniani (*ILO*) umewapatia mafunzo ya ujasiriamali vijana 5,338 katika Mikoa 15 hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya vijana wasio na ajira inaongezeka siku hadi siku. Vijana 5,338 waliopatiwa mafunzo hayo ya ujasiriamali ni ndogo sana ukilinganisha na uhitaji uliopo kati ya vijana. Je, kuna mpango gani wa kupanua mafunzo hayo kwa vijana wengi zaidi ili kupunguza changamoto zilizopo za ukosefu wa ajira kwa vijana hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi hasa wafanyakazi wanaoweka akiba katika Mifuko ya Jamii kama vile *NSSF*, hawana uelewa kuhusu miradi mikubwa inayofanywa kwa kutumia fedha zao za akiba. Wengine wanadhani Mifuko ya Jamii kama vile *NSSF* wanafanya biashara/uwekezaji kwa kutumia fedha zao, jambo ambalo wao wanapohitaji fedha zao walizoziweka akiba kwa muda mrefu, wanapostaafu hupigwa danadana na kupata usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mamlaka husika itoe ushirikiano kwa wananchi/wafanyakazi wanaoweka akiba zao mfano *NSSF*, *PPF* na kadhalika kuhusu miradi inayofanywa kwa fedha zao. Pia wastaafu wasipate usumbufu pale wanapohitaji fedha zao. Aidha, riba wanayoipata baada ya kuweka akiba kwa muda mrefu ni ndogo mno ukilinganisha na faida ambayo Mifuko inatengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Watanzania wanapenda akiba wanazoweka katika Mifuko ya Jamii ziwanaufaishe katika kukabiliana na ugumu wa maisha uliopo badala ya kuwaongezea kero hasa pale wanapohitaji fedha zao baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, usalama kazini ni mojawapo ya hitaji muhimu kwa maslahi ya wafanyakazi. Waajiri wengi wa sekta binafsi wameshindwa kutengeneza mazingira rafiki na salama kwa wafanyakazi wa viwanda vyao. Kuna baadhi ya viwanda mfano vya nondo, bati, misumari na vyuma vyenye ncha kali ambavyo wafanyakazi hawapewi *protective gears* na waajiri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *OSHA* iwezeshe kwa kupewa vitendea kazi na kutengewa fungu la kutosha ili waweze kudhibiti hali hiyo ya mazingira ya hatari ya mahali pa kazi kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuhakikisha usalama upo mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ihakikishe kwamba Vyama vya Wafanyakazi vinaundwa na vipo katika maeneo mengi yanayotoa ajira na hasa katika sekta binafsi. Hiyo itasaidia sana kujenga tija katika kazi. Waajiri wengi kwa kukosa utu, wanazuia uanzishwaji wa Vyama vya Wafanyakazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi ufanyike ili kubaini makampuni yasiyoruhusu uanzishwaji wa Vyama vya Wafanyakazi na hatua zinazostahili zitumike. Hii itasaidia sana wafanyakazi wanaogandamizwa na kunyanyasika mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, kazi na uwiano wa kisheria katika maeneo mbalimbali hauko sawa. Mfano katika Wilaya ya Serengeti, Hifadhi ya Taifa uwiano uliopo ni kandamizi kwa vile kati ya watumishi 106 waliopo ni asilimia 14 badala ya asilimi 75 kama mwongozo unavyoelekeza ndio wanatoka Serengeti. Je, Wizara ina mpango gani kuondoa hali iliyojaa uonevu kwa wananchi na hasa vijana wa Wilaya ya Serengeti?

Mheshimiwa Spika, kuhusu pensheni ya wasaafu ni kidogo sana, kwa nini haipandishwi na pia kwa nini haiongezeki kadri mishahara inavyopandishwa?

Mheshimiwa Spika, majumba makubwa (maghorofa) yanayojengwa kutokana na fedha za wamachama wakiwemo wastaafu wa Mifuko mbalimbali, inawasaidiaje wastaafu na watumishi kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, je, hali ya kutokuwa na ajira, *unemployment rate level* ni kiasi gani? Serikali ina mpango gani wa kupunguza kiwango hiki na ni kwa nini kuwango hicho kinazidi kuongezeka?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *Social Support System* kwa makundi mbalimbali nchini wakiwemo wazee, wastaafu, wasio na kazi, walemavu na kadhalika katika mfumo mmoja?

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwako **Mheshimiwa Spika** na Bunge kwa kupata fursa ya kutoa maoni, kero na ushauri wangu kwa Serikali kupitia Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa ajira imekuwa shida sana hasa kwa vijana na hii ni kwa kuwa wengi tumekuwa walalamikaji kuliko watoaji wa suluhisho. Kazi zipo ila ajira hakuna. Hii inatokana na watu wengi kutoa tafsiri finyu ya ajira, wengi wanajua ajira ni kupewa kazi na mtu au shirika au kampuni na kupewa ujira baada ya kufanya kazi kwa kipindi cha makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza sasa Wizara iweke kitengo maalum chenye wataalam watakaoshirikiana na Wizara nyingine kama ile ya Viwanda na Biashara ili kuhamasisha na kuelimisha juu ya kujajiri na kupunguza lawama kwa Serikali na jamii kuwa hakuna ajira.

Mheshimiwa Spika, hata kilimo cha bustani ni kujajiri na ni ajira, tatizo ni pale ambapo hata aliye shambani naye anataka kuajiriwa kiwandani au kwenye shirika au kampuni. Hii inatokana na ukweli kwamba bado tafsiri ya ajira hajafanyika na kutoa elimu ya kutosha kwa raia wengi hasa vijana waliopo mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Viwanda na Biashara inatoa mikopo na elimu kwa wajasiriamali wadogo na usindikaji basi ni vizuri sasa kukawepo na ushirikiano wa moja kwa moja na Wizara ya

Kazi na Ajira siyo tu kwa kupata takwimu ila kuanisha aina ya watu na ajira za kujijiri na pia semina na mitaala mashuleni iwe yenye uwezo wa kufundishia na kujijiri na kutoa ajira kwa wengine. Wanafunzi wajifunze stadi za kazi ili wanapohitimu hata kama ni elimu ya msingi wawe na uwezo wa kujijiri na kuzalisha mali. Kama hili litatiliwa mkazo basi nina uhakika kabisa lawama za ukosefu wa ajira zitapungua kwa kipindi kifupi sana.

Mheshimiwa Spika, sina hakika kama Wizara ya Kazi na Ajira inazo takwimu za ajira zilizotokana na vijana wanaotoa huduma ya bodaboda na bajaji, ikiwemo mafundi wa vyombo hivi, wauzaji wa vipuri na wanaofaidika na ajira ya bodaboda. Ni vigumu kwa hali ya kawaida kutoa takwimu hiyo sasa hivi ila ni rahisi sana kwa kipindi kijacho cha bajeti kwa kushirikisha Wizara ya Fedha, Idara ya Forodha kutoa takwimu ya usajili wa vyombo hivi na idadi ya wanaolipa kodi kwa ajili ya bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana Wizara ikaonekana kama haijafanya sana kazi kama takwimu hizi hazitasomwa kwa umma, ni vema sasa Serikali ikawa na kawaida ya kutoa takwimu za ajira mpya kila robo mwaka ili kusaidia kuhabarisha umma ni kwa namna gani kumekuwa na ongezeko la ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pensheni kwa wazee, nina uhakika kabisa suala hili lipo mezani kwa Mheshimiwa Waziri ila bado kumekuwa na sintofahamu kama Serikali imeridhia au la na jambo la kwanza kabisa la utekelezaji wa jambo hili ni kuchukua hatua ya sensa kwa wazee na kuainisha umri wa wanufaika wa pensheni na utaratibu wa malipo kwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua zipo changamoto nyingi kwenye jambo hili ila ni muda wa utekelezaji mbali na changamoto hizo kuwepo. Nategemea kupata majibu yenye kukidhi haja na yenye matumaini kwa wazee wetu



waliotumikia Taifa letu wakati wakiwa na nguvu. Hata kama siyo mwaka huu wa fedha kuambiwa utekelezaji basi tuambiwe ni lini utekelezaji utafanyika.

Mheshimiwa Spika, kama nitapata fursa basi pia nitachangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nielekeze mchango wangu moja kwa moja kuhusiana na *OSHA*. Kwa mujibu wa ripoti ya *OSHA* ya mwaka 2011 inayo wakaguzi 50 tu wanaotakiwa kuhudumia sehemu za kazi elfu ishirini zilizosajiliwa. Napenda Mheshimiwa Waziri alielezee Bunge lako, katika mwaka huu wa fedha Wizara imejipanga kuajiri wakaguzi wangapi wa Afya na Usalama Kazini?

Mheshimiwa Spika, katika robo ya kwanza mwaka 2012/2013, *OSHA* iliweza kukagua sehemu za kazi elfu kumi na tano, katika robo ya pili walikagua wafanyakazi elfu kumi na katika robo ya tatu wafanyakazi elfu kumi, walau kuna ongezeko la ukaguzi wa afya na usalama kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua *OSHA* imejipangaje na kufanya kaguzi katika migodi mbalimbali nchini na katika viwanda vikubwa vya kufua vyuma? Huko kuna matatizo makubwa, wengine wanafanyishwa kazi bila ya vifaa vya kujikinga.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iweke mkakati maalum wa kukagua migodi na sehemu nyingine, iongeze watumishi wa kufanya kaguzi kwani tunajua mgodi kama wa Bulyankhulu, Geita na North Mara kila mmoja wanafikisha idadi ya si chini ya watumishi 1,200 hivyo kitendo cha kutuma wakaguzi sita kwa mgodi mmoja tu ni idadi ndogo maana hapo unakuwa ni wastani wa Daktari mmoja kwa watumishi 200 wa mgodi? Naishauri Wizara iongeze idadi hii ya Madaktari kama kweli tunataka ufanisi na kuboresha afya za wafanyakazi wetu nchini.

Mheshimiwa Spika, *OSHA* tumeona imejikita zaidi kwenye sekta rasmi, ni wakati mwafaka sasa itanue kutoa huduma na kaguzi katika sekta isiyo rasmi ambayo ina changamoto nyingi zinazowakabili wafanyakazi na inaajiri watumishi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, baadhi ya Watanzania wako nyuma katika soko la ajira na hata wale ambao wanapata ajira ni wavivu. Wenzetu Kenya wapo makini katika sekta ya ajira na hata katika kutafuta ajira. Leo hii ukienda Marekani soko la ajira la Lugha ya Kiswahili limechukuliwa na Wakenya na hata kwenye baadhi ya Mashirika ya Ndege wafanyakazi wengi wanatoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Hoteli nyingi za Tanzania wafanyakazi wengi ni Wakenya na hata zile nafasi za kazi nzuri zimechukuliwa na Wakenya. Watanzania wengi wanaishia kufanya kazi za *house keeping, public area, dishwash* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wengi bado ni tatizo kwani wanakuja na idadi kubwa ya wafanyakazi tofauti na Sheria inavyosema. Ni kwa nini hawa wawekezaji wanaovunja Sheria wasichukuliwe hatua za kisheria? Kwani hawa wawekezaji kwa kufanya hivyo kunawanyima ajira Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajira Serikalini, kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi kuhusu suala la ajira Serikalini. Kwani ajira hii inatoka kwa upendeleo, unakuta kuna baadhi ya watu wana taaluma lakini hawaajiriwi na wanaajiriwa watu ambao hawana taaluma. Kwani wanapoajiriwa watu ambao hawana taaluma wanakuwa utendaji wao wa kazi si mzuri na kuisababishia Serikali hasara kubwa kwani wanakuwa hawana taaluma ya kazi hiyo. Mheshimiwa Waziri ili kuepuka

lawama hizi huoni sasa hivi kupitia Wizara yako ya Ajira, watu waajiriwe kutokana na taaluma zao bila kubebana ndugu, jamaa na marafiki?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la vijana kukimbilia mjini, kumekuwa na utitiri wa vijana wanaotoka vijijini na kukimbilia mjini, kwa kudhani kuwa mjini kuna ajira. Matokeo yake wamekosa kazi na kujiingiza katika vikundi vya uhalifu kwa mfano wizi, uzaji wa dawa za kulevya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na Serikali kushindwa kuwawezesha vijana kulekule vijijini waliko ili waweze kujiajiri wenyewe katika sekta ya kilimo na kadhalika na hasa ukizingatia vijana hawa wanakuwa wana vipaji lakini vipaji vyao vinashindwa kuendelezwa na Serikali. Suala la vijana wengi kukosa ajira ni sawasawa na bomu ambalo linataka kulipuka. Kwa hiyo, Serikali inatakiwa ishughulikie suala hili kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Hifadhi ya Mifuko ya Jamii, Mifuko hii imekuwa mingi na wanachama wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu Mifuko hii ya Jamii na wengine wamekuwa wanalalamika wanakatwa michango mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuipongeza *NSSF* pamoja na Mkurugenzi wake Mkuu (Ndugu Ramadhani Dau) na watendaji wote wa *NSSF* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa semina mara kwa mara kwa wanachama wa Mfuko huu. Vilevile wameisaidia Serikali katika miradi mingi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naiomba *NSSF* kupitia mifuko hii hii ya jamii, sasa hivi wawekeze vijijini kwa sababu vijijini hakuna nyumba bora na kuna wimbi la vijana wanaokimbilia mjini kutokana na kukosa ajira vijijini. Hata wanachama wa *NSSF* wapewe kipaumbele katika kukopeshwa nyumba na washirikishwe katika miradi ya *SACCOS* na pia napendekeza wastaafu ambao wamechangia kwa muda mrefu katika Mifuko hii ya Hifadhi waboreshewe mafao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna malalamiko kutoka kwa wanachama wa *NSSF* kuhusu hospitali wanazotibiwa kwani wanapata usumbufu wa dawa, msongamano wa watu wengi na kadhalika. Kuna malalamiko kutoka kwa wanachama kuwa hawashirikishwi kwenye miradi ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru *NSSF* kwa miradi waliyotusaidia Zanzibar na Pemba. Pia naiomba *NSSF* hii miradi ya *SACCOS* wanayoifanya Tanzania Bara wafanye na Zanzibar. Vilevile watushirikishe na wanachama na wazidi kutoa elimu kwa wanachama ambao hawana elimu kuhusu *NSSF* ili kuondosha malamiko.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchangia dhuluma dhidi ya vijana maskini Tanzania. Kupitia mtindo huu wa ajira za *Recruitment Agency*, baadhi ya Taasisi zinakiuka Sheria ya Kazi na Ajira ya mwaka 2004. Kwa mfano, *NBC* inatoa kazi moja *let say customer service*, inakuwa na watu waloagizwa kupitia *Recruitment Agency* kama *Ero Link* na kadhalika na walioajiriwa moja kwa moja, ambao wanaweza kuwa na sifa moja ya ajira na elimu lakini wanalipwa tofauti kabisa huku walioajiriwa kupitia *Ero Link* wananyimwa haki na stahili za wanafanyakazi kama *health insurance, bonus, housing allowance, mikopo, tea and breakfast staff*, kitu ambacho ni kinyume na kifungu cha 7(i) kinachopinga *discrimination in employment policy or practice*.

Mheshimiwa Spika, mikataba ya miezi mitatu mitatu ni kinyume na kifungu cha 14(i) cha Sheria ya Kazi na Ajira. Wafanyakazi walio chini ya *Ero Link* na kadhalika wamekuwa wakipewa mikataba ya miezi mitatu mitatu na wengine kufanya mpaka miaka miwili kwa utaratibu wa miezi mitatu mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mazingira ya ajira zao na usiri mkubwa kati ya makubaliano kati ya waajiri na *Ero Link*, vijana hao wamejikuta hawana mwakilishi wa kuwatetea maslahi yao kwa kuwa si waajiriwa wa moja kwa

moja, hawana ushiriki katika Chama cha Wafanyakazi wala Mifuko ya Kijamii. Je, Serikali ina mpango gani wa kulinda haki za vijana hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini sasa isitungwe Sheria kwa ajili ya ku-*regulate* hizi *Recruitment Agency* na sasa Serikali inachukua hatua gani dhidi ya unyonyaji huu? Je, wanaokiuka kifungu hiki cha 14 (i) cha Sheria ya Kazi na Ajira ni hatua gani wanapaswa kuchukuliwa, hasa kwa makampuni yanayokiuka?

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yoyote hupimwa kwa uwezo wake wa kuzalisha na kuwapatia ajira wananchi wake. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kuwa uwezo wa wananchi unaongezeka ili waweze kukidhi ushindani katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ina maana kuhakikisha Watanzania wanapata taarifa zote zinazohusu fursa za ajira Tanzania na Duniani. Aidha, vijana kuwapatia mafunzo ya jinsi ya kutengeneza *CV*, kuhudhuria *interview* ya kazi, mafunzo jinsi ya kujiieleza na kadhalika hivi vyote vitasaidia katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukuza ajira, kwa vile Serikali haina uwezo wa kumuajiri kila mtu, naishauri Serikali kujenga mazingira mazuri ya wawekezaji wa nje na wa ndani kwa kuwataka miongoni mwa ajira wanazozitoa angalau asilimia 50 wawe Watanzania. Kama hawataki ni vizuri kukawa na Sheria kuwa ni lazima kwa kila mwekezaji wa nje kuajiri asilimia 50 ya Watanzania na kila mwekezaji wa ndani aajiri asilimia 70 ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna kesi nyingi tu za udhalilishaji wafanyakazi hasa kwenye mahoteli ya watu wa nje. Kwanza huwa hawana mkataba wa ajira, wanafukuzwa kazi ovyo, wanakatwa mishahara yao bila sababu, wanafanya kazi masaa mengi na malipo ni duni. Naiomba Serikali iwasaidie vijana hao ambao wamekata tamaa, wanafanyakazi kwa

shida kubwa na ni wanyonge katika nchi yao wakiona wafanyakazi wa nje wakipewa upendeleo kwenye maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, nina masikitiko makubwa sana kwa Wizara hii muhimu sana kupewa bajeti ndogo. Naiomba Serikali iitizame Wizara hii na ilipe umuhimu wa pekee na ikiwezekana iongezwe bajeti ili iweze kufanya mambo waliojipangia. Kama hamna za kuongeza basi hii bajeti yao wapewe yote isiwe na hiki kidogo hawapewi chote.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba Wizara hii itusaidie wananchi wa Wilaya ya Kasulu katika kututafutia mafunzo ya ujasiriamali kwa kupitia *SIDO* na maafisa au wataalam mbalimbali kuwasaidia akina mama hasa wa Jimbo la Kasulu Vijijini ambao wana vikundi vingi vya uzalishaji lakini tatizo ni mitaji au mikopo.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba tena vijana ambao wamejiajiri wenyewe kwa njia ya kuendesha pikipiki maarufu kama (bodaboda) wapewe mafunzo, mikopo na Wizara ya Kazi na Ajira iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Ndani ili kuondoa usumbufu unaofanywa na Jeshi la Polisi kwa maana ya kupitia kwa Askari wake kuwasumbua waendesha pikipiki hao ambao wamejiajiri. Pia Serikali iwaondolee kodi ambazo ni kandamizi ili kuwawekea manufaa katika kazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, yapo malalamiko mengi kutoka kwa watumishi ambao wanafanyakazi katika mazingira magumu hasa katika Jimbo la Kasulu Vijijini ambako miundombinu ni duni sana. Je, Wizara hii haioni ni wakati muafaka wa kuishauri Serikali na kuwapatia posho maalum watumishi hao kwa kuwapa nafuu ya maisha ili walitumikie Taifa lao kwa moyo?

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa hotuba nzuri na naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii nichangie bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira na mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri yenye kuonyesha dhahiri kutatua tatizo la kazi na ajira hapa nchini ambalo limekuwa sugu kwa vijana wetu na majukumu mengine mengi ya kuongeza ajira na kuhakikisha wafanyakazi wanafanya kazi kufuatana na mikataba yao na mwajiri anatoa haki, mazingira mazuri ya kufanyia kazi, pamoja na kushughulikia migogoro ya kazi sehemu za kazi na kuangalia fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini na kuangalia shughuli za vyama vya wafanyakazi nchini na kusimamia Sheria za Kazi mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazingira ya kufanyia kazi kwa maofisa wanaosimamia mashauri ya migogoro ya wafanyakazi na waajiri ni magumu sana. Katika ofisi za Kazi hakuna vitendea kazi muhimu kama komputa, magari, kalamu, makaratasi, mafaili, vitu ambavyo ni muhimu sana kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba maofisa wa kazi wana wajibu wa kwenda kukagua mazingira ya kufanyia kazi katika sehemu mbalimbali ikiwemo viwandani na maofisini. Mara nyingi unakuta kutokana na hali ya umaskini ya wafanyakazi inamlazimu kufanyakazi katika mazingira magumu na hatarishi bila kulalamika kwa kuwa hana namna nyingine ya kupata ajira nyingine au anaogopa mamlaka, hili ni tatizo kubwa sana na linawaathiri zaidi wafanyakazi wa viwandani na migodini.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara hii kwa kushirikiana na wadau wengine wa Wizara nyingine zinazoshughulikia uwekezaji na biashara katika sekta mbalimbali iwe madini, viwanda, kilimo, mifugo na ujenzi kupanga mikakati ya

kuhakikisha wawekezaji hawa wanaelimishwa kuhusu Sheria za Kazi za hapa Tanzania na pia mara kwa mara wataalamu wa Wizara wawe wanaandaa semina kwa wafanyakazi hasa viongozi wa vyama vya wafanyakazi watambue haki na wajibu wao katika ajira zao na namna ya kuwakilisha wafanyakazi wenzao kwa kutenda haki kwa pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi, kutapunguza migogoro ya kazi kati ya wafanyakazi na waajiri. Siku zote mwekezaji anavutiwa kuja kuwekeza katika nchi ambayo anaona wafanyakazi wake wanafahamu taratibu za kazi na hakuna migogoro ya wafanyakazi na mwajiri. Hivyo mazingira ya amani kazini ni kigezo kimoja kitakachoongeza ajira na kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali kuangalia upya suala la ajira kwa vijana, kwani mpaka sasa idadi ya vijana wasiokuwa na ajira inazidi kukua siku hadi siku. Vijana hawa imefikia kukata tamaa na kutokujua nini hatma yao. Serikali yetu imekuwa ikitangaza nafasi za kazi nyingi lakini upatikanaji wake umekuwa mdogo na mgumu sana na hata zikitangazwa baadhi ya nafasi zinakuwa chache mno kiasi ambacho hata upatikanaji wake unakuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanaomaliza vyuo vikuu kila mwaka ni wengi na wanaobahatika kupata ajira ni wachache mno, hata wale wanaomaliza darasa la saba, *form four* na *form six* pia ni tatizo kupata ajira. Ukiangalia kwa wastani huo utagundua kuwa tatizo ni kubwa sana. Naiomba Serikali kuweka utaratibu wa kuwapa elimu ya ujasiriamali vijana hawa tokea wakiwa vyuoni, hali hiyo itawasaidia pale wamalizapo elimu zao kujajiri wenyewe na si kusubiri Serikali kuwaajiri.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi za kuweza kuwawezesha hawa vijana waliomaliza vyuo na kufaulu vizuri. Nashauri ungewekwa utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo



midogomidogo kutoka kwenye mabengi yetu ili waanzishe miradi midogomidogo kwa njia nyingine watakuwa wamejiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuweka utaratibu wa kuchukua vyeti vyao vya vyuo walivyomaliza yaani (*original certificate*) vikawa kama dhamana kwenye hayo mabengi ambayo watapatiwa hiyo mikopo. Kufanya hivyo itawasaidia na utaratibu huu utasaidia sana pale tu Serikali itakapokaa na haya mabengi na kuzungumza nayo na kuangalia mahali pa kuboresha utaratibu huu, kwani tatizo hili la kukosa ajira likizidi litageuka kuwa hatarishi baadaye.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na tatizo la vijana kukosa ajira, tuna mifano mbalimbali toka nchi nyingine kuwa matatizo kama haya ya kuwa na vijana wengi waliosoma na kukosa ajira, kumesababisha kutokea vurugu na uvunjifu wa amani na nchi kuingia katika majanga makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatma ya hawa vijana na tatizo hili lazima lipewe kipaumbele kwani nguvu kazi kubwa ya Taifa ambayo ingekuwa na ajira ingefanya uzalishaji mkubwa na kukuza uchumi wa nchi yetu. Tatizo hili kupatiwa ufumbuzi linawezekana sana tukiamua kuweka mkakati wa kitaifa wa kutokomeza tatizo hili kama tufanyavyo kwenye matatizo mengine na kuweka mikakati ya kitaifa kuyamaliza.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwekwe Sheria kama wafanyavyo nchi jirani. Wenzetu wameweka Sheria kuwa mwekezaji yeyote anapotaka kuwekeza, Sheria hiyo husema asilimia kubwa ya ajira wapewe wazawa na si zile nafasi za chini tu bali hata zile za juu, hii inasadia sana kuwajali wazawa na kupunguza matatizo ya ajira katika nchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo limekuwa kikwazo kikubwa katika upatikanaji wa hizi ajira ni suala la uzoefu tena ikibidi uzoefu usiopungua miaka mitatu (3). Hivi huyu kijana anayetoka shule ama chuo huo uzoefu anakuwa kaupatia wapi tena wa miaka mitatu? Kila idara ndio wameweka vigezo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuweka tangazo maalum kwa kuamrisha kipengele hicho kitolewe katika ajira za kawaida ila tu kwa ajira ambazo zitakuwa zinahitaji uzoefu. Kwa kufanya hivyo itawasaidia sana walio wengi kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashauri sekta zote kutokujali sana kipengele hicho cha uzoefu kwani badala yake wafanye kama baadhi ya mashirika mengine hapa nchini na nje ya nchi pale wanapomwajiri mfanyakazi mpya ambaye hana uzoefu wowote zaidi ya taaluma aliyonayo basi wanampeleka mafunzo elekezi ya muda mfupi (*training*) ambayo yatamsaidia kupambana na changamoto zozote awapo kazini.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuikumbusha tu Serikali kupitia Wizara hii kuwa vijana hawa endapo wataachwa bila kujengewa uwezo na mazingira ya maendeleo, tutakuwa tunatengeneza Taifa ambalo baadaye litakuwa maskini kwani vijana wengi kwa sasa hivi wanatoka vijijini na kuja mijini kutafuta ajira na pale wanapozikosa hujiingiza katika vitendo vya kijambazi na uhalifu, uzururaji na madawa ya kulevya, hii inatokana na kukata tamaa ya maisha.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijijini walio wengi hali zao ni duni, sehemu za kuajiriwa ni ndogo kwani Jimbo ni changa. Naomba Mheshimiwa Waziri atupie jicho lake la huruma jinsi ya kuwasaidia wananchi hawa kwa kupatiwa mikopo kupitia Mfuko wa Dhamana na mikopo kwa Jina la Mamilioni ya JK, wengi wao ni wakulima na wafugaji na wanajitahidi sana katika shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu Eric Shitindi na timu yake ya wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwajengea utaalim watumishi wa Wizara; ninavyofahamu hii ni Wizara ambayo haina wataalam kwa miaka mingi, sijui kama hali imebadilika. Mafunzo kwa watumishi ili kuwapatia *skills* ni muhimu sana. Sijui Wizara hii inasimamiaje na kuelekeza mashirika yaliyoko chini yake wakati watumishi wa mashirika hayo wana weledi zaidi kuliko watumishi wa wizara. Ni muhimu kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vibali vya ajira kwa wageni; Tanzania imekuwa *a plastic society* ambayo ni *porous*, wageni wanaingia na kutoka wanavyotaka. Wako wageni wengi wanafanya kazi za ajabu. Kazi ndogo ndogo ambazo zingefanywa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina hakika kama vibali vya ajira vinatolewa kwa makini. Siku zote nailaumu Wizara hii pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani (Uhamiaji) kwa vurugu za kuwa na wageni wengi ambao siyo wawekezaji, lakini wameruhusiwa kufanya kazi ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi za umma chini ya Wizara; wakati Wizara hii ina jukumu la kuongeza na kusimamia haki katika kuwaajiri Watanzania kwa usawa, ni aibu kwa baadhi ya mashirika yaliyoko chini ya Wizara hii kuendekeza ajira za upendeleo na hasa upendeleo wa kidini. Kuna udini mkubwa katika baadhi ya mashirika chini ya Wizara hii. Namwomba Mheshimiwa Waziri akomeshe udini huu katika suala la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya watumishi na ajira katika makampuni binafsi; bado kuna mashirika mengi ambayo bado yanapendelea kuajiri wageni kwa kazi zinazoweza kufanywa na wazawa. Makampuni hayo binafsi yanaajiri watumishi kutoka India, Pakistani na Kenya bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wageni hao wanapewa maslahi mazuri zaidi kuliko wazawa wenye sifa sawa. Mbaya zaidi makampuni hayo yanalipa mishahara midogo sana

chini ya kima cha chini. Wafanyakazi wazawa wananyanyaswa na kudharauliwa. Naiomba Wizara ifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la tija la Taifa (*NIP*); kama kuna Shirika la Mafunzo, Utafiti na *Consultancy* ambalo ni *dormant* ni hili la *NIP* halijitangazi, *it's not proactive* na sina hakika kama lina *capacity* ya kuweza kuyasaidia mashirika mbalimbali kuboresha ufanisi (*to increase productivity*). Shirika hili lilianza zamani sana na niliwahi kwenye miaka ya 80 kuwa Mkurugenzi kwenye Bodi ya Shirika hili. *Impression* yangu na watu wengi shirika hili halikui. Wizara ifikiri namna ya kulisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mifuko ya Pensheni; nakubali kwamba, Mifuko hii inafanya kazi nzuri katika kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali na inasaidia Serikali katika kuchangia maendeleo katika sekta mbalimbali:-

(i) Lakini sina hakika kama Mifuko hii inafanya vizuri kwenye *core business* yake ya kuwapa huduma nzuri na endelevu wanachama wake.

(ii) Mifuko hii imewekeza sana katika vitega uchumi vya majengo makubwa, lakini pensheni za wanachama wake haziboreshwi ipasavyo kutokana na uwekezaji huu. Naiomba Wizara iangalie jambo hili ikisaidiwa na *SSRA*.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko kubwa la watu, idadi ya watoto wanaomaliza elimu ya msingi sasa inakaribia watoto milioni moja. Kati ya hawa ni wastani wa watoto 400,000 wanaopata nafasi ya kuendelea na elimu katika shule za sekondari na vyuo mbalimbali vikiwemo vya *VETA*.

(i) Idadi ya watoto takribani 600,000 hukosa fursa ya kuendelea na elimu na umri wao ni chini ya miaka 18 na hivyo hawana fursa au sifa ya kuajiriwa.

(ii) Ni ukweli ulio wazi kuwa, kwa kuzalisha watoto 600,000 kila mwaka wasio na elimu wala ujuzi wa kuwapatia ajira yenye tija na vigezo vya kisheria. Idadi hii inaondoa kabisa uwezekano wa kuondoa umaskini.

(iii) Pamoja na uwezo mdogo wa Serikali, ni muhimu sasa kuanza kutafakari namna ya kutengeneza sera stahiki itakayoweke mpango mkakati wa kukabilliana na janga hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ongezeko la watu; kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu kunaondoa au kupunguza kasi ya kuondoa umaskini. Kwa utafiti usio rasmi, familia zisizo na elimu ndizo zinazoongoza kwa kasi ya kuzaana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazazi wenye elimu ya juu huwa na wastani wa watoto wawili au watatu, wazazi wenye elimu ya kati (Sekondari) huwa na wastani wa watoto wanne na idadi hii inaongezeka na kufikia watoto watano au sita kwa wale wenye elimu ya msingi au wasio na elimu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuruhusu watu waendeleo kuzaliana bila *control*, tunaongeza mzigo mkubwa kwa Serikali. Ni muda muafaka sasa kufanya maamuzi magumu na kutengeneza sheria ya kudhibiti ongezeko la watu na kuzaliana kusiko na kikomo.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kuwapongeza kwa kuleta hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara hii ni finyu sana ukilinganisha na majukumu mazito iliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo ningeomba kupata ufafanuzi:-

(1) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Pensheni; mfanyakazi anapostaafu nchini kwetu huwa anaishi katika mateso na taabu kutokana na pensheni ndogo anayolipwa.

Ushauri wangu ni kwamba, mtu akistaafu kazi ni vema awe anapatiwa pensheni kulingana na cheo cha mtu au kima cha mshahara aliokuwa analipwa, badala ya kulipwa kima cha chini shilingi 50,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeiga mfano kwa baadhi ya nchi kama Uholanzi, Ubelgiji na kadhalika. Wenzetu unapostaafu unalipwa asilimia themanini (80%) ya mshahara uliokuwa unalipwa.

(2) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafanyakazi wa majumbani; ajira za sekta zisizo rasmi Watanzania wananyanyasika sana. Mkataba wa kuridhia ulisainiwa mwaka 2011 Geneva. Kimsingi mikataba ya Kimataifa huwa inaweza kuridhiwa au ikachagua maeneo fulani baadaye unawasilisha Bungeni ili uhalalishwe na sheria mama kwa mazingira ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria na. 6 ya mwaka 2004, wote tunajua sheria hii ndio inatoa haki na stahiki na wajibu wa mfanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka mwaka jana tuliambiwa Serikali ipo kwenye mchakato, muda umekuwa mrefu sana. Naomba nipatiwe majibu ni lini utaletwa ili uweze kupitishwa humu Bungeni

(3) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sheria ya fidia; Sheria hii ni ya toka mwaka 2008, imepitishwa hapa Bungeni lakini mpaka hivi sasa sheria hiyo haitumiki. Tatizo ni nini? Tulipouliza walisema eti kanuni bado na mpaka sasa bado haujafunguliwa Mfuko wa Fidia na Mkurugenzi wa Mfuko. Naomba pia kupatiwa jawabu, tatizo ni nini la kutoanza kutumika kwa sheria hiyo?

(4) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoajiriwa kwa ajili ya uzoefu wa kazi; naomba Serikali iangalie kwa makini kuhusu vijana wetu wanaohitimu masomo yao ya Chuo Kikuu na vyuo vingine. Baadhi ya waajiri kutangaza nafasi za kazi na kuweka vigezo vya kutaka uzoefu wa kazi wakati wakijua vijana wetu ndio wamehitimu tu, sasa uzoefu wanautoa wapi?

Naomba suala hili liangaliwe upya na Serikali iweke mkakati wa *Voluntianism*, vijana wakimaliza wawe wanajitolea ili kupata huo uzoefu wanaoutaka. Pia ni kwa nini Serikali bado inawapa mikataba wastaafu wakati kazi hizo vijana wanaweza kufanya?

(5) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Walemavu ilipitisha sheria kuwa kila Taasisi inapotoa ajira itenge 2% kwa ajili ya walemavu. Mbona hata Utumishi wala Wizara hii haijasema lolote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya jamii *PSPF* fedha ambazo Serikali imeahidi kuhusu *PSPF* hazitoshi kwani ni kinyume na makubaliano ya Sh. 71 billioni kila mwaka *arrears* za nyuma hazijalipwa. Hivyo, kuna haja fedha kuongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* fao la *SHIB* ni fao muhimu sana kwa wanachama wa *NSSF*, fao la afya (Bima ya afya) ndio fao pekee ambalo linamgusa mwananchi bila kusubiri kuzuka. Hili ni fao ambalo likifanyiwa kazi vizuri litajenga heshima kubwa sana kwa *NSSF*. Mwaka ujao wa fedha bajeti ya matangazo, kuelimisha wananchi juu ya fao hili iongezwe sana, pia watoa huduma waboreshe huduma zao ili kutoudhi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo za *SSRA* kutoka Mifuko zianze mara moja ili kuwezesha mamlaka kufanya kazi Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna fao la kujitoa bali kujitoa kwenye mafao tusingie kwenye kosa hili.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi 2012/2013 ni Halmashauri 20 za Wilaya/Mji, Majiji ziliunda Mabaraza ya Wafanyakazi. Ni vyema tukaelezwa hadi sasa nchini kuna Mabaraza mangapi ya Wafanyakazi katika Wizara, taasisi na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, imebainishwa kwamba *OSHA* itapima afya za wafanyakazi 50,000. Hata hivyo, *OSHA* itatoa elimu kwa wafanyakazi 1,500 ili kupanua wigo wa elimu kwa umma. Nashauri wote watakaopimwa afya wapatiwe pia elimu, hii itasaidia kutoa elimu hii kwa watumishi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *OSHA* kwa mipango ya kuanzisha mfumo wa kuripoti na kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi. Aidha, ingekuwa vyema endapo Bunge lako lingepata takwimu kuhusu ni wafanyakazi wangapi ambao wamepata magonjwa na ajali kazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* inafanya kazi nzuri sana katika nyanja mbalimbali za maendeleo nchini mwetu. Aidha, tumeona na *NSSF* imewekeza na mikopo kwa taasisi mbalimbali. Nashauri endapo inawezekana na wafanyakazi wanachama wa *NSSF* nao wakopeshwe kwa masharti na utaratibu utakaowekwa na *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukishuhudia wafanyakazi kukosa/kuachishwa kazi na wengine kukosa ajira. Je, ni lini Serikali/Wizara itaanzisha utaratibu wa kuwa na Mfuko wa Bima kwa watu wasio na ajira (*Unemployment Insurance Fund*)? Ili kuwawezesha kuwa na kipato wakati wanaendelea kutafuta ajira nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa mchakato wa kuridhia *Domestic Workers Convention na Maternity Protection Convention* ili ziidhinishwe na Bunge lako ni wa muhimu, hivyo ni vyema ukaharakishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Kazi na Ajira kwa Hotuba nzuri na kazi nzuri wanayofanya. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wasaidizi wote na wakuu wa taasisi zilizopo chini ya Wizara hii.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kupongeza kwa kazi ambazo zimefanywa na Wizara katika kipindi cha 2012/2013. Hata hivyo, katika aya ya 15 na nyinginezo haijaelezwa ni sehemu zipi za kazi zipo nchini (zilizotambuliwa) na Wizara ili kubaini kazi 3,094 zilizofanyika ni asilimia gapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko mengi ya wafanyakazi wa makundi mbalimbali wakiwemo madereva wa vyombo mbalimbali vya usafiri, wafanyakazi wa majumbani, walenzi, wafanyakazi wa mashambani, *tour Guide* (waongoza watalii) na kadhalika. Napenda kutoa rai kwa Wizara kuongeza wigo wa uhakiki wa mikataba ya ajira katika makundi haya na mengine kwani wengi hawapatiwi mikataba na wananyasika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo ni muhimu ni utoaji wa elimu kwa umma kuhusu Sheria za kazi. Nimeona Wizara imejitahidi kutoa elimu hii. Hata hivyo, katika 2013/2014, tujitahidi zaidi kutoa elimu hii ili iwafikie wafanyakazi wengi zaidi na kwa waajiri wa sekta mbalimbali kwani kama ni ukiukwaji kwa kiasi kikubwa unafanywa na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa wafanyakazi; eneo hili ni muhimu sana. Niupongeze uongozi wa Wizara kwa kuendelea na mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kupata maradhi wakiwa kazini. Mchakato huu umechukua muda mrefu sana hasa ukizingatia Sheria ya Fidiala kwa wafanyakazi wanaoumia kazini ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwaka 2008. Ni vyema mchakato ukakamilika mapema ili wafanyakazi wanaoumia au kupata maradhi wakiwa kazini wapewe haki yao stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Pensheni kwa wazee nchini; napongeza kwa kufanyika kwa utafiti na tathmini ya malipo ya fao la kujitua. Hata hivyo; ni vyema SSRA/Wizara ikaharakisha matokeo ya utafiti wa mpango wa Pensheni kwa wazee na mapendekezo inayoyatoa ili wazee hawa waweze kunufaika na Pensheni kwani kwa takwimu

na tafiti zilizofanywa na taasisi mbalimbali, nchi inao uwezo, suala ni kupiga hesabu ni kiwango kipi kitakachokuwa endelevu kitolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Wilaya/Mikoa za kutokomeza Ajira mbaya/hatarishi kwa watoto; je, hadi hivi sasa ni Kamati ngapi zimekwishaundwa na ni nini matokeo/faida zilizopatikana baada ya kuundwa kwa Kamati hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa usalama na afya mahali pa kazi; napongeza kazi inayofanywa na *OSHA*, hata hivyo, nadhani ni vyema utekelezaji wao kwa 2012/2013, ungebainishwa hususani nini kilitekelezwa kitakwimu/Ki-sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya wafanyakazi kwenye kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli za Vyama vya Wafanyakazi; ziko taasisi/waajiri mbalimbali ambao hawawaruhusu wafanyakazi wao kujiunga na vyama vya wafanyakazi. Inasemekana moja ya taasisi hizi ni *TRA*. Je, nini tamko la Wizara kuhusu taasisi zinazowakataza wafanyakazi kujiunga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwamba *TaESA* inashughulikia pia suala la kupokea maombi ya usajili wa wakala binafsi wa kutoa huduma za ajira nchini. Kwanza kabisa zipo wakala nyingi binafsi zinazotoa huduma za ajira ambazo hazijasajiliwa. Ni vyema endapo itawezekana aanzishwe msajili wa wakala binafsi za kutoa huduma za ajira (*Registrar of private employment agencies*), itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inafanyika katika nchi nyingi zikiwemo *South Africa* na nyinginezo. Ningeshukuru endapo Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho anaweza kulieleza Bunge ni wakala ngapi binafsi za ajira zimesajiliwa nchini, kwa sekta zipi na mikoa ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA*), chombo hiki ni muhimu sana, kinafanya kazi nzuri sana katika utatuzi wa migogoro. Hata hivyo, ni vyema Bunge lako likapatiwa ni migogoro mingapi ilisajiliwa 2012/

2013, mingapi ilisikilizwa? Migogoro mingapi iko hivi sasa, ikijumlisha pia mlundikano wa migogoro iliyosajiliwa/ iliyoandikishwa? Wastani wa asilimia (%) ya kusikiliza migogoro hii ukoje? Wizara/CMA ina mkakati gani wa kupunguza mlundikano wa migogoro hii ili isikae muda mrefu katika Tume (CMA)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. THUWAYBA I. MUHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi ni moja katika kioo cha nchi, ili kiweze kuona na kuwasaidia vijana, wastaafu na mashirika au kampuni ambazo zitaweza kusaidia Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa mahoteli, viwandani na makampuni makubwa hudhalilishwa kwa kutopewa mikataba ya kazi au wengine hupewa mikataba ya miezi mitatu na hii hujitokeza kwa vijana wetu wa Kitanzania tu, lakini wale ambao wanaotoka nje ya Tanzania hupewa mikataba ya kikawaida kama sheria za Serikali zinavyozungumza. Je, Sheria hii ni kwa waajiriwa wa nje tu? Hatuoni kwamba tunaleta *discrimination* ya Watanzania na wa nje? Kama sheria hii ni kwa wote, haya makampuni yanayofanya hivi ni hatua zipi zilizochukuliwa dhidi yao? Naomba Waziri alifafanue hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa afya mahali pa kazi; Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi (OSHA), bado halijaenea katika Tanzania hii, ni baadhi ya kanda tu ambazo ofisi zao zipo au wanajishughulisha, ukiachia mbali kwamba hawana vifaa vya kutosha, wala wafanyakazi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda hapa Morogoro kama cha *21<sup>st</sup> Century* na kile cha Ngozi, ambavyo mazingira ya wafanyakazi, pamoja na mazingira ya eneo la kazi si ya kuridhisha, hasa hiki cha Ngozi. Wafanyakazi hawana vifaa vya kazi kama *gloves*, viatu, *musk* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wanapoteza hata hisia zao kama harufu hawajui kama ni harufu mbaya au nzuri, wao harufu wanayoiona ni ya kawaida. Kiafya hawana mtazamo mzuri wamedhoofu sana. Ni vyema *OSHA* ikaweza kueneza mikono yake katika maeneo mbalimbali ili iweze kuwasaidia wafanyakazi hawa, kwani wanateseka sana na hakika wakipimwa wote wataonekana wameathirika kiafya kwa njia moja au nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili pia lilijitokeza kwa Kamati ya *PAC* mwaka jana ilipokwenda kukiangalia kiwanda hiki, Wanakamati hawakupewa kifaa chochote cha kujihifadhi walipoingia katika kiwanda hicho, hasa sehemu ya kusafishwa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira mbaya kwa watoto; ingawa Wizara inajitahidi kukomesha utumikishwaji wa ajira mbaya kwa watoto ambao hawastahili kufanya kazi kulingana na umri wao na pia kutoa elimu kwa wazazi, lakini bado watoto hawa wanaajiriwa hasa katika uchimbaji na kukosa haki yao ya lazima ya kupata elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Wizara, Halmashauri zikazidi kujitahidi kutunga Sheria au kutoa adhabu kali kwa wale wote ambao wanadhallisha watoto wadogo ambao hawastahili kufanya kazi, lakini huwafanyisha kutokana na umaskini wao. Pia huwalipa fedha ndogo kama ni ujira wao, ambao wana hakika kwamba watoto hawa au wazazi wao hawana elimu ya kutosha ya kwenda popote kudai haki yao. Je, kuna mikakati yoyote ile ambayo mmeipanga ili kuondoa kadhia hii, isiendeleo katika nchi yetu?

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira; vijana wengi karibu asilimia thelathini hawana ajira, lakini cha kusikitisha kwa sasa hivi unakuta wafanyakazi wengi wa Serikali waliofikia kustaafu, Serikali imekuwa ikiwaongezea mikataba ya kazi kwa kazi ambazo wangeweza kuzifanya wengine, mfano, kazi kama ya Wakurugenzi wa Halmashauri. Ni kwa nini Serikali inawaongeza muda wa kazi na kigezo kinachotumika cha

uzoefu wa kazi unakuta kijana ndio kamaliza tu chuo, je, atapata wapi uzoefu bila kuajiriwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kinachochangia vijana wengi kukosa ajira ni kwa baadhi ya wageni kufanya kazi ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania kwa kisingizio cha kuleta wataalam wanapofungua biashara au vitega uchumi vyao. Sheria inasema mwekezaji ataleta watu watano (5) watakaofanya kazi kuelekeza Watanzania na hatimaye kazi hizo hufanywa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haipo hivyo, wawekezaji wengi hasa Wahindi/Wachina kwenye maduka mfano *shopaz supermarket* iliyopo Dar es- Salaam, Mwai Kibaki Road, unakuta mpaka walinzi wakuchunga nyuma ya *till machine* wanatoka India. Je, hivi ndivyo sheria inavyoelekeza, Serikali itawachukulia hatua gani mabosi hawa wa *Shopaz supermarket*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *garage* za Wachina unakuta vijana wa Kichina wakikwangua hata rangi za magari zunguka katika garage zote za Kichina utawakuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni kwa wazee; tukumbuke kila mtu kila siku anaelekea kuwa mzee na wote siku moja kila mtu kwa wakati wake ni mstaafu mtarajiwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha sera na Sheria hii ya Wazee na kuleta hapa Bungeni? Kwa kuwa Sera na Sheria zilizopo kuhusu huduma za wazee haziwezi kuondoa matatizo yanayowakabili wazee wetu. Hivyo mchakato wa fao la wazee likamilishwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*), Sheria Na. 30 ya mwaka 1997, (*OSHA*) ilianzishwa ili kusimamia usalama wa afya mahali pa kazi kwa waajiri kuhakikisha wanazingatia usalama katika sehemu za kazi kwa wafanyakazi.

Cha kusikitisha waajiri wengi hawazingatii hili katika viwanda, unakuta wafanyakazi hawana vitu vya kuwakinga

na ajali, wajenzi hawana kofia (*helment*) baadhi ya *garage* za magari vijana wanachomelea magari bila miwani ya kuzuia cheche, wanakata chuma na mikono mitupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *OSHA* inashindwa kufanya kazi nchi nzima kwa kuwa na uhaba wa wafanyakazi wa kutosha na uhaba wa vitenda kazi. Ushauri ni kuwa, Serikali iiwezeshe *OSHA* kwa kuwapatia vifaa na wafanyakazi wa kutosha ili waweze kufanya kaguzi na kuokoa maisha ya Watanzania, mfano, 18% ya wajenzi walipata ajali wakiwa kazini.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa Hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Mbunge ni ya *Risk* kubwa kwa sababu ya mazingira tunayofanya kazi na safari za mara kwa mara. Ni kwa nini Wabunge hawana bima ya maisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ya Mbunge ni ya mkataba kwa miaka mitano na anafanya kazi kubwa kutumikia Taifa na wananchi wake. Ni kwa nini mpaka leo Serikali haijaamua kuweka pensheni kwa Wabunge? Wabunge wakimaliza muda wao wa utumishi wanakufa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imekuwa inatumia fedha za wanachama kujenga vitega uchumi/nyumba maeneo mbalimbali na wanalipwa fedha nyingi. Je, wanachama wa Mifuko wanashirikishwaje kwenye maamuzi ya kuwekeza huko? Wanachama wananufaikaje na faida inayotokana na vitega uchumi hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachama wengi wa Mifuko hii ni watumishi wa kawaida ambao vipato vyao ni vya chini sana, wanahangaika kuweza kukidhi mahitaji yao

na familia zao. Ni kwa nini Mifuko hii isitumike kuwakopesha wanachama kwa riba nafuu ili waweze nao kufaidika na michango yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatumia busara na hekima kulipa deni la Mifuko ya Jamii lililokopwa kwa muda mrefu shilingi billioni 50 ni hela ndogo sana kwa Serikali kama wataamua kwa dhati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina kigugumizi gani kutoa pensheni kwa wazee ambao wamelitumikia Taifa hili kwa miaka yote? Serikali inaona raha kuwaona wako barabarani wanaomba misaada? Wanaona raha kuwaona wanakufa kwa kukosa matibabu? Mataifa yote wanawaenzi na kuwajali wazee, sisi tunaziba masikio kwa nini? Tunaomba Waziri atoe melezo yenye tumaini leo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya Watanzania wameajiriwa kwenye sekta binafsi. Wengi wao wananyanyasika sana kwenye ofisi hizo. Baadhi ya mashirika/Makampuni/watu binafsi wanalipa mishahara ya chini ya ile inayotamkwa na Serikali, ni kwa nini? Wanatumikishwa zaidi ya masaa ya kazi bila malipo yoyote/wakati mwingine mpaka usiku bila hata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiugua hawatibiwi na wakidai stahiki zao wanafukuzwa kazi. Viwandani kwenye mitambo, akiumia basi hiyo ni tiketi ya kuachishwa kazi. Haki kweli Serikali imekuwa inapata malalamiko mengi kutoka kwa watumishi hawa wa Sekta binafsi. Ni kwa nini bado haya yote yanaendelea kutokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ndogondogo za Wamachinga za kuuza matunda na mbogamboga ni ajira pia, Serikali iweke utaratibu mzuri wa vijana na akinamama wanaofanya ajira hii wafanye kazi zao kwa utulivu na ufanisi. Wasibaguliwe kila leo, ni aibu, kuwafukuza kwenye ajira zao tunawatuma wakaibe na wana watoto wataishije?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana zaidi ya 400 wamekuwa wanafanya kazi kwenye Makampuni ya mabasi pale Ubungo *Terminal* zaidi ya miaka 15 bila kuajiriwa. Mwaka huu walipoanza kudai ajira zao wamefukuzwa na kukamatwa kupelekwa *lock-up* bila kosa lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya vijana 350 wamewekwa *lock-up*. Makampuni mapya ya *Taqwa, Sumry, New Force* wameleta mabasi mengi – wameajiri vijana 20 kila Kampuni watu wanaojiita *DABOA* wamewashinikiza wawaachishe kazi na kubakiza wawili (2) tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa tunataka wakawe majambazi?

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Wizara hii imejitahidi sana kubadilisha sura ya nchi hii kila mtu anaona, lakini labda tatizo lililopo ni uelimishaji, bado kunahitajika elimu kubwa kuwaelimisha wananchi, juhudi zinazofanywa na Wizara kupitia mifuko mbalimbali, mfano *NSSF*. Haeleweki kwa Watanzania wote, kwa hiyo, elimu inahitajika sana kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni mafao ya wazee, wazee walipwe mafao na pensheni zao kwa wakati, muda ni mrefu mno. Pia wazee wote wafikiriwe hata wale ambao walikuwa hawafanyi kazi kwa mikataba ya pensheni, kwa hiyo walipwe mafao kwani walitumika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu



Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote pamoja na taasisi hususani Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi nzuri, kutoa mafao mbalimbali, lakini pia kupanua washiriki wa mifuko hii na jinsi inavyoshiriki katika miradi ya maendeleo na vilevile kutoa mikopo kuwezesha wajasiriamali wadogo na hata Makampuni ya Biashara ya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira, sekta mtambuka; ajira ni sekta mtambuka ambayo inahusisha karibu Wizara na Taasisi zote nchini. Hivyo, ni lazima wote tuhusike katika kuboresha ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa vijana; suala la ajira kwa vijana sasa hivi ni suala siyo tu la kipaumbele, lakini ni suala la usalama na utulivu nchini. Vijana ni asilimia isiyopungua 65 na takwimu zinaeleza kuwa takribani milioni moja wanaingia kwenye soko la ajira kila mwaka. Hivyo, ni lazima sote tuelekeze nguvu kuona ni jinsi gani suala la ajira kwa vijana linashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai ifuatayo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tuanzishe kauli mbiu ambayo itashirikisha kila mtu na kusimamiwa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri, wakati Mheshimiwa Rais alipotoa kauli mbiu "Tanzania Bila UKIMWI Inawezekana", "*Malaria* Haikubaliki", "Kilimo Kwanza" na kadhalika zote ambazo zilisimamiwa na Mheshimiwa Rais zilitoa matunda na uelewa mzuri kwa jamii na hata kupata misaada toka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tusiwe na kauli mbiu kama "Ajira kwa Vijana Wote Nchini Inawezekana". Ajira katika sekta zote lakini muhimu kama kilimo, viwanda na biashara inaweza kutoa matokeo mazuri na ya haraka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira toka kilimo na viwanda; nilipochangia Wizara ya Kilimo nilieleza ni

jinsi gani kwa utashi wa dhati wa Serikali, kilimo cha tija kinaweza kutoa mchango mkubwa sana kwenye ajira. Nilieleza jinsi Serikali inavyoweza kuandaa mashamba makubwa kwenye maeneo yenye rutuba na maji ya umwagiliaji kuhakikisha kilimo cha tija kwa kutumia nyenzo za kisasa yaani trekta, mbegu bora, dawa na masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kujitahidi kuandaa sehemu mbalimbali kuzindua ajira, lakini hoja yangu ni kutafuta fedha ndani na nje ya nchi mahsusi kwa ajili ya kukuza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kujidanganya kudhani kuwa tunaweza kuzindua/kukuza ajira kwa kutegemea fedha za bajeti tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuibua ajira mpya, shule zetu toka ngazi ya msingi, vyuo, hata vyuo vikuu, ni lazima mitaala ihakikishe elimu ya ujasiriamali, biashara na fedha itolewe kwa wanafunzi wote, ili wanapohitimu wanakuwa na uelewa wa kuweza kujiajiri na kuweza kuendesha shughuli zao kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tena, naunga mkono hoja na naipongeza Wizara na Taasisi zote.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi ya mimi kuchangia kidogo katika hoja hii ya Wizara ya Kazi na Ajira. Nianze moja kwa moja kwa kuchangia baadhi ya mambo na mengine atakuja kumaliza Mheshimiwa Waziri.

Naanza na suala la ukosefu wa ajira na hasa kwa vijana; hili ni tataizo kubwa, hakuna anayepinga na ni tatizo siyo Tanzania tu, ni tatizo la Dunia nzima. Sisi kwa Tanzania na tumeleza katika bajeti yetu kuwa, sasa hivi tunaandaa kutayarisha ile *intergrated labour force survey*, ambayo tukiikamilisha, mwaka ujao wa fedha tutaweza kujua ni kwa kiwango gani hasa ajira inakosekana hapa nchini kwetu.

Takwimu za haraka ni kwamba, hatuko chini ya asilimia 12. Tunafahamu kabisa kuwa, wenzetu hata wa hapa Afrika; Kenya, South Africa ni zaidi ya asilimia 40. Nchi za Ulaya hasa hizo zilizokumbwa na matatizo, tunajua ni tatizo kubwa. Ugiriki ukosefu wa ajira sasa hivi ni asilimia 62.5, Hispania ni asilimia 55.9, Italia asilimia 38.4 na hivyo hivyo hali ni mbaya kwa nchi zote za Dunia. Kama Wizara, sisi kazi yetu ni kusimamia zile Sera na Mikakati na Sheria za Kukuza Ajira Nchini. Katika ukuzaji huu wa ajira, Wizara ya Kazi na Ajira, tunaangalia ajira zote kwa ujumla; kuna ajira ambazo ni za Sekta ya Umma na ajira ambazo zipo kwenye Sekta Binafsi na kwa wawekezaji. Katika Sekta ya Umma, tunajua kabisa kuwa, tuna ajira ya moja kwa moja ya Watumishi ndani ya Serikali, ambao wanaajiriwa na Serikali na kulipwa mshahara na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ajira ambayo ipo kwenye Sekta ya Umma, lakini inatokana na uwekezaji wa fedha za Umma kwenye Miradi ya Maendeleo, kilimo, maji, viwanda, biashara, utalii, migodi na kadhalika. Serikali inaweka fedha nyingi kwenye maeneo hayo na kwa kufanya hivyo, pamoja na uchumi kukua, ajira nayo inakuzwa. Kwenye Sekta Binafsi, wawekezaji wanapokuja kuweka watoke nje au wa ndani, wakiwekeza tunategemea ajira itoke na kwa maana hiyo, ajira kama ilivyosema na ninamshukuru Mheshimiwa Madabida na Wabunge wengine, akina

Mheshimiwa Msabaha kwamba, ajira ni suala mtambuka siyo suala kuwa sisi kama Wizara ya Kazi ndiyo tutalimaliza.

Ukiacha ajira hizo, tunaangalia vilevile ajira ya watu ambao hawawezi kuajiriwa moja kwa moja na kupewa mshahara kila mwisho wa mwezi. Kuna ambao hawawezi kupata ajira, wamemaliza mafunzo yao lakini ajira za kuajiriwa hakuna. Wapo wengine ambao hawaajiriki na hili limezungumzwa humu ndani; tunafanyaje? Tunaangalia zile programu za kuweza kuwapatia ajira, mafunzo ya ujasiriamali baadaye waweze kupata ajira kwa kukopeshwa au wao kuwa wabunifu katika masuala ya kujiajiri. Kwa hiyo, katika hili la pili ndiyo tumeweka hizo programu, tumesema ndani ya miaka mitatu ijayo, tunategemea ajira laki sita kuzalishwa katika programu ambayo tunaendelea nayo. Vilevile kuna programu nyingine ya wahitimu wa Vyuho Vikuu ambapo miradi 200 ya wahitimu hawa hasa kwenye Sekta ya Kilimo na Viwanda tutazalisha ajira.

Kwa hiyo, ni programu hizi ambazo sisi tunazisimamia na kuangalia kwenye Wizara zingine kuna programu gani ambazo inawezekana ajira zikatokea na pale tukaweza kukuza ajira. Kwa hiyo, ninawashukuru sana wote waliochangia na mimi ninataka nikubaliane nao kwa yote walioyosema.

Mheshimiwa Murji, amezungumzia kwa nini tusifanye vyeti kuwa *collateral*; ni jambo zuri la kuendelea kuliangalia. Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Jenista Mhagama, amezungumzia sana suala hilo la ajira.

Ndugu yangu Mheshimiwa Vincent Nyerere, amezungumzia suala la kujiajiri, msemu uwe ni kwamba, kazi zipo lakini ajira hakuna. Inapokuwa hakuna ajira haina maana kuwa kazi hakuna, kwa sababu ajira maana yake ni kuwa uajiriwe na kulipwa mshahara; lakini kumbe unaweza kujiajiri ukapata kazi, ukafanya kazi na ukaweza kujikimu. Hili ni suala la msingi la kuliangalia.

Mheshimiwa Amina Amour naye amezungumzia suala hili, lakini akazungumzia udhalilishaji katika ajira na mikataba ambayo haifai na hii yote tumekuwa tukiifuatilia. Mheshimiwa Agripina Buyogera, naye alizungumzia masuala ya mafunzo ya ufundi na haya yatakuwepo kwenye miradi hii na mipango yetu hii au programu zetu za kukuza ajira. Kule Kasulu tutakuja, vijana wa bodaboda na kadhalika. Nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Mwaiposa kwamba, tunahitaji vilevile vijana hawa kuwa waaminifu, kuwa wabunifu, kuwa na bidii na kuwa na *commitment* ili waweze kuajirika na waweze kuhudumu kwenye ajira zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sivyo, wanaweza wakanyang'anywa hizo kazi na watu kutoka nje ya nchi kupata, kama ambavyo tumekuwa tukiona.

Mheshimiwa Felista Bura amezungumzia sana suala hili, pamoja na Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Dkt. Kebwe. Nasi tunakubaliana, kule Serengeti ni hili la kuwa Wanaserengeti hawaajiriwi kwenye Hoteli za Kitalii zinazozunguka Serengeti. Wapo kama asilimia14 tu ndiyo wanaotoka ndani ya Serengeti, Wilaya ya Serengeti. Hili ni suala la kuangalia kwamba; je, tatizo ni la vijana wenyewe au ni Sera au ni hawa wawekezaji. Tatalifuatilia.

Mheshimiwa Ali Khamis Seif, naye amezungumzia umuhimu wa kilimo na viwanda. Nami ninataka nisisitize kwamba, kwa kweli kilimo na viwanda ndiyo njia sahihi ya kuondoa au kupunguza tatizo la ajira na uwekezaji mwingine ambao nimeusema.

Ninakubaliana na Mheshimiwa Aliko Kibona kuhusu vijana kujitegemea na waone kuwa kazi ya kutafuta ajira ni ya kwao.

Ninamshukuru Mheshimiwa Rebecca Mngodo, naye amezungumzia masuala hayohayo, pamoja na Mheshimiwa Mheshimiwa Ole-Nangoro, kwa *polytechnics*. Mimi ninadhani ni suala zuri ambalo vijana watapata elimu ya ajira.

Mambo ya upendeleo ambayo ameyazungumzia Mheshimiwa Ntukamazina katika ajira ni suala la kufuatilia. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbowe kuhusu ukweli kuwa, labda Tanzania tunazaliana sana na tuweke Sheria, sasa ni mjadala wa Kitaifa huo labda tuje tuangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu karibu 600,000 hawaajiriki, kwa sababu wanaingia kwenye soko la ajira wakiwa darasa la saba; ndiyo maana tumeweka mpango huu ambao umetangazwa kwamba wanafunzi wakae miaka kumi. Kwa hiyo, ukiongeza na miaka yao, utakuta vijana wanatoka shuleni wakikaribia miaka 18 ambayo wanaweza kujitegemea. Kwenye nchi nyingine wameweka kabisa kuwa, mtoto ambaye yuko chini ya miaka 18 ni lazima awe ama shuleni, chuoni au kwenye chuo cha ufundi. Huko ndiko tunakoelekea ili watu waingie kwenye soko la ajira wakiwa na miaka 18 na kuendelea; ni jambo ambalo kama Sera, tutaendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa sana suala la ajira kwa watoto na hili sisi kama Wizara, tunalifanyia kazi na kwa sababu ipo Sera ambayo inasema kuajiri mtoto ni makosa na Sheria ya Kazi inakubana kuwa mtoto ambaye yuko chini ya miaka ya kuajiriwa hawezi kuajiriwa la sivyo utakuwa unaenda kinyume cha Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Anna MaryStella Mallac, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed na Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, wote wamezungumzia suala hili. Wengine wamezungumzia kuhusu ajira ya mtoto na hili tutaendelea kulikazania na mmeona kwa jinsi Waziri alivyosema, watoto ambao wameondolewa kwenye ajira ya watoto na wakapelekwa mashuleni na wengine wakapewa elimu ya ufundi.

Wabunge wengi wameongelea suala la *TaESA* kwenye eneo hili la ajira. Ninamshukuru Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Mtemvu na wengine waliozungumzia suala la *TaESA* na hasa lile la *Recruitment Agencies*.

Kwa upande wa *TaESA* kama *TaESA*, wamefanya kazi pamoja na ufinyu wa bajeti ambao upo. Wengine wamezungumzia kazi imekuwa ikiendelea kufanyika na tumeona jinsi ambavyo wameweza kuunganisha hata waajiriwa na waajiri. Ninakumbuka kuwa, karibu watu 1,500 wameunganishwa na waajiri na Mawakala kama 60 ambao wamekuwa wakisaidia katika suala la kupatia wafanyakazi hawa vijana ajira. Hili la *Employment Agencies* ni suala ambalo tunalo na *TaESA* kazi yao kubwa katika hili ni kuangalia kuwa, wanafanya kazi kulingana na Sheria na kufuata taratibu ambazo zipo. Wapo *Employment Agencies* ambao wanatafuta waajiri kwa ajili ya viwanda au waajiri walioko nchini, lakini kuna wengine ambao wanatafuta wafanyakazi kwa ajili ya kuwatafutia kazi nje ya nchi. Wote hawa *TaESA* wanawa-*regulate* kuangalia kama wanafanya kazi yao sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezingatia maoni yenu ambayo mmeyatoa kuwa, inawezekana hawa watu wakawa wanawanyonya wafanyakazi wao kwa kupata hela nyingi zaidi na hawa wakapata hela kidogo. Kubwa zaidi ni kwamba, wafanyakazi hawa hasa wa ndani, hawana uhusiano wa moja kwa moja na mwajiri wanayemfanyia kazi. Suala hili tutalifanyia kazi kama Wizara, tuweze kuona hii Sheria au utaratibu huu wa *Employment Agencies* ni namna gani unaweza kufanya kazi vizuri zaidi, bila kuwanyonya wafanyakazi na bila kuwanyanyasa, kwa sababu wanakuwa hawana uwezo wa kuzungumza na yule wanayetoa huduma kwake. Tukishakamilisha hiyo, tutarekebisha pale ambapo tutaona kuna hali ambayo siyo nzuri na kama kuna ulazima, tutaangalia kama kuna umuhimu wa kuwa na hizi *Employment Agencies* au hapana, lakini kwa sasa wanatoa huduma na *TaESA* wanawafuatilia vizuri.

Suala lingine ni kuhusu ajira ya majumbani ambalo lilizungumzwa na Mheshimiwa Anna Mallac na Mheshimiwa Angellah Kairuki, wamezungumzia sana suala hili. Niseme tu kuwa, hii ni ajira, kama tunavyojua, ni sawa na ajira zingine, Sheria inawalinda wafanyakazi wa majumbani na lazima kila mtu atekeleze hiyo Sheria na kwa sasa hata mishahara

wamewekewa kima cha chini ambacho Mheshimiwa Waziri ametangaza ongezeko la asilimia fulani. Hawa wanacho Chama vilevile cha Wafanyakazi ambacho kinaangalia maslahi yao. Kwa hiyo, wote tukishirikiana, sisi tunaowaajiri wafanyakazi wa majumbani, Chama chao cha Wafanyakazi na Wizara kwa kutumia Sheria, ninadhani hawa wataweza kupata haki zao.

Natoa onyo kuwa, kwa wale wanaokuwa na wafanyakazi majumbani na hawawalipi inavyostahili na wanawanyanyasa, wajue kuwa wanafanya makosa na Sheria inaweza kuchukua mkondo wake. Limezungumzwa sana suala la ajira kwenye hoteli na baadhi ya viwanda kuwa kuna manyanyaso makubwa na hapa Mheshimiwa Thuwayba amezungumzia na akatoa mifano kwa upande wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri tu kuwa, kuna matatizo kwenye baadhi ya hoteli zetu hasa zinazomilikiwa na watu wa nje. Manyanyaso haya yapo na wengine hawafuati Sheria sawasawa, lakini tumekuwa tukifanya kaguzi. Kinachofanywa na Wizara yangu ni kuendeleza kaguzi hizi ili kuhakikisha wafanyakazi kwenye hoteli hizi hawanyanyaswi kama ambavyo inaonekana. Vilevile wanapewa ujira unaostahili. Ningeomba na wao wanalalamika kuwa, Vijana wa Kitanzania kama alivyosema Mheshimiwa Mwaiposa, wengine hawawi waaminifu, hawafanyi kazi kwa bidii, ruhusa kila siku, kufiwa ndiyo kila siku. Sasa na hili kama wafanyakazi au Vijana wa Kitanzania, tuione, ni lazima tuwe na bidii tuweze kushindana. Tukiwa wavivu tukanyang'anywa kazi zetu tusije tukalaumu kumbe tatizo ni la kwetu. Sisi kwa upande wa sheria tutaendelea kuliangalia na tutafanya kaguzi kwenye hoteli.

Tuwaonye tu wale wanaoanzisha hoteli hizi na wenzetu kutoka nchi za Asia, wamekubuhu katika hizi hoteli ambazo hawalipi vizuri wafanyakazi wa Kitanzania na hili ni kosa kubwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ajira au manyanyaso ya wanawake kwenye maeneo ya kazi na hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa Ummu Mwalimu. Pale ambapo hata wajawazito wanafukuzwa kazi, kwa kweli ni makosa, kwa sababu huyu mfanyakazi analindwa na anapokuwa na ujauzito kuna Sheria yake ya kupewa likizo bila manyanyaso na kulipwa kama inavyostahili. Natoa onyo tena hapa kwamba, kwa wale wanaowanyanyasa hawa akina mama wajawazito, kwa sababu tu wamepata ujauzito, ni makosa na Sheria itachukua mkondo wake.

Naomba pia kama Wizara, tupate taarifa hizi *specific* kwamba ni kiwanda gani au mwajiri gani amenyanyasa akina mama kwa sababu ya ujauzito au kwa sababu nyingine yoyote, ili sisi tuweze kupeleka watu wetu waweze kukagua na kuchukua hatua zinazostahili. Kwa hiyo, ninamshukuru sana Mheshimiwa Ummu Mwalimu.

Mheshimiwa Angella Kairuki na Mheshimiwa Margareth Mkanga, wamezungumzia suala la walemavu. Nalo niliseme hapa kuwa, Sheria ipo na ukimnyanyasa au ukimdhaliisha mtu mwenye ulemavu, kwa sababu ya ulemavu wake kwenye ajira ni kosa la jinai kwenye Sheria yetu ya Ajira na Mahusiano Kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tutaendelea kulifuatilia, tuendeleo kupata taarifa na tutaimarisha kaguzi ili kuhakikisha kuwa hili halitokei.

Ajira kwa wageni, limezungumzwa sana kuwa wageni wanachukua ajira zetu. Mheshimiwa Hamoud Jumaa, amelizungumzia hili, Mheshimiwa Felister Bura, umezungumzia suala hili na Mheshimiwa Maryam Msabaha, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Lucy Owenya na hata Mheshimiwa Ntukamazina. Suala hili ni kweli kuna udanganyifu ambao upo, lakini sisi kama Wizara, pale ambapo tunapata hizi taarifa na kwa kuangalia Sheria zetu, kwa bahati mbaya mpaka sasa vibali vya ajira vilikuwa vinatolewa maeneo tofauti; kuna *T/C*, kuna Uhamiaji, kuna Wizara ya Kazi. Sasa ni kweli kuwa, ile Sheria Namba 9 ya Mwaka 1999 ya Huduma

za Ajira inatuhusu sisi kushughulikia suala hili na Uhamiaji vilevile Sheria Namba 9 ya mwaka 1995. Tumekuwa tukishirikiana lakini imeonekana kuwa, kuna haja ya kuweka suala hili la vibali vya ajira katika eneo moja; na kwa maana hiyo, sasa hivi tunaandaa Sheria kwenye Wizara ya Kazi na ya Vibali ambayo sasa vibali vya kazi nchini vitatolewa na Wizara ya Kazi na Ajira na siyo Uhamiaji.

Uhamiaji watatoa vibali vya kuishi nchini na Wizara ya Kazi na Ajira itatoa vibali vya ajira. Hii itaondoa mgongano ambao umekuwepo na itatuwezesha kujua vizuri sana hawa watu wako wapi. Mzee Ntukamazina amesema kuwa, nchi yetu imekuwa *Plastic Society*, watu wanaingia na kutoka, wanafanya kazi na kutoka wakati wowote. Ninadhani hili litadhibitiwa baada ya Sheria hii kupita.

Mambo mengi yamezungumzwa, sasa twende kwenye *OSHA*; Mheshimiwa Catherine Magige, ninakubaliana na wewe kuwa wakaguzi ni wachache, fedha kidogo na madaktari waongezeke.

Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Thuwayba Muhamed na Mheshimiwa Naibu Waziri Angellah Kairuki wamezungumzia kuhusu viwanda vya chuma kwa uchungu sana na hasa kuhusiana na ajali ambazo zinatokea. Niseme tu kuwa, *OSHA* kweli ina matatizo ya nyenzo na uwezo wa kifedha, lakini tunaendelea kuwawezesha hao wenzetu na ndiyo maana unaona wamekuwa wakifanya kaguzi; mwaka jana wamefanya kaguzi karibu 6,900. Zile kaguzi za kawaida na maalumu 6,900 tena na mwaka ujao wa fedha wamepanga kufanya kaguzi 20,000 za kawaida na 25,000 maalum na kuweza kupima afya za wafanyakazi 50,000, tofauti na 26,000 wa mwaka huu. Kwa hiyo, watafanya mara mbili. Hii ni kwa sababu wanaendelea kupata uwezo na sisi tutaendelea kuwasaidia. Ni kweli kwamba, kama alivyosema Mheshimiwa Angellah Kairuki, kwa mujibu wa takwimu za *OSHA*, kuna ajali 74 zilirekodiwa na 14 zilisababisha vifo, wafanyakazi 81 waliumia migongo,

wafanyakazi 39 kifua, 191 usikivu, lakini tunaendelea kuimarisha suala la *OSHA* ili wapate nguvu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CMA* imezungumzwa, wamefanya kazi kweli, wameombewa pesa na hata Mwenyekiti amesema, *Inshallah* watapata labda nyongeza ya hela kabla ya mwisho wa bajeti hii, ili wapate nguvu zaidi ya kufanya kazi zao. Kazi zao zimekuwa ni nzuri, wanaendelea kutoa elimu kama Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mheshimiwa Jenista Mhagama walivyosema na watapata uwezo kadiri wanavyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kuhusu *NIP* kidogo. Niseme tu, Mkurugenzi Mkuu ameshapatikana na Bodi taratibu zipo njiani karibu zitakamilishwa na wanaendelea kutoa elimu. Niseme tu kwamba, Sera ya Tija nayo karibu inakuja, kwa sababu hii Sheria ya Kazi inalinda zaidi wafanyakazi, lakini Sheria ya Tija ambayo waajiri wamekuwa wakiililia, itakapokuja ndiyo itabana wafanyakazi ambao ni wazembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni kuhusu suala la Mchikichini, limeulizwa na Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Mtemvu na Mheshimiwa Chomboh. *NSSF* watatekeleza Mradi huu. Suala ambalo lipo ni la Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, lakini kwa sababu Mwenyekiti na mimi tunajua kuna tatizo hili, tutamwomba Waziri wetu, akishirikiana na Waziri wa TAMISEMI, tukirudi Dar es Salaam, tukae na Manispaa ya Ilala na *NSSF*, tuone tatizo liko wapi. Mradi huu ni muhimu sana na hatuoni ni kwa nini haujaanza, kwa sababu ya migogoro midogo ya mambo ambayo tunaweza tukayamaliza ili mradi uanze na Wananchi wafaidike pale Mchikichini, siyo Wananchi wa Ilala lakini vilevile Dar es Salaam na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine yaliyobaki Mheshimiwa Waziri atajaribu kuyazungumzia. Natoa tena shukurani kwako, kwa kunipa nafasi hii na kuweza kuchangia. Mwisho, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa kunipa nafasi jioni hii ili nami niweze kutoa majibu kwa Wabunge ambao wamechangia asubuhi na mchana huu, kuhusiana na hoja ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kwa kuongea na wale waliochangia kwa maandishi. Tumepata bahati ya kupata wachangiaji saba kwa kuongea, wa mwisho akiwa ni Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Naibu Waziri, Mbunge wa Segerea, lakini pia tumepata Waheshimiwa 31 waliochangia kwa kuongea.

**MWENYEKITI:** Kwa maandishi.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** *Sorry*, waliochangia kwa maandishi, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ni Wabunge wengi sana na maandishi yalikuwa marefu na yalihusu vipengele vingi. Ni wazi kwamba, hatutaweza kuyajibu yote tukayamaliza sasa hivi, lakini muwe na imani kwamba, majibu yatakuja kwa maandishi kama ilivyo ada, lakini pia tutaendelea kupeana majibu kadiri tunavyoendelea kukaa hapa Bungeni. Kwa kifupi, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango hii yote inaonesha jinsi mlivyoanza kuielewa Wizara ya Kazi na Ajira na majukumu yake, kwa sababu kama huelewi kitu, kwa kawaida Mwalimu unasema kama Mwalimu akimaliza kufundisha halafu darasa halina maswali ina maana hakuna aliyeelewa. Kwa hiyo, kwa maandishi haya na michango hii, tunajua mmeanza kuielewa Wizara, majukumu yake na mmeweza kupata namna ya kuweza kutushauri ili tuweze kufanya kazi vizuri zaidi na ninawashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo na tatizo la ajira hasa ajira kwa Vijana. Namshukuru sana Naibu Waziri,

Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, amelieleza vizuri. Kama nilivyoeleza pia kwenye Hotuba yangu ni kwamba, Wizara imeandaa programu na mtakumbuka Bunge hili lilipitisha hapa Azimio la kuwa na programu mwezi wa kumi na moja na sisi tulilichangamkia. Tulifikiri kwamba, kama tungekuwa tume-*prolong* Bunge hili la Bajeti mpaka mwezi wa sita, ile programu tungeileta hapa ili tuijadili kwa pamoja na tukubaliane tuiendeshe vipi. Kwa hiyo, tumeandaa Programu ya Kitaifa ya Kukuza Ajira kwa Vijana, ambayo tunafikiri tuitekeleze kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa hivi mpaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema, programu hii inatarajia kutoa zaidi ya ajira laki sita kwa vijana na ilizingatia hoja nyingi za Wabunge. Wakati mnaijadili hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla, bahati mbaya hayupo na tuliangalia kwamba, vijana wengi wanaomaliza hasa Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu, wanamaliza wakiwa na taaluma walizosomea. Kama mtu amasomea uchumi, amesomea programu nyingine yoyote Chuo Kikuu au Elimu ya Juu, basi hiyo peke yake ndiyo anatoka nayo Chuoni. Kwa hali hiyo, kijana yule alipokuwa anasoma kama wengi mlivyosema, matarajio yake ni kwamba, atapata ajira katika ofisi ya Serikali au katika ofisi yoyote ya mtu binafsi ama sekta iliyo rasmi, lakini asipopata ajira ndiyo utamkuta sasa anamanga manga na cheti chake cha ile taaluma yake ofisi hadi ofisi au anafunua magazeti kila siku kutafuta ajira, kwa sababu hana maandalizi zaidi ya yale aliyotoka nayo katika kile chuo alichosoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo tumelitambua Serikali katika Wizara yangu, lakini pia na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambao tunashirikiana nao kwa karibu sana. Tumeona ipo haja ya kuwaandaa vijana wetu hawa kwa kuwajengea uwezo na ujuzi katika stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali. Kwa sababu hata ukimpa mtu pesa, utakumbuka wale walioenda kuchukua Mabilioni ya Kikwete, japo siyo wengi, walikuwa vijana. Walikuwa wakifika pale wanaambiwa waandike *Action Plan*, Andiko la Mradi, anajaza fomu pale ndiyo Andiko la Mradi limekwisha.

Kwa hiyo, akienda na zile pesa kwa kweli hawezi kuzitumia vizuri, kwa sababu hakutoka nyumbani na wazo la mradi ambao anataka kuufanya, mradi anaupata pale pale kwenye dirisha la *CRDB* au *NMB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ni vizuri vijana hawa tuwawezeshe kwa kuwapa, kwanza, stadi kwa ajili ya ujasiriamali, lakini pia stadi za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuliona kwamba, vijana hawa hata kama wakipata stadi hizi na tukaondoa ile *mindset* ya kupata ajira katika ofisi au kuajiriwa, kwa kuwa tunataka wajajiri, basi inabidi wajajiri katika sekta isiyo rasmi au iliyo rasmi, lakini wawe na mtaji.

Kwa hiyo, katika programu hii, kama tulivyosema, tumeshajipanga na tumewashirikisha wadau na wadau wakubwa ni mabenki na benki mojawapo ambayo imeonesha nia thabiti ni *CRDB*. Kwamba, Serikali ikiweka dhamana; kwa mfano, ya bilioni moja, *CRDB* watatoa mikopo ya bilioni mbili, tukiweka bilioni kumi watatoa bilioni 20. Kwa hiyo, hii ni dalili nzuri na ni mpango mzuri ambao tunaona tuuchangamkie vijana hawa waweze kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu umeanza na Chuo Kikuu cha Sokoine, ambapo wana *Association* yao inaitwa *SUGEKO*, ambayo inawasajili hawa vijana, lakini kwa kutumia *modality* hii hii tutaenda pia kwenye vyuo vingine. Vyuo vya *VETA* ambavyo pia vina-*train* vijana wetu kwenye taaluma mbalimbali, lakini baada ya hapo hawawezi kutumia zile taaluma kwa sababu hawana nyenzo na hawana mtaji. Kwa hiyo, jambo la pili ni mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo litasaidia vijana ni kuhamasisha kuwapa mazingira wezeshi katika masuala ya kiseru au masuala ya kisheria. Mtakumbuka mmezungumza hapa; kwa mfano, kijana anatoka Chuo Kikuu cha *SUA*, anataka kulima bustani, atapata wapi ardhi; kwa sababu sheria zetu za ardhi kama alivyozieleza Mheshimiwa Profesa Tibaijuka jana, ni lazima kwanza ufuata vikao,

ufahamike na vikwazo vingi. Kwa hiyo, tunataka tuongee na Wizara husika kwamba, hizi sheria tunafikiri zimepitwa na wakati hasa kwa vijana wanaotaka kujijiri, waweze kupewa ardhi wanapoitaka mahali pale walipo, lakini pia leseni. Unaombwa pesa kwa ajili ya kuanza kufanya biashara, hiyo pesa huna na leseni inakutaka uwe na pesa kabla hujaanza kupata leseni. Kwa hiyo, vyote hivi ni mazingira wezeshi ambayo tunafikiri yatawafaa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Programu hii utahusisha hasa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi. Mikoa na Mamlaka na Serikali za Mitaa ndiko wanakoishi vijana. Kwa hiyo, najaribu kulieleza hili ili Mheshimiwa Mchuchuli ambaye ameongea kwa uchungu kuhusiana na jambo hili, nimweleze Wizara inafanya nini kuwahamasisha vijana hawa. Hayo ndiyo tunatarajia kuyafanya na nafikiri muda siyo mrefu, tutaanza kufanya haya. Kwa sababu tumeshafikia hatua ya kuandika *Cabinet Paper*, hatujaipeleka Serikalini iweze kukubalika, tupate hii dhamana ya benki. Nafikiri kwa muda mfupi tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna vijana wameshaanza tayari; kuna mifano, Vijana wa Igunga wanaolima alizeti. Wapo Vijana wa Singida wanalima alizeti, wapo vijana Tabora na mikoa yote, tumesha-*survey* kama tulivyosema, vikundi 502 vya vijana wanajihusisha katika miradi mbalimbali. Kwa hiyo, kuna vijana tayari wameshagundua kwamba ajira siyo kwenda kuajiriwa ofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu imejikita katika kuwawezesha na kuwahamasisha vijana walengwa kujijiri na watakapojijiri wataajiri na wenzao. Tumeona mifano ya vijana waliofanya hivyo, wanafuga samaki, wengine wanafuga kuku na wanaajiri wasomi wenzao. Kwa sababu inawezekana wewe unafuga, lakini hujui masuala ya *accounts*, kwa hiyo, utamtafuta *accountant* na huyo atatoka katika Chuo kingine kuja kufanya kazi kwako. Kwa hiyo, tunafikiri kwamba hii itakuwa ni *viable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mlivyosema, vijana wajajiri zaidi katika kilimo na sisi tunakubaliana, lakini katika kilimo hicho kama tulivyosema ni kilimo cha biashara, yaani hiki kilimo kiwe na mnyororo wa thamani, *value added chain*. Hapo hapo kijana aweze ku-*process* mazao yake ili aongeze thamani na katika kuongeza thamani atapata faida kubwa. Kwa hiyo, nakubaliana na Wabunge kwamba, masuala haya ni mtambuka, yatahusisha Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi, Halmashauri zetu, Mikoa na Wizara nyingine nyingi, ikiwemo Sekta ya Uwezeshaji, ambayo anaishughulikia Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu pamoja na Wizara ya Vijana, Habari, Utamaduni na Michezo na Wizara nyinginezo ambazo tunafikiri kwamba, zitashiriki pamoja na Taasisi za Umma, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Wabia wengine wa Maendeleo; kwa mfano, kama tutahitaji masuala mengine kama fedha basi tutawahusisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepokea ushauri wa Wabunge kuhusu kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hii ni muhimu kabisa, kwa sababu tutakapokuwa tumefanya utafiti ambao tunataka kushirikiana na *NBS* kufanya utafiti wa nguvukazi, utafiti huu utatusaidia kuangalia hali halisi ya taaluma inayotakiwa katika soko la ajira. Siyo sasa hivi Chuo kitoe tu ilimradi kitoe taaluma, kwa sababu hata mwaka huu tumepata tatizo la kuajiri vijana waliosoma *psychology* katika vyuo vyetu vya elimu; amesoma *psychology* lakini hana somo la kufundishia. Imechukua muda mrefu Wizara ya Elimu kuwaajiri, lakini baadaye imewaajiri katika Vyuo vya Ualimu. Kwa hiyo, tunataka sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, tukubaliane soko la ajira linataka nini, taaluma ipi, vigezo vipi ambavyo vinatakiwa na hivi viwanda kusudi vijana waweze kuajirika au kujajiri pia wenyewe. Kwa hiyo, hili ni angalizo zuri na sisi tumeshaliona, tutashirikiana na Wizara ya Elimu na tumeshaanza kushirikiana nao. Kwa mfano, sasa hivi vyuo vingi vinafundisha somo la ujasiriamali kama maandalizi kwa vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa waajiri kuwa, vijana wengi wanaomaliza elimu katika ngazi mbalimbali katika vyuo vyetu



nchini, wanakuwa hawana uwezo ukilinganisha na vyeti walivyonavyo. Kwa mfano, katika sekta ya hoteli, utakuta kijana ana Diploma ya Hoteli, lakini ikilinganishwa na kijana mwenye Diploma kutoka Vyuo vya Kenya, viwango vyake ni hafifu. Hii ndiyo inasababisha vijana wengi wanaachwa katika ajira. Nafikiri kuna kitu kina-*miss*, hiki ndiyo tunataka Wizara ya Elimu sasa ikiangalie kwa undani pamoja na vyuo vyenye vinavyofundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kushirikiana na wadau ili tuwezeshe vijana wetu kuhimili ushindani wa soko. *TaESA* wanafanya kazi hii vizuri sana, wanawasaidia vijana hata jinsi ya kuandika *CV*, hata jinsi ya ku-*appear* kwenye *interview*. Juzi juzi amechangia Mheshimiwa Leticia Nyerere amezungumza; ni kweli unapokwenda kwenye *interview*, kuna namna ya kuingia ofisini, kuna namna ya kujibu, kuna namna hata ya ku-*predict* maswali yatakayotokea kwa taaluma unayoenda kuchukua. Haya yote yanafaa katika kuwaandaa vijana wetu. Kwa sababu mimi nilishawahi kuambiwa na *Human Resource Manager* mmoja kutoka Taasisi Binafsi kwamba, nikipata vijana kumi, saba wakiwa Watanzania, watatu wametoka nchi nyingine za Afrika Mashariki, *for sure* na ninahitaji vijana wawili, wote watakuwa wanatoka katika nchi nyingine za Afrika Mashariki. Kwa sababu anapoingia tu mtoto wa Kitanzania unajua huyu ametokea hapa hapa, lakini anapoingia yule mwingine unajua kabisa *confidence* anayoingia nayo, anavyojiamini na mambo mengine. Yote haya ni muhimu sana katika kupata ajira na hivi ndiyo vitu vinavyotakiwa katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inafuatilia sana kuhakikisha kuwa, uwekezaji kwenye Miradi ya Kitaifa na Sekta Binafsi inachangia ipasavyo katika kuongeza fursa za ajira kwa vijana wetu. Hili limezungumzwa na watu wengi ingawa siwataji, nikitaja tu mada unajua kwa kweli tume-*catch up* katika yale uliyozungumza, maana naona muda utakuwa haunitoshi nikiendelea kutaja majina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, tayari imeshachambua mahitaji ya idadi ya fursa za ajira zitakazopatikana kutokana na uwekezaji katika Miradi ya Maendeleo. Hii tayari tumefundisha Wizara 13, jinsi ya ku-*identify* fursa za ajira kwa miradi yao yote ya maendeleo. Tunachotaka kufanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, wanapo-*identify* hizi ajira, sisi sasa tupewe idadi ya ajira tuweze kuzitangaza kwamba hizi ndiyo ajira zitakazokuwa zimepatikana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu tafadhali.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Naomba mnisikilize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na utafiti wa hali ya ajira na mapato wa mwaka 2011 uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, utafiti huu umeonesha kwamba, ajira zinaongezeka, Watanzania ni wengi. UKiangalia idadi ya vijana wanao-*graduate* kutoka kwenye vyuo vyetu ni kubwa. Nilikuwa nasoma hapa, vijana wanao-*graduate* kutoka kwenye Vyuo vyetu ukiangalia kwa mfano mwaka 2008 walikuwa vijana 1,161, ingawa siyo vyuo vyote vilileta taarifa. Mwaka 2009 walikuwa wahitimu 6,171, mwaka 2010 vijana walikuwa 9,885 na kama ninavyosema siyo vyuo vyote vimeleta taarifa. Mwaka 2011, wahitimu 10,031. Kwa hiyo, mpaka hapa tunapongea, mwaka 2012, mwaka uliopita, walio-*graduate* pamoja na kwamba kuna Vyuo vingi havikuleta lakini vijana 28,000 walihitimu. Siyo rahisi kuwapa ajira wote hawa, lakini ajira zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti huu, unaonesha kwamba, ajira kwa ujumla katika Sekta Rasmi; Sekta Rasmi maana yake Sekta katika Taasisi za Umma, Serikalini, lakini pia katika sekta ambazo ni za binafsi, lakini rasmi kama viwanda na sehemu kama hizo. Ajira iliongezeka kwa asilimia 77.6 ya nafasi zote za ajira zilizotangazwa, hizi siyo ambazo zilihhitaji uzoefu, hizi hazikuhitaji uzoefu wowote ni kwa wanachuo tu wanaotoka katika vyuo wanatangaziwa wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 14 ndiyo zilizohitaji uzoefu na hizi zilikuwa za mwaka mmoja au miwili wala siyo miaka mitano. Asilimia 5.1 ndiyo zilizohitaji uzoefu wa miaka mitatu hadi minne na asilimia 2.8 ndiyo zilizohitaji uzoefu zaidi ya miaka mitano.

Kwa hiyo, ile wanayosema uzoefu, siyo ajira zote zinahitaji uzoefu. Ajira zinazohitaji uzoefu ni zile za kupata mamlaka na madaraka ya kuongoza. Sasa hii inaonesha nini? Hii inaonesha kuwa waajiri wameanza kuzingatia hili suala la kutoweka masharti magumu kwa wahitimu hasa wale wanaotoka katika vyuo na mashule moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utoaji vibali limezungumzwa vizuri na Mheshimiwa Dkt. Makongoro. Taratibu zinafuatwa na zinasimamiwa vizuri na kwa wageni wale ambao wanapenya na kuingia na hasa hasa kwenye migodi, Serikari kwa ushirikiano wa Wizara yangu na Wizara ya Mambo ya Ndani upande wa Uhamiaji, tunawaondoa. Labda niwape mfano tu kwamba, hii kazi kweli inafanyika. Ukichukulia kwa mfano mwaka 2011, katika Mgodini wa Nyamongo, *North Mara Gold Mine*, kuna wageni waliondolewa.

Sasa *don't mind* majina haya; kuna mfanyakazi alikuwa anaitwa Josephine Wegesa Mkono, Josephine Wegesa Mwita, Josephine Magabe Mwita, wote hawa waliondolewa. Wana majina ya Kitanzania lakini tuligundua kwamba, siyo Watanzania wakaondolewa na wana majina karibu yanafanana na ya Watanzania, kwa sababu wanaishi jirani. Kwa hiyo, hili lote linatoa taarifa za wageni ambao wanaondolewa. Kwa hiyo, vibali hivi tunavitoa kwa kweli kwa kufuata taratibu na Sheria ingawa mnapowakuta wageni ambao wapo bila vibali, wamepenya kwa njia zao, wamekuja kwa shughuli zao, baadaye wakajifanya wanafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Waziri amekwishazingatia hilo kwamba, sasa vibali vya ajira vitolewe sehemu hii moja, mamlaka moja, ambayo ni Wizara ya Kazi na Ajira. Baada

ya hapo tutawapelekea sasa Uhamiaji kwamba mtu ana-*qualify*, mpeni sasa kibali cha ukaazi. Nafikiri hapo tutakuwa tumemaliza huu mzizi wa fitina. Imeshaelezwa hawa ndiyo wanaajiriwa wengine katika nafasi ambazo Watanzania wanaweza. Pia nimeshatoa mfano kwa nini hasa majirani zetu wanapata nafasi zaidi kuliko Watanzania kutokana na hali halisi ambazo tayari zimeshaelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye masuala ya Hifadhi ya Jamii, ambayo yamezungumzwa siyo kwa uchungu, lakini mengi yalikuwa ni ushauri. Mengi yalikuwa ni ushauri na tumeuchukua. Labda nizungumzie hili la *PSPF*; kwamba, ina hali mbaya kifedha kwa kuwa ina madeni ya shilingi trilioni 6.87 na hili lilisemwa kwenye hotuba ya ndugu zetu wa Kambi ya Upinzani.

Naomba nieleze kwamba, kwanza, kwa ujumla Mifuko ya Hifadhi ya Jamii haitengenezi faida wala hasara. Tuelewane kuanzia hapo; hiyo ndiyo (a), haitengenezi faida wala hasara, inatengeneza ziada na nakisi. Nakisi ni *deficit*. Sasa kwa upande wa *PSPF*, shilingi trilioni 6.487 hii ni nakisi na mnakumbuka hili Shirika limeanzishwa 1999, likianza kutoa mafao kwa wastaafu ambao hawakulichangia, lakini liliendelea kutoa mafao mazuri. *So what do you expect*; lazima liendeleo kuwa na *deficit*.

Mashirika yote yanakuwa na *deficit*, yanaweza yakawa na *deficit*, lakini kama yanaendelea kuwekeza na kupata pesa ya kutosha, wanaendelea kulipa bila matatizo. Hili Shirika la Hifadhi ya Jamii (*PSPF*) limeendelea kulipa wakati wale wanaolipwa hawakuchangia na mimi ni mmojawapo. Kwa hiyo, liliendelea kupata nakisi. Sasa hiyo nakisi ndiyo iliyoelezwa na *CAG* na siyo hasara kama ilivyoelezwa na Kambi ya Upinzani.

Suala hili lilitolewa ufafanuzi na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu mwenyewe, tarehe 17 Aprili, alipoeleweka vibaya aliamua kulitolea ufafanuzi katika Taarifa yake ya kueleza kwamba, hii ilikuwa ni *actuarial deficit*, ambayo kama nilivyoeleza, imetokana na fedha ambazo malimbikizo ya

mafao, yalikuwa *accrued*, yakawa *accrued liabilities* ya watumishi wa umma kabla ya mwezi Julai mwaka 1999.

Sasa deni hilo ambalo linatokana na utumishi wa miaka ya nyuma ambao hawakuchangia hao, Mheshimiwa Rais vile vile alilieleza, akalitolea ufafanuzi siku ya Mei Mosi kule Mbeya. Kwa hiyo, hii haina maana Rais alitofautiana na CAG. CAG alilitolea ufafanuzi kama Mheshimiwa Rais alivyolitolea ufafanuzi na kama ninavyolitolea ufafanuzi. Kwa hiyo, naomba hii ieleweke jamani na tusiendeele kuwadanganya watu na kuwaogopesha hao *pensioners* wa PSPF. (Makofi)

Mheshimiwa Rais aliahidi hata juzi wakati wa Wiki ya Hifadhi ya Jamii, Wastaafu wataendelea kulipwa. Serikali imeamua sasa hii *deficit* ya PSPF iendeele kutoa kila mwaka bilioni 50 na hata kama hiyo bilioni 50 ikionekana haitoshelezi kulipa mafa, Serikali itafidia kiasi kile ambacho hakitakuwa kimetosheleza. Kwa hiyo, naomba hii ieleweke hivyo na tayari sasa hivi Serikali imeshalipa bilioni 30. Kwa hiyo, tunaenda vizuri. Mifuko iko vizuri, PSPF iko vizuri na inaendelea kuwekeza na tunaendelea kulipwa. Mimi ni mfano hai, naendelea kulipwa kila mwezi na sidhani kama kuna siku nitaachwa kulipwa.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Taarifa ya Kitaalam, *Actuarial Valuation*, inaonesha Mifuko ina hali nzuri ya fedha, inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kisheria.

Kambi ya Upinzani pia ilisema vitega uchumi vya Mifuko havisimamiwi. Hii siyo kweli, sitaki kusema ni uongo, lakini naomba niseme siyo kweli. (Kicheko)

Vitega uchumi vya Mifuko baada ya kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti, moja ya kazi ya Mamlaka hii ni kusimamia uwekezaji wa Mifuko yote, kwa kushirikiana na BoT, wanatoa miongozo au *guidelines*. Kwa wale waliohudhuria Mkutano wa Wadau wa NSSF uliopita huu wa mwisho, tulikuwa na mama kutoka BoT ambaye alikuwa na

mada ya *guidelines* kuhusiana na uwekezaji wa Mifuko. Wanatoa miongozo na *guidelines* ili kwamba sasa Mifuko yote inawezeza kutumia hizo *guidelines* kujua kwamba kwenye miondombinu wawezeze kiasi gani, kwenye majengo mengine, barabara na mabenki *and so forth* wawezeze kiasi gani.

Kwa upande wa Mfuko wa *PSPF* tena niseme katika masuala ya kusema kwamba, hizi pesa za *PSPF* hazijalipwa kutokana na deni la Bodi ya Mikopo hizi shilingi bilioni 21.9. Naomba niseme tena siyo kweli, zimeshalipwa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wameshapewa pesa yao na Serikali inaendelea kulipa na mikataba yote ambayo ilikuwa imeahidiwa imeshawekwa na itaendelea kulipa shilingi bilioni 54 zilizobaki na kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha, Serikali imetenga shilingi bilioni 20 kwa ajili ya malipo hayo. Kwa hiyo, Serikali inalipa. Pia kwa upande huo wa *PSPF*, kuna suala la Kiwira, shilingi bilioni 8.6 zimekwishalipwa kwa ajili ya mikopo hiyo ambao ulikuwa ni wa shilingi bilioni 5.0.

Shilingi bilioni 800 zimelipwa kwa ajili ya mkopo wa Kiwanda cha Madawa *TPI* na zimebaki shilingi milioni 440 ambazo zinaendelea kulipwa. Mikopo ya *Kagera Sugar 27<sup>st</sup> Century Textile* na *TANESCO* inalipa bila matatizo kwa mujibu wa mikataba, kwa sababu malipo hayo yote yameandikwa kwenye mkataba; kwa hiyo, inalipwa *according to their* mikataba. *UDOM, PCCB*, naomba niseme pia Serikali inaendelea kulipa kulingana na mikataba ilivyoonesha.

Kambi ya Upinzani pia walisema Mifuko hii iunganishwe. Jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi. Siyo jambo rahisi kama mnavyolifikiria ndugu zangu. Kwa sababu Mifuko hii ilianzishwa kwa Sheria mbalimbali na ipo chini ya Wizara mbalimbali. Sasa ukiunganisha hapa, Mifuko ipo hapa inasikia, wengine huwataki mema, mwingine aende wapi sasa aliyekuwa *DG* kwenye Mfuko mmoja aende wapi ghafla. Kwa hiyo, inatakiwa maandalizi. Ingawa hilo muhimu, lakini tunachosema kuna maandalizi yanatakiwa yafanyike kwa ajili ya kuendeleza. Tunajua *concern* yenu, lakini *so far* hamna tatizo la kutokuwa na muunganiko au kutokuwa na

Mifuko michache. Mnaona jinsi Mifuko inavyoshindana katika kuongeza wigo.

Mliohudhuria Wiki ya Hifadhi ya Jamii, mtakubaliana na mimi; Watanzania sasa hivi wana wigo mpana kuamua niingie *NSSF*, niingie *GPF* au niingie *PSPF*, kwa sababu sasa hivi hamna *restriction* kwamba *PSPF* ni kwa ajili ya Watumishi wa Umma, *PPF* kwa ajili ya Mashirika ya Umma, *LAPF* kwa ajili ya TAMISEMI, hapana, sasa hivi unaingia Mfuko unapoanza kazi. Sasa nafikiri huo wigo ni mzuri zaidi kuliko uunganishe ubaki na Mfuko mmoja. Wenzetu Kenya wana Mfuko mmoja wa *NSSF*. Sasa matatizo yake yapo. Kwa hiyo, nafikiri tusitafute matatizo haya ya upande mwingine, tu-*enjoy* kwanza hii hali iliyoipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie *NSSF*, Shirika ambalo liko kwenye Wizara yangu, nalo ni kuhusiana na masuala ya Miradi ya Ujenzi kama *UDOM*, Daraja la Kigamboni, Umeme Mkuranga na hivi vyote vimepongezwa. Nashukuru sana kwa pongezi zimepokelewa, wahasika wako hapa na sisi Wizara. *NSSF* ipanue wigo wa Wanachama. Kamati imesema na mimi nasema, tunashukuru sana katika kupanua wigo wa Wanachama, *NSSF* imeandaa mpango mkakati wa kuwashirikisha Wanachama kutoka makundi mbalimbali katika sekta isiyo rasmi.

Mfano, Wakulima wa Kahawa Kigoma, Wavuvi Tanga, Vikundi vya *VICOBA*, wachimbaji wadogo wadogo wa madini katika Mikoa ya Mwanza na Geita, pia madereva na makondakta wa daladala na kadhalika. Hadi sasa idadi hiyo imeshafikia elfu sita; kwa kweli wamejitahidi. Kwa hiyo, wanaendelea kupanua wigo. Kamati pia imesema Serikali ifuate mifano ya nchi nyingine kwa kutumia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kupiga vita umaskini na kukuza uchumi; ni kweli tunakubaliana nao kabisa. Serikali kwa kutumia Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii imefanya miradi mingi inayosaidia kupiga vita umaskini.

Miradi hii ni pamoja na *Kegera Sugar*. Naomba ndugu zangu mkiweza mtembelee *Kagera Sugar*, ni mahali ambapo

Mifuko hii imewekeza. Ukiingia pale, huwezi kujua kama uko Tanzania, ni *heavy mechanized* kilimo; ndiyo KILIMO KWANZA kiko pale, lakini kuna wale wakulima wa pembeni ambao pia wana-*feed* hiyo *Kagera Sugar*. Hii yote ni Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kuna *Katani Limited*, kuna Mikopo ya SACCOS na Miradi mingine mingi, yote ya uwekezaji inayotoa ajira kwa watu wengi. *Kagera Sugar* inajiri zaidi ya vijana 3,000; ni wengi, lakini inajiri wale *skilled* na *unskilled*. Hawa *unskilled* ndiyo wanaokata miwa, wapo karibu 3,000. Kuna vijana wa *SUA* sasa hivi ajira yao kubwa ipo *Kagera Sugar*. Mfano, nimeshasema Mradi huo umeajiri watu wengi na umezalisha ajira nyingi kama nilivyosema.

Kamati imeshauri *NSSF* iendelee kutoa elimu kwa Wanachama na Umma. Elimu hii inatolewa kwanza kwa mikutano ya wadau ambayo sasa imeshafika mitatu na mkutano wa nne utakuwepo, lakini pia kwa matangazo mbalimbali yanayotolewa kwa njia ya redio. Sasa hivi mtaona lile fao la afya (SHIBU), linatolewa mara kwa mara kuhusu namna ya kujiunga na nanufaa yake, na kwamba hutakatwa mwisho wa siku. Hiyo ni elimu. Pia wanatumia magazeti, majarida ya kuelimisha Wanachama kwa ujumla na Wananchi kuhusu mafao yatolewayo na *NSSF*. Mfano, kwenye TV wanatumia *ITV*, *Channel Five*, *Arusha Radio*, *Sports FM*, Dodoma na katika majarida ya *Bang*, *The Manager*, *Hifadhi News*, *Jambo University Directory*, Tovuti ya *NSSF* [www.nssf.or.tz](http://www.nssf.or.tz).

Vipindi maalum katika *Television* na *Radio* mbalimbali, Maonesho ya Kitaifa ya Tanga, Maonesho ya Wiki ya Hifadhi ya Jamii, Semina kwa Waajiri nchi nzima, Maonesho ya Nane Nane na pia katika michezo ambayo wanafadhili wanajitangaza sana.

Serikali ilipe madeni ya *NSSF*, Kamati imeshauri. Serikali imeshaanza kulipa madeni ya *NSSF* kwenye miradi mbalimbali; nimeshatoa mfano, hamna haja ya kurudia. *NSSF* ichukue hatua kali kwa Kamati na waajiri wanaochelewesha michango. Hii ni kweli na kwa wale ambao wamejiandikisha,



*NSSF* itaendelea kuchukua hatua kali kwa waajiri wanaochelewesha kulipa michango ya wafanyakazi hao.

Hii inajumuisha adhabu ya kulipa asilimia tano kwa kila mwezi uliocheleweshwa. Hiyo ni adhabu kali sana. Aidha, jumla ya waajiri 120 wamefunguliwa mashtaka Mahakamani kwa makosa ya kutokulipa michango.

Kambi ya Upinzani imesema, Mifuko ipanue wigo wa Wanachama; hii nimeshajibu. Mifuko wa Hifadhi ya Jamii ina udhaifu katika kusimamia Miradi hii; hili nimeshajibu. *SSRA* wanasimamia vizuri na *BoT* wametoa miongozo. *NSSF* haijasaini mkataba wa Serikali na *UDOM*; imeshasaini. Jibu ni hivyo. Serikali haijaanza kulipa *NSSF*; imeshaanza.

Serikali haijalipa fedha za ujenzi wa Jengo la Bunge. Jamani, Jengo la Bunge linalipwa *up to date*, yaani lenyewe ndiyo linalipwa vizuri sana. Kwa nini hamtafuti hizi taarifa kabla hamjaandika haya mambo jamani? Kwa sababu hivi vitu, watu wakisia wanasikitika. Sasa watu ambao ni wahusika ni wadau wakishasikia hivyo, wanakuwa *surprised*. Muwe mnatuuliza, muwe mnaniuliza mimi niko *available* hapa nitakuwa nawaeleza. Limeshalipwa, wanaendelea kulipa. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba hawajaanza kulipa, *up to date*. (*Makoff*)

*NSSF* haijalipwa madeni ya Miradi ifuatayo: Mradi wa Jeshi Tanzania, shilingi milioni 24 zilitumika kutekeleza Mradi huu hadi kukamilika. Serikali inaandaa utaratibu wa kuanza kulipa. Hapa sasa ndiyo inaanza kulipa na hili deni ni la miaka kumi, kwa hiyo italipa tu.

Mimi nafikiri mengi yaliyosemwa nimeyajibu. Madeni yanatia mashaka afya ya Mfuko; hiyo ondoa mashaka kabisa na wasiwasi. Afya ya Mifuko yote ni salama, ina afya nzuri. Majengo ya *UDOM* hajayakabidhiwa Serikalini. Majengo haya yameshakabidhiwa, kwa hiyo, siyo kweli na ndiyo maana majengo haya hayamo katika Vitabu vya *NSSF*. Aidha, matengenezo madogo madogo, *maintenance* na bima na majengo mengine yanashughulikiwa na *UDOM*.

Pensheni ya wazee nakumbushwa hapa. Jamani pensheni ya wazee, naomba niseme Serikali imeji-*commit* italipa. *I mean* sijui tuite pensheni, kwa sababu kwa kawaida pensheni ni mtu aliyechangia, sijui ni hifadhi ya jamii ya wazee. Kwa sababu pensheni maana tunafikiria 17,000, 20,000; pensheni ya 20,000 umeiona wapi? Kwa hiyo ni kama vile Hifadhi ya Jamii. Kama vile matibabu ya wazee bure. Kama vile kuwapa wapande basi bure na mambo kama hayo. Kabla hatujalipa hii pensheni na hii ndiyo inayogomba, lazima tujihakikishie kwamba, chanzo cha pesa cha kulipa hiyo pensheni ni endelevu. Hatutaki kuanza kulipa pensheni leo mwaka mmoja kwa mkupuo, mwaka unaofuata wazee hawana pensheni; watatulaumu, watasikitika, wataleta tabu katika nchi, afadhali wasingelipwa kabisa.

Kwa hiyo, kinachogomba ni kuangalia vyanzo, tujue wazee hawa ni wangapi sasa hivi. Walikuwa milioni mbili mwaka 2007; je, bado ni milioni mbili? *NBS* hawajatoa *statistics* za wazee sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutawalipaje kwa M-pesa, kwa njia gani, na je tutawafikiaje, *administrative costs* ni zipi? Kwa hiyo, pensheni ya wazee kwa kifupi ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mjue kwamba, Serikali imeshaji-*commit* italipa, lakini baada ya kujihakikishia kwamba inaweza kulipa. Kwa hiyo, ndugu zangu wa Upinzani, msiseme tuanze kulipa mwaka huu, hatujajua kama pesa hiyo itakuwa *sustainable*; ni hilo tu, *sustainability* ndiyo inagomba, *otherwise, commitment* iko wazi na dhamira iko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, najua hamtaondoa shilingi kabisa katika maelezo haya yote tuliyotoa mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa hiyo, naomba mpitishie hii bajeti, ni ndogo lakini itatutosha kutushughulisha kwa mwaka mzima, tuendeleo kufanya yale ambayo tumejipangia, tukija hapa mwakani tuwaeleze tumefanyaje, tuombe na nyingine. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote, tushirikiane na nawashukuru tena sana kwa maoni yenu na tutayatekeleza yale ambayo

yanatekelezeka, yale ambayo hayatekelezeki naomba mtusamehe, lakini tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi**

Kif.1001 – *Administration and HR*

*Management* ... .. Sh. 1,924,748,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 65 - Wizara ya Kazi na Ajira**

Kif.1001 – *Administration and HR*

*Management...* ... .. Sh. 3,103,011,500

**MWENYEKITI:** Majina ambayo yapo Kikanuni kwenye meza ni matano; Mheshimiwa Muhammad Chomboh, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Rajab Mbarouk. Tutatazama kama muda utabakia, tutaweza kuwapa nafasi na wengine. Tunaanza na Mheshimiwa Muhammad Chomboh.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo katika kifungu 1001.

Kwenye mchango wangu wa maandishi, nilimwandikia Mheshimiwa Waziri anieleze kuhusu Mradi wa Mchikichini Dar es Salaam, ambao unasimamiwa au umeingia ubia Shirika la *NSSF* na Kampuni ya Malaysia. Mradi

huu ulikuwa kila kitu kipo tayari mpaka mikataba tayari na nyumba zimeshavunjwa kwa utekelezaji wa Mradi huu, lakini mpaka sasa hivi Wananchi wamekuwa *desperate*, hatujui umefikia wapi. Shirika la *NSSF* kama tunavyojua ni moja katika mashirika yanayosaidia Wananchi kwa hali nzuri kabisa, linafanya kazi zake vizuri kabisa na ni moja katika Shirika tunalolitegemea sana Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnakumbuka jana hapa tulikuwa tunazungumzia habari ya Shirika la *NHC* linavyosaidia, lakini na Shirika la *NSSF* ni moja katika mashirika ambayo yanatusaidia sana Watanzania kwa hali na mali. Sasa Mradi huu una maslahi ya moja kwa moja kwa Wananchi, wanategemea sana mafanikio ya Mradi huu, wako *desperate* na hawajui kinachoendelea.

Mheshimiwa Waziri nataka unipe hatima ya Mradi huu na kwa mara ya kwanza naweza nikauzuia mshahara wako au shilingi nitaitoa kama sijapata jawabu la kuniridhisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sera ya nchi ni kuwaandalia wafanyakazi, ofisi za kufanyia kazi, lakini Mikoa yetu mingi, Taasisi mbalimbali za Serikali na zisizokuwa za Serikali, zinakosa maeneo ya kufanyia kazi. Kwenye mchango wangu wa maandishi nilishauri kwamba, kwa nini Serikali isiendelee kuitumia *NSSF* ambayo inafanya kazi nzuri, kujenga majengo kama ilivyojenga pale *UDOM*, ijenge majengo kwenye Mikoa yetu ikiwemo Mkoa wa Singida ili taasisi hizi zipate maeneo ya kufanyia kazi kuliko zinavyohangaika sasa hivi?

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba uniruhusu nilipongeze Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (*TUCTA*), kwa kulifufua upya Gazeti la Mfanyakazi, ambalo ndiyo sauti ya Wafanyakazi. Nilitegemea Mheshimiwa Waziri ingeingia kwenye hotuba yake, kwa sababu yeye ndiyo alilizindua kule Mbeya, lakini niwatakie kila la kheri Wafanyakazi wa Gazeti la Mfanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu migomo na migogoro makazini inachangia sana kuleta athari katika uchumi na katika huduma za jamii na kwa sababu tunacho chombo cha *ATE, TUCTA* pamoja na Serikali; vimejiandaa namna gani kuondoa migogoro makazini?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuanzia ukurasa wa pili mpaka ukurasa wa kumi na moja, Kambi Rasmi ilieleza kutoridhishwa na namna ambavyo Serikali inatekeleza Sera ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kuanzia kwenye ahadi iliyoko kwenye Ilani ya CCM ya kuhamisha mafao ya Mifuko kwenda kwenye ahadi ya kupanua wigo wa pensheni kwa Wananchi wengi na kuhusiana na uendelezaji wa Mifuko.

Sasa Mheshimiwa Waziri katika majumuisho ametoa majibu ambayo bado hayajaridhisha na kwa haya nitakayoyahoji kutaka ufafanuzi iwapo sitaridhika na ufafanuzi, naomba niseme tu kwamba, nakusudia kuondoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri ili tuweze kupewa ufafanuzi wa kina zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mheshimiwa Waziri amepotosha mambo yaliyohojiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani. Mheshimiwa Waziri, amezungumza na kujaribu kuwaaminisha Watanzania kama vile taarifa zilizomo kwenye Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni taarifa tu ambazo Kambi imeziokota okota. Wakati ambapo katika Hotuba hii kwenye kila ukurasa, Kambi Rasmi ya Upinzani imenukuu kwa maneno kutoka kwa Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Kama Serikali ilikuwa na ufafanuzi wa kuridhisha ufafazi huo ingeutoa kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali asingeonesha mashaka kwa maeneo mbalimbali. Maneno ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani imeyatumia kama ukurasa wa sita kwamba, Mifuko imekuwa ikipata hasara yapo kwenye Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu

za Serikali. Neno nakisi halikutumika bali lilitumika neno hasara, maneno ya kwamba, Mifuko ipo kwenye hali mbaya ya kifedha yametumiwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe kwenye Ripoti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo ambayo tunahitaji bado ufafanuzi ni mgongano wa kauli. Wizara ieleze ukweli ni nani ambaye yuko sahihi kati ya Mheshimiwa Rais katika Hotuba yake ya mwezi Mei kwa Wafanyakazi iliyosema kwamba, nanukuu: "Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii ipo kwenye hali nzuri kifedha na ni endelevu." Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali nyingine ikiwa ni ya karibuni kabisa, mwezi Machi mwaka 2013, ndiyo alikabidhiwa Mheshimiwa Rais; hii Ripoti inasema hivi: "Hali ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uko katika hatari ya kutoendelea kama hatua madhubuti hazitachukuliwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ikalieleza ukweli Bunge na hiyo mikataba ambayo Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, tayari Serikali imekwishaingia kwa ajili ya kulipa madeni ni muhimu ikaletwa hapa Bungeni ili tuhakikishe, kwa sababu Mheshimiwa Waziri *commitment* ilikuwa ...

**MWENYEKITI:** Umeshaeleweka, nakushukuru. Mheshimiwa Rajab!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nimeamua kutoondoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri hasa pale aliposema kwamba, yupo tayari kutujibu na yuko *available*. Nataka nitumie nafasi hiyo kwa kuwa yeye yuko *available*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwiano katika michango ndani ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii bado ni utatanishi. Uwiano uliopo kati ya Mfuko na Mfuko inatofautiana. Sasa hii inahatarisha na inapelekea kwamba mbele ya safari huenda Mifuko hii ikaanza kuwa na mifarakano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ndani ya Mifuko hii inawezekana pengine labda katika *NSSF*, mwajiri analipa asilimia kumi, mwajiriwa analipa asilimia tano, lakini katika Mfuko mwingine waajiriwa haohao wa Serikali wanalipa kwa viwango tofauti. Hili limelalamikiwa sana na bado linaendelea kulalamikiwa na Mifuko pamoja na wadau wengine.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu limelalamikiwa muda mwingi, naomba anipatie maelezo ni kwa namna gani suala hili mpaka sasa wamelichukulia hatua ili huu uwiano uwepo sawa, kusiwe na *double standard* katika kuchangia. Ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nataka kuuliza kuhusu Sera ya Serikali. Naona huu utaratibu ambao Wizara inakuja nao wa ku-*identify* Miradi kwa watu ambao wako Vyuho Vikuu kama walivyofanya *SUA*, ni kitu kizuri, wana-*identify* Miradi, wanafuatilia ile Miradi wanawakopesha watu fedha, zile fedha baadaye zinarudi zinaendelea kukopesha watu wengine. Sasa kwa kuwa Serikali imeanzisha utaratibu huu, kwa nini Serikali isiache zile fedha ambazo zinapitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi, fedha ambazo zinapitia Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, fedha ambazo zinapitia *TASAF* Awamu ya Tatu, ambazo zinakwenda zinagawiwa kwa Wananchi na hazirudi, ziweze kuendelea kugawiwa kwa watu wengine na kuondoa tatizo la ajira. Kwa nini Serikali isitumie mfumo huu wa Wizara kuliko kuendelea kugawa fedha hizi zingine zinagawiwa kwenye vikundi tu vya CCM, wanagawiwa watu fedha hazirudi?

Kwa nini fedha hizi zinazokwenda kwa Wananchi zisipitie mfumo huu wa kukopesha watu kuliko kutengeneza Taifa la watu ambao wanapewa fedha kupitia Mifuko mbalimbali halafu hazirudi? Kwa nini fedha zisipitie kwenye utaratibu huu; watu wakopeshwe fedha zirudi wakopeshwe watu wengine?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwanza hoja ya Mheshimiwa Chomboh, suala la Mchikichini. Sisi kwa maana ya *NSSF*, kwa sababu hapa tuko upande wa *NSSF* hatuko upande wa Manispaa ya Ilala, kwa sababu kuna pande mbili; *NSSF* na Ilala, sasa sisi tunajibia *NSSF*. Tunachosubiri kwa maana ya *NSSF* ni kupata kibali cha michoro na kupata kibali cha ujenzi, ambavyo vyote vinatoka kwa *partner* wetu wa pili kwa maana ya Manispaa ya Ilala.

Vilevile wanasubiria wenzetu wa *NSSF* kuwa hati miliki ya maeneo yale yahamie kwa Kampuni ambayo itakuwa imeanzishwa na pande zote tatu; Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, *NSSF* na Mwekezaji kutoka nje, kuna kampuni ambayo imeanzishwa kwa ajili hiyo hati zile zihamishwe. Mambo haya hayajakamilika.

Kama nilivyojibu kwa sababu kunaonekana kuna uchelewefu, basi *NSSF* na Ilala hebu wakae na ikiwezekana sasa wakae na mabosi wao *NSSF* waende na Wizara ya Kazi, kwa maana ya Waziri wa Kazi na Ajira na Manispaa ya Ilala, waje na Waziri wa TAMISEMI ili tulizungumzie suala hili, tuone kwa nini tumekwama. Baada ya hapo, nadhani suala hilo litakuwa halina matatizo na Mradi utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chilolo amezungumzia Ofisi za Serikali Singida. *NSSF* haina shida katika kujenga Ofisi za Serikali, mradi tu kuwe na tija. Tija kwa *NSSF* ni kwamba, hela hizi zirudi kwa sababu ni hela za Wanachama. Kwa hiyo, kama ni Serikali ya Mkoa wa Singida, utasema tutawalipa sisi au Serikali Kuu itawadhamini Serikali ya Mkoa wa Singida kwamba wajengeeni tutawalipa kwa utaratibu huu, *NSSF* watajenga tu. Kwa hiyo, ni kuleta tu mapendekezo kama ni ya kutoka Serikalini au kutoka Serikali ya Mkoa na *NSSF* watajenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ndassa amezungumzia migogoro. Mimi niseme kwamba, migogoro kwa sasa ya maeneo ya kazi nadhani imepungua sana toka *CMA* wameanza kufanya kazi zao. Bado kunatokea



migogoro, lakini ukiangalia ile *speed* ya *CMA* ku-*handle* migogoro hii, kwa sababu taratibu ni kwamba, wewe mfanyakazi, kwanza, kwa kutumia Chama cha Wafanyakazi, tawi lako kwenye kazi pale, suala lile mlijadili na mwajiri, likishindikana kwamba bado mgogoro upo, basi mnakwenda *CMA*. Tumeleza hapa katika kipindi hiki kilichopita, *CMA* wame-*handle* migogoro 5,722 na 2,214 imemalizika kwa usuluhishi na 1,513 imemalizika kwa upatanishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, unaona kwamba, kazi imekuwa ikifanyika vizuri na mimi naomba watu wajue kwamba, kama kuna mgogoro ambao umeshindikana kati yako na mwajiri, *CMA* ndiyo tumeianzisha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Mheshimiwa Mkosamali, nashukuru kwamba umependa sana utaratibu huu ambao tunauanzisha katika kujaribu kuwakopesha vijana waweze kujijiri na hela zirudi ziweze kufaidisha na wengine. Kama utaratibu huu utaonekana ni mzuri kwa mipango na miradi mingine uliyoitaja ambayo inasimamiwa na Wizara zingine, itakuwa vyema basi waje tuwaelezee jinsi ambavyo tumepanga kuutekeleza huo Mradi ili kama Miradi hiyo mingine ina kasoro kweli, basi wafuate mfumo huu ambao sisi tutaufuata. Mheshimiwa Waziri atajibu mengine. (*Makoff*)

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu suala aliloelezea Mheshimiwa Mnyika, kuhusiana na Ripoti ya *CAG*. Kwanza, lazima niseme kwamba, sija-*water down* maoni ya Kambi ya Upinzani, hapana, lakini nilichojaribu kuleza ni kwamba, ile Ripoti ya *CAG* haikuwa na maana ya hasara iliyopatikana kutokana na hiyo Mifuko. Haikuwa hasara, ilikuwa ni hiyo *deficit* ambayo wenyewe wataalam wanaita *actuarial deficit*. Kumbuka hawa wanapofanya tathmini, tathmini yao ni tofauti na ukaguzi unaofanywa kwenye mashirika mengine ya fedha; kwa hiyo, wana hiyo *actuarial evaluation* ambayo ndiyo inaonesha hasa afya ya Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa alipokagua *CAG*, alichooona ni kwamba; kwa mfano, *PSPF* walikuwa

wanaendelea kupata hiyo *deficit* yao kutokana na kwamba, walipoanza hawakuanza na pesa ya watu waliokuwa wameuchangia Mfuko. Kwa hiyo, ikaonekana kuna hiyo sijui ni bakaa au nakisi kwa Kiswahili na siyo kwamba Mfuko ulikuwa unaendelea, kwa sababu kama ni kufa Mfuko ungeshakufa tayari mpaka sasa hivi, *PSPF* ingekuwa *hai-exist*.

Ilikuwa ni namna ya *CAG* kuelezea kwamba, *something must be done* na sasa hivi Serikali inasema *yes something is going to be done* kwenye Mfuko wa *PSPF*, kuondoa hiyo *deficit* kwa kuendelea kulipa ile pesa ambayo wangechangia wale wanaolipwa sasa hivi, nimesema mimi ni mmojawapo, Serikali itatuchangia. Maana Mfuko kufa, maana yake unabaki *bankrupt*. Mfuko huu wa *PSPF* una vitega uchumi vingi tu, kwa hiyo, kama ni kufa basi utauza vitega uchumi ili usife.

Kwa hiyo, Mifuko hii haitakufa, *NSSF* haitakufa na Mifuko mingine haitakufa, kwa sababu mifuko yote dhamana yake ni Serikali. Kwa hiyo, Serikali italipa pale ambapo inaona kuna hiyo *deficit* inayozungumziwa. Mimi nafikiri ukitaka upate ufafanuzi zaidi wa hili, hebu angalia kwenye *website* ya *SSRA*. Mimi naomba ukaangalie kwenye hiyo *website* na ungekuwa umeangalia labda sasa hivi tungekuwa tunaongea lugha moja.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, alikuwa sahihi kwamba, Mifuko haifi. *CAG* alikuwa sahihi kwenye ukaguzi wake kwamba, *something must be done* kusudi Mifuko isiendeleo kuwa na *deficit*. Yeye anataka *all the time* Mifuko iwe na pesa ambayo ina ziada na inapokuwa ina ziada Mifuko ndiyo sasa inalipa hata Wanachama wake pesa nzuri zaidi. Lakini inapokuwa na *deficit*, itaendelea kulipa pesa ileile ambayo inalipa kila wakati, kwa hiyo, inakuwa ni *constant*.

Mfuko unapowekeza unakuwa na ziada, unaongeza na mafao. *That is the only difference* kati ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na biashara nyingine hizi. Ukienda kwenye hii *website* ya *SSRA*, ambayo ni [www.ssra.go.tz](http://www.ssra.go.tz) utaelewa vizuri kuhusiana na hii Ripoti ya *CAG*.

**MWENYEKITI:** Bado swali la Mheshimiwa Rajab.

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Kuhusiana na uwiano, nafikiri alimaanisha uwiano wa Mifuko inapotoa mafao. Tukumbuke Mifuko hii ilianza kwa sheria mbalimbali, ilikuwa na malengo mbalimbali na walengwa mbalimbali; kwa hiyo, ilijipangia hivi viwango mbalimbali. Baada ya ujio wa Mdhibiti na Msimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, kazi mojawapo anayoifanya ndiyo hiyo. Sasa hivi tunapoongea, hata kama ulikuwa Mfuko tuseme wa *LAPF* au *PSPF*, labda ulikuwa unafanya katika Wizara baadaye ukapelekwa Serikali za Mitaa. Unapostaafu, sasa hivi kuna hicho kikokotoo ambacho kinajumuisha hayo mafao ili usipunjike, unakuwa kama vile toka mwanzo ulikuwa kwenye huo Mfuko ambao unaishia mwisho.

Kwa hiyo, *SSRA* inajaribu sasa hivi kuhakikisha kwamba, angalau kikokotoo kinakuwa sawa, kwa wale ambao wako kwenye Mifuko tofauti au kwa wale ambao ni mtu mmoja, lakini anajikuta yuko kwenye Mfuko tofauti wakati wa kustaafu. Hilo tulisubiri litafanyiwa kazi hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muhammad Chomboh!

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo kuna kitu ambacho nilikuwa nataka kuongezea.

Kwa mujibu wa kauli yake ni kwamba, Wizara yake ndiyo Wizara Mama ya *NSSF*, lakini hili jambo linaingiliana na Wizara ya *TAMISEMI*, kwa maana ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Hawa ndiyo waliokuwa kikwazo na siyo mara moja. Mimi nipo katika Kamati ya Ardhi na Nyumba. Halmashauri ya Manispaa ya Ilala badala ya kujenga mji wao wanapangua Mji. Huu Mradi wa Mchikichini siyo Mradi ambao umeibuka tu, kuna nyumba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chomboh, nimekuelewa hoja yako, sasa unaendelea kuichukua shilingi au unairudisha?

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Shilingi nataka kwanza Waziri wa TAMISEMI yuko hapa, ilite wazo alilolitoa Naibu Waziri wa Kazi, nataka kujua yeye atalichukua kwa uzito gani ili Mradi huu uweze kuendelea. Baada ya hapo ndiyo naweza nikatoa uamuzi. Waziri yupo naona atanijibu kwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chomboh, shilingi yako haipo kwa watu wa TAMISEMI, ipo kwa Waziri wa Kazi.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Serikali hii ni moja, TAMISEMI nataka wanijibu, wazo la Waziri wa Kazi anakubaliana nalo? Wakae wakubaliane ili Mradi uendeleo, Wananchi wako *desperate* wanawapelekea kuichukia Serikali yao kwa maslahi ya watu fulani tu kwa sababu gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI una kauli yoyote?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nikiri kwamba, mimi nilimkuta Mheshimiwa Makongoro akizungumza hapa na kwa hiyo na-*respond* kwenye hilo ambalo amelisema.

Leo tumekaa ofisini na tumekutana na wenzetu wa *NSSF*, nimewapigia simu watu wa Ilala kuwaambia kwamba, kuna haja ya kukutana na *tentatively* tume-*suggest* kwamba, ikiwezekana tukutane Siku ya Jumamosi. Kwa hiyo, nadhani kubwa hapa tunalohitaji na nakubaliana kabisa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Makongoro kwamba, waje wote, hata na Dkt. Dau tulikuwa naye na wale wengine wote, nimewaambia leo na nataka nipate *substantive report* kuhusu jambo hili. Kwa sababu, jambo hili lilikuja ofisini kwetu leo mchana huu.

Kwa hiyo, naafiki kabisa na kama Mheshimiwa Mbunge anafikiri ana wasiwasi, hili ni jambo ambalo tunachukua uzito ukubwa wala hakuna tatizo, kwa sababu ni mambo ambayo walikuwa wameelewana na mambo

ambayo sasa tutaendelea kuyapeleka na kwa maana hiyo, naamini hiki ninachojibu ndicho mlichokuwa mnataka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Chomboh?

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Kwa kauli hiyo, basi sichukui shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba, wakati wa kujibu safari hii, Mheshimiwa Waziri walau amekubali kwamba, hakupuuzia Ripoti ya Kambi ya Upinzani, lakini bado kuna jambo ambalo linahitaji ufafanuzi. Nimesoma tovuti ya *SSRA*, nimesoma Ripoti au Taarifa kwa Vyombo vya Habari iliyotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufafanua. Nafahamu vilevile yaliyojiri kwenye majadiliano kati ya Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali baada ya Ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali juu ya jambo hili kutolewa.

Kwa hiyo, ninachokizungumza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naelewa makando kando yote ya taarifa zake. Sasa Mheshimiwa Waziri, kuna mambo ni vizuri Serikali ikakiri na ikasema kwamba itayarekebisha. Kwanza, ni ukweli ulio wazi kwamba, kuna matatizo kwenye vitega uchumi vya Hifadhi ya Jamii, ndiyo maana leo Taifa tumehamisha tu, badala ya kulipa kwa fedha za mafao za wafanyakazi, tumetoa kutoka kwenye kodi ambazo wafanyakazi wanalipa ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, unakwenda kwenye hoja nyingine.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nataka kutoa hoja ya kuondoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Na ukiondoa shilingi, uwe *specific* kwenye hoja ile ile ambayo ulisema ya athari ya *PSPF*.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ndiyo nasema, hoja hiyo hiyo ya *PSPF, commitment* ya Serikali kwa mujibu wa makubaliano na kwa mujibu wa Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali, ilikuwa ni kulipa shilingi bilioni 71.6 kila mwaka kuanzia mwaka 2010. *Commitment* ambayo Serikali haitekelezi kwenye kulipa madeni.

*Commitment* ya Serikali kwenye Mradi wa Kiwira kutokana na pesa za wafanyakazi zilizozingizwa Kiwira ilikuwa ni kusimamia ufanisi wa matumizi ya fedha za wafanyakazi. Leo Taifa limelipia shilingi bilioni 28 kwenye Ufisadi wa Kiwira, kwa sababu ya udhaifu wa usimamizi wa fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Sasa ninaomba Serikali itoe majibu hapa, kwa sababu mwanzoni niliomba tuletewe mikataba ili tupate *schedule of payments*.

**MWENYEKITI:** Nakushuru Mheshimiwa Mnyika, hoja yako nimeifahamu, Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme; unajua mara nyingine Ripoti ya *CAG* tusiichukue kabla haijapatiwa majibu. Nimesema kwa upande wa Hifadhi ya Jamii, Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii, *CAG* mwenyewe alitoa maelezo sahihi kabisa, tukubaliane kwamba, hii haikuwa ni hasara na wala haioneshi kwamba Mifuko inakufa, lakini pia nimeeleza Serikali inalipa. Si nimesema hapa Serikali inalipa, inalipa kiasi gani; hiyo ni *immaterial*, lakini Serikali inalipa na *finally* italipa kwa sababu inaandaa na mikataba maeneo mengi.

Mmesema hata hapa ndani ya Bunge kwamba, Jengo hili halilipiwi, tena hili liko *up to date* malipo yake. Kagera *Sugar* iko *up to date*, wapi kule *TANESCO* iko *up to date*. Malipo yote yanaenda kulingana na mkataba; hivyo, sioni maana ya kutoa shilingi yangu, kwa sababu nimeshajibu na hayo ndiyo majibu sahihi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, nafikiri wewe ni mzoefu na ni msomi mzuri. Ripoti ya CAG inapotoka anaweka *query*, kwa bahati mbaya anatoa Ripoti yake kabla *query* haijajibiwa na *now the government is paying*. Mheshimiwa Mnyika, nakupa fursa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ninakubaliana na ufafanuzi kwa kiasi ambacho kimetolewa, Ripoti ya CAG inakuwa *raw* kama ni Ripoti ya sasa, kama hii ya Machi, 2013. *Commitment* ya kwamba, Serikali itaanza kulipa shilingi bilioni 71.6 kila mwaka ni ya Ripoti ya CAG ya mwaka 2009/2010, ikawa *carried* kwenye Ripoti ya mwaka 2010/2011, ambayo kwenye Ripoti ya 2009/10 Serikali ilipewa nafasi ya kujibu.

Serikali baada ya kupewa hiyo *query* kwamba inatakiwa ilipe bilioni 71.6...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Mnyika, Mheshimiwa Waziri amejibu kuwa, Serikali inaanza kutekeleza *commitment*, je...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Serikali inatekeleza *commitment* kidogo, imelipa shilingi bilioni 30, inaahidi mwaka ujao kulipa shilingi bilioni 50; kwa nini isikubali kulipa shilingi bilioni 71.6 kama inavyotakiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba ukae. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mnyika kutoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - Finance and Accounts ... ..	Sh. 363,530,600
Kif. 1003 - Policy and Planning ... ..	Sh. 364,355,900
Kif. 1004 - Internal Audit Unit ... ..	Sh. 142,102,000
Kif. 1005 - Procurement Management Unit ...	Sh. 191,588,000

Kif. 1006 - *Government Communication Unit* ...Sh. 55,227,000

Kif. 1007 - *Information and Communication*

*Tech Unit* .... Sh. 107,295,000

Kif. 1008 - *Legal Service Unit* ... Sh. 4,469,057,000

Kif. 2001 - *Labour* ... Sh. 6,304,093,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Employment Division* ... Sh. 2,136,071,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naamini kwa hili Serikali itakubali, kwa sababu limetokana na Maoni ya Kamati, ukurasa wa 22. Nazungumzia kifungu hicho, Kasma 221100 - *Travel out of Country*. Kifungu hiki kimeongezewa kutoka shilingi milioni 16.2 na safari za kwenda nje zimeongezwa zimefika shilingi milioni 63.4 za Idara hii.

Sasa Kamati ya Bunge ambayo ina Wabunge wa pande zote, katika ukurasa wa 22, imependekeza kwamba, kasma hiyo ipunguzwe kwa sababu safari zimeongezwa kwa kiwango kikubwa sana; ipunguzwe kwa kiwango cha shilingi milioni kumi ili zielekezwe kwenye kifungu cha 221000 cha safari za ndani ya nchi watendaji wa hii Idara ya Kazi waweze kwenda Mikoa mbalimbali, kuhakiki vibali vya ajira vya wageni, kwa ajili ya kupunguza ongezeko la wageni ambao wanafanya kazi ndani ya nchi kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho hakusema kama amekubaliana na Maoni ya Kamati au la, ningepomba ufafanuzi na iwapo Wizara haitakubaliana na Maoni ya Kamati, nitaomba nitumie Kanuni za Bunge kutoa hoja ya kuhamisha hili fungu kama ambavyo Kamati ilipendekeza ili mapendekezo ya Kamati yazingatiwe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja na maoni ya Kamati, tulikubali fedha hizo



zihamishwe na kwa sababu *Subvote 2002* bado itakuwa ni kiasi hicho hicho ambacho kimetajwa hapo, haibadili ile *total*, haina madhara yoyote na tulishakubali; kwa hiyo, haina shida.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2003 - *Registrar of Trade Unions* ... .. Sh. 124,927,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lllirudia)*

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira na Taasisi zake, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu, liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Nachukua nafasi hii, kukushukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na kuwashukuru Wabunge wote, kwa namna tulivyoendesha kikao cha leo. Vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru Wakurugenzi wote wa

Mifuko hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli, wanahitaji kutiwa moyo na Bunge hili litaendelea kuwaunga mkono kuleta maendeleo katika Taifa lao.

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi Mheshimiwa James Mbatia, aliomba mwongozo kuhusu hoja yake. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi Mheshimiwa James Mbatia, alipenda kujua utaratibu wa *extra-budgetary finance* una msingi gani kwa sababu mradi wa Kigamboni hauonekani kama una fedha za kutosha na nimeainisha kwamba hela zitapatikana. Serikali imetoa hela za kuusimamisha Mradi, lakini hela nyingi zinatokana na *extra-budgetary finance mechanism*.

Utaratibu huo ni utaratibu ambao kama Serikali haina fedha za kutosha kuendesha Mradi, sasa inausimika kishirika. Kwa ngazi za Halmashauri, tunasema ni *municipal finance*, sasa unaweka utaratibu kama tayari ulivyo pale Kigamboni, *KDA imeshaundwa, Kigamboni Development Agency* na mchakato wa kuunda *Kigamboni Investment Trust*, yaani Mfuko wa Kuendesha ule Mradi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema jana, labda ilikuwa ni kwa kifupi sana, tunakwenda sasa kwenye soko la fedha, kwenye *Capital Market* kwa wawekezaji, kutafuta fedha zinazotosha kuweza kuendesha ule Mradi kwa viwango vya kisasa na kwa Karne hii. Utaratibu ni kwamba, ukiweshaweka ile *Investment Trust*, mtu wa kwanza, tunasema *first tire investor*, mtu wa kwanza kabisa mwekezaji wa kwanza atakuwa ni Mwananchi wa Kigamboni mwenyewe.

Kwa hiyo, ile fidia anayopewa kuanzia asilimia kumi kadiri ya utashi wake, inabaki ndani ya Mfuko, kwa hiyo, mtu anabaki kwenye ardhi yake kwa kupitia soko la fedha. Anaweza akahama *physically* lakini hahami kiuchumi, kifedha. Kwa sababu baada ya muda lile shirika litaanza kutoa faida. Labda niseme kwa urahisi kabisa, haina tofauti

na kama tunavyofanya kwenye mashirika ambapo Wananchi wamewekeza. Kwa mfano, watu wa kwanza kabisa kuwekeza *Tanzania Oxygen Ltd*, wengine mnajua kwamba walionunua hisa zile ni kama zilisinyaa na nadhani mpaka sasa hivi hawajapata faida kubwa sana. Walionunua hisa za *CRDB*; kwa mfano, mnajua kwamba, sasa hivi walio wengi wanafaidika. Sasa huu ndiyo utaratibu tunaoutumia.

Serikali hapa nikimaanisha Baraza la Mawaziri, katika kupitisha Mradi huu wa Kigamboni, ilitoa ridhaa kwamba tutumie utaratibu huu kutafuta hela zinazohitajika. Kwa mfano, bajeti ya mwaka huu peke yake ni shilingi bilioni 650. Sasa shilingi bilioni 650 hazikuweza kupatikana kwenye bajeti, lakini ni utaratibu ambao sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kutafuta fedha. Hivi sasa tunapozungumza, Mheshimiwa Rais ameshatangulia, tunatafuta fedha kwa mfano tunakwenda Singapore na sehemu nyingine, fedha hizi tunaanza kabisa kwenye Soko la Dar es Salaam. Utaratibu tutakaoutumia sasa hivi, tulikuwa tunazungumzia Mifuko yetu ya *NSSF* na *PPF*, nayo inaweza ikawekeza, Wananchi watawekeza, lakini Serikali yenyewe itawekeza ndani ya Mfuko.

Kwa meneno mengine niseme, *extra-budgetary financing*, haipiti Bungeni kwa namna kwamba, hizi ni pesa ambazo zinatarajiwa kupatikana lakini hazijapatikana na zinapopatikana ni za wale waliowekeza. Faida inayopatikana inagawiwa kwa wale waliowekeza. Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu.

Mheshimiwa mwenyekiti, ninaamini kwamba, nimeelewewa. Naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, mimi nikisimama wewe unakaa.

Kuna tangazo hapa; Mwili wa Marehemu Ernest Zullu, aliyekuwa Mtumishi wa Ofisi ya Bunge, umewasili leo tarehe 29 Dar es Salaam. Kesho tarehe 30 kuanzia saa 6.00 mchana, mwili wa marehemu utaagwa nyumbani kwake Ubungo

29 MEI, 2013

Kibangu, karibu na Kanisa la *Father Nkwera* na baadaye kusafirishwa kwenda Peramiho, ambapo mazishi yatafanyika Siku ya Ijamaa tarehe 31. Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Tangazo lingine, naomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Bunge kuwa, kesho Alhamisi tarehe 30 Mei, 2013, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Uongozi saa 3.30 asubuhi kwenye Ukumbi wa Spika, Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.05 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 30 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*